# Alhidaayah

# Katika Manaasik Za

# Hajj Na 'Umrah

Imekusanywa na kuandaliwa na:
www.alhidaaya.com

Yaliyomo

01- Utangulizi

02- Historia Fupi Ya Makkah Na Kuhusu Hajj Na 'Umrah

- Ramani Maeneo Ya Hajj

03- Aina Za Hajj

- Chati Ya Hajj *Tamattu'*

04- Kuwajibika Hajj

05- Fadhila Za 'Umrah Na Hajj

06- Hajj Ya Rasuli Wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم)

07- Matayarisho Kabla Ya Hajj

08- Du'aa Za Kujitayarisha Kuzihifadhi

09- Yanayotegemewa Kutoka Safarini

10- Nasaha Za Mafanikio Ya *Hajjum-Mabruwr*

11- Nasaha Za Afya

12- Yanayowahusu Wanawake

13- *Miyqaat*

14- *Ihraam*

15- Utekelazaji wa 'Umrah

16- Utekelezaji Wa Hajj

17- Kuzuru Madiynah

18- Swalaah Ya Janaazah

19- Du'aa Zilizopokelewa Kutoka Kwa Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم)

20- Mazingatio Na Mafunzo Ya Hajj

21- Aayaat Katika Suwratul-Hajj Kuhusu Hajj

22- Wasiojaaliwa Kwenda Hajj

23- Makosa Yanayofanywa Baada Ya Kumaliza Hajj na Kurudi Nyumbani

24- Faharasa

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

## 01- Utangulizi

AlhamduliLlaah - Sifa njema zote Anastahiki Allaah (سبحانه وتعالى) Pekee, Mola wa walimwengu, Rahmah na amani zimshukie Nabiy wetu Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) na jamaa zake, na Swahaba zake (رضي الله عنهم) na wote waliotangulia kwa wema mpaka Siku ya Mwisho.

Muislamu mwenye uwezo, inamuwajibikia kwake kutekeleza nguzo ya Hajj mara moja katika maisha yake, isipokuwa akiwa na wasaa wa mali na afya na akipenda anaweza kuirudia tena. Hikmah ya kuwajibika mara moja katika maisha ya Muislamu ni kwa sababu ya taabu, mashaka na gharama zake ambazo ingelikuwa taklifu kwa Waislamu pindi ingeliwajibika zaidi ya mara moja. Hivyo basi, kuna umuhimu mkubwa wa Muislamu kudhamiria kuitekeleza 'ibaadah hii tukufu bila ya mapungufu ili aikamilishe kisawasawa khasa kama inavyotakikana kwa taratibu zake na nidhamu zake kama ilivyopokelewa kutoka kwa Nabiy wetu (صلى الله عليه وآله وسلم). Aghlabu humsikia mtu kusema: "Natamani kwenda tena Hajj kwani sikufanya kadhaa na kadhaa," au "Nimekosea kufanya kadhaa na kadhaa." Hakuna shaka kwamba hata ukipata maelezo na mwongozo wa kutosha kabla ya safari huenda ukakosea bado, lakini angalau utakuwa na ujuzi fulani wa kukuongoza katika mengi kutokana na mafunzo utakayoyapata humu In Shaa Allaah. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى)

﴿ هَلۡ يَسۡتَوِي ٱلَّذِينَ يَعۡلَمُونَ وَٱلَّذِينَ لَا يَعۡلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُوْلُواْ ٱلۡأَلۡبَٰبِ ٩ ﴾

**((Je, wanalingana sawa wale wanaouja na wale wasiojua?" Hakika wenye akili ndio wanaokumbuka))**[1]

Kuitekeleza ukiwa na elimu na ujuzi nayo, itakupatia pia Radhi za Allaah (سبحانه وتعالى), na hilo halipatikani ila tu kwa kuitekeleza

[1] Az-Zumar (39: 9).

kutokana na mafunzo sahihi kabisa tuliyoyapata kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ambaye alikuwa akisema alipoanza kuitekeleza:

((لِتَأْخُذُوا عني مَنَاسِكَكُمْ))

***((Mchukue kutoka kwangu Manaasik (taratibu) zenu))***[2]

Tumejaribu kadiri tuwezavyo kukusanya mafunzo yatakayomwezesha Muislamu kuitekeleza 'ibaadah hii kwa njia sahihi na sahali In Shaa Allaah, na hilo litapatikana pindi tu ukijiandaa vizuri kwa mafunzo yake. Kubwa zaidi kwa mwenye kunuia kufanya 'ibaadah hii, ni kumwomba Allaah (سبحانه وتعالى) Amruzuku subira ya kila wakati na katika kila hali kwani hilo ndilo atakalohitaji zaidi huko.

Tumetegemea zaidi mafunzo mbalimbali ya Wanachuoni, kadhaalika kutoka katika kazi mbalimbali tulizokwishaandaa katika mtandao wetu www.alhidaaya.com.

Tutashukuru endapo tutatanabahishwa kwa kasoro au kosa lolote litakalokuwepo katika kazi hii ili tuweze kurekebisha na kuboresha zaidi mbeleni In Shaa Allaah.

22 Swafar 1434H – 5 Januari 2013M
Kimehaririwa 3 Dhul-Qa'dah 1436H

[2] Muslim, Abu Daawuwd, An-Nasaaiy na wengineo.

### 02 - Historia Fupi Ya Makkah Na Kuhusu Hajj Na 'Umrah

#### Makkah

Imeanza pale Allaah (سبحانه وتعالى) Alipomuamrisha Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) ahamie huko pamoja na mkewe wa pili Haajar na mwanawe Ismaa'iyl. Wakati huo Makkah ilikuwa ni bonde tu ambalo hapakuwa na chochote wala wakazi wowote.

﴿ وَإِذْ قَالَ إِبْرَٰهِـۧمُ رَبِّ ٱجْعَلْ هَـٰذَا بَلَدًا ءَامِنًا وَٱرْزُقْ أَهْلَهُۥ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ مَنْ ءَامَنَ مِنْهُم بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْـَٔاخِرِ ۖ ﴾

**((Na (taja) aliposema Ibraahiym: "Rabb wangu Ufanye mji huu kuwa wa amani na Waruzuku watu wake katika matunda atakayemwamini Allaah miongoni mwao na Siku ya Mwisho"))**[3]

#### *Al-Ka'bah*

Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِى بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَـٰلَمِينَ ﴿٩٦﴾ ﴾

**((Hakika nyumba ya awali iliyowekwa kwa ajili ya watu (kufanya 'ibaadah) ni ile ambayo iko Bakkah (Makkah), yenye barakah na mwongozo kwa walimwengu.))**[4]

#### *Twawaaf*

Nayo pia imeanza wakati huo huo wa Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) pale Allaah (سبحانه وتعالى) Anaposema:

---

[3]Al-Baqarah (2: 126).
[4]Aal-'Imraan (3: 96).

﴿ وَإِذْ جَعَلْنَا ٱلْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا وَٱتَّخِذُوا۟ مِن مَّقَامِ إِبْرَٰهِـۧمَ مُصَلًّى ۖ وَعَهِدْنَآ إِلَىٰٓ إِبْرَٰهِـۧمَ وَإِسْمَـٰعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِىَ لِلطَّآئِفِينَ وَٱلْعَـٰكِفِينَ وَٱلرُّكَّعِ ٱلسُّجُودِ ﴿١٢٥﴾ ﴾

**((Na (taja) Tulipoifanya Nyumba kuwa ni mahali pa kurejewa na watu na (mahali pa) amani, na chukueni kutoka mahali pa kusimama Ibraahiym kuwa ni pahala pa kuswalia. Na Tulichukua ahadi kwa Ibraahiym na Ismaa'iyl kwamba: "Itakaseni Nyumba Yangu kwa wanaotufu na wanaokaa i'tikaaf, na wanaorukuu na kusujudu"))**[5]

### *Ar-Raml*

*Ar-Raml* ni kuenda mwendo wa mbio mbio kwa hatua fupi fupi. Ni Sunnah inayotakiwa kutekelezwa katika *Twawaaful-Quduwm*. Sunnah hii haitekelezwi na wanawake wala watoto bali wanaume pekee. Ilianza Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alipowaamrisha Maswahaba watufu *Al-Ka'bah* kwa mwendo wa haraka katika *Twawaaf* tatu za mwanzo kwa sababu ya kudhihirisha nguvu mbele ya makafiri ili isidhaniwe kuwa hali yao bado ni dhaifu kutokana na ugonjwa waliopata kabla ya kuingia kufanya 'Umrah mara ya kwanza kabisa baada ya Hijrah:

عن ابن عباس (رضي الله عنهما) قال : "قدم رسول الله صلى الله عليه وسلم وَأَصْحَابِهِ، فَقالَ الْمُشْرِكُونَ: "إِنَّهُ يَقْدُمُ عَلَيْكُمْ قَوْمٌ قَدْ وَهَنَتْهُمْ حُمَى يَثْرِب". فَأَمَرَهُمُ النَّبِيّ (صلى الله عليه وسلم) أنْ يَرْملوا الأَشْوَاط الثَّلاثَة (وفي رواية زيادة): قال: ((**اِرْملوا لِيرَى الْمُشْرِكُون قُوَّتكُمْ**))

Imetoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba alifika Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) na Maswahaba zake (Makkah) washirikina wakasema: "Wamekufikieni watu ambao wamedhoofika kutokana na homa ya Yathrib". Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akawaamrisha wafanye *Ar-Raml* mizunguko mitatu" (ya

[5]Al-Baqarah (2: 125).

*Twawaaf*) na katika riwaaya nyingine imezidi: ***((Fanyeni Ar-Raml ili washirikina waone nguvu zenu))***[6]

### Fadhila za *Twawaaf*

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) kwamba amemsikia Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema:

((مَنْ طَافَ بِهَذَا الْبَيْتِ سُبُوعًا فَأَحْصَاهُ كَانَ كَعِتْقِ رَقَبَةٍ)) صحيح الترمذي

***((Atakayetufu Nyumba hii, mara saba, akazihesabu barabara atapata fadhila za kuacha huru mtumwa))***[7]

Na pia kamsikia akisema:

((لَا يَضَعُ قَدَمًا وَلَا يَرْفَعُ أُخْرَى إِلَّا حَطَّ اللَّهُ عَنْهُ خَطِيئَةً وَكَتَبَ لَهُ بِهَا حَسَنَةً))

***((Hakanyagi mtu mguu wala haunyanyui mwengine isipokuwa Allaah Humfutia dhambi na Humuandikia jema moja))***[8]

### *Rukn Al-Yamaaniy*

Imesemekana imejengwa na mtu kutoka Yemen[9]. Pia tokea 'Abdullaahi bin Zubayr (رضي الله عنه) alipojenga *Al-Ka'bah* akaiweka ikabakia hadi leo[10]. Inapendekeza kugusa tu kama alivyofanya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) bila ya kubusu au kuleta *takbiyr*.

### Fadhila za *Rukn Al-Yamaaniy*

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

---

6 Al-Bukhaariy na Muslim.
7 *Swahiyh At-Tirmidhiy*.
8 Hadiyth ya 'Abdullaah bin 'Umar - Sunan At-Tirmidhiy (959) na katika *Swahiyh At-Targhiyb* (1139).
9 *Mu'jam Al-Buldaan (3/64) – Yaaquwt Al-Hamwy.*
10 *At-Taariykh Al-Qadiym li-Makkah wa-Bayt Allaahil-Kariym* – Muhammad Twaahir Al-Kurdiy Al-Makkiy (3/256).

((إِنَّ الرُّكْنَ وَالْمَقَامَ يَاقُوتَتَانِ مِنْ يَاقُوتِ الْجَنَّةِ طَمَسَ اللَّهُ نُورَهُمَا وَلَوْ لَمْ يَطْمِسْ نُورَهُمَا لأَضَاءَتَا مَا بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ))

***((Hakika Ar-Rukn na Al-Maqaam ni yaquti mbili katika yaquti za Jannah, Allaah Amezima mwanga wake, na lau kama Hakuzima mwanga wake, ungeliangaza yaliyoko baina ya Mashariki na Magharibi))***[11]

### *Al-Hajar Al-As-wad*

*Al-Hajar Al-As-wad* liko pembe ya Mashariki ya *Al-Ka'bah* kutoka *Rukn Al-Yamaaniy* ambayo iko Kusini Mashariki mwa *Al-Ka'bah*. Ni jiwe tukufu kabisa duniani na pia ni tukufu kabisa katika *Al-Ka'bah* Jiwe ni kubwa mno ila limeingizwa ndani zaidi ya *Al-Ka'bah* hivyo sehemu inayoonekana ni sehemu ndogo kabisa kulingana na iliyoingizwa ndani. *Al-Hajar Al-As-wad* limeteremshwa kutoka Jannah akalipokea Ismaa'iyl kutoka kwa Jibriyl kumalizia kujenga *Al-Ka'bah*.

*Al-Hajar Al-As-wad* ni alama ya pahali pa kuanzia na kumalizia *Twawaaf* na linabusiwa panapokuwa na uwezekano.

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) akisema: "Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alifanya *Ar-Raml* kuanzia *Al-Hajar Al-As-wad* (jiwe) mpaka *Al-Hajar Al-As-wad* mara tatu kisha akatembea (kikawaida katika kutufu *Al-Ka'bah*) mara nne"[12]

Pia imetoka kwa Jaabir bin 'Abdullaah (رضي الله عنه) kwamba: "Tulitoka pamoja na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) katika *Hajjat Al-Widaa'* hadi tulipofika katika Nyumba (*Al-Ka'bah*) alilibusu *Al-Hajar Al-As-wad* kisha akatufu mizunguko mitatu kwa *Ar-Raml* na (*Twawaaf*) nne kwa mwendo wa kawaida"[13]

### Fadhila Za *Al-Hajar Al-As-wad*

[11] Hadiyth ya 'Abdullaah bin 'Amru - *Swahiyh At-Tirmidhiy* (878), Ibn Khuzaymah (4/220), Ahmad (1/207-229-373).
[12] Muslim katika Kitaab *Al-Hajj* (2213).
[13] Muslim 1218.

((الْحَجَرُ الْأَسْوَدُ مِنْ الْجَنَّةِ))

***((Al-Hajar Al-As-wad linatoka Jannah))*** [14]

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ (رضي الله عنهما) قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ((نَزَلَ الْحَجَرُ الْأَسْوَدُ مِنْ الْجَنَّةِ وَهُوَ أَشَدُّ بَيَاضًا مِنْ اللَّبَنِ فَسَوَّدَتْهُ خَطَايَا بَنِي آدَمَ))

Imepokelewa toka kwa ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Al-Hajar Al-As-wad limeteremka kutoka Jannah likiwa jeupe kuliko maziwa, likasawijika (kuwa jeusi) kwa dhambi za bin Aadam))*** [15]

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الْحَجَرِ: ((وَاللَّهِ لَيَبْعَثَنَّهُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ لَهُ عَيْنَانِ يُبْصِرُ بِهِمَا وَلِسَانٌ يَنْطِقُ بِهِ يَشْهَدُ عَلَى مَنْ اسْتَلَمَهُ بِحَقٍّ))

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Naapa kwa Allaah! Allaah Atalileta Siku ya Qiyaamah likiwa na macho mawili ambayo litaweza kuona na ulimi utakaosema, na litashuhudia kwa kila aliyeligusa kwa haki))*** [16]

((إِنَّ مَسْحَ الْحَجَرِ الأَسْوَدِ ، والركنَ اليمانِيّ، يَحُطَّانِ الخطايا حطًّا))

***((Kugusa Al-Hajar Al-As-wad na Ar-Rukn al-Yamaaniy ni kufutiwa madhambi))*** [17]

### *Maqaam Ibraahiym*

Ni mahali aliposimama Ibraahiym (عليه السلام) kumalizia kujenga kuta za juu za *Al-Ka'bah*. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِى بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَٰلَمِينَ ﴿٩٦﴾ فِيهِ ءَايَٰتٌۢ بَيِّنَٰتٌ مَّقَامُ إِبْرَٰهِيمَ ۖ ﴾

[14] Hadiyth ya Anas katika *Swahiyh Al-Jaami'* (3175).
[15] Ibn Maajah katika *Swahiyh Al-Jaami'* (6756), *Swahiyh At-Tirmidhiy* (877).
[16] *Swahiyh At-Tirmidhiy* (961), Ibn Maajah (2944).
[17] Hadiyth ya Ibn 'Umar katika *Swahiyh Al-Jaami'* (2194).

**((Hakika nyumba ya awali iliyowekwa kwa ajili ya watu (kufanya 'ibaadah) ni ile ambayo iko Bakkah (Makkah), yenye barakah na mwongozo kwa walimwengu. Ndani yake kuna *Aayaat* (ishara, dalili) zilizo wazi; mahali pa kisimamo cha Ibraahiym.))**[18]

Inasemekana pia ni mahali aliposimama Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) kuwatangazia watu kuja kutekeleza 'Ibaadah ya Hajj.

Mahujaji wanapomaliza kutufu *Al-Ka'bah* wanatakiwa waende hapo na kuswali rakaa mbili:

﴿ وَٱتَّخِذُواْ مِن مَّقَامِ إِبۡرَٰهِـۧمَ مُصَلًّىۖ ﴾

**((Na chukueni kutoka mahali pa kusimama Ibraahiym kuwa ni pahala pa kuswalia))**[19]

***Hijr***

Inadhaniwa na wengi kuwa ni *'Hijr Ismaa'iyl'* (chumba cha Ismaa'iyl) na kwamba ni chumba alichozikiwa pamoja na mama yake Haajar ndio maana pakaitwa hivyo. Hakuna uthibitisho wa hilo, na si kweli kwa sababu ingelikuwa ni hivyo mahali hapo pasingelifaa kuswaliwa kwani haifai kuswalia mbele ya kaburi. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ameitambulisha sehemu hiyo kuwa ni 'Hijr' pekee. Sehemu hiyo imetajwa katika usimulizi ufuatao pale *Al-Ka'bah* lilipoharibiwa na kujengwa tena:

عَنْ عَائِشَةَ قَالَتْ: سَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ الْجَدْرِ: أَمِنْ الْبَيْتِ هُوَ؟ قَالَ: **((نَعَمْ))** قُلْتُ: فَلِمَ لَمْ يُدْخِلُوهُ فِي الْبَيْتِ؟ قَالَ: **((إِنَّ قَوْمَكِ قَصَّرَتْ بِهِمْ النَّفَقَةُ))** قُلْتُ: فَمَا شَأْنُ بَابِهِ مُرْتَفِعًا؟ قَالَ: **((فَعَلَ ذَلِكِ قَوْمُكِ لِيُدْخِلُوا مَنْ شَاءُوا وَيَمْنَعُوا مَنْ شَاءُوا, وَلَوْلَا أَنَّ قَوْمَكِ حَدِيثٌ عَهْدُهُمْ فِي الْجَاهِلِيَّةِ, فَأَخَافُ أَنْ تُنْكِرَ قُلُوبُهُمْ, لَنَظَرْتُ أَنْ أُدْخِلَ الْجَدْرَ فِي الْبَيْتِ وَأَنْ أُلْزِقَ بَابَهُ بِالْأَرْضِ))**

Imetoka kwa 'Aaishah (رضي الله عنها) amesema: "Nilimuuliza Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) kuhusu ukuta (upande wa Hijr). Je huo ni

---

[18] Aal-'Imraan (3: 96-97).
[19] Al-Baqarah (2: 125).

sehemu ya Nyumba (yaani *Al-Ka'bah*?)" Akajibu: ***((Ndio*))** Nikasema: "Kwa nini basi usiingizwe ndani ya Nyumba?" Akajibu: ***((Watu wako walipungukiwa na uwezo wa fedha))***. Nikasema: "Kwa nini basi mlango wake umeinuka juu?" Akajibu: ***((Watu wako wamefanya hivyo ili wamuingize wamtakaye na wamzuie wamtakae. Na ingelikuwa watu wako si waliotoka kubadili Dini na si khofu kuwa itawachukiza nyoyo zao, ningeliungiza ukuta ndani ya Nyumba na ningeliuteremsha mlango wake usawa na ardhi))***[20]

**Maji ya Zamzam, *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah***

Historia yake imeanza pale Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alipomwacha Makkah mkewe wa pili Haajar na mwanawe Ismaa'iyl akiwa ni mtoto mchanga wa kunyonya. Wakati huo Makkah kulikuwa hakuna chochote. Imepokelewa toka kwa ibn 'Abbaas kama ifuatavyo:

"Ibraahiym (عليه السلام) alikuja na Haajar na mwanawe Ismaa'iyl akiwa anamnyonyesha mpaka alipowasili Makkah penye bonde baina ya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah* mahali kilipo kisima cha maji ya Zamzam hivi sasa, na wakati huo nyumba ya Allaah (سبحانه وتعالى) (*Al-Ka'bah*) ilikuwa ni sehemu iliyonyanyuka tu juu ya ardhi, ikishambuliwa na upepo mkali pamoja na mikondo ya maji ya mvua iliyokuwa ikizikwanguwa pembe nne za nyumba hiyo. Hapakuwa na mtu anayeishi mahali hapo wala nyumba wala maji isipokuwa mti mmoja alipowaacha mkewe na mwanawe chini yake, akawawekea birika la maji pamoja na chombo alichowatilia tende ndani yake, kisha akageuka na kuianza safari ndefu ya kurudi Shaam.

Mama yake Ismaa'iyl alipomuona mumewe akirudi na kuwaacha mahali hapo walipopafikia baada ya safari ndefu iliyowachukuwa siku nyingi njiani, mahali pasipo na mji wala kijiji. Hapakuwa na hata dalili ya kuwepo mtu mahali popote karibu na hapo, akamfuata mumewe na kumuuliza:
"Unatuachia nani mahali hapa pasipo na mtu yeyote?" Akamuuliza hivyo mara nyingi lakini Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) hakumjibu.

[20] Muslim 1333.

Mwisho Mama yake Ismaa'iyl akamuuliza: "Allaah Ndiye Aliyekuamrisha?"
Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) akamjibu: "Naam, ndiyo."

Kwa iymaan iliyothibiti, kwa utiifu mkubwa na kwa moyo uliosalimu amri, Bibi Haajar akamwambia: "Kwa hivyo Hatotupoteza".
Hapo ndipo Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alipogeuka na kuianza safari ndefu ya kurudi Palestina (Shaam) akimuacha nyuma mkewe na mwanawe wa mwanzo na wa pekee wakati ule, na baada ya kutembea muda kidogo mahali ambapo mkewe hakuweza kumuona, Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) akageuka nyuma na kuomba du'aa ifuatayo:

﴿ رَّبَّنَآ إِنِّيٓ أَسۡكَنتُ مِن ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيۡرِ ذِي زَرۡعٍ عِندَ بَيۡتِكَ ٱلۡمُحَرَّمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ فَٱجۡعَلۡ أَفۡـِٔدَةٗ مِّنَ ٱلنَّاسِ تَهۡوِيٓ إِلَيۡهِمۡ وَٱرۡزُقۡهُم مِّنَ ٱلثَّمَرَٰتِ لَعَلَّهُمۡ يَشۡكُرُونَ ٣٧ ﴾

**(("*Rabb* wetu! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuria wangu katika bonde (la Makkah) lisilokuwa na mmea wowote, kwenye Nyumba Yako Tukufu. Rabb wetu, ili wasimamishe Swalaah na Ujaalie nyoyo za watu zielekee kwao na Uwaruzuku mazao ili wapate kushukuru))**[21]

Bibi Haajar akawa anakula zile tende alizowekewa na mumewe huku akimnyonyesha mwanawe, lakini haukupita muda mrefu maji yakaanza kupunguwa na hatimaye kumalizika, na mwanawe alipoanza kuona kiu, Bibi Haajar akaanza kuhangaika huku na kule akimtafutia maji. Akaliendea jabali lililokuwa karibu yake. '*Jabal Asw-Swafaa*' na kulipanda, na alipofika kileleni akaanza kutizama huku na kule akitafuta maji au msafara wa watu watakaokuwa na maji, lakini hakuona kitu. Akateremka na kuanza kutembea taratibu penye bonde lililopo baina ya jabali *Asw-Swafaa* na jabali *Al-Mar-wah*, na alipofika kati kati ya bonde akaanza kukazana huku akiliendea jabali *Al-Mar-wah* na kulipanda, na alipofika kileleni akaanza kutizama huku na kule, lakini bila mafanikio yoyote.
Anasema Ibn 'Abbaas kuwa Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Hiyo ndiyo As-Sa'-y mnayotembea baina ya Asw-Swafaa na Al-Mar-wah)).***

[21] Ibraahiym (14: 37).

Bibi Haajar aliendelea kufanya hivyo mara saba, na alipokuwa akiliendea jabali *Al-Mar-wah* akasikia sauti ngeni ikimsemesha. Alinyamaza kimya ili aisikie vizuri huku akitazama mahali alipo mwanawe, akamuona Malaika amesimama mahali kilipo kisima cha Zamzam hivi sasa, huku akichimba kwa ubawa wake mpaka maji yalipofurika, ndipo mamake Ismaa'iyl alipoyaendea na kuanza kuyachota kwa mikono yake huku akimnywesha mwanawe na kunywa yeye mwenyewe. Alipokuwa akinywa na kumnywesha mwanawe, Malaika akamwambia: "Usiogope, hutopotea, kwani hapa ndipo ilipo nyumba ya Allaah itakayojengwa na mtoto huyu na baba yake."[22]

### *Minaa*

*Minaa* iko kilo mita tano kutoka Makkah. Ni mahali ambako shaytwaan alimfuata Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) kumshawishi asitekeleze ndoto yake ya kumchinja mwanawe Ismaa'iyl. Alimfuata mahali patatu; *Jamaraat Al-Kubraa*, *Al-Wuswtwaa* na *Asw-Swughraa*.

Mahujaji huanzia taratibu zao za Hajj *Minaa* wanapokuja kutoka Makkah tarehe 8 Dhul-Hijja wakiwa wameingia katika Ihraam. Makazi yao kwa wakati huo ni katika mahema na hubakia hapo hadi tarehe 12 au 13 Dhul-Hijjah ili wapate kumalizia 'Ibaadah za kurusha vijiwe katika minara ya *Jamaraat*. Tarehe 9 Dhul-Hijjah Alfajiri huelekea *'Arafah*, halafu huelekea *Muzdalifah*, baadae hurudi *Minaa* na kubakia hapo mpaka  Wanapomaliza kurusha vijiwe ambayo huwa ni tarehe 12 au 13 Dhul-Hijjah hurudi tena Makkah na kubakia hapo au kufanya *Twawaaf Al-Wadaa'i*.

Wanapobakia *Minaa* wanapaswa kumdhukuru sana Allaah (سبحانه وتعالى)[23]

### *'Arafah*

Inasemekana kuwa ni mahali ambapo Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alisimama pia kuwatangazia watu kuja kuhiji kama

[22] Al-Bukhaariy.
[23] Al-Baqarah (2: 203).

alivyoamrishwa na Allaah (سبحانه وتعالى). Alipofika alisema: عَرَفْتُ (nimepajua).

Jabali la *'Arafah* ndipo wanaposimama Mahujaji na ndio kilele cha 'Ibaadah hii tukufu kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

**((الْحَجُّ عَرَفَة))**

**((Hajj ni *'Arafah*))**[24]

Jina la *'Arafah* limetajwa pia katika Aayah[25]

Imesimuliwa toka kwa Yaziyd bin Shaybaan kwamba: "Tulikuwa tumesimama *'Arafah* mahali mbali na *mawqif* (sehemu aliyosimama Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم). Ibn Mirba' Al-Answaariy akaja kutuambia: "Mimi ni mjumbe wa Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amenituma nikuambieni: ***((Simameni mlipo (kwani hapo pia ni mahali pa wuquwf) kwani hapo ndipo mahali aliposimama baba yenu Ibraahiym (عليه السلام)))***[26]

Jabali hilo alisimama Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kuwakhutubia Maswahaba katika *Hajjatul-Wadaa'i* yake ambayo alitoa khutbah yenye nasaha kadhaa na mwishowe kuwataka Maswahaba wafikishe ujumbe kwa kila aliyekuwa hakufika siku hiyo na kuendeleza kizazi baada ya kizazi.

## Fadhila Za Siku ya *'Arafah*

Siku hii ni tukufu mno na fadhila zake zimetajwa katika Hadiyth kadhaa kama ifuatavyo:

- Siku iliyokamilika Dini yetu:

عَنْ طَارِقِ بْنِ شِهَابٍ قَالَ: قَالَ رَجُلٌ مِنْ الْيَهُودِ لِعُمَرَ: يَا أَمِيرَ الْمُؤْمِنِينَ لَوْ أَنَّ عَلَيْنَا نَزَلَتْ هَذِهِ الْآيَةُ: ﴿ ٱلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ

[24] At-Tirmidhiy 2975).
[25] Tazama chini ya *Muzdalifah* (Al-Baqarah 2: 198).
[26] Abu Daawuwd na At-Tirmidhiy na imerekodiwa katika *Swahiyh Abi Daawuwd* (1688) ya Al-Albaaniy.

ٱلۡإِسۡلَٰمَ دِينٗاۚ ﴾ لَاتَّخَذْنَا ذَلِكَ الْيَوْمَ عِيدًا. فَقَالَ عُمَرُ: إِنِّي لَأَعْلَمُ أَيَّ يَوْمٍ نَزَلَتْ هَذِهِ الْآيَةُ, نَزَلَتْ يَوْمَ عَرَفَةَ فِي يَوْمِ جُمُعَةٍ.

Imepokelewa kutoka kwa Twaariq bin Shihaab (رضي الله عنه) amesema: Myahudi mmoja alimwambia: 'Umar: "Ewe Amiyr wa Waumini, lau ingeliteremka kwetu sisi Aayah hii **((Leo Nimekukamilishieni Dini (yenu), na Nimekutimizieni neema Yangu, na Nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe (ndio) Dini yenu))**[27], tungeliifanya 'Iyd siku hiyo. Akasema 'Umar: "Hakika naijua siku gani imeteremka Aayah hii. Imeteremka Siku ya *'Arafah* siku ya Ijumaa"[28]
Na kukamilika Dini yao ni kukamilisha nguzo zote za Kiislamu.

- Siku Ambayo Allaah Amechukua fungamano (ahadi) kutoka kizazi cha Aadam.

Imesimuliwa kwamba Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) amesema: Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Allaah Amechukua fungamano kutoka mgongo wa Aadam katika Na'maan yaani 'Arafah. Akatoa mgongoni mwake kizazi chake chote na Akawatandaza mbele Yake. Kisha Akawakabili kuwauliza*:**

أَلَسۡتُ بِرَبِّكُمۡۖ قَالُواْ بَلَىٰ شَهِدۡنَآۚ أَن تَقُولُواْ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ إِنَّا كُنَّا عَنۡ هَٰذَا غَٰفِلِينَ ﴿١٧٢﴾ أَوۡ تَقُولُوٓاْ إِنَّمَآ أَشۡرَكَ ءَابَآؤُنَا مِن قَبۡلُ وَكُنَّا ذُرِّيَّةٗ مِّنۢ بَعۡدِهِمۡۖ أَفَتُهۡلِكُنَا بِمَا فَعَلَ ٱلۡمُبۡطِلُونَ ﴿١٧٣﴾

**(("Je, Mimi siye Rabb wenu?" Wakasema: "Ndiye, tunashuhudia!" (Allaah Akawaambia): "Msije kusema Siku ya Qiyaamah (kwamba) hakika sisi tulikuwa tumeghafilika nayo haya. Au mkasema: Hakika baba zetu ndio walioshirikisha kabla, nasi tulikuwa kizazi baada yao. Basi Utatuangamiza kwa yale waliyoyafanya wabatilifu"[29]**))
Hadiyth[30]

---

[27] Al-Maaidah (5: 3).
[28] Al-Bukhaariy.
[29] Al-A'raaf (7: 172-173).
[30] Imesimuliwa na Ahmad ameisahihisha Al-Albaaniy.

- Siku Ambayo Allaah Ameiapia

﴿ وَٱلسَّمَآءِ ذَاتِ ٱلْبُرُوجِ ﴿١﴾ وَٱلْيَوْمِ ٱلْمَوْعُودِ ﴿٢﴾ وَشَاهِدٍ وَمَشْهُودٍ ﴿٣﴾ ﴾

**((Naapa kwa mbingu zenye buruji. Na siku iliyoahidiwa (Qiyaamah). Na shahidi na kinachoshuhudiwa))**[31] Imepokelewa toka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) amesema: "Siku ya kuahidiwa ni siku ya kufufuliwa. Siku ya kushuhudiwa ni siku ya *'Arafah*, na Siku ya kinachoshuhudiwa ni Siku ya Ijumaa))[32].

- Ni Siku Bora Kabisa Ambayo Wataokolewa Waja Kutokana Na Moto.

عَنْ عَائِشَةُ (رضي الله عنها) إِنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: **((مَا مِنْ يَوْمٍ أَكْثَرَ مِنْ أَنْ يُعْتِقَ اللَّهُ فِيهِ عَبْدًا مِنْ النَّارِ مِنْ يَوْمِ عَرَفَةَ وَإِنَّهُ لَيَدْنُو ثُمَّ يُبَاهِي بِهِمْ الْمَلَائِكَةَ فَيَقُولُ مَا أَرَادَ هَؤُلَاءِ))** وفي رواية: **((اشْهَدُوا أَنِّي قَدْ غَفَرْتُ لَهُمْ))**

Imepokelewa toka kwa 'Aaishah (رضي الله عنها) kuwa Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Hakuna siku Anayoacha Allaah huru waja kwa wingi kutokana na moto kama siku ya 'Arafah. Na huwa karibu kisha Anajigamba kwao kwa Malaika na Husema: Wametaka nini hawa?))***[33] Na katika riwaayah nyingine ***((Shuhudieni Malaika wangu kwamba hakika Nimewaghufuria))***[34]

- Siku Ya Kutakabaliwa Du'aa:

Imepokelewa toka kwa babu yake 'Amru bin Shu'ayb (رضي الله عنه) kwamba Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

**((خَيْرُ الدُّعَاءِ دُعَاءُ يَوْمِ عَرَفَةَ, وَخَيْرُ مَا قُلْتُ أَنَا وَالنَّبِيُّونَ مِنْ قَبْلِي: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ))**

---

31 Al-Buruwj (85: 1-3).
32 At-Tirmidhiy na ameisahihisha Al-Albaaniy.
33 Muslim.
34 Swahiyh At-Targhiyb ya Al-Albaaniy (1154).

***((Du'aa bora kabisa ni du'aa katika siku ya 'Arafah, na yaliyo bora kabisa niliyosema mimi na Mitume kabla yangu ni: 'Laa Ilaaha Illa Allaah Wahdahu laa shariyka Lahu, Lahul-Mulku wa-Lahul-hamdu wa Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr – Hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah Peke Yake, Hana mshirika. Yeye Ndiye Mwenye Ufalme na Ndiye Mwenye kuhimidiwa, Naye ni Muweza wa kila kitu***))[35]

***Muzdalifah***

*Muzdalifah* ni mahali ambako Mahujaji wanafikia baada ya kutoka *'Arafah*, huingia hapo Magharibi na huswali kwa kujumuisha Swalah mbili za Maghrib na 'Ishaa. Hupumzika na kukesha usiku wake hadi asubuhi wanapokwenda kutekeleza taratibu nyinginezo zilizobakia; *Muzdalifah* ni bonde takatifu na hapo wanapaswa Mahujaji kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa wingi kama Anavyoamrisha[36].

***Jamaraat* na Kuchinja**

*Jamaraat* ni mahali pa kurushwa vijiwe kwa ajili ya kufuata Sunnah ya baba yetu Nabiy Ibraahiym (عليه السلام), pale alipokuwa akimrushia vijiwe shaytwaan kumfukuza, alipokuwa akija kumshawishi asimchinje mwanawe baada ya kuota kuwa kapewa amri hiyo. Shaytwaan huyo alimfuata sehemu tatu na kila sehemu Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alimfukuzilia mbali kwa kumpiga vijiwe. Sehemu hizo ni *Jamrat Al-Kubra, Al-Wuswtwaa* na *Asw-Swughraa.*

Kisa chake kinaanza pale Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alipokwenda Makkah kumzuru mkewe na mwanawe, baada ya kuoteshwa amchinje mwanawe Ismaa'iyl (عليه السلام). Alipomuelezea mwanawe kuhudu ndoto yake, mwanawe alikubali kutii amri hiyo. Alimlaza mwanawe kifudifudi ili asiuone uso wake na ili asije kumhurumia akashindwa kutekeleza amri hiyo. Ismaa'iyl (عليه السلام) akasalimu amri na Ibraahiym (عليه السلام) akijitayarisha kumchinja mwanawe. Hapo Allaah (سبحانه وتعالى) Akamfunulia Wahyi Nabiy Ibraahiym ( عليه

[35] At-Tirmidhiy na ameisahihisha Al-Albaaniy katika *Swahiyh At-Tirmidhiy* 3585.
[36] Al-Baqarah (2: 198-199).

السلام) kuwa asimchinje mwanawe na badala yake akamkomboa kwa kondoo. Maelezo yamekuja katika Qur-aan:

﴿ فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ ٱلسَّعْىَ قَالَ يَٰبُنَىَّ إِنِّىٓ أَرَىٰ فِى ٱلْمَنَامِ أَنِّىٓ أَذْبَحُكَ فَٱنظُرْ مَاذَا تَرَىٰ ۚ قَالَ
يَٰٓأَبَتِ ٱفْعَلْ مَا تُؤْمَرُ ۖ سَتَجِدُنِىٓ إِن شَآءَ ٱللَّهُ مِنَ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿١٠٢﴾ فَلَمَّآ أَسْلَمَا وَتَلَّهُۥ لِلْجَبِينِ ﴿١٠٣﴾
وَنَٰدَيْنَٰهُ أَن يَٰٓإِبْرَٰهِيمُ ﴿١٠٤﴾ قَدْ صَدَّقْتَ ٱلرُّءْيَآ ۚ إِنَّا كَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿١٠٥﴾ إِنَّ
هَٰذَا لَهُوَ ٱلْبَلَٰٓؤُا۟ ٱلْمُبِينُ ﴿١٠٦﴾ وَفَدَيْنَٰهُ بِذِبْحٍ عَظِيمٍ ﴿١٠٧﴾ ﴾

**((Alipofikia (makamo ya) kwenda na kurudi pamoja naye; akasema: "Ee mwanangu! Hakika mimi nimeona ndoto usingizini kwamba mimi nakuchinja, basi tazama unaonaje?" (Ismaa'iyl) Akasema: "Ee baba yangu! Fanya yale uliyoamrishwa, utanikuta In Shaa Allaah miongoni mwa wanaosubiri." Basi wote wawili walipojisalimisha, na akamlaza juu ya kipaji (ili amchinje) Tukamwita: "Ee Ibraahiym! Umekwisha sadikisha ndoto! Hakika Sisi hivyo ndivyo Tunavyowalipa watendao ihsaan. Hakika hii bila shaka ni jaribio bayana". Na Tukamfidia kwa dhabihu adhimu))**[37]

**Hajj**

Hajj Maana yake kilugha: Kukusudia

Maana yake kishariy'ah: Kukusudia kwenda *Baytul-Haraam* Makkah kwa ajili ya kutekeleza taratibu za 'ibaadah makhsusi katika kipindi makhsusi.

Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) na mwanawe Ismaa'iyl (عليه السلام) walipomaliza kujenga *Al-Ka'bah* wakaomba Du'aa:

﴿ وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَٰهِۦمُ ٱلْقَوَاعِدَ مِنَ ٱلْبَيْتِ وَإِسْمَٰعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ
ٱلْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾ رَبَّنَا وَٱجْعَلْنَا مُسْلِمَيْنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَآ أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ

[37] Asw-Swaffaat (37: 102-107).

عَلَيْنَآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ ﴿١٢٨﴾ رَبَّنَا وَٱبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا۟ عَلَيْهِمْ ءَايَـٰتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلْكِتَـٰبَ وَٱلْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ ۚ إِنَّكَ أَنتَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾ ﴾

**((Na (taja) aliponyanyua Ibraahiym na Ismaa'iyl msingi wa Nyumba (*Al-Ka'bah*): "Rabb wetu, Tutakabalie, hakika Wewe ni *as-Samiy'ul-'Aliym* (Mwenye kusikia yote - Mjuzi wa yote). "Rabb wetu, Tujaalie tuwe wenye kujisalimisha Kwako pamoja na *kizazi chetu* wawe ummah wenye kujisalimisha Kwako na Tuonyeshe taratibu za 'ibaadah zetu na Pokea tawbah zetu, hakika Wewe ni *at-Tawwaabur-Rahiym* (Mwingi wa kupokea tawbah - Mwenye kurehemu) "Rabb wetu, wapelekee Rasuli miongoni mwao ataewasomea *Aayaat* Zako na ataewafunza Kitabu na Hikmah na atakayewatakasa. Hakika Wewe ni *Al-'Aziyzul-Hakiym* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika - Mwenye hikmah wa yote))**[38]

Kisha Allaah (سبحانه وتعالى) Akaamrisha iwe nyumba ya kutekelezwa 'ibaadah bila kumshirikisha na chochote.

﴿ وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَٰهِيمَ مَكَانَ ٱلْبَيْتِ أَن لَّا تُشْرِكْ بِى شَيْـًٔا وَطَهِّرْ بَيْتِىَ لِلطَّآئِفِينَ وَٱلْقَآئِمِينَ وَٱلرُّكَّعِ ٱلسُّجُودِ ﴿٢٦﴾ ﴾

**((Na (taja) Tulipomwonyesha Ibraahiym mahali pa Nyumba (*Al-Ka'bah* Tukamwambia): kwamba: "Usinishirikishe na chochote; na twaharisha Nyumba Yangu kwa wafanyao *Twawaaf*, na wanaosimama (kuswali) na wanaorukuu (na) kusujudu.))**[39]

Kisha Allaah (سبحانه وتعالى) Akamuamrisha Nabiy Ibraahiym (عليه السلام)

﴿ وَأَذِّن فِى ٱلنَّاسِ بِٱلْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِن كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ ﴿٢٧﴾ ﴾

**((Na tangaza kwa watu Hajj; watakufikia kwa miguu na juu ya kila ngamia aliyekonda, watakuja kutoka katika kila njia pana za milima zilioko mbali kabisa))**[40]

---

38 Al-Baqarah (2: 127-129).
39 Al-Hajj (22: 26).
40 Al-Hajj (22: 27).

Alipoamrishwa hivyo, Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alisema: "**Ee Mola wangu nitawatangaziaje watu na hali sauti yangu haitaweza kuwafikia watu wote?"** Allaah (سبحانه وتعالى) Akamjibu: "Wewe tangaza kisha ni juu Yetu kufikisha". Akasimama mahali panapojulikana *'Maqaam Ibraahiym'* na kauli nyingine inasemekana kuwa alisimama juu ya jabali la *Asw-Swafaa* au jabali la Abu Qubays, (Allaah Anajua zaidi) akaita: **"Enyi watu! Mola wenu Ameifanya Nyumba (*Al-Ka'bah* kuwa nyumba ya 'Ibaadah) basi njooni muhiji".** Inasemekana kwamba milima yote ilijiinamisha ili sauti yake ifikie sehemu zote za dunia (na wakazi wake) hata ikawafikia walioko matumboni au ambao hawakuzaliwa bado. Akaitikiwa na kila kilichosikia sauti yake miongoni mwa miji, mawe, miti na kila kiumbe ambacho Allaah (سبحانه وتعالى) Ameandika (katika *Lawh Al-Mahfuwdhw*), majaaliwa ya kutekeleza Hajj mpaka Siku ya Qiyaamah. Na vyote vikaitikia kwa kusema: "*Labbayka Alllaahumma Labbayka*".[41]

'Ibaadah hiyo ikaendelea kutekelezwa na Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) kila mwaka alipokwenda Makkah na baada ya kifo chake ikaendelezwa na mwanawe Nabiy Ismaa'iyl na kuendelea kizazi hadi kizazi.

Lakini 'Ibaadah ya masanamu ikakithiri Bara Arabu na 'Ibaadah ya Hajj ikaingizwa upotofu ndani yake kwa kumshirikisha Allaah (سبحانه وتعالى) ikawa inatekelezwa kwa itikadi potofu na ma'asi. Masanamu yakatundikwa katika *Al-Ka'bah*, kuta zikajaa mashairi na picha za viumbe zikatundikwa kwenye *Al-Ka'bah*. Maovu yalikithiri hadi kwamba wanawake walitufu *Al-Ka'bah* wakiwa uchi kama walivyozaliwa wakiitakidi kwamba wanapaswa kumkabili Allaah (سبحانه وتعالى). Machafu ya kila aina yalitendwa wakati wa Hajj, kunywa pombe, kuimba, dansi za wanawake n.k. Mashindano ya kila aina ya uovu; kamari, nyimbo, mashairi yalikuwa na nafasi kubwa wakati huo wa Hajj. Pia walishindana kuhusu nani mbora wa ukarimu wa kuwahudumia Mahujaji mpaka akawa anachaguliwa mkuu wa kabila kwa ukarimu wake wa kugawa chakula na maji. K*affaarah* zao za kuchinja zilikuwa za kumshirikisha Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kuimwaga damu katika kuta za *Al-Ka'bah* na kutundika nyama katika nguzo zake

---

[41] Tafsiyr Ibn Kathiyr (3/221) kama ilivyopokelewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas, Mujaahid, 'Ikrimah, Sa'iyd bin Jubayr na wengineo katika Salaf.

wakiitakidi kuwa Allaah (سبحانه وتعالى) Amekusudia kutaka nyama na damu za wanyama.

Kutufu kwao pia kulikuwa ni kwa kuimba mashairi na kupiga makofi na miruzi. Qur-aan imetaja hali hiyo:

﴿ وَمَا كَانَ صَلَاتُهُمْ عِندَ ٱلْبَيْتِ إِلَّا مُكَآءً وَتَصْدِيَةً ﴾

**((Na haikuwa Swalaah zao (makafiri) kwenye Nyumba (*Al-Ka'bah*) isipokuwa ni miruzi na kupiga makofi))**[42]

Hata *Talbiyah* zao ziliongezwa maneno ya kumshirikisha Allaah (سبحانه وتعالى) walikuwa wakisema:

لبيك لا شريك لك، إلا شريكاً هو لك، تملكه وما ملك

"Nimekuitikia huna mshirika isipokuwa aliyeidhiniwa Nawe, unammiliki naye ni mwenye kumiliki anavyomiliki!"

Kinyume na *Talbiyah* ya Tawhiyd:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ, لَبَّيْكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ, إِنَّ الْحَمْدَ, وَالنِّعْمَةَ, لَكَ وَالْمُلْكَ, لاَ شَرِيكَ لَكَ

**"Nimekuitikia Ee Allaah nimekuitika, nimekuitika Huna mshirika nimekuitika, hakika kuhimidiwa na neema na ufalme ni Vyako Huna mshrika"**

Hivyo ndivyo ilivyokuwa hali ya Hajj kabla kutumilizwa kwa Nabiy Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم). Washirikina waliipotosha kabisa 'Ibaadah hii tukufu iliyoanzishwa kwa Tawhiyd ya Allaah (سبحانه وتعالى) na baba yetu Nabiy Ibraahiym (عليه السلام). Hali ikaendelea hivyo hadi Allaah (سبحانه وتعالى) Alipokidhia du'aa ya Nabiy Ibraahiym ( عليه السلام) baada ya kujenga *Al-Ka'bah* alipoomba:

---

[42] Al-Anfaal (8: 35).

﴿ رَبَّنَا وَٱجْعَلْنَا مُسْلِمَيْنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَآ أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ عَلَيْنَآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ ﴿١٢٨﴾ رَبَّنَا وَٱبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولاً مِّنْهُمْ يَتْلُواْ عَلَيْهِمْ ءَايَـٰتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلْكِتَـٰبَ وَٱلْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ ۚ إِنَّكَ أَنتَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾ ﴾

**((“Rabb wetu, Tujaalie tuwe wenye kujisalimisha Kwako pamoja na *kizazi chetu* wawe ummah wenye kujisalimisha Kwako na Tuonyeshe taratibu za ‘ibaadah zetu na Pokea tawbah zetu, hakika Wewe ni *at-Tawwaabur-Rahiym* (Mwingi wa kupokea tawbah - Mwenye kurehemu. “Rabb wetu, wapelekee Rasuli miongoni mwao ataewasomea *Aayaat* Zako na ataewafunza Kitabu na Hikmah na atakayewatakasa. Hakika Wewe ni *Al-’Aziyzul-Hakiym* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika - Mwenye hikmah wa yote))**[43]

Du’aa ikatakabaliwa kwa kutumwa Nabiy Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) na baada ya miaka ya misukosuko ya da’wah yake akaweza kuitakasa Nyumba ya Allaah (سبحانه وتعالى) na shirki ikatoweka. Abu Hurayrah amesimulia kuhusu Hajj yao kabla ya Hijjat*ul-Wadaa’ii*:

"بَعَثَنِي أَبُو بَكْرٍ الصِّدِّيقِ فِي الْحَجَّةِ الَّتِي أَمَّرَهُ عَلَيْهَا رَسُولُ اللَّهِ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) قَبْلَ حَجَّةِ الْوَدَاعِ, فِي رَهْطٍ, يُؤَذِّنُونَ فِي النَّاسِ يَوْمَ النَّحْرِ: لَا يَحُجُّ بَعْدَ الْعَامِ مُشْرِكٌ وَلَا يَطُوفُ بِالْبَيْتِ عُرْيَانٌ"

Alinituma “Abu Bakr katika Hajj ambayo alichaguliwa na Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) kuwa Amiri kabla ya *Hajjatul-Wadaa’i*, pamoja na kundi la watu wawatangazie watu Siku ya *Nahr* kwamba: “***Hakuna kuhiji baada ya mwaka huu mshirikiana yeyote wala kufanya Twawaaf katika Nyumba wakiwa uchi***”[44]

Baada ya hapo Tawhiyd ya Allaah (سبحانه وتعالى) ikathibitika katika ‘Ibaadah hii tukufu hadi leo.

---

[43] Al-Baqarah (2: 128: 129).
[44] Muslim.

**Ramani Maeneo ya Hajj**



## 03- Aina Za Hajj

Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ ٱلۡحَجُّ أَشۡهُرٞ مَّعۡلُومَٰتٞۚ فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلۡحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي ٱلۡحَجِّۗ وَمَا تَفۡعَلُواْ مِنۡ خَيۡرٖ يَعۡلَمۡهُ ٱللَّهُۗ وَتَزَوَّدُواْ فَإِنَّ خَيۡرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقۡوَىٰۖ وَٱتَّقُونِ يَٰٓأُوْلِي ٱلۡأَلۡبَٰبِ ١٩٧ ﴾

**((Hajj ni miezi maalumu. Na atakayekusudia kuhiji (akahirimia), basi asifanye tendo la ndoa wala ufasiki wala mabishano katika Hajj. Na lolote mlifanyalo katika ya kheri Allaah Analijua. Na chukueni masurufu. Na hakika bora ya masurufu ni taqwa. Na nicheni Mimi enyi wenye akili!))**[45]

Wamekubaliana Wanachuoni kwamba miezi ya Hajj ni Shawwaal, Dhul-Qa'dah na Dhul-Hijjah. Kwa hiyo mtu anaweza kuelekea Makkah katika miezi hiyo.

عَنْ جَابِرِ (رضي الله عنه) عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ قَالَ: **((لَا يَنْبَغِي لِأَحَدٍ أَنْ يُحْرِمَ بِالْحَجِّ إِلَّا فِي أَشْهُرِ الْحَجِّ))**

Imepokelewa toka kwa Jaabir (رضي الله عنه) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Haipasi kwa yeyote aingie katika Ihraam isipokuwa katika miezi ya Hajj))***[46]

Kuna aina tatu za Hajj; *At-Tamattu', Al-Qiraan, Al-Ifraad*. Aina hizo zinategemea hali ya mtu na nchi anayoishi.

### *At-Tamattu'* - التَّمَتُّع

Ni aina ya Hajj kwa niyyah ya kufanya 'Umrah kisha Hajj. Anayetekeleza huitwa *Al-Mutamatti'*.

Haji atavaa Ihraam ya 'Umrah tu wakati wa miezi ya Hajj, (anapokwenda Makkah mapema) ambayo inamaanisha

45 Al-Baqarah (2: 197).
46 Tafsiyr Ibn Kathiyr.

kwamba atakapofika Makkah atafanya *Twawaaf* na *As-Sa'-y* ya 'Umrah. Kisha atanyoa au kukata nywele, hapo atakuwa amemaliza 'Umrah, na atavua Ihraam yake na kusubiri siku ya *Tarwiyah* ambayo ni siku ya tarehe 8 Dhul-Hijjah. Siku hiyo Haji atavaa nguo zake za Ihraam kwa ajili ya Hajj tu na atatekeleza yote yanayompasa kufanya.

*Hajj At-Tamattu'* Inatekelezwa kwa mpangilio ufuatao:

Utakapofika *Miyqaat*, utaingia katika Ihraam kwa niyyah ya 'Umrah.

- Utekeleze 'Umrah ndani ya miezi hiyo ya Hajj katika mwaka huo, na lazima umalize kabla ya tarehe 8.
- Ufanye *Twawaaf* ya 'Umrah moja kwa moja, hutakiwi kuanza na *Twawaaful-Quduwm*.
- Ufanye *As-Sa'-y* ambayo ni ya 'Umrah. (*As-Sa'-y* ya Hajj inatekelezwa pamoja na *Twawaaful-Ifaadhwah*).
- Utakata au unyoe nywele (kwa mwanamume), ikiwa una masiku ya kutosha hadi nywele ziote tena kwa ajili ya kunyoa utapomaliza Hajj; na ni vyema kunyoa kuliko kukata, kwani ina thawabu zaidi.
- Baada ya hapo utakuwa umesh'amaliza kutekeleza 'Umrah na umeshatoka katika Ihraam, na hutakuwa na vikwazo vyovyote vya Ihraam.
- Itakapofika tarehe 8 Dhul-Hijjah utaingia katika Ihraam tena kwa niyyah ya Hajj, na kuelekea *Minaa*.
- *Al-Mutamatti'u* lazima achinje. Ikiwa huna uwezo, unatakiwa kufunga siku kumi; tatu unapokuwa Hajj, na saba unaporudi nchini mwako. Hii kwa wanaoishi nchi za nje.

﴿ فَمَن تَمَتَّعَ بِٱلْعُمْرَةِ إِلَى ٱلْحَجِّ فَمَا ٱسْتَيْسَرَ مِنَ ٱلْهَدْيِ ۚ فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَٰثَةِ أَيَّامٍ فِى ٱلْحَجِّ وَسَبْعَةٍ إِذَا رَجَعْتُمْ ۗ تِلْكَ عَشَرَةٌ كَامِلَةٌ ۗ ﴾

**((basi mwenye kutekeleza 'Umrah (katika miezi ya Hajj) kisha Hajj, basi achinje mnyama aliye mwepesi. Na asiyepata (mnyama), afunge *Swiyaam* siku tatu katika Hajj na (siku) saba mtakaporejea. Hizo ni (siku) kumi timilifu))**[47]

---

[47] Al-Baqarah (2:196).

Ama wakaazi wa Makkah hawatakiwi kutekeleza aina hii ya Hajj kwa dalili:

﴿ ذَٰلِكَ لِمَن لَّمْ يَكُنْ أَهْلُهُۥ حَاضِرِى ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ ۚ ﴾

**((Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawaishi karibu na Al-Masjidil-Haraam))**[48]

[48] Al-Baqarah (2:196).

## Chati Ya Hajj Tamattu'

(Inapatikana katika faili la pekee la:

**Chati - Mukhtasari Hatua Za Hajj *Tamattu'***

Chapisha kurasa zake kisha unganishe hapa kwa ajili ya kukamilisha kitabu)

### *Al-Qiraan –* الْقِرَان

Ni aina ya Hajj inayochanganywa na ‘Umrah kwa niyyah moja, bila ya kutoka katika Ihraam. Anayetekeleza huitwa *Al-Qaarin*.

Haji atavaa Ihraam kwa niyyah ya 'Umrah na Hajj au anavaa kwanza Ihraam ya 'Umrah, kisha anatia niyyah ya Hajj kabla ya *Twawaaful-Ifaadhwah*. Vitendo vinavyowajibika kwa anayefanya Ifraad ni sawa sawa na anayefanya Qiraan, isipokuwa tu mwenye kufanya Qiraan inampasa achinje na mwenye kufanya Ifraad haimpasi kuchinja.

Inatekelezwa kwa mpangilio ufatao:

- Unapofika *Miyqaat* ingia katika Ihraam kwa niyyah ya ‘Umrah na ya Hajj.
- Lazima uwe na mnyama wa kuchinja kama walivyokubaliana Wanachuoni kuwa ni sharti ya aina hii ya Hajj. Na ikiwa huna basi itabidi ubadilishe niyyah na utekeleze Hajj ya *Tamattu’*. Kwa hiyo aliyekuwa na mnyama hawezi kubadilisha niyyah bali itabidi atekeleze taratibu za aina hii ya Hajj.
- Unaweza kufanya *As-Sa’-y* ya Hajj pamoja na hiyo *Twawaaful-Quduwm* au unaweza kuicheleweshа *As-Sa’-y* ukafanya baada ya *Twawaaful-Ifaadhwah*. Lakini kuifanya *As-Sa’-y* pamoja na *Twawaaful-Quduwm* ni bora zaidi.
- Lazima ubakie katika Ihraam siku zote tokea unapofika Makkah mpaka umalize taratibu za Hajj.
- Wakaazi wa Makkah hawatakiwi kutekeleza aina hii ya Hajj.

### *Al-Ifraad -* الإفراد

Ni aina ya Hajj inayotekelezwa bila ya ‘Umrah, nayo huwa kwa niyyah moja tu ya Hajj. Anayetekeleza huitwa *Al-Mufrid*.

Haji atavaa Ihraam kwa ajili ya Hajj pekee. Atakapofika Makkah atafanya *Twawaaful-Quduwm* akipenda (kwani ni Sunnah kwake) kisha ataelekea *Minaa*. Hanyoi wala kukata nywele zake kwani hatoki kwenye Ihraam yake, bali atabakia katika Ihraam mpaka ‘amalize kurusha vijiwe katika *Jamrah Al-'Aqabah* siku ya 'Iyd. Anaruhusiwa kucheleweshа *As-Sa’-y* yake ya Hajj mpaka ‘amalize *Twawaaful-Ifaadhwah*.

Unapofika *Miyqaat* ingia katika Ihraam kwa niyyah moja tu ya Hajj.

- Huhitaji mnyama wa kuchinja.
- Ukifika Makkah, ufanye *Twawaaful-Quduwm* ukipenda kwani unaweza kwenda moja kwa moja kutoka *Miyqaat* kuelekea *Minaa* tarehe 8 Dhul-Hijjah.
- Unaweza kufanya *As-Sa'-y* ya Hajj pamoja na hiyo *Twawaaful-Quduwm*? Hivyo utakuwa sawa na *Al-Qaarin* kuhusu kubadilisha niyyah kufanya ya *At-Tamattu'* isipokuwa wakaazi wa Makkah.
- Lazima ubakie katika Ihraam siku zote, tokea unapofika Makkah mpaka utakapomaliza taratibu za Hajj.
- Aina hii ya Hajj inawapasa watekeleze wakaazi wa Makkah au walio karibu na maeneo ya *Miyqaat*.
- Ikiwa muda upo, *Al-Mufrid* anaweza kubadilisha niyyah kutoka *Al-Ifraad* kufanya ya *Al-Qaarin* au ya *At-Tamattu'*.

Aina ya Hajj iliyo bora kabisa katika hizo ni ya *At-Tamattu'* kwa sababu ya usahali wa kutokubakia katika Ihraam masiku mengi. Pia Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alisisitiza wafuasi wake waitekeleze kama alivyosimulia Abu Sa'iyd (رضي الله عنه):

"خَرَجْنَا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ نَصْرُخُ بِالْحَجِّ صُرَاخًا فَلَمَّا قَدِمْنَا مَكَّةَ أَمَرَنَا أَنْ نَجْعَلَهَا عُمْرَةً إِلَّا مَنْ سَاقَ الْهَدْيَ، فَلَمَّا كَانَ يَوْمُ التَّرْوِيَةِ وَرُحْنَا إِلَى مِنًى أَهْلَلْنَا بِالْحَجِّ"

**"**Tulitoka pamoja na Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) wakinyanyua sauti zao (kwa *Talbiyah*) kwa ajili ya Hajj. Tulipofika Makkah alituamrisha tufanye 'Umrah isipokuwa ambaye amechukua *Hadyi* (mnyama wa kuchinja). Ilipofika siku ya *Tarwiyah* tukaenda *Minaa* tukatia niyya ya Hajj.[49]

Hata kama Mahujaji akitia niyyah ya kufanya Qiraan au Ifraad, anaruhusiwa kubadilisha niyyah yake kuingia katika Hajj ya *Tamattu'*. Na anaweza kufanya hivi hata kama baada ya kufanya *Twawaaf* na *As-Sa'-y* kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alipofanya *Twawaaf* na *As-Sa'-y* mwaka wa *Hajjatul-Wadaa'i* (Hajj ya kuaga) pamoja na Maswahaba zake, aliamrisha wote ambao hawakuleta mnyama kwa ajili ya kuchinja, wabadilishe

[49] Muslim.

niyyah zao za Hajj na kutia niyyah ya 'Umrah, wakate nywele zao, na wavue Ihraam mpaka Hajj. Akasema:

((**فَلَوْلاَ أَنّيِسُقْتُ الْهَدْيَ لَفَعَلْتُ مِثْلَ الَّذِيأَمَرْتُكُمْ بِهِ**)) البخاري

***((Ingelikuwa sikuleta mnyama ningelifanya hivyo nilivyokuamrisheni mfanye*))**[50]

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Kwamba mwezi wa Hajj pekee ndio zinaanza *Manaasik* za Hajj na hali miezi ya Hajj inaanzia Shawwaal mpaka siku za Hajj zenyewe.

- Kudhania kwamba Hajj ya *Al-Qiraan* ni bora kuliko ya *At-Tamattu'* kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alitekeleza ya *Al-Qiraan*. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliamrisha na kupendekeza Hajj ya *At-Tamattu'*:

  عن جابر بن عبد الله (رضي الله عنه) أنه حجَّ مع النبي صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يوم ساق البُدن معه، وقد أهلُّوا بالحجِّ مفرداً، فقال لهم: ((**أَحِلُّوا مِنْ إحْرامِكُم بِطَوَافِ بالبَيْتِ، وبَيْنَ الصَّفَا والْمروَة، وقَصِّرُوا، ثُمَّ أقِيمُوا حَلالاً، حَتَّى إذَا كَانَ يَوْمُ التَّرْوِيَةِ، فأهِلُّوا بالحَجِّ واجْعَلُوا التي قَدِمْتُم بها مُتْعَةٌ**)) فقالُوا: كَيْفَ نَجْعَلُها مُتْعَةً وَقَدْ سَمَّيْنَا الحَجَّ؟ فقال: ((**افْعَلُوا مَا آمُرُكُم به، فَلَوْلا أنِي سُقْتُ الهَدْى، لَفَعَلْتُ مِثْلَ الَّذي أَمَرْتُكُم بِهِ**))

  Imepokelewa toka kwa Jaabir bin 'Abdillaah (رضي الله عنه) kwamba alihiji pamoja na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) ambaye alichukua *Al-Hadyi* (mnyama wa kuchinja) na kwamba walitia niyyah ya kufanya Hajj ya *Ifraad*. Akawaambia: ***((Jitoeni Ihraam baada ya kufanya Twawaaf na baada ya As-Sa'-y baina Asw-Swafaa na Al-Mar-wah, kisha mkate nywele zenu. Kisha mbakie Makkah mkiwa mmeshajivua katika Ihraam mpaka siku ya Tarwiyah (8 Dhul-Hijjah) mtatia* niyyah *ya Hajj kisha mtafanya 'ibaadah zenu kuwa ni Tamattu'*))** Wakauliza: "Vipi tufanye *Tamattu'* na hali

---

[50] Al-Bukhaariy.

tumeshaitilia niyyah ya Hajj (*Al-Ifraad*)"? Akasema: ***((Fanyeni nilivyokuamrisheni, kwani ingelikuwa sikuleta Al-Hady, ningelifanya kama nilivyokuamrisheni))***[51]

[51] Al-Bukhaariy.

## 04- Kuwajibika Hajj

Hajj ni nguzo ya tano kwa Waislamu. Maamrisho yake yametajwa katika Qur-aan na Sunnah, Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلْبَيْتِ مَنِ ٱسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۚ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ ٱلْعَـٰلَمِينَ ﴿٩٧﴾

**((Na kwa ajili ya Allaah ni wajibu kwa watu watekeleze Hajj katika Nyumba hiyo kwa mwenye uwezo. Na atakayekanusha, basi hakika Allaah ni *Ghaniyy* (Mkwasi) kwa walimwengu))**[52]

Nguzo zote tano za Kiislaam zimetajwa katika Hadiyth ifuatayo:

عَنْ ابن عُمَرَ (رضي الله عنهما): قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: ((بُنِيَ الْإِسْلَامُ عَلَى خَمْسٍ, شَهَادَةِ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ وَالْحَجِّ وَصَوْمِ رَمَضَانَ))

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) kwamba: Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Uislamu umejengwa kwa [nguzo] tano; Kushuhudia kwamba hapana ilaah* (muabudiwa wa haki) *isipokuwa Allaah, na kwamba Muhammad ni Rasuli wa Allaah, na kusimamisha Swalaah, Kutoa Zakaah, kuhiji na kufunga Swawm Ramadhwaan*** ))[53]

Na katika Hadiyth ndefu maarufu ya Jibrily (عليه السلام) alipomfikia Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kufundisha mambo ya Dini ya Kiislamu…

((أَنْ تَشْهَدَ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَتُقِيمَ الصَّلَاةَ وَتُؤْتِيَ الزَّكَاةَ وَتَصُومَ رَمَضَانَ وَتَحُجَّ الْبَيْتَ إِنْ اسْتَطَعْتَ إِلَيْهِ سَبِيلًا))

***((…Ushuhudie kwamba hapana ilaah* (mwabudiwa Anayestahiki kuabudiwa kwa haki) *isipokuwa Allaah, na kwamba Muhammad ni Rasuli wa Allaah, na usimamishe Swalaah, utoe Zakaah, ufunge Swawm ya Ramadhwaan na uhiji ukiwa na uwezo))***[54]

---

[52] Aal-'Imraan (3: 97).
[53] Al-Bukhaariy na Muslim.
[54] Muslim.

Limekuwa ni jukumu kwetu, bali ni haki ya Allaah (سبحانه وتعالى) tunayopaswa kuitimiza kama Aayah hiyo inavyodhihirisha. Asiyeitimiza haki hii ya Allaah (سبحانه وتعالى) hali ya kuwa na uwezo, atakuwa amekanusha amri hiyo, na atakuwa hakutimiza Uislamu wake. Hapo itakuwa ni khasara kwake kwa vile manufaa ya 'ibaadah zote yanamrudia mtu mwenye kwa sababu Allaah (سبحانه وتعالى) Hanufaiki na chochote katika 'ibaadah zetu bali bin Aadam ndiye mwenye kupata manufaa na ni wenye kumhitaji Allaah (سبحانه وتعالى).

Allaah (سبحانه وتعالى), Hakuiwajibisha nguzo hii kutekelezwa zaidi ya mara moja katika uhai wa mtu. Juu ya hivyo, kuitekeleza kwake iwe kwa mwenye uwezo tu. Hii ni Rahmah ya Allaah (سبحانه وتعالى) kwa waja Wake kutokuwafanyia ugumu katika Dini hii tukufu. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliitekeleza nguzo hii mara moja tu katika uhai wake na aliamrisha hivyo kama ilivyo katika Hadiyth ifuatayo:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ (رضي الله عنه) قال: خطبنا رسول الله (صلى الله عليه وسلم) فقال: **((أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ فَرَضَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ الْحَجَّ فَحُجُّوا))** فَقَالَ رَجُلٌ: أَكُلَّ عَامٍ يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ فَسَكَتَ حَتَّى قَالَهَا ثَلَاثًا فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ): **((لَوْ قُلْتُ نَعَمْ لَوَجَبَتْ وَلَمَا اسْتَطَعْتُمْ ثُمَّ قَالَ: ذَرُونِي مَا تَرَكْتُكُمْ فَإِنَّمَا هَلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ بِكَثْرَةِ سُؤَالِهِمْ ,وَاخْتِلَافِهِمْ عَلَى أَنْبِيَائِهِمْ فَإِذَا أَمَرْتُكُمْ بِشَيْءٍ فَأْتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ وَإِذَا نَهَيْتُكُمْ عَنْ شَيْءٍ فَدَعُوهُ))**

Kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) amesema: "Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alitukhutubia akasema: ***((Enyi watu Allaah Amekufaridhisheni Hajj hivyo mhiji)).*** Mtu mmoja akasema: Kila mwaka ee Mjumbe wa Allaah? Akanyamaza kimya hadi yule mtu aliporudia mara tatu [swali lake] akasema Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم): ***((Ningelisema ndio, ingeliwajibika, na wala msingeliweza)).*** Kisha akasema: ***((Niacheni kwa yale niliyokuachieni kwani watu wa kabla yenu waliangamia kwa maswali yao mengi na ikhitilaaf zao [kujadiliana sana kwao] na Mitume yao. Hivyo nnapokuamrisheni jambo lifanyeni muwezavyo na ninapokukatazeni jambo jiepusheni nalo))***[55]

[55] Muslim.

Hakuna ubaya kwa mwenye uwezo kutekeleza zaidi ya mara moja kwa ajili ya kupata fadhila zaidi kutokana na dalili zifuatazo:

عن ابْنِ عَبَّاسٍ (رضي الله عنهما) أَنَّ الأَقْرَعَ بْنَ حَابِسٍ سَأَلَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ الْحَجُّ فِي كُلِّ سَنَةٍ أَوْ مَرَّةً وَاحِدَةً؟ قَالَ: ((**بَلْ مَرَّةً وَاحِدَةً، فَمَنْ زَادَ فَهُوَ تَطَوُّعٌ**)) رواه أَبُو دَاوُد وصححه الألباني

Kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba Al-Aqra' bin Haabis alimuuliza Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم): "Ee Rasuli wa Allaah, je, Hajj ni kila mwaka au mara moja tu?" Akasema: ***((Ni mara moja lakini mwenye kupenda kuzidisha ni tatwawwu')***) [kujitolea na anapata ujira wake].[56]

عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ (رضي الله عنه) أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((**قَالَ اللَّهُ: إِنَّ عَبْدًا صَحَّحْتُ لَهُ جِسْمَهُ، وَوَسَّعْتُ عَلَيْهِ فِي الْمَعِيشَةِ يَمْضِي عَلَيْهِ خَمْسَةُ أَعْوَامٍ لا يَفِدُ إِلَيَّ لَمَحْرُومٌ**))

Kutoka kwa Abu Sa'iyd Al-Khudriyy (رضي الله عنه) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Allaah Amesema: Hakika Nikimpa siha mja mwilini na nikampa uwezo wa maisha, ikampitia miaka mitano asije Kwangu [Kuhijji] ameharamishwa***)).[57]

Uwezo na masharti ya kuwajibika mtu kutekeleza nguzo hii:

1. Muislamu.
2. Huru (asiye mtumwa).
3. Aliyebaleghe.
4. Mwenye akili timamu.
5. Mwenye uwezo wa mali, asiwe na deni la mtu isipokuwa deni linaloendelea kulipwa.
6. Mwenye uwezo wa kiafya, ikiwa hali inamruhusu kusafiri bila ya kuathiri afya yake au kuhatarisha maisha yake. Mfano wa atakayehatarisha uhai wake ni mgonjwa ambaye mafigo yake hayafanyi kazi na anahitaji kusafishwa kila baada ya siku moja au mbili.
7. Mahram – kwa mwanamke.

[56] Abu Daawuwd ikasahihishwa na Al-Albaaniy.
[57] Ibn Hibban katika Swahiyh yake, Abu Ya'laa, 2/304; Al-Bayhaqiy, 5/262.

8. Kuwe na amani na usalama wa kufika Makkah.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Vijana kutokutekeleza nguzo hii kwa kungojea hadi wafike umri mkubwa. Hili ni kosa kubwa kwani hakuna ajuaye kama ataishi hadi afikie umri mkubwa. Na ametuonya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

(( **مَنْ أَرَادَ الْحَجَّ فَلْيَتَعَجَّلْ** )) رواه الإمام أحمد وأبو داود وابن ماجه. وفي رواية أحمد وابن ماجه: ((**فَإِنَّهُ قَدْ يَمْرَضُ الْمَرِيضُ، وَتَعْرِضُ الْحَاجَةُ**)) حسنه الألباني في صحيح ابن ماجه.

***((Mwenye kutaka kufanya Hajj basi aharakishe***))[58] Na katika riwaaya ya Ahmad na Ibn Maajah – ***((Kwani huenda akapata maradhi au akafikwa na haja))***

Vile vile amesema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

**((تَعَجَّلُوا إِلَى الْحَجِّ (يعني الفريضة) فَإِنَّ أَحَدَكُمْ لاَ يَدْرِي مَا يُعْرَضُ لَهُ)) أخرجه الإمام أحمد رحمه الله وحسَّنه الألباني في إرواء الغليل.**

***((Harakizeni [kutekeleza] Hajj, kwani hajui mmoja wenu nini kitamsibu***))[59]

- Kutokana na Hadiyth zinazodhihirisha kuhiji kila baada ya miaka mitano, baadhi ya watu wanadhania kwamba imewajibika hivyo. Wanachuoni wamekubaliana kwamba dalili hizo hazimaanishi kwamba Hajj imewajibika kila baada ya miaka mitano, bali ni '*Mustahabb*' (inapendekezeka) kwa sababu ni vyema kuwapa fursa Waislamu wengineo wasiokuwa na uwezo wa kuhiji. Muislamu mwenye wasaa ni vyema amlipie gharama nduguye Muislamu kutekeleza nguzo hii kuliko yeye kuikariri. Pia itasaidia kupunguza huko Makkah zahma zinazozidi kila mwaka na kusababisha ugumu wa kutekeleza 'ibaadah/nguzo hii.

---

[58] Ahmad, Abu Daawuwd, Ibn Maajah, akaipa daraja ya 'Hasan' Al-Albaaniy katika *Swahiyh-Ibn Maajah*.
[59] Ahmad, na kaipa daraja ya 'Hasan' Al-Albaaniy katika Irwaaul-Ghaliyl.

## 05- Fadhila Za 'Umrah Na Hajj

Kuna fadhila nyingi zinazopatika kwa kutekeleza 'ibaadah hizi tukufu. Muislamu anayetaka kuzipata fadhila hizo, lazima afuate amri ya Allaah (سبحانه وتعالى) kama Anavyosema:

﴿ ٱلْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَٰتٌ ۚ فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِى ٱلْحَجِّ ۗ وَمَا تَفْعَلُوا۟ مِنْ خَيْرٍ يَعْلَمْهُ ٱللَّهُ ۗ وَتَزَوَّدُوا۟ فَإِنَّ خَيْرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقْوَىٰ ۚ وَٱتَّقُونِ يَٰٓأُو۟لِى ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿١٩٧﴾

**((Hajj ni miezi maalumu. Na atakayekusudia kuhiji (akahirimia), basi asifanye tendo la ndoa wala ufasiki wala mabishano katika Hajj. Na lolote mlifanyalo katika ya kheri Allaah Analijua. Na chukueni masurufu. Na hakika bora ya masurufu ni taqwa. Na nicheni Mimi enyi wenye akili!))**[60]

Kadhaalika, kuna fadhila nyinginezo kadhaa ambazo Muislamu anafaidika nazo zinazohusu Dini na dunia yake: Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ لِّيَشْهَدُوا۟ مَنَٰفِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا۟ ٱسْمَ ٱللَّهِ فِىٓ أَيَّامٍ مَّعْلُومَٰتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنۢ بَهِيمَةِ ٱلْأَنْعَٰمِ ۖ فَكُلُوا۟ مِنْهَا وَأَطْعِمُوا۟ ٱلْبَآئِسَ ٱلْفَقِيرَ ﴿٢٨﴾ ﴾

**((Ili washuhudie manufaa yao; na walitaje Jina la Allaah katika siku maalumu kwa yale Aliyowaruzuku kati ya wanyama wenye miguu minne wa mifugo. Basi kuleni humo, na lisheni mwenye shida fakiri.))**[61]

Aayah hii imetaja baadhi ya manufaa ya kiDini na ya kidunia. Ya ki-Dini ni kujichumia thawabu tele katika kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwenye masiku machache matukufu yaliyojaa fadhila adhimu. Ama manufaa ya kidunia yaliyotajwa humo ni mnyama wa *kaffaarah* ambaye nyama yake inagaiwa kwa masikini. Manufaa mengineyo ni kama yafuatayo:

---

[60] Al-Baqarah (2: 197).
[61] Al-Hajj (22: 28).

**Manufaa Ya ki-Dini**

1. Kupata Radhi za Allaah (سبحانه وتعالى).

Hajj ina taathira kubwa katika moyo wa Muislamu. Humbakisha katika taqwa na iymaan ya hali ya juu. Kwa wengineo iymaan zao huwa nzuri zaidi na mabadiliko haya huwa ni ya kudumu katika uhai wao.

Hajj au 'Umrah humjaza mapenzi Muumini moyoni mwake apende kurudia kutekeleza 'ibaadah hizi tukufu. Hii ni kutokana na du'aa ya Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) baada ya kumaliza kujenga *Al-Ka'bah* alipoomba:

﴿ رَّبَّنَآ إِنِّيٓ أَسۡكَنتُ مِن ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيۡرِ ذِي زَرۡعٍ عِندَ بَيۡتِكَ ٱلۡمُحَرَّمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ فَٱجۡعَلۡ أَفۡـِٔدَةٗ مِّنَ ٱلنَّاسِ تَهۡوِيٓ إِلَيۡهِمۡ وَٱرۡزُقۡهُم مِّنَ ٱلثَّمَرَٰتِ لَعَلَّهُمۡ يَشۡكُرُونَ ٣٧ ﴾

**(("Rabb wetu! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuria wangu katika bonde (la Makkah) lisilokuwa na mmea wowote, kwenye Nyumba Yako Tukufu. Rabb wetu, ili wasimamishe Swalaah na Ujaalie nyoyo za watu zielekee kwao na Uwaruzuku mazao ili wapate kushukuru))**[62]

2. Kujichumia thawabu tele za kuswali katika *Masjid Al-Haraam*.

عَنْ جَابِرٍ (رضي الله عنه) أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((صَلاَةٌ فِي مَسْجِدِي أَفْضَلُ مِنْ أَلْفِ صَلاَةٍ فِيمَا سِوَاهُ إِلَّا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ، وَصَلاَةٌ فِي الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ أَفْضَلُ مِنْ مِائَةِ أَلْفِ صَلاَةٍ فِيمَا سِوَاهُ)) رواه أحمد وابن ماجه

Imepokelewa toka kwa Jaabir (رضي الله عنه) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Swalaah katika Msikiti wangu ni bora kuliko Swalaah elfu kwengineko isipokuwa***

[62] Ibraahiym (14: 37).

***Al-Masjid Al-Haraam. Na Swalaah katika Al-Masjid Al-Haraam ni bora kuliko Swalaah elfu mia (laki moja) kwengineko))***[63]

3. Kufutiwa madhambi yote.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ (رضي الله عنه) قَالَ: "سَمِعْتُ النَّبِيَّ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) يَقُولُ: **((مَنْ حَجَّ لِلَّهِ فَلَمْ يَرْفُثْ وَلَمْ يَفْسُقْ رَجَعَ كَيَوْمِ وَلَدَتْهُ أُمُّهُ))** متفق عليه

Kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kasema: "Nilimsikia Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: ***((Atakayefanya Hajj, kisha asiseme maneno machafu wala asitende vitendo vichafu atarudi akiwa kama siku aliyozaliwa na mama yake))***[64]

4. Jazaa yake Jannah.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ (رضي الله عنه) أَنَّ رَسُولَ اللهِ (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) قَالَ: **((الْعُمْرَةُ إِلَى الْعُمْرَةِ كَفَّارَةٌ لِمَا بَيْنَهُمَا، وَالْحَجُّ الْمَبْرُورُ لَيْسَ لَهُ جَزَاءٌ إِلَّا الْجَنَّةَ))** متفق عليه

Kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***(('Umrah hadi 'Umrah ni kufutiwa dhambi baina yao, na Al-Hajjul-Mabruwr haina jazaa isipokuwa ni Jannah)).***[65]

5. 'Amali bora kabisa:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ (رضي الله عنه) أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) سُئِلَ: أَيُّ الْعَمَلِ أَفْضَلُ؟ فَقَالَ: **((إِيمَانٌ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ))** قِيلَ: ثُمَّ مَاذَا؟ قَالَ: **((الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ))** قِيلَ: ثُمَّ مَاذَا؟ قَالَ : **((حَجٌّ مَبْرُورٌ))** متفق عليه

---

[63] Ahmad, Ibn Maajah.
[64] Al-Bukhaariy na Muslim.
[65] Al-Bukhaariy.

Kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kwamba aliulizwa Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم): "Ni ipi 'amali iliyo bora zaidi?" Akasema: ***((Kumuamini Allaah na Rasuli Wake))*** Akaulizwa: "Kisha ipi"? Akasema: ***((Jihaad katika Njia ya Allaah))*** Akaulizwa: "Kisha ipi"? Aakasema: ***((Hajjum-Mabruwr)).***[66]

6. Jihaad bora kabisa kwa wanawake.

عَنْ عَائِشَةَ أُمِّ الْمُؤْمِنِينَ (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا) قَالَتْ قُلْنَا: يَا رَسُولَ اللَّهِ، نَرَى الْجِهَادَ أَفْضَلَ الْعَمَلِ, أَفَلا نُجَاهِدُ مَعَكَ؟ قَالَ: **((لا وَلَكِنَّ أَفْضَلَ الْجِهَادِ حَجٌّ مَبْرُورٌ))**

Kutoka kwa Mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها) amesema: "Tulisema: Ee Rasuli wa Allaah, (kwa vile) tunaona jihaad kuwa ni 'amali bora kabisa. Je tusifanye jihaad pamoja na wewe?" Akajibu: ***((Hapana! Jihaad bora kabisa ni Hajjum-Mabruwr))***[67]

7. Inaondosha ufakiri na madhambi.

عَنْ ابْنُ عَبَّاسٍ (رضي الله عنهما) قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: **((تَابِعُوا بَيْنَ الْحَجِّ وَالْعُمْرَةِ، فَإِنَّهُمَا يَنْفِيَانِ الْفَقْرَ وَالذُّنُوبَ، كَمَا يَنْفِي الْكِيرُ خَبَثَ الْحَدِيدِ والذهب والفضة وليس للحج المبرور ثواب دون الجنة))** رواه أحمد والترمذي وصححه، والنسائي وابن خزيمة في صحيحه صححه الشيخ الألباني رحمه الله في السلسلة الصحيحة

Kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) amesema: Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Fuatilieni Hajj na 'Umrah kwani hizo [mbili] zinaondosha ufakiri na madhambi kama kinavyoondosha chombo cha kupulizia moto uchafu wa***

[66] Al-Bukhaariy na Muslim.
[67] Al-Bukhaariy.

***chuma na dhahabu na fedha, na Al-Hajjul-Mabruwr thawabu yake hakuna zaidi ya Jannah)).***[68]

8. Kuwa ni mgeni wa Allaah (سبحانه وتعالى) na kutakabaliwa du'aa.

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

**((الْغَازِي فِي سَبِيلِ اللَّهِ، وَالْحَاجُّ، وَالْمُعْتَمِرُ، وَفْدُ اللَّهِ، دَعَاهُمْ فَأَجَابُوهُ، وَسَأَلُوهُ فَأَعْطَاهُمْ))** رواه ابن ماجه-واللفظ له-، وابن حبّان في "صحيحه"

***((Anayepigana jihaad katika njia ya Allaah, na anayefanya Hajj na 'Umrah ni wageni wa Allaah, Amewaita wakamuitikia, wakamuomba Akawatakabalia))***[69]

9. Kuhudhuria darsa katika Misikiti mitukufu kabisa na kukutana na Wanachuoni.

**Manufaa Ya Kidunia**

1- Kukutana na kujuana na Waislamu wengineo kutoka pande mbali mbali za dunia, kutambua hali zao, kuunganisha mawasiliano na kushirikiana nao kwa kheri.

2- Kujua Historia ya Uislamu na baadhi ya matukio katika Siyrah ya Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم).

3- Kuliwazika na matembezi mbali mbali ya miji na yanayohusiana na safari kwa ujumla; mandhari za miji, kubadilisha hewa na chakula, kujinunulia mahitaji na zawadi.

4- Kufanya tijara kwani imeruhusiwa na Allaah (سبحانه وتعالى) Anaposema:

[68] Ahmad, At-Tirmidhiy na ameisahihisha, na An-Nasaaiy na ibn Khuzaymah katika Swahiyh yake na ameisahihisha Al-Albaaniy katika *Silsilat Asw-Swahiyhah*.
[69] Ibn Maajah, Ibn Hibban katika Swahiyh zao.

﴿ لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَن تَبْتَغُوا فَضْلاً مِّن رَّبِّكُمْ ﴾

**((Hapana dhambi kwenu kutafuta fadhila toka kwa Rabb wenu))**[70]

[70] Al-Baqarah (2: 198).

## 06- Hajj Ya Rasuli Wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم)

Usimulizi kutoka katika Swahiyh Muslim unaelezea jinsi Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alivyotekeleza Hajj.

Anasema Imaam Muslim:
"Nimehadithiwa na Abu Bakr bin Abi Shaybah na Is-haaq bin Ibraahiym, wote pamoja. Na kutoka kwa Haatim amesema kuwa Abu Bakr amesema: 'Nimehadithiwa na Haatim bin Ismaa'iyl Al-Madaniy, kutoka kwa Ja'far bin Muhammad, kutoka kwa baba yake (رضي الله عنه) kuwa alisema: "Tulimwendea Jaabir bin 'Abdillaah (رضي الله عنه) akaanza kutuuliza majina yetu mmoja mmoja mpaka akaishia kwangu. Nikamwambia: 'Mimi ni Muhammad bin 'Aliy bin Al-Husayn". Akakivamia kichwa changu, kisha akanifungua kifungo changu cha juu kisha cha chini yake, kisha akauweka mkono wake kifuani pangu, na wakati huo nilikuwa bado kijana. Akaniambia;

"Marhaban (karibu) ee mwana wa ndugu yangu. Uliza unalotaka kuuliza".

Nikamuuliza, na wakati ule alikuwa kipofu, na wakati wa Swalaah ulipowadia aliinuka huku akiikusanya kusanya nguo yake, kila akijifunika nayo upande mmoja wa bega lake, upande wa pili inaanguka kwa sababu ya udogo wake. Akatuswalisha, kisha nikamwambia:
"Tuhadithie juu ya Hajj ya Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم)."

Jaabir (رضي الله عنه) akasema: "Watu walipoarifiwa kuwa Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) atahiji mwaka huu, walianza kumiminika mjini Madiynah kwa wingi sana, kila mmoja akitamani aongozwe na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) na afanye kama atakavyofanya.

(Ilipowadia siku ya safari) Tukaondoka naye mpaka tulipowasili *Dhul-Hulayfah* (*Miyqaat* ya watu wa Madiynah), Asmaa bint Umays akamzaa Muhammad bin Abi Bakr Asw-Swiddiyq (رضي الله عنه) akamtuma mtu kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kumuuliza nini afanye.

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akamwambia: ***((Oga, kisha weka kitambaa na utie niyyah ya Ihraam))***

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akaswali Msikitini kisha akampanda ngamia wake anayejulikana kwa jina la Al-Qaswaa, na alipokuwa katikati ya jangwa nikainua kichwa changu kutazama waliokuwa mbele ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم), nikaona watu wengi sana, upeo wa macho yangu wakiwemo waliopanda wanyama na wanaokwenda kwa miguu, kisha nikatazama kuliani kwake, nikaona hivyo hivyo, kisha upande wake wa kushoto nikaona hivyo hivyo, na nyuma yake hivyo hivyo, na Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akiwa pamoja nasi huku wahyi ukimteremkia, huku akituhadithia, na kila anachokifanya, sisi tulikuwa tukimfuata. Kisha akaanza kusema: ***((Labbayka Allaahumma Labbayka, Labbayka laa shariyka laka Labbayka. Innal-Hamda wan-ni'mata Laka wal mulk, laa shariyka laka))***

Na watu wakawa wanasema kama anavyosema".

Jaabir bin 'Abdillaah (رضي الله عنه) akaendelea kusema:

"Hatukuwa tukitia niyyah nyingine isipokuwa niyyah ya Hajj, (hatukuwa tukijua aina nyingine za Hajj), hatukuwa tukijua juu ya 'Umrah. Tukaendelea na Safari mpaka tulipoifikia *Al-Ka'bah* tukiwa pamoja naye, akaligusa *Al-Hajarul-As-wad* kisha akaanza kutufu. Katika mizunguko mitatu ya mwanzo alikuwa akienda kwa kukazana, na katika minne iliyobaki akienda mwendo wa kawaida. Alipomaliza akaenda penye *Maqaam Ibraahiym* (عليه السلام), akasoma:

﴿ وَٱتَّخِذُواْ مِن مَّقَامِ إِبْرَٰهِـۧمَ مُصَلًّىۖ ﴾

**((Na chukueni mahali pa kusimama Ibraahiym kuwa ni pahala pa kuswalia))**[71]

Akaelekea Qiblah na kuswali rakaa mbili mahali hapo, akasoma katika rakaa ya mwanzo (Alhamdu pamoja na) *Qul Yaa Ayyuhal-Kaafiruwn* na katika rakaa ya pili akasoma (Alhamdu pamoja na) *Qul Huwa Allaahu Ahad*, kisha akarudi penye jiwe jeusi, akaligusa kisha akatokea mlangoni kuelekea *Asw-Swafaa*.

[71] Suwratul-Baqarah (2: 125).

Alipokaribia *Asw-Swafaa* akasoma:

﴿ إِنَّ ٱلصَّفَا وَٱلْمَرْوَةَ مِن شَعَآئِرِ ٱللَّهِ ۖ ﴾

**((Hakika *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah* ni katika alama za (Dini ya) Allaah))**[72]

أَبْدَأ بِمَا بَدَأَ الله بِه

***Abdau bimaa bada-a Allaahu bihi ((Naanzia pale Alipoanzia Allaah))***

Akaanzia *Asw-Swafaa*, akapanda jabali hilo mpaka alipoweza kuiona *Al-Ka'bah* akaelekea Qiblah akasema:

لاَ إِلَهَ إِلاَّ الله – الله أَكْبَرَ

***"Laa ilaaha illa Allaahu - Allaahu Akbar"***

Kisha akasema:

لا إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الحَمْدُ وهُوَ عَلى كُلِّ شَيءٍ قَديرٌ، لا إِلَهَ إلا اللهُ وَحْدَهُ أَنْجَزَ وَعْدَهُ، وَنَصَرَ عَبْدَهُ وَهَزَمَ الأَحْزَابَ وَحْدَهُ

***Laa Ilaaha Illa-Allaahu, Wahdahu Laa shariyka Lahu, Lahul Mulku wa Lahul Hamdu, wa Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr. Laa Ilaaha Illa-Allaahu, Wahdahu, Anjaza wa'dahu, wa Naswara 'Abdahu, wa Hazamal ahzaaba Wahdah".***

"Hapana ilaah (muabudiwa wa haki) isipokuwa Allaah, hali ya kuwa Peke Yake, wala Hana mshirika, ni Wake Ufalme na kuhimidiwa ni Kwake, Naye juu ya kila kitu ni Muweza. Hapana ilaah isipokuwa Allaah, hali ya kuwa Peke Yake, Ametekeleza ahadi Yake, na Amemnusuru mja Wake, na Amevishinda vikosi peke Yake."

Kisha akaomba du'aa, kisha akarudia kusema hivyo mara tatu, kisha akashuka kuelekea *Al-Mar-wah*, alipofika katikati ya bonde akawa anakwenda mwendo wa kukazana, na alipolifikia jabali la *Al-Mar-wah* akalipanda kwa mwendo wa kawaida, na alipolifika

[72] Al-Baqarah (2: 158).

juu yake akasoma na kufanya kama alivyofanya alipokuwa juu ya *Asw-Swafaa*.

Akaendelea hivyo mpaka *Twawaaf* yake ilipomalizikia *Al-Marwah* akasema:

***((Lau kama amri niliyopewa [hivi sasa] ningelipewa kabla, nisingechukuwa pamoja nami mnyama na ningeijaalia (Twawaaf yangu na As-Sa'-y yangu) kuwa 'Umrah, na kama yupo kati yenu asiyekuwa na mnyama basi avue nguo za Ihraam na aijaalie iwe 'Umrah)).***

Akainuka Suraaqah bin Maalik bin Ja'athum (رضي الله عنه) akasema: "Ee Rasuli wa Allaah, (hukmu hii) ni kwa ajili ya mwaka huu tu au milele?" Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akaviingiza vidole vyake vya mkono wa kulia ndani ya vidole vya mkono wa kushoto na kusema: ***(('Umrah na Hajj zishaingiliana)).*** Akasema hivyo mara mbili, kisha akasema; ***((Laa, bali milele)).***

'Aliy (رضي الله عنه) akawasili kutoka nchi ya Yemen akiwa na ngamia wa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم), akamkuta Faatwimah (رضي الله عنها) amekwisha vua nguo za Ihraam na kuvaa nguo za kawaida za rangi rangi na ametia wanja. Akamkataza, kwa ajili hiyo, lakini Faatwimah (رضي الله عنها) akamwambia: "Baba yangu ameniamrisha kufanya hivi".

Akaenda kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kumshtakia kuhusu Faatwimah kwa vile alivyofanya (kuvua nguo za Ihraam na kupaka wanja) na kwa kule kusema kwake kuwa Baba yake ndiye aliyemuambia, akamjulisha kuwa yeye alimkataza kwa kufanya kwake vile.

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akamjibu: ((***Ni kweli. [na wewe umetia niyyah gani ya kuhiji ulipokuwa unakuja?))*** Akasema: "Nilisema; 'Allaahumma mimi natia niyyah ile ile aliotia Nabiy wako". Akamwambia: ***((Basi mimi ninaye mnyama, kwa hivyo tusivuwe [nguo za Ihraam])).***

Idadi ya wanyama aliokuja nao 'Aliy (رضي الله عنه) kutoka Yemen ikichanganywa na idadi ya wanyama aliokuja nao Rasuli ( صلى الله عليه وآله وسلم ) ikafikia ngamia mia moja.

Watu wote wakavua Ihraam zao na kukata nywele isipokuwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) na wachache waliokuja na wanyama wao.

Ilipofika siku ya *Tarwiyah* - siku ya tarehe 8 Dhul-Hijjah, watu wakaondoka kuelekea *Minaa* wakitia niyyah ya Hajj, na Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akampanda mnyama wake na kuelekea huko pamoja nao. (Walipowasili *Minaa*), wakaswali Adhuhuri, Alasiri, Magharibi, 'Ishaa na Alfajiri kwa kupunguza (*Qaswran*, kila Swalah katika wakati wake).

(Baada ya kuswali Alfajiri) Akasubiri kidogo mpaka jua lilipochomoza akaamrisha lisimamishwe hema mahali paitwapo *Namirah*, - karibu na *'Arafah*. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akaondoka kuelekea *Namirah* na akapitiliza *Muzdalifah* bila ya kusimama kwenye *Mash'ar Al-Haraam*, juu ya kuwa Ma-Quraysh walidhania atasimama hapo kama walivyokuwa wakifanya wakati wa Ujahiliyyah.

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) hakusimama mpaka alipowasili *'Arafah*, akaliona hema lishasimamishwa pale Namirah kama alivyoamrisha, akashuka na kupumzika hapo mpaka ulipoingia wakati wa Adhuhuri, akaamrisha aletwe ngamia wake Al-Qaswaa, akampanda na kwenda moja kwa moja mpaka alipofika katikati ya bonde la *'Arafah* akasimama na kuwahutubia watu akasema:

**((إِنَّ دِمَاءَكُمْ وَأَمْوَالَكُمْ حَرَامٌ عَلَيْكُمْ كَحُرْمَةِ يَوْمِكُمْ هَذَا فِي شَهْرِكُمْ هَذَا فِي بَلَدِكُمْ هَذَا, أَلَا كُلُّ شَيْءٍ مِنْ أَمْرِ الْجَاهِلِيَّةِ تَحْتَ قَدَمَيَّ مَوْضُوعٌ، وَدِمَاءُ الْجَاهِلِيَّةِ مَوْضُوعَةٌ، وَإِنَّ أَوَّلَ دَمٍ أَضَعُ مِنْ دِمَائِنَا دَمُ ابْنِ رَبِيعَةَ بْنِ الْحَارِثِ كَانَ مُسْتَرْضِعًا فِي بَنِي سَعْدٍ فَقَتَلَتْهُ هُذَيْلٌ. وَرِبَا الْجَاهِلِيَّةِ مَوْضُوعٌ، وَأَوَّلُ رِبًا أَضَعُ رِبَانَا رِبَا عَبَّاسِ بْنِ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ، فَإِنَّهُ مَوْضُوعٌ كُلُّهُ. فَاتَّقُوا اللَّهَ فِي النِّسَاءِ, فَإِنَّكُمْ أَخَذْتُمُوهُنَّ بِأَمَانِ اللَّهِ, وَاسْتَحْلَلْتُمْ فُرُوجَهُنَّ بِكَلِمَةِ اللَّهِ, وَلَكُمْ عَلَيْهِنَّ أَنْ لَا يُوطِئْنَ فُرُشَكُمْ أَحَدًا تَكْرَهُونَهُ, فَإِنْ فَعَلْنَ ذَلِكَ فَاضْرِبُوهُنَّ ضَرْبًا غَيْرَ**

مُبَرِّحٍ, وَلَهُنَّ عَلَيْكُمْ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ، وَقَدْ تَرَكْتُ فِيكُمْ مَا لَنْ تَضِلُّوا بَعْدَهُ إِنْ اعْتَصَمْتُمْ بِهِ: كِتَابُ اللَّهِ، وَأَنْتُمْ تُسْأَلُونَ عَنِّي, فَمَا أَنْتُمْ قَائِلُونَ؟) قَالُوا: نَشْهَدُ أَنَّكَ قَدْ بَلَّغْتَ وَأَدَّيْتَ وَنَصَحْتَ، فَقَالَ بِإِصْبَعِهِ السَّبَّابَةِ يَرْفَعُهَا إِلَى السَّمَاءِ وَيَنْكُتُهَا إِلَى النَّاسِ: اللَّهُمَّ اشْهَدْ)) ثَلَاثَ مَرَّاتٍ

***((Hakika ya damu zenu na mali zenu [ni tukufu sana kwa hivyo] ni haraam baina yenu [kumwaga damu zenu na kudhulumiana baina yenu] kama ulivyokuwa utukufu wa siku yenu hii, katika mwezi wenu huu, katika mji wenu huu, visasi vyenu vyote vya wakati wa ujahiliyyah viko chini ya mguu wangu - nishavibatilisha - na kisasi cha mwanzo cha kumwaga damu yetu ninachokibatilisha ni kisasi cha [kumwaga] damu ya Ibn Rabi'ah bin Al-Haarith. Na Ribaa iliyokuwa ikichukuliwa wakati wa Ujahiliyyah ishabatilika, na Ribaa ya mwanzo ninayoibatilisha ni Ribaa yetu, Ribaa ya 'Abbaas bin 'Abdil-Mutwtwalib, ishabatilika yote, na Mcheni Allaah katika wake zenu, kwani nyinyi mumewachukuwa kwa dhamana ya Allaah, na mkahalalishiwa tupu zao kwa neno la Allaah, na nyinyi mna haki zenu juu yao. Wasiwaingize nyumbani kwenu yeyote msiyempenda [awe mwanamume au mwanamke], na wakifanya hivyo, mnayo haki ya kuwapiga kipigo kisichoumiza. Na haki yao juu yenu ni kuwalisha na kuwavisha kwa wema. Na nimekuwachieni ambayo hamtopotea baada yake ikiwa mtashikamana nayo, Kitabu cha Allaah. Mkiulizwa juu yangu mtasema nini?)) Wakasema:*** "Tutashuhudia kuwa umefikisha na umekamilisha na umenasihi." Akanyanyua kidole cha shahada akawa mara anakielekeza mbinguni mara anakielekeza kwa watu, akasema***: ((Mola wangu shuhudia***)) – [mara tatu].

Kisha akaadhini, akakimu na kuswali Swalaah ya Adhuhuri, kisha akakimu tena na kuswali Swalaah ya Alasiri bila kuswali Sunnah baina yao. Kisha akampanda ngamia wake na kuelekea naye moja kwa moja mpaka mahali pa kusimama [katika uwanja wa '*Arafah*], akamuelekeza ngamia wake Al-Qaswaa penye majabali na yeye akaelekea Qiblah.

Akasimama mahali hapo mpaka wakati wa Magharibi ulipoingia na umanjano wa jua kutoweka na jua kuzama kabisa, ndipo alipoondoka akiwa amempakia Usaamah nyuma yake.

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akampanda ngamia wake Al-Qaswaa na kuianza safari ya kwenda *Muzdalifah*. Akawa anazikaza kamba za hatamu za ngamia wake na kumbana nazo ili asiweze kwenda mbio kwa ajili ya zahma ya watu. Akawa anaashiria watu kwa mkono wake wa kulia huku akiwaambia: ***((Enyi watu! [Nendeni kwa] utulivu [nendeni kwa] utulivu)).***

Na kila anapolifikia jabali akawa anailegeza kamba ili mnyama wake aweze kupanda kwa wepesi. Akawa anafanya hivyo mpaka alipowasili *Muzdalifah*, akaswali hapo Swalaah ya Magharibi na 'Ishaa kwa Adhana moja na Iqaamah mbili, bila ya kusabbih baina ya Swalaah hizo.

Kisha Rasuli wa Allaah akapumzika mahala hapo mpaka Alfajiri ilipoingia, akaswali Alfajiri pale ilipombainikia kuwa wakati wa Swalaah ya Alfajiri ushaingia, kwa Adhana na Iqaamah.

Kisha akampanda Al-Qaswaa mpaka alipowasili *Masha'ar Al-Haraam* akaelekea Qiblah na kuomba du'aa huku akikabbir na kumtukuza na kumpwekesha Allaah. Akawa katika hali hiyo mpaka kulipopambazuka.

Kisha akaondoka na kuianza safari ya kuelekea *Minaa* kabla ya jua kupanda akiwa amempakia Al-Fadhwl bin 'Abbaas aliyekuwa kijana mwenye nywele nzuri, mweupe, na mwenye sura nzuri. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alipokuwa akiondoka naye, akapita mbele yao ngamia aliyebeba wanawake wawili, na Al-Fadhwl akawa anawaangalia wanawake hao. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akauweka mkono wake usoni pa Al-Fadhwl ili asiweze kuwatazama, lakini Al-Fadhwl aliugeuza uso wake upande wa pili na kuendelea kuwatazama, na Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akaukamata uso wa Al-Fadhwl na kuugeuza upande mwingine. Akaendelea na safari yake mpaka alipolifikia bonde la Muhsir akaongeza mwendo kidogo, kisha akapita njia ya kati inayopeleka moja kwa moja mpaka penye *Jamrat Al-Kubraa* na alipolifikia Jamarah (hilo) lililokuwa karibu na mti akalirushia vijiwe saba huku akikabbir kila anaporusha kijiwe.

Kisha akaondoka kuelekea mahali pa kuchinja, akachinja (ngamia) sitini na tatu kwa mkono wake, kisha akampa 'Aliy achinje waliobaki, kisha akaamrisha nyama ikatwe katwe, ikatiwa

ndani ya vyungu vya kupikia, ikapikwa, wakala katika nyama ile na kunywa supu yake.

Kisha Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akampanda ngamia wake na kuelekea penye *Al-Ka'bah*, akaswali Adhuhuri alipowasili Makkah.

Baada ya kuswali akawaendea watu wa kabila la Bani 'Abdil-Mutwtwalib waliokuwa na jukumu la kuwahudumia watu katika kunywa maji ya Zamzam, akawaambia: ***((Wanyweshеni maji enyi watu wa kabila la Bani 'Abdil-Mutwtwalib, ingekuwa sikuogopeeni watu kukuchukulieni kazi hii ya kunywesha maji, basi ningelikusaidieni)).***

Wakampa maji (ya Zamzam), akanywa.

## 07- Matayarisho Kabla Ya Hajj

Safari ya Hajj inahitaji matayarisho kama vile inavyohitajika katika safari zozote nyinginezo. Ila safari hii inahitaji zaidi ikhlaasw, taqwa na subira ya hali ya juu. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ ٱلْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَـٰتٌ ۚ فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِى ٱلْحَجِّ ۗ وَمَا تَفْعَلُوا۟ مِنْ خَيْرٍ يَعْلَمْهُ ٱللَّهُ ۗ وَتَزَوَّدُوا۟ فَإِنَّ خَيْرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقْوَىٰ ۚ وَٱتَّقُونِ يَـٰٓأُو۟لِى ٱلْأَلْبَـٰبِ ﴿١٩٧﴾

**((Hajj ni miezi maalumu. Na atakayekusudia kuhiji (akahirimia), basi asifanye tendo la ndoa wala ufasiki wala mabishano katika Hajj. Na lolote mlifanyalo katika ya kheri Allaah Analijua. Na chukueni masurufu. Na hakika bora ya masurufu ni taqwa. Na nicheni Mimi enyi wenye akili!))**[73]

Kwa hiyo jiandae vizuri kwa yafuatayo ili safari yako na 'ibaadah zako zote ziwe sahali na kamilifu In Shaa Allaah.

### *1*-Niyyah

Kwanza kabisa weka niyyah moyoni mapema kabla ya lolote kwa ajili ya kutekeleza 'ibaadah hii kwamba unaitekeleza kutimiza maamrisho ya Allaah (سبحانه وتعالى) na Rasuli Wake (صلى الله عليه وآله وسلم) na isiwe niyyah yako kwa lengo la manufaa ya kidunia au kujionyesha kwa watu. Muombe Allaah (سبحانه وتعالى) Ajaalie iwe yenye kumridhisha Yeye Pekee ili Akulipe malipo mema kama Alivyotuahidi.

### 2-Du'aa

Baada ya niyyah, omba du'aa kwa wingi Allaah (سبحانه وتعالى) Akuruzuku *Tawfiyq* ya kuifanikisha safari hiyo na uweze kukamilisha fardhi hii kwa sahali na ukamilifu na Akutakabalie juu

[73] Al-Baqarah (2: 197).

ya kuweko mapungufu katika 'ibaadah zako. Pia muombe Allaah (سبحانه وتعالى) Akurudishe nyumbani kwa salama na amani.

**3-Matayarisho Ya Usafiri**

Kawaida mahitajio yote ya safari na huduma safarini zinaandaliwa na shirika linalopeleka Mahujaji. Kila nchi ina kanuni zake za utoaji viza. Unahitajika kuwa na pasipoti isiyokuwa inamalizika muda wake chini ya miezi sita. Maandalizi yote; viza, tiketi, makazi ya huko, usafiri, matembezi n.k. yanashughulikiwa na shirika unalojiunga nalo. Ulizia mashirika kadhaa upate kujua huduma zao na gharama zake kisha ulinganishe na uchague iliyokuwa munaasib kwako. La **muhimu kabisa** ni kuchagua shirika linalotoa mafunzo kutokana na Qur-aan na Sunnah na Manhaj ya *Salafus-Swaalih* ili uweze kutekeleza Hajj yako kama alivyoamrisha Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ***((Chukueni manaasik zenu (za Hajj) kutoka kwangu)).***

Utakapokwisha jiunga na shirika la kuhudumia Mahujaji, utaanza kujiandaa kwa yafuatayo:

**4-Deni**

Lipa madeni yako yote. Unaweza kutekeleza Hajj ikiwa unalo deni ambalo litawezekana kulipwa wakati haupo, mfano kulipwa kwako mshahara unaopokea kila mwezi. Andika *wasiyyah* kwa watu wako kuhusu deni lolote ambalo unaliacha nyuma yako na ambalo litaweza kulipwa kutokana na mali utakayoiacha pindi ukiaga dunia safarini. Ikiwa ni deni ambalo huna uwezo nalo kulilipia nyuma yako, basi haikupasi kutekeleza Hajj kwanza mpaka ulipe deni la watu. Kutokulipa deni ni jambo la hatari linaloweza kumzuia mtu kuingia katika Jannah. Kwa hiyo hakikisha umelipa madeni yote au umeandaa lilipwe.

***5-Waswiyyah***

Andika *wasiyyah* wako kama inavyokubalika kishariy'ah. Muislamu inampasa aandike *wasiyyah* wake na kurekebisha lolote kila baada ya siku tatu. Basi anayekwenda Hajj anawajibika zaidi kuandika *wasiyyah* kwani huenda ikawa ndio majaaliwa yake ya kuaga dunia huko.

**6-Kuaga Watu Na Kuomba Msamaha[74]**

Adabu za Kiislamu katika mas-ala ya safari zinafundisha kuagana na kuombeana du'aa zilizothibiti katika Sunnah. Pia ni vizuri kuomba msamaha kwa ndugu akiwa wa damu au udugu wa Kiislamu ambaye umekhasimikiana naye. Mwanachuoni Ibn Baaz (رحمه الله) amesema katika Fataawa za Hajj Mlango wa: ***'Adaab As-Safar lil-Hajj*** (baada ya kutaja kukimbilia kuomba tawbah ya kweli kutokana na kila dhambi) **"…**juu ya hivyo ikiwa madhambi hayo yanahusiana na kuwatendea ubaya watu; kuua, kuiba, kumtukana mtu, basi watu hao (waliomkosea ndugu yao) warudishe walichochukua kwa dhulma au waombe msamaha kwa ambao wamewakosa kabla ya kusafiri". Pia Hadiyth zifuatazo zimekemea vikali kuhusu kukhasimikiana kwamba amali za Muislamu hazipokelewi pindi kukiweko na uhasama kati yake na nduguye Muislamu.

Hadiyth ya Abu Huraryah (رضي الله عنه) kwamba Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

((تُعْرَضُ الْأَعْمَالُ فِي كُلِّ يَوْمِ خَمِيسٍ وَاثْنَيْنِ فَيَغْفِرُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ فِي ذَلِكَ الْيَوْمِ لِكُلِّ امْرِئٍ لَا يُشْرِكُ بِاللَّهِ شَيْئًا إِلَّا امْرَأً كَانَتْ بَيْنَهُ وَبَيْنَ أَخِيهِ شَحْنَاءُ فَيُقَالُ ارْكُوا هَذَيْنِ حَتَّى يَصْطَلِحَا ارْكُوا هَذَيْنِ حَتَّى يَصْطَلِحَا))

***(('amali njema hutandazwa kila Alkhamiys na Jumatatu, kisha Allaah Aliyetukuka Humghufuria kila mtu asiyemshirikisha na kitu Allaah, isipokuwa mtu aliyekuwa baina yake na baina ya ndugu yake uhasama, Husema: Waacheni hawa wawili mpaka wapatane; Waacheni hawa wawili mpaka wapatane))***[75]

Juu ya hivyo, safari ya Hajj ni safari ya kutegemea mtu kufutiwa madhambi yote, kwa hiyo inapasa kwanza ujisafishe na dhambi khasa zinazohusiana na dhulma za watu. Pia hakuna uhakika wa kurudi nyumbani kwani huenda kifo kikakukuta huko safarini. Kwa hiyo imuingie khofu kila mmoja wetu kwamba pindi mtu akiaga dunia hali ya kuwa amekhasimiana na mwenziwe hatoingia katika Jannah kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

---

[74] Rejea Hiswnul-Muslim na Hiswnul-Mu-umin kupata du'aa za kuaga watu.
[75] Muslim.

**((لا يَحِلُّ لِمُسْلِمٍ أَنْ يَهْجُرَ أَخَاهُ فَوْقَ ثَلاثِ لَيَالٍ، يَلْتَقِيَانِ فَيُعْرِضُ هَذَا وَيُعْرِضُ هَذَا، وَخَيْرُهُمَا الَّذِي يَبْدَأُ بِالسَّلامِ))** رواه البخاري ومسلم وَ في رواية أبو داود بإسناد على شرط البخاري ومسلم: **((فَمَنْ هَجَرَ فَوْقَ ثَلاَثٍ فَمَاتَ دَخَلَ النَّارَ))**

***((Haimpasi Muislamu amhame ndugu yake zaidi ya siku tatu hata wanapokutana huyu anamgeuzia (uso) huyu na huyu anamgeuzia (uso) huyu. Na aliye mbora wao ni yule anayeanza kutoa salaam)***[76]

***((Atakayemhama (mwenzake) zaidi ya siku tatu akafariki basi ataingia Motoni))***[77]

**7-Pesa za matumizi**

Kawaida muongozo hutolewa na shirika utakalojiunga nalo, lakini huenda haya yakakusaidia:

- Badilisha pesa kiasi za kuanzia matumizi huko, nyinginezo badilisha katika hundi ya wasafiri ('traveller's cheque') au tumia kadi za benki maarufu ambazo utaweza kutoa kila unapohitaji huko. Shirika unalokwenda nalo watakuarifu masiku mangapi jumla ya safari, hivyo utaweza kujipangia kiasi cha pesa za kuchukua kutokana na haja na uwezo wako. Utahitaji nakala ya pasipoti kwa ajili ya benki kukubadilishia pesa zako kwa hiyo andaa kuchukua nakala kadhaa za vitambulisho vyako.

- Fanya nakala ziada za kila kitu; pasipoti, vitambulisho, hundi ya wasafiri n.k.

- Vizuri ukiwa na uwezo kuchukua pesa ziada kwa ajili ya kutolea swadaqah huko kwani malipo yake ni maradufu.

- Andika namba za cheki zote katika kijitabu kidogo na thamani zake. Pia fanya nakala ya kila moja uweke akiba pindi za asili zikipotea

---

[76] Al-Bukhaariy na Muslim.
[77] Abu Daawuwd kwa isnaad yenye sharti ya Bukhaariy na Muslim.

- Weka pesa zako katika kipochi kilicho madhubuti na usitembee na pesa zako zote nje ya hoteli kwani inasikitisha kutanabahisha kwamba kuna wezi ambao hata wakati wa kutufu *Al-Ka'bah* wanaibia watu! Unapoweka pesa zako katika begi lako, usiweke katika sehemu husika, bali weka sehemu asiyotegemea mwizi; mfano katika mfuko wa nguo zako begini, au kipaketi cha dawa meno n.k.

- Unapoweka pesa zako hotelini katika begi lako, hakikisha umelifunga vizuri na ufunguo unauhifadhi vizuri mwenyewe katika mkanda utakaouvaa kiunoni (wanaume). Ama wanawake, shonea nguo yako ya ndani kifuko cha zipu uweze kuhifadhi humo funguo zako.

**8-Jifunze Fiqh Ya Hajj**

Jifunze Fiqh ya Hajj ili uweze kujiandaa vizuri utekelezaji wa 'ibaadah hii tukufu ambayo inahitaji ufanisi wa 'amali ili usipoteze muda na mali yako bure kwa kuiharibu pindi ukiitekeleza ndivyo sivyo. La kuzingatia zaidi ni kujiepusha na kila jambo lisilothibiti katika mafunzo ya Qur-aan na Sunnah na hakikisha mafunzo yote unayoyapata ni mafunzo swahiyh yasiyo na shaka. Mashirika ya Hajj, kawaida huwa yanatoa mafunzo kabla ya safari.

**9-Hifadhi Du'aa Za Manaasik**

Rejea mlango wake katika kitabu hiki ujitahidi kuzihifadhi du'aa hizo ili iwe wepesi kabisa kwako kutekeleza 'Umrah na Hajj yako kwa sababu kutokana na zahma kubwa, inakuwa vigumu mtu kutazama kitabu kuzisoma hizo du'aa; na vitabu vingi vya du'aa vinavyouzwa huko, havina mashiko; du'aa zake hazijathibiti, bali ni taklifa. Ukiweza kuzihifadhi hizo du'aa chache zilizothibiti, itakuwa sahali mno kwako na utaweza kutimiza kikamilifu Hajj yako.

**10-Chunguza Magonjwa Na Chanjo**

Ni vyema kufanya vipimo hospitalini kabla ya kuondoka ili kuhakikisha huna magonjwa yoyote ambayo huenda

yakachomoza huko safarini yakakuzuia kutekeleza 'ibaadah yako.

Pia piga chanjo zote zinazohitajika uchukue vyeti vyake. Bila shaka utafahamishwa hili na shirika unalojiunga nalo.

## 11-Begi

- Jaribu kununua begi lisilokuwa zito wala kubwa mno kwani kuna taabu yake katika usafiri na pia dhiki ya sehemu ya kuliweka hotelini kwani vyumba huko si vyenye nafasi kubwa ya kutosheleza mizigo mikubwa. Kumbuka pia kwamba zawadi kubwa watu wanayopenda kuchukua kurudi nayo ni maji ya Zamzam ambayo hayatoingia katika begi bali utahijtaji kuyabeba pekee.

- Chukua pia kibegi kidogo cha kitambaa na zipu, au kibegi cha mgongoni, kutumia wakati utakapoelekea *Minaa* kwa masiku hadi umalize taratibu za huko; yaani kuanzia tarehe 8 Dhul-Hijjah hadi tarehe 12 au 13 Dhul-Hijjah.

- Baada ya kufunga begi lako, weka alama kama ribini au kitambaa cha rangi kwenye mkono wa begi, au andika jina lako ili uweze haraka kulitambua begi lako unaposubiri mabegi kuteremeshwa kutoka katika ndege.

## 12-Vitu Utakavyohitaji Kuchukua

Aghlabu ya vitu vinapatikana kwa usahali Makkah na Madiynah, lakini tunavitaja hapa pamoja na maelezo ziada ya kutanabahisha. Kwa hiyo orodha hii ya vitu unaweza kununua huko huko Makkah au Madiynah. Kwa hiyo mtu atapima mwenyewe kama atapendelea kununua hivi vitu mapema nchini mwake au atapenda kununua huko, lakini ni bora kununua kabla ya safari ili ujifanyie wepesi kwani uendako ni ugenini na utaweza kuhifadhi muda wako kwa 'ibaadah badala ya kwenda madukani.

Kwa wale ambao watahirimia katika ndege kwa ajii ya kufanya 'Umrah, hutohitaji vitu vya kufanya ghuslu kwa sababu utahitajika kufanya ghuslu tokea nyumbani kwako. Ama wanaofikia

Madiynah kwanza, hao watahitaji kuwa na vitu vyao tayari kwa sababu watahirimia katika Miyqaat ambako atahitajika kufanya ghuslu (kuoga josho).

| Mahitaji ya Msalani (Chooni) | |
|---|---|
| **Cha kuchukua** | **Tanbihi** |
| Shampuu | Wanawake zaidi wanahitaji lakini zisiwe zenye manukato. |
| Karatasi za tisshu | Vipaketi vidogo dogo ambavyo vinaingia katika kibegi cha mkononi cha mwanamke. Hakikisha usinunue zenye manukato. |
| Sabuni ya maji ya kuogea | Inakuwa sahali kuitumia safarini khasa utakapokuwa *Minaa*. Pia ni afya zaidi kutumia kuliko sabuni ya kawaida. Hakikisha kuwa haina manukato. |
| Sabuni ya maji ya mkono iwe ya kuua viini, vidudu. | Ni sahali kutumia na kusafiri nayo na ni afya zaidi kuitumia. |
| Waipa za karatasi za kuua viini vidudu | Daima weka katika kibegi cha mkononi kutumia khasa kabla ya kutawadha au kula chakula kwani si wepesi kupata maji ya kunawaia mkono. Utazihitaji msalani pia. |
| Dawa ya mswaki | Miswaak ya Sunnah pia inapatikana tele huko na vizuri kuitumia kila mara. |
| Dawa ya kusukutilia mdomo au karafuu, hiliki. | Ni vyema kuwa na dawa ya kusukutilia mdomo kuhifadhi harufu ya mdomo khasa asubuhi unapoamka na kwenda Masjid. Tahadhari! Aghlabu ya dawa hizi zina alkoholi lakini ziko pia zisizo na alkoholi, kwa hivyo hakikisha au chukua karafuu na hiliki katika kichupa kidogo, uwe unazitafuna na kuzisukutulia baada |

| | |
|---|---|
| | ya kupiga mswaki kwani zinakata vizuri harufu mbaya ya mdomo. Tambua kwamba kuna Hadiyth ya Rasuli ( صلى الله عليه وآله وسلم) aliyotamani kuamrisha Muislamu apige mswaki kabla ya kila Swalaah! Na tambua pia kwamba Malaika wanaridhika na harufu nzuri na wanaudhika na harufu mbaya! |
| Diodorani - dawa ya kwapani | Isiwe yenye manukato. Au tumia shabu ambayo haina harufu na unaweza kuichanganya na podari isiyokuwa na manukato. |
| Pedi na vibandiko vya chupi. | Wanawake watahitaji ili kujihifadhi pindi imewatokezea hedhi. Vibandiko vya chupi vinasaidia mno kubakisha chupi ya mwanamke safi na kujipunguzia mashaka ya kuzifua kwani hizo huwa unabadilisha tu pindi ikichafuka na chupi inabakia kuwa safi kwa muda wa siku nzima. Hii itakusaidia sana katika Ihraam kwani pindi chupi ikichafuka si wepesi kupata kuifua msalani hadi urudi hotelini.<br><br>Weka chache katika handbag yako kila mara uwe nazo akiba. |

| **Mahitaji Ya Ihraam** | |
|---|---|
| **Cha kuchukua** | **Tanbihi** |
| Wanaume - shuka za Ihraam na mkanda wa kujifunga kiunoni wenye sehemu ya kuhifadhi pesa. | Zinapatikana kwa urahisi madukani katika nchi unayotoka. Ni vyema kununua jozi mbili ya nguo za Ihraam kwani utabakia katika Ihraam siku 3 takriban kuanzia tarehe 8 Dhul-Hijjah. |
| Makubadhi | Viatu vya ngozi – vinapatikana maduka |

| | |
|---|---|
| | ya nguo za Ihraam. |
| Vifaa vya kunyolea nywele na sehemu za siri – vya kutumia na kutupa. | Ikiwa umekosa kinyozi wakati wa kujivua Ihraam. Na pia kujisafisha nywele sehemu za siri khasa siku ya tarehe 10 Dhul-Hijjah.<br><br>Tanabahi: Ihraam ya mwanzo kwa ajili ya 'Umrah ni vizuri kujisafisha ukiwa bado uko kwako ili usipate tabu tena utakapofika *Miyqaat* ikiwa unatokea Madiynah. Ama wanaotanguliza 'Umrah moja kwa moja baada ya kufika mjini Jeddah, wao wanapaswa wawe wameshaingia Ihraam katika ndege na hivyo watakuwa wameshaoga majumbani mwao. |
| Mkoba mdogo | Wa mkanda unaovaliwa shingoni na kubakia mbele yako unapotembea kuhifadhi pesa na vitu vidogo muhimu; simu, kadi za benki n.k. |
| Nguo na mahitaji ya wanawake katika Ihraam na nje ya Ihraam | Nguo zozote zinafaa ila ziwe zimetimiza masharti ya hijaab[78]. Si lazima kuvaa nguo nyeupe au ya kijani wala si katika Sunnah bali mwanamke anaweza kuvaa nguo zake zozote zile. Chukua nguo nyepesi zilizo wepesi kuzifua na zisizohitaji kupigwa pasi. Utahitaji kubadilisha nguo ukiwa katika Ihraam kwa muda wa siku nne takriban.<br><br>Wanawake washoneshe mifuko ndani ya nguo zao za ndani ili wahifadhi pesa zao. Juu yake wavae 'abaayah. |
| Baibui/'abaayah | Kiasi matatu. Ukiwa katika Ihraam *Minaa*, utahitaji angalau mawili kwani ni wepesi kuchafuka. 'Abaayah zisiwe za kuonyesha mwili, na zisizo na marembo wala rangi, yawe pleni kabisa bila ya urembo wowote |

[78] Tazama mlango unaohusu Wanawake.

| | |
|---|---|
| | ule bali ziwe pana zisizobana mwili, zisizo na uwazi wowote, bali zenye kufunika nguo nzima na mwili mzima mpaka miguuni. |
| Khimaar au mtandio | Utahitaji Khimaar au mitandio mirefu na mipana ya kukufunika tokea kichwani hadi angalau magotini ili ubakie katika sitara ya hijaab inayopasa kishariy'ah.<br><br>**MUHIMU:** Mwanamke haimpasi kufunika uso wake na kuvaa glavu katika Ihraam ila inapokuwa kuna wanaume akachelea fitnah, kwa hali hiyo atatakiwa kujifunika uso wake lakini si kwa niqaab au burqah bali kwa ghashwah au kitambaa chepesi kisichobana uso.[79] |
| Suruwali ndefu za kuvalia ndani badala ya gaguro. | Kwa ajili ya kujisitiri. Hizi ni vyema kuzitumia kila mahali kwani ni sitara kubwa kwa mwanamke pindi unapopanda na kushuka gari ujisitiri miguu yako isionekane. Pia inapotokea ajali (Allaah Atuhifadhi), unasitirika kwa kutokukashifu mwili wako na sehemu za siri. Katika Ihraam ndio kuna umuhimu mkubwa wa kuzivaa. |
| Soksi. | Ufunike miguu yako wakati wote mpaka katika Swalaah. Chukua jozi kadhaa kwani ni wepesi kuchafuka, utahitaji kubadilisha mara kwa mara. Soksi zitakusaidia pia kufanya *Mas-hul-Kufayn*[80] . |
| Mkoba mdogo wa mkanda mrefu | Utahitaji mkoba mdogo wa kutumia wakati unapofanya *Twawaaf* na *As-Sa'-y* kwani kubeba mkoba mkubwa unachosha. Mkoba mdogo wenye mkanda unaoweza kuuvaa begani kwa upande ili mkoba uwe mbele yako |

[79] Tazama mlango unaohusu Wanawake katika nukta ya 'Ihraam'
[80] Kufanya wudhuu juu ya soksi.

| | |
|---|---|
| | unapouvaa kwa ajili ya kujilinda na kuibiwa pesa na wachomoaji. Humu unaweza kujitilia vitu vyako vya muhimu kabisa kiasi cha muda huo wa kutekeleza *Twawaaf, As-Sa'-y* n.k. |
| Taulo | Ya kiasi kujifutia maji, nyepesi na nyinginezo ndogo ndogo. Ni vizuri kutumia taulo ndogo kulikoni kubwa kwa sababu ya usahali wa kufua na kuanika ikiwa unafikia hoteli zisizotowa huduma za vitu kama hivyo. |
| Sabuni ya kuogea. | Mahujaji watumie sabuni zisizokuwa na manukato. |
| Viatu | Wanawake viatu vyovyote ambavyo vinaweza kutumika kufanyia wudhuu na kuingia navyo msalani. Pia viwe vyepesi kuvibeba na kuingia navyo Msikitini unapiviweka katika mifuko. |
| Mfuko mdogo wa kitambaa au plastiki | Kwa ajili ya kutilia viatu vyako unapoingia Masjid hasa kwa ajili ya Masjid An-Nabawiy kwani mifuko ya bure inapatikana Masjid Al-Haraam unapoingia tu ndani ya Msikiti. |
| Mkasi mdogo | Wanawake kwa ajili ya kukata nywele zao kidogo kujitoa katika Ihraam. Usipeki mkasi katika mkoba wa mkononi kwani hairuhusiwi kuingia nao katika ndege. |

| **Nguo Za Kawaida** | |
|---|---|
| **Cha Kuchukua** | **Tanbihi** |
| Kanzu, fulana, shuka au suruwali ya kuvalia ndani ya | Wanaume: Haifai kuchukua fulana au mashati yenye picha, nembo n.k. |

| | |
|---|---|
| kanzu | Tanbihi kwa wanaume na wanawake: Huduma za udobi zimejaa barabarani huko kwa hiyo usijibebeshe nguo nyingi. |
| Nguo za ndani, niqaab, skafu za hijaab, mitandio (shela), kanga mbili tatu n.k. | Mwanamke atahitaji kubadilisha nguo za ndani mara kwa mara, kwa hiyo chukua za kukutosheleza. Kanga na mitandio ya pamba utahitaji kujifunikia hotelini ingawa si muda mrefu utakaokuwa unashinda humo.<br><br>**MUHIMU!** Kina dada jifunikeni nyuso zenu kwa niqaab au ghashwah (mtandio unaoufunika uso), kuepukana fitnah za wanaume na fitnah za video na wahalifu wanaorekodi huko kila sehemu! |
| Nguo za kulalia | Wanaume kanzu nyepesi au fulana na msuri (kikoi).<br><br>Wanawake nguo za nyepesi za pamba. |

| **Misahafu, Vitabu** | |
|---|---|
| **Cha Kuchukua** | **Tanbihi** |
| Mus-haf (Qur-aan) | Mdogo utakaoweza kuuweka katika mkoba wako kila mahali kwani wakati mwengine si wepesi kuipata Misahafu iliyoko Masjid. Unaweza kuifuatilia lakini utakaporudi utakuta mahali pako pameshakaliwa! |
| Msahafu wa Tarjama mdogo. | Ni vizuri Muislamu kutumia muda wake wa faragha kusoma na kufahamu maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى). Utakapokuwa *Minaa* chukua fursa hii kusoma Tarjama ya Qur-aan. |

| | |
|---|---|
| Miwani ya kusomea | Kwa wenye udhaifu wa macho khasa ikiwa utachukua msahafu mdogo.<br>Ni vyema kuchukua moja ziada kama akiba pindi ikipotea moja. |
| Kitabu cha du'aa | Hiswnul-Muumin au Hiswnul-Muslim ambacho kina adhkaar za asubuhi na jioni pamoja na du'aa mbali mbali anazozihitaji Muislamu katika maisha yake kila siku. Ni vyema kuzihifadhi khasa zile za Swalaah ili uweze kutekeleza Swalaah zako kikamilifu na kwa uzuri kabisa.<br><br>Ukitaka kuchukua vitabu vinginevyo vya du'aa na adhkaar, hakikisha unachukua vilivyothibiti katika Sunnah, usije ukapoteza muda wako na juhudi kwa 'amali zisizokubaliwa. Rejea mlango wa 19 mlango wa du'aa za Sunnah ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) katika kitabu hiki zimeandaliwa ambazo zinamtosheleza Muislamu kuzisoma. |
| Kitabu cha Fiqh ya Hajj | Kinapatikana maduka ya vitabu, na pia hiki kitakutosheleza.<br><br>Ukiwa na swali ambalo hukulipata mwelekezo, kuna huduma za Fataawa katika *Masjid Al-Haraam*. Kila mahali zimewekwa simu ukinyanyua tu anapokea mtu kukujibu swali lako. Au pia uliza wahusika uliojiunga nao. Ni vyema kuuliza jambo kuliko kuona haya kuuliza ukafanya makosa. |

| Mahitaji Mengineyo | |
|---|---|
| **Cha Kuchukua** | **Tanbihi** |
| Viatu vya raba vya mazoezi. | Pia ni vizuri kuwa na jozi ya viatu vya aina hii kwa ajili ya kuvitumia utakapokuwa *Minaa* kwa vile utakuwa na mwendo wa panda shuka huku na kule kuliko kuvaa ndara au makubadhi. |
| Kifuko kidogo mno cha plastiki au kitambaa (viwe vitatu) | Kutilia vijiwe vya *Jamaraat* ukihofia kuvipoteza baada ya kuviokota. |
| Mkoba au mfuko | Wa kuweza kuchukua Masjid na kila mahali na kutia vitu vyako muhimu kama Msahafu, dawa, miwani, mswala mwepesi, karatasi za tisshu, pesa za matumizi kidogo, n.k. |
| Pochi ya pesa | Inayokufaa. |
| Mswala wa kujikunja au midogodogo ya kuingia katika mkoba mdogo | Kwa ajili ya kuuchukua kila uendapo safarini kwani huenda ukakosa mahali ndani ya Masjid au baadhi ya Misikiti ya njiani haina mazulia masafi. Pia unaweza kuutumia kulalia utakapokesha *Muzdalifah*. |
| Kalamu na kitabu kidogo. | Cha kuandikia maelezo na orodha ya kujikumbusha. |
| Simu ya mkono. | Kwa ajili ya mawasiliano ya dharura. Kadi za simu zinapatikana Saudia na zimejaa kila mahali kwa bei nafuu kabisa.<br><br>**Lakini Hakikisha unazima simu yako kila unapokuwa Msikitini**!<br><br>Ni busara kila mmoja; mume na mke awe na simu yake kwani huenda |

| | |
|---|---|
| | mkahitaji kuwasiliana baada ya kutoka Masjid na khasa ikitokea mmepoteana. |
| Chaji ya simu na adapta (kirekebishi) | Hakikisha chaji inafanya kazi na ukiweza kuchukua moja ziada ni vizuri. Adapta ni muhimu kabisa uweze kuchaji simu yako kwani baadhi ya hoteli hawaweki. |
| Kufuli ya begi | Tengeneza ufunguo mwengine ikiwezekana ili ukipotea mmoja uwe na wa pili. |
| Begi dogo la kubeba mgongoni. | Utalihitaji wakati wa safari ndogo kama kwenda baina ya *'Arafah*, *Muzdalifah*, Makkah na *Minaa*. |
| Kikatio kucha | Kwa kukata kucha zako kabla hujahirimia, na baada ya kumaliza Hajj. |
| Kitana, brashi | Chukua ndogo ndogo tu. |
| Saa ya kengele ikiwa hutumii ya simu. | Ikuamshe nyakati za 'ibaadah. Aghlabu simu za mkono zinazo huduma hii. |
| Chupa ndogo ya maji ya kunywa. | Utaweza kujitilia maji ya zamzam ukipenda kila unapotoka Masjid. Utahitaji haya khasa siku za joto lakini maji ya kuuzwa chupani yanapatikana kwa sahali huko. |

| **Visivyopasa Kuchukua** | |
|---|---|
| **Kisichopasa Kuchukua** | **Tanbihi** |
| Kamera pamoja na video kamera, n.k. Hata simu zenye kamera. | Hairuhusiwi kwani huko ni sehemu ya kutekeleza 'Ibaadah na haendi mtu kwa ajili ya matembezi au utalii. Jambo hili linapaswa kukatazwa mno kwani imekuwa ni fitnah kubwa siku hizi |

| | |
|---|---|
| | kurekodi hata katika kutufu *Al-Ka'bah*, *As-Sa'-y* na kwengineko. Na simu zote za mkono siku hizi zina kamera, na kupiga au kupigwa picha zisizo za dharura ni haraam! kwa hiyo **TAHADHARI** na kuingia katika fitnah hii usiharibu Hajj yako. |
| Mapambo ya thamani; dhahabu, saa za ghali n.k. | Mwanamke hatakiwi kujipamba kabisa kwa mapambo yoyote yale. |
| Visu, aina zozote za silaha, vitu vya maji. | Hairuhusiwi kubeba hivi katika ndege utaweza kujitia mashakani ukazuilika safari. |
| Nguo za fakhari, vipodozi vya wanawake n.k. | Haifai kabisa kuchukua kwani unatakiwa ujiepushe na kila linalochukiza ili usalimike na 'ibaadah zako. |

## 08- Du'aa Za Kujitayarisha Kuhifadhi

Du'aa na adhkaar zifuatazo ni zile zilizothibiti katika Sunnah ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alizozisoma katika sehemu zinazohusika. Zimekusanywa katika mlango huu ili iwe sahali mtu kuzihifadhi kabla ya safari. Kufanya hivyo utajifanyia sahali mno na utatekeleza 'Ibaadah yako ipasavyo na pia utaepukana na kusoma du'aa au adhkaar zisizothibiti katika mafunzo ya Qur-aan na Sunnah. Kwa maelezo zaidi na kupata maana zake, rejea kila du'aa au adhkaar katika mlango husika. Pia, rejea mlango wa Swalaah ya Janaazah kuhifadhi Du'aa humo. Vile vile chukua kitabu cha Hiswnul-Muumin ambacho ndio sahihi zaidi, au Hiswnul-Muslim ambacho kimefasiriwa kwa Kiswahili upate tarjama na marejeo yake. Tumia vijitabu hivi daima kupata du'aa za kila siku anazohitaji Muislamu.

1- Du'aa ya kupanda kipando na safari

الله أكبَر، اللهُ أكبَر، اللهُ أكبَر، ﴿ سُبْحَـٰنَ ٱلَّذِى سَخَّرَ لَنَا هَـٰذَا وَمَا كُنَّا لَهُۥ مُقْرِنِينَ ﴿١٣﴾ وَإِنَّآ إِلَىٰ رَبِّنَا لَمُنقَلِبُونَ ﴿١٤﴾ ﴾ اللّهُمَّ إِنّا نَسْأَلُكَ في سَفَرِنا هذا البِرَّ وَالتَّقْوى، وَمِنَ الْعَمَلِ ما تَرْضى، اللّهُمَّ هَوِّنْ عَلَينا سَفَرَنا هذا وَاطْوِ عَنّا بُعْدَه، اللّهُمَّ أَنْتَ الصّاحِبُ في السَّفَر، وَالْخَليفَةُ في الأهلِ، اللّهُمَّ إِنّي أَعوذُبِكَ مِنْ وَعْثاءِ السَّفَر، وَكَآبَةِ الْمَنْظَر، وَسوءِ الْمُنْقَلَبِ في المالِ وَالأَهْل.

***Allaahu Akbar, Allaahu Akbar, Allaahu Akbar. Subhaanal-Ladhiy Sakkhara lanaa haadhaa wamaa kunnaa Lahu muqriniyn, wainnaa ilaa Rabbinaa lamunqalibuwn. Allaahumma innaa nas-aluka fiy safarinaa haadhal-birra wat-taqwaa, waminal'amali maa-Tardhwaa. Allaahumma hawwin 'alaynaa safaranaa haadhaa, wa-ttw-wi 'annaa bu'dah. Allaahumma Antasw-Swaahibu fis-safari, wal-Khaliyfat fil-ahli. Allaahumma inniy a'uwdhu Bika min wa'thaais-safari, wakaabatil-mandhwar, wasuw-il-munqalabi filmaali wal-ahli[81]***

[81] Rejea Hiswnul Muslim (Du'aa za Safari) kupata tarjama (maana) na marejeo yakey.

Wakati wa kurudi safari utayasema hayo yalioko juu na kisha utazidisha:

آيِبُونَ تائِبُونَ عابِدُونَ لِرَبِّنا حامِدُونَ

***Aayibuwna, taaibuwna, 'aabiduwnaa, li Rabbinaa haamiduwna***

2- Niyyah baada ya kuingia katika Ihraam

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ عُمْرَة

***Labbayka-Allaahumma 'Umrah***

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ حَجًّا

***Labbayka-Allaahumma Hajjaa***

3- *Talbiyah*

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ, لَبَّيْكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ, إِنَّ الْحَمْدَ, وَالنِّعْمَةَ, لَكَ وَالْمُلْكَ, لاَ شَرِيكَ لَكَ

***Labbayka-Allaahumma Labbayk. Labbayka laa shariyka Laka Labbayk. Innal-Hamda Wan-Ni'imata Laka wal-Mulk laa shariyka Lak***

4- Du'aa ya Kuingia Masjid

أَعُوذُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ, وَبِوَجْهِهِ الْكَرِيمِ, وَسُلْطَانِهِ الْقَدِيمِ, مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ، (بِسْمِ الله، وَالصَّلاةُ) (وَالسَّلامُ عَلى رَسولِ الله)، اللَّهُمَّ افْتَحْ لي أَبْوابَ رَحْمَتِك

***A'uwdhu biLlaahil-'Adhwiym, wabi Wajhihil-Kariym wa-Sultwaanihil-qadiym, minash-shaytwaanir-rajiym (BismiLLaahi wasw-swalaatu) (was-salaamu 'alaa Rasuwli-LLaah) Allaahummaftah-liy abwaaba Rahmatika***

5- Kuanza *Twawaaf*

بِسْمِ اللَّهِ اللَّهُ أَكْبَرَ

***BismiLLaah, Allaahu Akbar***

*Twawaaf* ya pili na kuendelea ni kusema '*Allaahu Akbar*' pekee

6- Baina ya *Rukn Al-Yamaaniy* na *Al-Hajar Al-As-wad*

﴿ رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِى ٱلْءَاخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ﴿٢٠١﴾ ﴾

7- Maqaam Ibraahiym

﴿ وَٱتَّخِذُوا۟ مِن مَّقَامِ إِبْرَٰهِـۧمَ مُصَلًّى ﴾

8- Unapoanza *Asw-Swafaa* Na *Al-Mar-wah*

﴿ ۞ إِنَّ ٱلصَّفَا وَٱلْمَرْوَةَ مِن شَعَآئِرِ ٱللَّهِ ﴾

9- Du'aa Baina ya vilima viwili Vya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah*

لا إِلَهَ إلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ وَلَهُ الحَمْدُ وهُوَ عَلى كُلِّ شَيءٍ قَديرٌ، لا إِلَهَ إلا اللهُ وَحْدَهُ أَنْجَزَ وَعْدَهُ، وَنَصَرَ عَبْدَهُ وَهَزَمَ الأَحْزَابَ وَحْدَهُ

***Laa Ilaaha Illa-Allaah, Wahdahu laa shariyka Lah, Lahul-Mulku Walahul-Hamdu wa Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr. Laa Ilaaha Illa-Allaahu Wahdahu, Anjaza wa'dahu wa-Naswara 'Abdahu wa-hazamal-ahzaaba Wahdahu***

10- Du'aa kuu ya '*Arafah*

لا إِلَهَ إلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ ولَهُ الحَمْدُ وهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَديرٌ.

***Laa Ilaaha Illa-Allaah Wahdahu laa shariyka Lah, Lahul-Mulku walahul-Hamdu wa-Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr***

11- Du'aa ya *Jamaraat* Kila ukirusha jiwe

اللَّهُ أَكْبَرَ

***'Allaahu Akbar'***

12- Du'aa ya kuzuru kaburi la Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

Wanaume Wanapozuru kaburi la Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

السَّلامُ عَلَيْكَ أَيُّها النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُه

***Assalaamu 'alayka ayyuhan-Nabiyyu wa-Rahmatu-Allaahi wa Barakaatuh***

اللّهُمَّ صَلِّ عَلى مُحَمَّدٍ وَعَلى آلِ مُحَمَّد كما صَلَّيْتَ عَلى آلِ إبْراهيم وَعَلى آلِ إبْراهيم إِنَّكَ حَميدٌ مَجيد, اللّهُمَّ بارِكْ عَلى مُحَمَّدٍ وَعَلى آلِ مُحَمَّد كما بارِكْتَ عَلى إبْراهيم وَعَلى آلِ إبْراهيم إِنَّكَ حَميدٌ مَجيد

***Allaahumma Swalliy 'alaa Muhammad wa 'alaa aali Muhammad kamaa Swallayta 'alaa Ibraahiym wa 'alaa aali Ibraahiym Innaka Hamiydum-Majiyd. Allaahumma Baarik 'alaa Muhammad wa 'alaa aali Muhammad kamaa Baarakta 'alaa Ibraahiyma wa 'alaa aali Ibraahiym Innaka Hamiydum-Majiyd***

أشْهَد أنَّكَ رَسُولُ الله حَقاً، وَأنَّكَ قَدْ بَلَّغْتَ الرِّسَالَةَ، وَأدَّيْتَ الأَمَانَةَ، وَنَصَحْتَ الأُمَّةَ، وَجَاهَدْتَ فِي اللهِ حَقَّ جِهَادِه، فَجَزاكَ اللهُ عَنْ أُمَّتك أَفْضَل ما جَزَى نَبِيًّا عَنْ أُمَّتِه.

***Ash-hadu Annaka Rasuwlu-Allaah haqqan, wa annaka qad ballaghtar-Risaalah, wa addaytal-amaanah, wa naswahtal-Ummah, wa jaahadta fiyLLaahi haqqa jihaadih, fa-Jazaaka-Allaahu 'an Ummatika afdhwal maa jazaa Nabiyyan 'an Ummatih***

Wanawake haipendezi kuzuru makaburi, na kutokana na zahma kubwa inayokuweko huko mpaka watu kusukumana, inamtosheleza mwanamke kumswalia Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) popote alipo katika Masjid An-Nabawiy.

13- Du'aa ya kuzuru Kaburi la Abu Bakr na 'Umar (رضي الله عنهما)

السَّلاَمُ عَلَيْكَ. رَضِيَ اللَّهُ عَنْكَ وَجَزَاكَ اللَّهُ عَنْ أُمَّة مُحَمَّد أَفْضَل جَزَاء

***Assalaamu 'alayka. Radhiya-Allaahu 'anka wa Jazaaka-Allaahu 'an Ummati Muhammad afdhwal jazaa.***

14- Du'aa ya Kuzuru Makaburi Ya Maswahaba[82]

السَّلامُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الدِّيارِ مِنَ المؤْمِنينَ وَالْمُسْلِمينَ، وَإِنّا إِنْ شاءَ اللهُ بِكُمْ لاحقون، وَ يَرْحَمُ اللَّهُ الْمُسْتَقْدِمِينَ مِنَّا وَالْمُسْتَأْخِرِينَ, نَسْاَلُ اللهَ لَنَا وَلَكُمُ العَافِيَةَ.

***Assalaamu 'Alaykum Ahlad-Diyaari Minal-Muuminiyna Wal-Muslimiyn, Wa In-shaa-Allaah Bikum Laahiquwn, Wayarhamu-LLaahul-Mustaqdimiyna Minnaa Walmusta-akhiriyn) Nas-alu-Allaaha Lanaa Wa Lakumul-'Aafiyah***

[82] Inafaa kusomwa unapozuru au kupitia katika makaburi ya Waislamu.

## 09- Yanayotegemewa Kutoka Safarini

Anza safari yako kwa kuomba du'aa za kipando na safari[83]. Katika ndege jishughulishe na kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kusoma Qur-aan, *istighfaar, tasbiyh, tahmiyd, tahliyl, takbiyr*, du'aa, kumswalia Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) n.k. Usitizame filamu za anasa zinazowekwa katika ndege, zipuuze kabisa na epusha macho na masikio yako kusikiliza na kutazama maasi.

### 1-Kuchelewa Uwanja Wa Ndege Au Mpakani

Huenda mkachelewa sana kiwanja cha ndege cha Jeddah, kwa hiyo jitayarishe kwa kuvuta subira. Ikiwa unatoka nchi za karibu jichukulie vitafunio katika begi la mkono. Usichukue vyakula vya kupikwa nyumbani kwani serikali ya Saudia inatahadharisha kukhofia magonjwa. Bora zaidi ubadilishe pesa kwa Riyali za Saudia kununulia chakula kwenye kiwanja cha ndege. Hali ni hiyo hiyo mpakani kwa wanaosafiri kwa gari.

### 2-Zahma

Bila shaka utakutana na zahma kila mahali. Na hakuna kuepukana na jambo hili isipokuwa kuvuta subira ya hali ya juu na kujiepusha kusukumana na Mahujaji na kusababisha maudhi na magomvi ukaja kuharibu Hajj yako.

### 3-Safari Baina Ya Makkah Na Madiynah

Huenda mkasimama vituoni kuswali. Chukua malapa kwa ajili ya kuingia msalani. Usisahau kuchukua mfuko wako ambao una vitu muhimu.

### 4-Chakula

Vyakula vya kila aina vinapatikana mahotelini na mikahawani. Hakikisha unanunua chakula katika sehemu zilizo safi ili ujikinge kula chakula kichafu au kilichoharibika.

---

[83] Rejea mlango wa Du'aa za Kuhifadhi.

**5-Hali ya hewa**

Inategemea miezi unayokwenda. Siku za joto ni kuanzia mwezi wa Mei mpaka takriban Oktoba. Ama kuanzia Novemba hadi Machi, hali ya hewa kawaida huwa ni nzuri na huenda hata ikawa baridi ya kiasi. Kwa hiyo chukua nguo kulingana na hali ya hewa huko.

**6-Kupotea**

Kupotea au kupoteana huko ni jambo lisiloepukika hasa katika Haram mbili; Masjid Al-Haraam na Masjid An-Nabawiy wakati wa kutoka nje. Kupoteana kunasababika zaidi kutokana kutokujiandaa vizuri na wenzako kuhusu hatua za kuchukua. Kujiandaa huko ni muhimu kwa sababu anaweza mtu kuchanganyikiwa akili kwa khofu na zahma iliyoko huko hasa kwa ambaye hana uzoefu wa kuweko huko! Hatua zifuatazo huenda zikasaidia:

- Ainisha muda maalumu wa kukutana na wale watakaochelewa kutoka Masjid huku ukichunga kutokucheleweshа kutekeleza taratibu za 'Ibaadah zinazokupasa kuzitenda wakati huo.
- Agana na wenzako kabla ya kuingia Masjid mkutane sehemu maalumu mnapotoka Masjid. Mfano, chagua jumba au duka iwe ni alama yenu ya kukutana.
- Wanawake wanaweza kujiwekea alama maalumu katika 'abaayah zao kwa ajili ya kutambuana, au kuvaa kanga ili watambuane. Lakini alama au kanga zisiwe zenye maneno au picha za viumbe kwani hizo hazifai kuswalia.
- Hakikisha kila mtu katika kikundi chenu amefahamu sawasawa muongozo kuhusu hatua za kuchukua wakati wa kupotea.
- Usiache kuvaa kadi au beji yako uliopewa na shirika ili utambulike haraka inapofika hali ya dharura kama kupotea, kuzimia, kufariki. Unaposwali ivue kwani kuswali na picha haifai
- Jaribu kuangaza kwa makini jengo la Masjid Al-Haraam lilivyo na maeneyo yake ya nje pamoja na hoteli zinazokabiliana nalo, uweze kutambua njia ya kuelekea hoteli uliyofikia.

Picha ifuatayo inaonyesha mageti mawili makubwa yaliyoko kati ya minara miwili; wa kuliani kwako ukiwa unaangalia katika ukurasa huu, ni Geti la Malik 'Abdul-'Aziz na wa kushotoni ni Geti la Malik Fahd. Geti la Malik 'Abdul-'Aziz linakabiliana na 'Waqf Malik 'Abdul-Aziz'; mahoteli na maduka katika jengo lenye mnara wa saa ya kijani.
Geti la Malik Fahd linakabiliana na hotel ya 'Dar At-Tawhiyd', na kuna upanuzi mkubwa wa Masjid Al-Haraam katika maeneo hayo miaka tokea mwaka 1434 hadi 1436H.



- Kumbuka jina la mlango mnaoingilia kwani kila mlango umeandikwa jina lake, hivyo itakuwa sahali kukutana hapo.

**7-Kupotelewa pesa, simu n.k.**

Kuna sehemu ya kuripoti vitu vilivyopotea. Ripoti haraka huenda ukajaaliwa kupata kilichokupotea. Tahadhari na wezi kwani kuna watu wasio na iymaan wala hayaa ambao wanakuja kwenye 'ibaadah hiyo huko watokapo kuja kuwaibia Mahujaji!! Ni wezi stadi wanaoibia watu hata kwenye *Twawaaf*, Allaah Awahidi.

**8-Madukani - Sokoni**

Yamejaa tele barabarani. Lakini, nasaha muhimu kuwa usipoteze muda wako mwingi humo kwani ululiendea kuu ni kutekeleza Hajj. Pia unaponunua usibishane sana na muuzaji ukaharibu Hajj yako; mambo hayo Amekataza Allaah (سبحانه وتعالى):

فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي ٱلْحَجِّ

**((Na atakayekusudia kuhiji (akahirimia), basi asifanye tendo la ndoa wala ufasiki wala mabishano katika Hajj.))**[84]

**9-Wazee Na Wagonjwa**

Kuna huduma za *Twawaaf* na *As-Sa'-y* kwa watu wazima wasiojiweza. Wanaitwa *Mutwawwif*. Huwabeba katika viti na kukufanyisha *Twawaaf* na *As-Sa'-y* kwa malipo.

**10-Vifo**

Utahudhuruia Swalaah ya Janaazah takriban kila baada ya Swalaah. Jifunze Swalaah hiyo katika mlango wa 18.

[84] Al-Baqarah (2: 197).

### 10- Nasaha Za Mafanikio Ya *Hajjum-Mabruwr*

Hadiyth za Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) zimetaja kwamba *Hajjum-Mabruwr* jazaa yake ni Jannah [85] na kila mwenye kuhiji anatarajia malipo hayo matukufu kabisa. Lakini vipi mtu aweze kuipata *Hajjum-Mabruwr*? Nasaha zifuatazo zitasaidia kufanikisha hilo In Shaa Allaah.

**1-Ikhlaasw**

Weka niyyah safi kuitekeleza Hajj yako kwani 'amali yoyote isiyokuwa kwa niyyah safi haipokelewi. Niyyah isiwe kwa ajili ya lolote jingine isipokuwa kutaka Radhi za Allaah (سبحانه وتعالى).

**2-Kuitekeleza Kwa Kufuata Sunnah Ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):**

Muislamu anapaswa kutekeleza 'Ibaadah zake zote kwa kufuata mafunzo ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم). Baadhi ya watu hutekeleza 'ibaadah na taratibu kinyume na amri yake aliposema:

((خُذو عنِّي مَنَاسِكَكُمْ))

***((Chukueni kutoka kwangu manaasik zenu))*** [86]

Atakayefanya hivyo, atakuwa amepoteza juhudi zake na mali yake na hatofaulu katika kufikia lengo la Hajj na kupata thawabu zake kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ameonya:

((مَنْ أَحْدَثَ فِي أَمْرِنَا هَذَا مَا لَيْسَ فِيهِ فَهُوَ رَدٌّ))

***((Atakayezusha katika jambo letu hili lisilokuwa (katika Dini) yetu basi litarudishwa))*** [87]

**3-Subira**

Jifunze na jitayarishe kuwa na subira ya hali ya juu kwa sababu huko ni mkusanyiko wa watu wasiopunguka milioni tatu! Na

[85] Tazama Mlango wa Fadhila Za Hajj.
[86] Muslim na wengineo
[87] Al-Bukhaariy na Muslim

sehemu kadhaa inabidi wakusanyike watu wote kwa wakati mmoja. Kwa hivyo kunakuwa na msongamano mkubwa wa watu. La kutahadhari zaidi ni kwamba huenda mtu akasukumwa na aliye nyuma yake apate kusogea mbele. Kitendo hicho ni cha kumkasirisha mtu, na hapo ndipo inapohitajika subira ya hali ya juu ili usije kugombana naye au yeyote mwengine atakayekufanyia dhulma ya aina yoyote, kwani kutokuvumilia kutasababisha ukose kutimiza kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) Aliyokataza mabishano, magomvi n.k.

**4-Kujiepusha Na Shirki**

Shirki ni jambo linalobatilisha 'amali za mwana Aadam kwa hivyo itakuwa ni khasara kubwa mno kupoteza muda wako, gharama, tabu na mashaka kukosa malipo ya Hajj. Anaonya Allaah ( سبحانه وتعالى):

﴿ لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ ٱلْخَـٰسِرِينَ ﴿٦٥﴾ ﴾

**(("Ukifanya shirki bila shaka zitaporomoka 'amali zako na bila shaka utakuwa miongoni mwa waliokhasirika"))**[88]

Ni muhimu kabisa kuhakikisha kwamba humshirikishi Allaah ( سبحانه وتعالى) na jambo lolote katika 'ibaadah zako. Miongoni mwa yanayotendeka ya shirki ni kuomba du'aa kwa kumuita asiyekuwa Allaah (سبحانه وتعالى) amtakabalie, au kugusa kuta za *Al-Ka'bah*, za Masjid au kaburi la Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) na kujipangusa mwilini. Au kuelekea makaburi kuomba du'aa au kuitakidi jambo fulani au kitu fulani kina manufaa nawe.

**5-Kuhifadhi 'Amali Kutokana Na Maasi Na Dhulma**

Muislamu anapaswa kujiepusha na aina zote za maasi; uongo, kutotazama wanawake na wanawake kutokutazama wanaume. Wanaume kutokuwagusa wanawake makusudi kubishana katika biashara, kujiepusha na mijadala na upuuzi wowote, kupiga soga n.k.

---

[88] Az-Zumar (39: 65).

Tahadhari kumdhulumu mtu; kumsukuma, kumuumiza kwa vyovyote, kumpiga, kumtusi, kumvunjia heshima yake kwa njia yoyote, kumuibia mali yake, kughushi, kumsengenya, kumkejeli, istihizai, kumcheka n.k. Hayo yote ni dhulma inayoharibu 'amali za mtu. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ameonya aliposema:

***((Je, mnamjua muflis?))*** *Wakasema [watu]: "Muflis kwetu sisi ni yule miongoni mwetu asiyekuwa na dirhamu [pesa] wala vyenye kumnufaisha yeye hapa duniani." Akasema (صلى الله عليه وآله وسلم)* ***((Hakika muflis katika Ummah wangu ni yule atakayekuja Siku ya Qiyaamah na Swalaah, Swawm na Zakaah, lakini amemtusi huyu, amemsingizia huyu mwingine kuwa amezini, amekula mali ya huyu, amemwaga damu ya mwingine na kumpiga mwengine. Thawabu zake zitapatiwa huyu na yule mpaka zimalizike. Na zinapokwisha basi madhambi ya hao [aliowadhulumu] atabandikwa nayo, kisha aingizwe Motoni))***.[89]

**6-Jizidishie Elimu**

Kuwa karibu na watu wema na wenye elimu ili uweze kufaidika nao katika mafunzo yanayohusu Hajj na mengineyo yatakayokufaa Aakhirah. Hudhuria darsa Misikitini unufaike kwa elimu. Wenye elimu waandae darsa watakapokuwa *Minaa*, darsa za mafunzo mbali mbali yakiwemo Fiqh ya Hajj, kuamrishana mema na kukatazana maovu.

**7-Kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى)**

Fanya jitihada kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) wakati wote kwa kuomba maghfirah na tawbah, kuomba du'aa, kuleta *tasbiyh, tahmiyd, tahliyl, takbiyr*, kusoma Qur-aan, kumswalia Nabiy(صلى الله عليه وآله وسلم), n.k.

**8-'Ibaadah Za Naafilah n.k.**

Jitahidi ujichumie thawabu maradufu kwa kufanya 'ibaadah ziada za Sunnah; kuswali kila unapopata fursa ukiwa Masjid Al-

---

89 Muslim.

Haraam na Masjid An-Nabawiy kwani fadhila zake ni maradufu.[90] Swalaah ya Adhw-dhwuhaa, Swalaah zilizo Muakkadah na zisizo Muakkadah, Swalatul-Witr, Tahajjud, kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) baada ya Swalaatul-Fajr mpaka jua lichomoze kisha uswali rakaa mbili ambayo thawabu zake ni kama za Hajj na 'Umrah. Ukiweko muda mrefu huko funga Swawm za Sunnah, toa swadaqah na kutenda kila aina ya wema kwa wenzako.

[90] Tazama Mlango wa "Fadhila Za Hajj Na 'Umrah."

## 11- Nasaha Za Afya

### 1-Usafi

Usafi ni alama ya iymaan. Ahaadiyth kadhaa zimesisitiza kuhusu usafi wa kiwiliwili cha mtu na kuweka mazingira katika hali ya usafi:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ (رضي الله عنه) قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ (صلى الله عليه وسلم): ((**الإِيمَانُ بِضْعٌ وَسَبْعُونَ**)) أَوْ ((**بِضْعٌ وَسِتُّونَ شُعْبَةً, فَأَفْضَلُهَا قَوْلُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ, وَأَدْنَاهَا إِمَاطَةُ الأَذَى عَنْ الطَّرِيقِ, وَالْحَيَاءُ شُعْبَةٌ مِنْ الإِيمَانِ**)) متفق عليه.

Imepokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) amesema: Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: *((**Iymaan ni sabiini na kitu**[91]))* *au alisema ((**Tanzu sitini na kitu. Ilio bora kabisa ni kauli ya 'Laa ilaaha illa-Allaah', na ya chini kabisa ni kuondosha taka njiani. Na kuona hayaa ni utanzu katika tanzu za Iymaan**)).*[92]

Imepokewa kutoka kwa Abu Dharr (رضي الله عنه) kwamba Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: *((**Nilionyeshwa 'amali za Ummah wangu, nzuri na mbaya. Nikapata katika 'amali zao nzuri ni udhia unaoondoshwa njiani. Na nikapata katika 'amali zao mbaya kohozi linaloachwa Msikitini pasi na kuzikwa**)).*[93]

Bali maonyo makali ya kulaaniwa pindi mtu asipotekeleza amri hii:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ (رضي الله عنه) أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((**اتَّقُوا اللَّعَّانَيْنِ**)) قَالُوا: وَمَا اللَّعَّانَانِ يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ قَالَ: ((**الَّذِي يَتَخَلَّى فِي طَرِيقِ النَّاسِ أَوْ فِي ظِلِّهِمْ**)) مسلم

Imepokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Jilindeni** [jiepusheni]* ***na sehemu mbili zinazopelekea mtu kulaaniwa))***. [Maswahaba]

---

[91] "*Bidhw'*" ni idadi baina ya tatu na tisa.
[92] Al-Bukhaariy na Muslim.
[93] Muslim.

Wakauliza: Ni sehemu zipi hizo zinazopelekea mtu kulaaniwa? Akasema: ((***Ni mtu kufanya haja katika njia wanazopita watu au katika vivuli wanavyoketi***)).[94]

Kwa hivyo, huna budi kuusafisha moyo wako, kiwiliwili chako, chakula chako, kinywaji chako pia pahala pa 'Ibaadah. Vile vile wahimize watu wengine kufanya usafi hasa unapomaliza kujisaidia msalani.

Hakikisha unachunga sana jambo hili kwani isijekuwa wewe ni sababu ya wenzio kukirihika, kuudhika au kudhurika kutokana na uchafu wako. Jiepushe na kuwaudhi watu kwa njia yoyote ile ukizingatia uko katika 'Ibaadah tukufu na mahali patukufu. Kumbuka kuwa Muislamu hatakiwi kumdhuru Muislamu mwenziwe.

**2-Maji**

Kunywa maji masafi mengi khasa siku za joto kunapokuwa na uwezekano wa kwenda msalani kila mara. Nufaika kwa kunywa maji ya Zamzam kwa wingi.

**3-Chakula**

Fuata maelekezo yafuatayo ili uwe na mpangilio mzuri wa kula.

- Jiepushe na kula chakula kingi kwa sababu si katika kujijenga afya njema na pia haisaidii katika kutekeleza 'Ibaadah bali itakutia uvivu.

- Vyakula bora vya kuliwa ni matunda, na vinywaji bora ni maji na juisi freshi; vinapatikana kila pahala kwa bei rahisi.

- Jiepushe na kula vyakula vya mafuta mafuta ili kujiepusha na usumbufu wa matumbo na pia itakusaidia kuwa mwepesi wa kufanya 'Ibaadah, na kuweza kuhimili harakati zako.

- Jitahidi kuagiza chakula utakachoweza kumaliza, na endapo kimekushinda kumaliza na hakuna wa kukusaidia, basi kihifadhi ukile baadae badala ya kukitupa. Kutupa chakula ni israafu.

[94] Muslim.

**4-Matibabu**

Tembea na dawa zako ambazo ni muhimu kwako kuzitumia. Pia unaweza kupata huduma za matibabu kwenye sehemu zote za 'ibaadah.

**5-Hifadhi Ya Joto Kali**

Jihadhari na kukaa sehemu zenye joto kali. Jiepushe kupigwa na jua kwa muda mrefu. Chukua mwavuli na vinywaji vya kutosha.

**6-Huduma Kwa Wasiojiweza**

Huduma maalumu zinapatikana kwa walio dhaifu, wagonjwa, wasiojiweza, na wazee. Viti na vitanda vya kubebea vinakodishwa kwa wale wanaohitajia. Uliza wasimamizi wa huduma hizi ndani ya Msikiti. Wakati mwengine huduma hii hupatikana bure, lakini kwa kawaida hupatikana kwa bei rahisi. Faidika na huduma hizi pindi ukizihitajia.

## 12- Yanayowahusu Wanawake

Mlango huu ni mas-alah yanayowahusu wanawake, ingawa mengineyo yametangulia kutajwa kwa ufupi katika sehemu husika za kitabu hiki.

### 1-Mahram

Mwanamke lazima awe na mahram wake ili aweze kwenda kutekeleza Hajj. Wala haipasi kudanganya kabisa kwa kupanga mume au kaka au mjomba n.k. ili kudanganya serikali kwamba una mahram na hali huna uhusiano naye wowote! Itambulike kwamba Wanachuoni wetu wamefutu kwamba kuwa na mahram ni mojawapo wa sharti ya kuwajibika Hajj kwa mwanamke. Hivyo basi asiyekuwa na mahram anaingia katika wale waliokusudiwa kuwa hawana uwezo wa kutekeleza Hajj. Makatazo katika Hadiyth zifuatazo za Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) yanathibitisha jambo hili:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: **((لَا يَحِلُّ لِامْرَأَةٍ تُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ أَنْ تُسَافِرَ مَسِيرَةَ يَوْمٍ وَلَيْلَةٍ لَيْسَ مَعَهَا حُرْمَةٌ))**

Imepokelewa toka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) amesema: Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Haimpasi mwanamke anayemwamini Allaah na Siku ya Mwisho kusafiri mwendo wa mchana na usiku bila ya mahram))***[95]

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: **((لَا يَخْلُوَنَّ رَجُلٌ بِامْرَأَةٍ إِلَّا مَعَ ذِي مَحْرَمٍ))** فَقَامَ رَجُلٌ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ امْرَأَتِي خَرَجَتْ حَاجَّةً وَاكْتُتِبْتُ فِي غَزْوَةِ كَذَا وَكَذَا قَالَ: **((ارْجِعْ فَحُجَّ مَعَ امْرَأَتِكَ))**

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Mwanamume na mwanamke wasiwe faragha bila ya kuweko mahram)).*** Akasema mtu mmoja: "Ee Rasuli wa Allaah. Mke wangu ametoka kwenda Hajj nami

[95] Al-Bukhaariy, Muslim, Ahmad.

nimejaaliwa kwenda vita kadhaa wa kadhaa". Akasema: ***((Rudi uende kuhiji na mkeo))***[96]

Serikali ya Saudia imetoa ruhusa mwanamke aliyefikia umri wa miaka 45 kutekeleza Hajj maadam anafuatana na kikundi cha watu wanaopeleka Mahujaji Hajj kwa sharti apate ruhusa ya kimaandishi kutoka kwa Mahram wake; mumewe, mwanawe wa kiume au kaka yake. Barua hiyo iwe rasmi iliyogongwa muhuri wa Baraza au Kamati inayotambulika ambayo inasimamia mambo ya Dini.

**2-Hijaab**

Mwanamke Muislamu lazima ajisitiri kwa vazi la hijaab wakati wote. Vazi liwe la kujifunika sehemu zote za mwili wake isipokuwa uso na viganja.[97] Miguu ya mwanamke, mpaka sehemu za nyayo pia zinapaswa kufunikwa, na ikiwa si wepesi kuvaa nguo ndefu mno itakayofunika mpaka kwenye nyayo, inabidi mwanamke avae soksi. Ajifunike hivyo mpaka katika Swalaah. Wanawake wengi wameghafilika nalo jambo hili, huswali miguu iko wazi. Itambulike kwamba sharti ya Swalaah kwa mwanamke ni kujisitiri sehemu zote isipokuwa uso na viganja vya mikono. Pia picha za paspoti lazima ziwe za kuvaliwa hijaab. Masharti ya nguo za hijaab ni yafuatayo:

- Ajifunike jilbaab au khimaar inayofunika mwili wote isipokuwa uso na viganja.
- Nguo isiwe yenye kuvutia kwa mapambo au rangi mbali mbali. Inampasa mwanamke kuvaa 'abaayah wakati wote anapotoka nje.
- Isiwe yenye kubana mwili hadi ikadhihirisha umbo lake, bali iwe pana.
- Isiwe nyepesi hadi kudhihirika mwili na kilichovaliwa ndani.
- Isiwe yenye kufanana na vazi la mwanamume au makafiri.
- Vazi lisiwe ni la kujionyesha au kujifakharisha.
- Lisipakwe manukato.

---

[96] Al-Bukhaariy na Muslim.

[97] Wanachuoni wametofautiana kuhusu kufunika uso na viganja, lakini rai yenye nguvu ni kuwa hata uso na viganja viwe vimefunikwa.

Pia asiwe mwenye kujilaza ovyo ovyo Msikitini na maeneo mengineyo huku wanaume wakimpitia kwani huenda akawa hajastirika vizuri akadhihirisha umbo la mwili wake.

**3-Kuvaa Soksi**

Mwanamke anaruhusuiwa kuvaa soksi, bali ndivyo inavyopendekezwa ikiwa ‘abaayah lake halimfuniki mpaka miguuni kabisa katika nyayo. Kuvaa soksi kutakusaidia kufanya *Mas-hul-khuffayn* ukiwa safarini hasa katika ndege.

**4-Yanayohusu Ihraam Ya Wanawake:**

**i-Kuingia katika Ihraam ukiwa katika hedhi**

Mwanamke mwenye hedhi anapaswa aingie katika *Ihraam* kwa sababu *twahaarah* si sharti la kuingia katika Ihraam. Ikiwa ametia niyyah ya *Tamattu’* kisha ikamfikia hedhi na ikawa siku zilobakia ni chache kufika tarehe 8 Dhul-Hijjah, anaruhusika kubadili niyyah yake kuingia katika Hajj ya Al-Qiraan. Atekeleze ‘ibaadah zote za Hajj isipokuwa *Twawaaf* na *As-Sa’-y*. Kwa maana atakwenda *Minaa*, atasimama *‘Arafah*, atalala *Muzdalifah*, atarusha vijiwe *Jamaraat* kisha atakapotwaharika arudi Makkah kufanya *Twawaaful-Ifaadhwah* na *As-Sa’-y*. Dalili ni Hadiyth ifuatayo:

عَنْ عَائِشَةَ (رضي الله عنها) قَالَتْ: خَرَجْنَا مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَا نَذْكُرُ إِلَّا الْحَجَّ, فَلَمَّا جِئْنَا سَرِفَ طَمِثْتُ فَدَخَلَ عَلَيَّ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَأَنَا أَبْكِي فَقَالَ: ((**مَا يُبْكِيكِ؟**)) قُلْتُ: لَوَدِدْتُ وَاللَّهِ أَنِّي لَمْ أَحُجَّ الْعَامَ. قَالَ: ((**لَعَلَّكِ نُفِسْتِ؟**)) قُلْتُ: نَعَمْ. قَالَ: ((**فَإِنَّ ذَلِكِ شَيْءٌ كَتَبَهُ اللَّهُ عَلَى بَنَاتِ آدَمَ, فَافْعَلِي مَا يَفْعَلُ الْحَاجُّ غَيْرَ أَنْ لَا تَطُوفِي بِالْبَيْتِ حَتَّى تَطْهُرِي**))

Kutoka kwa ‘Aaishah (رضي الله عنها) amesema: “Tulitoka pamoja na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) kutekeleza Hajj, tulipofika Sarifa nikapata hedhi. Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) aliingia kwangu nikiwa nalia. Akauliza: ***((Nini kikulizacho?))*** Nikajibu: “Yalaiti nisingelikuja kufanya Hajj mwaka huu”. Akasema: ***((Isijekuwa umepata hedhi?))*** Nikajibu: “Ndio”. Akasema: ***((Hilo ni jambo Allaah***

***Amewaandikia mabinti wa Aadam, kwa hiyo fanya yote wanayofanya Mahujaji isipokuwa usitufu Al-Ka'bah mpaka utwaharike))***[98]

Pia anaruhusika wakati huo wote kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa*; istighfaar, tasbiyh, tahmiyd, tahliyl, takbiyr,* kusoma Qur-aan[99], tarjama ya Qur-aan, kuomba du'aa n.k.

Itambulike kwamba kuingia katika Ihraam ni kitendo cha *waajib* katika Hajj na asipofanya hivyo akapita *Miyqaat* bila ya kuingia Ihraam, itambidi arudi *Miyqaat* ili aingie katika Ihraam. Na asiporudi *Miyqaat* kuingia katika Ihraam itambidi alipe *kaffaarah* yake kwa sababu amekosa kutimiza kitendo cha waajib.

**ii- Kutokujifunika Uso Na Kutokuvaa Glavu**

Mwanamke anapoingia tu katika Ihraam hapaswi kujifunika uso kwa 'niqaab' au 'burqah' kwa sababu imekatazwa na Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

**((لَا تَنْتَقِبُ الْمَرْأَةُ الْمُحْرِمَةُ وَلَا تَلْبَسُ الْقُفَّازَيْنِ))**

***((Mwanamke katika Ihraam asivae Niqaab wala glavu))***[100]

Mwanamke akifanya hivyo juu ya kwamba ameshatambua kuwa ni kosa, yaani amefanya ukaidi, itambidi alipe *kaffaarah* ambayo ni mbuzi mmoja agaiwe kwa maskini wa Makkah.

Lakini wanapokuweko wanaume mbele yake, anapaswa kujifunika uso kwa ghashwah[101] au kuangusha ushungi au mtandio mwepesi usoni mwake, lakini zisiwe zenye kubana uso wake kama vile niqaab au burqah. Hivyo ndivyo hali za Swahabiyaat ilivyokuwa katika Ihraam kama ilivyo dalili katika Hadiyth ya 'Aaishah (رضي الله عنها)

[98] Al-Bukhaariy na Muslim.
[99] Baadhi ya Wanachuoni wamejuzisha kusoma na baadhi wamekataza.
[100] Al-Bukhaariy.
[101] Mtandio au shungi jepesi la kufunika uso bila ya kubanika uso.

"كَانَ الرُّكْبَانُ يَمُرُّونَ بِنَا وَنَحْنُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مُحْرِمَاتٌ, فَإِذَا حَاذَوْا بِنَا سَدَلَتْ إِحْدَانَا جِلْبَابَهَا مِنْ رَأْسِهَا عَلَى وَجْهِهَا فَإِذَا جَاوَزُونَا كَشَفْنَاهُ"

"Wapandaji vipando vya safari walikuwa wakitupitia tulipokuwa katika Ihraam pamoja na Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم). Walipotukaribia tuliteremsha jilbaab zetu kufunika nyuso zetu, na walipoondoka tulijifunua."[102]

**iii- Manukato**

Mwanamke ni haram kwake kujitia manukato kwa hali yoyote ile anapotoka nje ya nyumba yake. Pia anapoingia katika Ihraam haimpasi kujitia manukato ya aina yoyote yale mwilini au katika nguo zake. Kwa hiyo hata sabuni, shampoo, vitia harufu nzuri kwapani n.k. zinatakiwa zitumike zile sizizo na manukato.

**iv- *Talbiyah***

Mwanamke haimpasi kutamka *Talbiyah* kwa sauti, bali atamke pole pole bila ya kusikika sauti yake na asiyekuwa mahram wake.

**v- Kutumia Dawa Kuzuia Hedhi**

Wanachuoni wamekubaliana kwamba mwanamke anayetaka kwenda Hajj anaweza kutumia dawa za kuzuia hedhi kwa sharti kwamba haitomletea madhara. Wamekubaliana hivyo kwa sababu ya umbali wa safari hii, tabu, mashaka, na gharama inakhofiwa kwamba mwanamke afike huko kisha ashindwe kutekeleza fardhi ya Hajj.

**5- Kujiingiza Katika Zahma**

Ingawa jambo hili limekatazwa hata kwa wanaume, ila kwa wanawake huwa ni baya zaidi kwa vile wao ni dhaifu na haipendezi kabisa wanawake kusukumana. Pia wanahitaji kusitirika kutokugusana, kutokusukumana na wanaume. Kwa hiyo

[102] Abu Daawuwd, na Al-Albaaniy ameihakikisha kuwa Swahiyh.

mwanamke ajiepushe mbali kuingia katika zahma. Sehemu kuu za zahma ni kwenye *Al-Ka'bah* kutaka lazima mtu aliguse *Al-Hajar Al-As-wad* au kugusa *Al-Ka'bah*. Pia katika Masjid An-Nabawiy wakati wa kwenda *Ar-Rawdhwah* huweko zahma kubwa wanawake husukumana hadi kupigana na kutukanana. Kufanya hivyo ni katika madhambi, na huenda mtu akaharibu Hajj yake kwa madhambi kama haya kwani yanahusiana na dhulma kwa watu kuvunjiana heshima, kuumizana n.k. Inatosha kabisa kuswali mahali popote katika Masjid An-Nabawiy au sehemu inayofunguliwa kwa ajili ya wanawake waingie *Ar-Rawdhwah*. Kumbuka kwamba kila unapomcha Allaah (سبحانه وتعالى) katika 'ibaadah zako ndipo ujira unathibiti na Hajj yako inakuwa haina kasoro, kwani niyyah pekee inatosheleza maadamu hakuna uwezekano wa mtu kufikia sehemu kutokana na zahma.

### 6- *Ar-Raml* Na *Ar-Rakdhw*[103]

Mwanamke haimpasi kufanya *Ar-Raml* katika *Atw-Twawaaf* na *ar-rakdhw* katika *As-As-Sa'-y* kwa sababu hiyo ni Sunnah inayowahusu wanaume pekee.

### 7- Kukata Nywele

Wanawake wengi hukata nywele zao baada ya kumaliza *As-Sa'-y* mbele za watu katika jabali la *Al-Mar-wah* au pembeni mwake huku wanaume wanapita mbele yao. Haiwezekani kabisa kutokuweko wanaume sehemu hiyo kutokana na wingi wa Mahujaji, kwa hiyo ni vyema mwanamke asubiri hadi atakapofika hotelini ndio akate nywele zake kwani haifai kabisa nywele za mwanamke kuonekana na asiyekuwa mahram.

### 8- *Muzdalifah* Na *Jamaraat*

Wanawake wameruhusiwa kutekeleza *Jamaraat* kabla ya kufikia Alfajiri na inapokuwa zahma au hali ya kutokumwezesha kwenda *Jamaraat*, wameruhusiwa kuchelewesha hadi usiku. Imeruhusika kumpa mtu akurushie kwa dharura, kama kwa wagonjwa au wazee wasiojiweza.

[103] Kukimbia katika *As-Sa'-y*.

**9- Kuzuru Makaburi**

Suala hili ni miongoni mwa waliyokhitilafiana Wanachuoni; wengi wakiona kuwa haifai mwanamke kuzuru makaburi, na baadhi wameona kuwa hakuna ubaya wanawake kuzuru makaburi ikiwa mwanamke hatozuru sana makaburi kwa sababu ya makatazo ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

**عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ (رضي الله عنه) أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَعَنَ زَوَّارَاتِ الْقُبُورِ**

Imepokelewa toka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kwamba: "Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amelaani wanawake wanaozuru sana makaburi."[104]

**10- *Twawaaf Al-Wadaa'i***

Mwanamke akiwa katika hedhi haiwajibiki kwake kutekeleza *Twawaaf Al-Wadaa'i* kutokana na dalili ifuatayo:

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ: **"أُمِرَ النَّاسُ أَنْ يَكُونَ آخِرُ عَهْدِهِمْ بِالْبَيْتِ إِلَّا أَنَّهُ خُفِّفَ عَنْ الْحَائِضِ"**

Kutoka kwa ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) amesema: "Wameamrishwa watu iwe jambo lao la mwisho kutekeleza ni (kutufu) *Al-Ka'bah* isipokuwa imesahilishiwa kwa wanawake wenye hedhi."[105]

[104] Ahmad, At-Tirmidhiy, Ibn Maajah.
[105] Al-Bukhaariy na Muslim.

## 13- *Miyqaat*

*Miyqaat* ni mipaka iliyoko sehemu nne inayozunguka Makkah. Yeyote atakayeivuka bila ya kuingia katika Ihraam atakuwa hakutimiza moja wa nguzo za 'Umrah na Hajj, itabidi arudi kwenye *Miyqaat* ili ahirimie huko. Akishindwa hivyo basi Wanachuoni wengi wameona kwamba itabidi alipe *kaffaarah* ya kuchinja na kugawa nyama yake kwa masikini wa Makkah kwa sababu ameacha kutekeleza kitendo cha waajib.

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alidhihirisha mipaka hiyo kama ifuatavyo:

عَنْ إِبْنِ عَبَّاسٍ (رضي الله عنهما): أَنَّ رَسُولَ اللهِ صلى الله عليه وسلم وَقَّتَ لأَهْلِ الْمَدِينَةِ: ذَا الْحُلَيْفَةِ. وَلأَهْلِ الشَّامِ: الْجُحْفَةَ .وَلأَهْلِ نَجْدٍ: قَرْنَ الْمَنَازِلِ. وَلأَهْلِ الْيَمَنِ: يَلَمْلَمَ هُنَّ لَهُنَّ وَلِمَنْ أَتَى عَلَيْهِنَّ مِنْ غَيْرِهِنَّ, مِمَّنْ أَرَادَ الْحَجَّ أَوْ الْعُمْرَةَ. وَمَنْ كَانَ دُونَ ذَلِكَ: فَمِنْ حَيْثُ أَنْشَأَ, حَتَّى أَهْلُ مَكَّةَ مِنْ مَكَّةَ.

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba: "Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) ameweka *Miyqaat* kwa ajili ya watu wa Madiynah kuwa ni *Dhal-Hulayfah*. Watu wa Shaam ni *Al-Juhfah*. Watu wa Najd ni *Qarnal-Manaazil* na watu wa Yemen ni *Yalmama*. *Miyqaat* hizo ni kwa ajili ya wenyeji wa huko na wengineo wenye kuzipita kwa anayetaka kufanya Hajj au 'Umrah. Na anayeishi katika maeneo hayo anaweza kuingia Ihraam katika sehemu anayoanzia hata watu wa Makkah waanze Ihraam zao kuanzia Makkah."[106]

Kwa maana kuwa, ukiwa unatoka Afrika Mashariki sehemu yako ya kuhirimia ni *Yalamlam* kama unaelekea Makkah moja kwa moja. Lakini ikiwa mathalani Mahujaji watakwenda Madiynah kwanza kwa ajili ya kuzuru Msikiti wa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kisha ndiyo baadaye waende Makkah kwa ajili ya Hajj, hapo sehemu ya kuhirimia itakuwa ni ile ya watu wa Madiynah yaani *Dhul-Hulayfah* na si ile ya kawaida waliopangiwa yaani *Yalamlam*.

[106] Al-Bukhaariy.

| *Miyqaat* | Eneo Na Umbali Wake (takriban) | Mahujaji Kutoka |
|---|---|---|
| *Dhul-Hulayfah* | Kilo mita 450 Kaskazini ya Makkah (Kilomita 10 nje ya Madiynah) | Mahujaji wa kutoka Madiynah na Kaskazini. |
| *Dhaat-'Irq* | Kilo mita 94 Kaskazini-Mashariki ya Makkah | Mahujaji wa kutoka pande za Iraq. |
| *Qarn Al-Manaazil* | Kilomita 94 Mashariki ya Makkah. | Najd. |
| *Yalamlam (As-Sadi'ah)* | Kilomita 54 Kusini ya Makkah | Hii ni kwa ajili ya watu wanaotoka Yemen na pande za Kusini. (Afrika Kusini, Nigeria, Afrika Mashariki, Afrika ya Kati). |
| *Al-Juhfah* | Kilomita 197 Kaskazini Magharibi ya Makkah karibu na mji wa Rabiygh | Mahujaji kutoka Shaam (Syria, Jordan, Palestina, Egypt na pande hizo. Vilevile USA, Canada na UK). |




**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Mahujaji wengine wanavuka *Miyqaat*, kituo kilichoteuliwa kwa ajili kuhirimia katika njia za msafara wao bila ya kuwa katika Ihraam hapo. Wanaendelea hadi wanafika Jeddah au sehemu nyingine katika mipaka ya vituo ambako huko ndio wanaingia katika Ihraam. Hivi ni kinyume na amri ya Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) ambayo inaamrisha kuwa kila Haaj anapaswa ahirimie katika *Miyqaat* iliyoko katika njia ya msafara wake. Inapomtokea mtu hivyo, ni lazima arudi katika *Miyqaat* yake, aingie katika Ihraam. Au

itambidi afanye *kaffaarah* kwa kuchinja kondoo atakapokuwa Makkah na kuigawa nyama yote kuwalisha masikini. Hii inawahusu Mahujaji wote, wanaopita *Miyqaat* wakiwa wamesafiri kwa njia ya angani, baharini au nchi kavu.

- Baadhi ya Mahujaji wanaosafiri kuingia Jeddah, wanaingia Ihraam Jeddah wakidhania kuwa ni *Miyqaat*. Haipasi kabisa kwani ni kuvunja kanuni ya Ihraam. Anayeingia katika Ihraam Jeddah, ni wakazi wake pekee wanaotakiwa kuingia Ihraam majumbani mwao. Mahujaji hutangaziwa wakiwa angani, dakika chache kabla ya kufikia mpaka wa *Miyqaat* ili watie niyyah zao za Ihraam.

- Kutoka nje ya *Miyqaat* kila siku kwa ajili ya kufanya 'Umrah. Ingawa inaruhusiwa, ila inasababisha zahma kuzidi katika Masjidil-Haraam kwenye *Twawaaf* na *As-Sa'-y*.

## 14- Ihraam

### 1-Maana ya Ihraam

Maana ya Ihraam kilugha: ni haraam, yaani ni jambo lililoharamishwa.

Kiistilahi: Ni kuweka niyyah ya kuingia katika 'ibaadah ya Hajj au 'Umrah; kwa maana mtu anapoazimia kutekeleza 'Umrah au Hajj akaanza taratibu zake *Miyqaat* na kutamka *Talbiyah*, huwa ameshaingia katika Ihraam na kwa hivyo kuna baadhi ya vitendo huwa ni haraam kwake kuvitenda, hadi atakapojitengua na Ihraam.

Muislamu anapoazimia kufanya 'Umrah au Hajj lazima ahirimu kabla ya kuvuka '*Miyqaat*.' Kwani hapa ndipo panapoanzia taratibu za 'Umrah na Hajj. Kufanya ghuslu na kuvaa nguo pekee haimaanishi kwamba mtu ameshaingia katika Ihraam, na ingawa shuka mbili zinaitwa 'Ihraam' lakini sharti ya kuingia Ihraam ni lazima ahirimu *Miyqaat*. Anayeingia katika Ihraam huitwa 'Muhrim'.

Wanaosafiri kwa gari wakataka kuingia Makkah, lazima wasimame *Miyqaat* zao ikitegemea nchi wanazotokea. Wanaosafiri kwa ndege kufikia Makkah kupitia Jeddah kutekeleza 'Umrah kwanza kabla ya kwenda Madiynah, wanahirimia ndani ya ndege. Kwa hiyo wanatakiwa wajitayarishe kuingia katika Ihraam kufanya *ghuslu* kabisa tokea nyumbani. Wanawake wavae nguo zao nyumbani. Wanaume huvaa katika ndege wakipenda au huvaa kabisa tokea nyumbani. Kawaida inatangazwa kwenye ndege inapokaribia *Miyqaat*. Ni vyema wanaume waharakize kuvaa shuka zao za Ihraam na pia kutia niyyah moyoni kabisa kwani huenda ikawapita *Miyqaat* bila ya kujua, jambo litakalokalifisha kulipa *kaffaarah* hapo Makkah. Itambulike kwamba ni makosa kutokuhirimia kabla ya Miyqaat ukashuka kiwanjani bila ya kuhirimia au hadi ukafika Makkah. Ukifanya kosa hili, basi inakupasa kurudi *Miyqaat* ili uingie katika Ihraam, na ukishindwa, basi hukmu yake itakuwa ni utoe fidia ya kuchinja mnyama ukifika Makkah na uwagawie masikini wa Makkah na wala huruhusiwi kumla mnyama huyo wala kuwapa matajiri kwa kuwa ni mnyama wa *kaffaarah* ambaye anatakikana aliwe na masikini tu.

**Kujitayarisha Kabla Ya Kuingia Katika Ihraam**

- Kukata kucha zote.
- Kunyoa nywele za kwapani na sehemu za siri.
- Kuchana nywele vizuri ili zisitoke nyingi unapofanya ghuslu.
- Kukata, kupunguza masharubu. Ndevu ziachwe bila ya kukatwa au kupunguzwa.
- Kununua nguo za Ihraam mapema. Ni vyema kuchagua iliyo nzito na si nyepesi kwani inapokuwa joto, hutokwa majasho na kuganda mwilini.
- Wanawake kutumia sabuni, shampoo isiyo na manukato.
- Wanaume kufanya mazoezi ya kuvaa Ihraam na kutembea kidogo ili ahakikishe ameijulia kuivaa isije ikamvuka.
- Ikiwa ni msafiri kwa gari, kuwa na mfuko wa kutilia nguo za Ihraam, sabuni, shampoo na unavyohitaji katika kufanya *ghuslu*. Vyote hivi vitakuwa kwenye begi la mkononi.

**2-Kuoga na kuingia katika Ihraam**

Ukiwa nyumbani au *Miyqaat*, fanya ghuslu, kisha jitie manukato (wanaume pekee). Vaa nguo zako. Wanawake wavae nguo zozote zinazotimiza masharti ya hijaab. Wanawake hawatakiwi kujitia manukato yoyote.

**3-Namna Ya Kuivaa Ihraam kwa Mwanamme**

Shuka mbili nyeupe zinazouzwa tayari. Unaweza kununua mapema kabla ya kusafiri katika nchi yako au pia zinauzwa katika maduka pembezoni ya *Miyqaat*.

Shuka moja inafungwa kiunoni. Inaruhusiwa kuvaa mkanda wa kuwekea pesa kusaidia kuikaza vizuri shuka. Ya pili inatupwa kufunika mabega yote. Unapoanza kufanya *Twawaaf* unatakiwa

uivae kama inavyojulikana kuwa ni '*Idhwtwibaa'* kuwa utafungua upande wa bega la kulia liwe wazi.

**4-Yanayoruhusiwa kuvaa**

Saa, miwani ya macho na ya jua, lenzi ya jicho, viatu, kanda mbili, makubadhi visivyofunika vifundo vya mguu.

**5-Vazi La Ihraam kwa Mwanamke**

Kishariy'ah hakuna vazi maalum kwa mwanamke, bali anatakiwa avae vazi linalotimiza hijaab kishariy'ah.

**6- *Talbiyah***

Baada ya kwishatiya niyyah moyoni, ambayo pia imeshaaingia moyoni tokea ulipoazimia safari ya 'Umrah au ya Hajj, inapendekezeka kuanza *Talbiyah* kwa kumuitikia Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kutaja aina ya Hajj au Umrah unayoitekeleza kama alivyofanya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

عن بَكرِ بنِ عبدِ اللَّهِ المزنيِّ ، قالَ سمعتُ أنسًا ، يحدِّثُ قالَ : سَمعتُ النَّبيَّ صلَّى اللهُ عليْهِ وسلَّمَ يلبِّي بالعمرةِ والحجِّ جميعًا ، فحدَّثتُ بذلِكَ ابنَ عمرَ فقالَ : لبَّى بالحجِّ وحدَه ، فلقيتُ أنسًا فحدَّثتُهُ ، بقولِ ابنِ عمرَ فقالَ أنسٌ : ما تعدُّونا إلَّا صِبيانًا ، سمعتُ رسولَ اللَّهِ صلَّى اللهُ عليْهِ وسلَّمَ يقولُ: ((لبَّيْكَ عُمرةً ، وحَجًّا)) معًا

Imepokelewa toka kwa Bakr bin 'Abdillaah Al-Muzniyy ambaye amesema: "Nilimsikia Anas akihadithia: Nimesikia Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) akitamka *Talbiyah* ya 'Umrah na Hajj kwa pamoja. Nikamhadithia hayo ibn 'Umar". Akasema: "Akatamka *Talbiyah* ya Hajj pekee. Nikakutana na 'Anas nikamhadithia kuhusu kauli ya Ibn 'Umar. Akasema Anas: 'Mnatufanya kama watoto' nimemsikia Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: ***((Labbayka-'Umratan wa Hajjaa)***)[107]

[107] Muslim, Swahiyh Ibn Maajah, Swahiyh Abu Daawuwd, Swahiyh An-Nasaaiy.

| ‘Umrah au aina ya Hajj | *Talbiyah* | Matamashi na maana |
|---|---|---|
| ‘Umrah pekee au ‘Umrah ya Hajj *At-Tamattu’* | لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ عُمْرَةً | ***Labbayka-Allaahumma ‘Umrah***<br><br>Ee Allaah naitikia kutekeleza ‘Umrah. |
| Tarehe 8 utakapokwenda *Minaa* au ikiwa ni Hajj Ya *Al-Ifraad* | لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ حَجًّا | ***Labbayka-Allaahumma Hajjaa***<br><br>Ee Allaah naitikia kutekeleza Hajj. |
| Hajj na ‘Umrah pamoja (*Al-Qiraan*) | لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ عُمْرَةً وَحجًّا | ***Labbayka-Allaahumma ‘Umrah wa Hajjaa***<br><br>Ee Allaah naitikia kutekeleza ‘Umrah na Hajj. |

Ikiwa unamfanyia mtu ‘Umrah au Hajj umtaje jina lake useme kama hivyo ila umalizie:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ حَجًّا عَنْ فَلاَنِ بِنْ فُلاَنِ

***Labbayka-Allaahumma Hajjaa ‘an fulaan bin fulaan***

Fadhila za *Talbiyah:*

عَنْ سَهْلِ بْنِ سَعْدٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: **((مَا مِنْ مُسْلِمٍ يُلَبِّي إِلَّا لَبَّى مَنْ عَنْ يَمِينِهِ أَوْ عَنْ شِمَالِهِ مِنْ حَجَرٍ أَوْ شَجَرٍ أَوْ مَدَرٍ حَتَّى تَنْقَطِعَ الْأَرْضُ مِنْ هَاهُنَا وَهَاهُنَا))**

Imepokelewa toka kwa Sahl bin Sa'd amesema: Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Hakuna Muislamu yeyote anayetamka Talbiyah, isipokuwa kila kilokuweko kuliani au kushotoni kwake; ikiwa ni kutokana na jiwe au mti au udongo vinasoma pamoja naye mpaka ardhi inapoishia huku na kule [kuliani kwake na kushotoni kwake]***))[108]

Kisha endelea kutamka *Talbiyah*

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ, لَبَّيْكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ, إِنَّ الْحَمْدَ, وَالنِّعْمَةَ, لَكَ وَالْمُلْكَ, لاَ شَرِيكَ لَكَ

***Labbayka-Allaahumma Labbayk. Labbayka laa shariyka Laka Labbayk. Innal-Hamda Wan-Ni'imata Laka wal-Mulk laa shariyka Lak.***

"Nimekuitikia Ee Allaah nimekuitika, nimekuitika Huna mshirika nimekuitika, hakika Sifa njema zote na Neema na Ufalme ni Vyako Huna mshirika."

Mwanamume atasema kwa sauti na mwanamke atasema kiasi cha kumsikia wa pembezoni mwake ikiwa ni wanawake wenzake. Dalili ni Hadiyth ifuatayo ya kutoka kwa baba yake As-Saaib bin Khallaad amesema: Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

((أَتَانِي جِبْرِيلُ فَأَمَرَنِي أَنْ آمُرَ أَصْحَابِي أَنْ يَرْفَعُوا أَصْوَاتَهُمْ بِالْإِهْلَالِ وَالتَّلْبِيَةِ))

***((Amenijia Jibriyl akaniamrisha niwaamrishe Maswahaba zangu wapandishe sauti zao katika kuchinja na Talbiyah))***[109]

Anatakiwa mtu kusema *Talbiyah* kila mara khaswa anapofika na kubadilisha kituo. Mfano anapopanda na kushuka kipando wakati wa safari au wakati wa usiku unapoingia na asubuhi kunapopambazuka. Pia Amuombe Allaah (سبحانه وتعالى) Ridhaa Yake ya kupata Jannah na aombe kujikinga kwa Rahmah ya Allaah (سبحانه وتعالى) dhidi ya moto.

[108] At-Tirmidhiy - *Swahiyh At-Tirmidhiy* (828).
[109] At-Tirmidhiy – Ameisahihisha Al-Albaaniy katika Swahiyh At-Targhiyb wat-Tarhiyb (1135).

Anatakiwa mtu aseme *Talbiyah* wakati wa 'Umrah tokea anapovaa Ihraam yake hadi anapoanza *Twawaaf*. Wakati wa Hajj aseme *Talbiyah* kutokea mwanzo wakati anapovaa Ihraam yake mpaka anapoanza kurusha vijiwe *Jamrat Al-'Aqabah* tarehe 10 Dhul-Hijjah (*Yawm An-Nahr*).

| **Yanayoharamishwa Katika Ihraam** | | |
|---|---|---|
| **Wanaume Na Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** |
| Wasikate nywele. Hapana ubaya kukuna kichwa au kuchana nywele na ikiwa zitatoka kwa ajili hiyo hakuna ubaya. | Haifai kujifunika kichwa kama kuvaa kofia, kilemba, ghutrah na kadhalika. Ama kujifunika mwavuli kwa ajili ya kujihifadhi jua hakuna ubaya. Pia hakuna ubaya akibeba begi lake kichwani. | Asivae niqaab na glavu. Kuna Ma'ulamaa waliosema kuwa haifai kujifunika uso wake kwa niqaab au chochote kingine ila kama kuna wanaume karibu yake, basi inambidi ajifunike uso wake kwa ghashwah[110] (kuepusha fitnah). |
| Wasikate kucha. Ikikatika kucha na ikiwa inamuudhi hakuna ubaya kuikata. | Asijitie manukato mwilini, au katika nguo zake baada ya kuingia katika Ihraam. Ama kabla ya Ihraam inafaa (kama ilivyoelezwa mwanzo). Vile vile katika chakula kama kutia zaafarani kwani zaafarani ni katika harufu nzuri. Vilevile | Hawaruhusiwi kabisa kutia manukato ikiwa kabla ya Ihraam au baada yake.<br><br>Vile vile katika chakula kama kutia zaafarani kwani zaafarani ni katika harufu nzuri. Vilevile ajiepushe na kuoga |

[110] Mtandio au shungi jepesi la kufunika uso bila ya kubanika uso.

| | | |
|---|---|---|
| | ajiepushe na kuoga sabuni iliyo na manukato. Hakuna ubaya ikiwa manukato aliyotia kabla ya Ihraam yamebakia katika nguo zake. | sabuni iliyo na manukato. |
| Wasigusane kwa hamu au kubusiana, au kujimai (kitendo cha ndoa). | Asivae nguo zilizoshonwa kama fulana, shati, suruwali, chupi, soksi, viatu na kadhalika.<br><br>Anaruhusiwa kuvaa saa, miwani visaidizi vya kusikia au kuzungumzia. | Avae nguo zake za kawaida ziloshonwa zinazokubalika ki-Shariy'ah. |
| Wasifunge nikaah (ndoa) wala kupeleka posa kwa mwanamke kwa ajili yake au mwenzake. | | |
| Wasivae glavu, lakini hakuna ubaya kufunika mikono kwa nguo yake. | | |
| Wasiwinde, wasikate miti, wasiue wanyama, wadudu. | | |
| Wasifanye maasi yoyote. | | |
| Wasiingie katika | | |

| | | |
|---|---|---|
| mabishano, ugomvi, kutukanana, wala kuongea ya upuuzi n.k. | | |

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Wanawake kudhani kwamba lazima kuvaa nguo nyeupe au kijani au aina nyenginezo. Nguo zozote zile zinafaa kuvaliwa, la muhimu ziwe zenye kumstiri na kutimiza masharti ya hijaab.

- Kulazimika kuswali Rakaa mbili baada ya kufanya ghuslu ya kuingia katika Ihraam. Unapokuwa nyumbani huhitaji kuswali bali unaweza kuswali kwa niyyah ya *Sunnatul-Wudhuw*, na ukiwa uko *Miyqaat* ni kuswali *Tahiyyat Al-Masjid*.

- Kutamka *Talbiyah* kwa pamoja, mmoja anasema na wengine wanafuata. Haipasi hivi kwani ni bid'ah. Kila mtu anatakiwa atamke pekee.

- Wanaume kutokujifunika kichwa (kuvaa kofia) baada ya kufanya *ghuslu* kabla ya kuhirimu. Anaweza mtu kuvaa kofia lakini anapofika *Miyqaat* akahirimu hapo asijifunike kitu kichwani.

- Wanawake kutamka *Talbiyah* kwa sauti, khasa pale wanaume wanapotamka katika mabasi. Mwanamke anatakiwa atamke *Talbiyah* yake kwa sauti ya kujisikia mwenyewe tu (moyoni).

- Kudhania kwamba mtu anapoingia katika Ihraam, hawezi tena kwenda kujisaidia msalani au kula. Bali anaweza mtu kwenda haja ndogo au kubwa kisha akafanya wudhuu wake kama anavyofanya kwa ajili ya Swalaah.

- Kudhania kwamba mtu hawezi kubadilisha nguo zake za Ihraam. Unaweza kuoga na kubadilisha nguo, kwani Ihraam ni niyyah na *Talbiyah* na si nguo.

- Wanawake kujifunika uso kwa niqaab na kuvaa glavu. Haifai hivyo isipokuwa kunapokuwa na fitnah ndipo anaruhusiwa kujifunika uso kwa kuangusha mtandio.[111]

- Kujiwekea kivuli juu ya kichwa akiwa katika gari, basi au khema.

- Wanaume kufunika mabega yote mawili kwa shuka ya juu na hivyo kutokuacha bega la kulia kuwa wazi wakati wa *Twawaaf.*

- Baada ya Twawaaf wanaume kuacha mabega wazi wakidhania ni lazima kuwa hivyo nyakati zote.

- Wanaume kukaa ovyo hadi kuonekana sehemu zao za siri kwa vile hawakuwa wamevaa suruwali ya ndani (chupi).

- Wanaosafiri kwa ndege kutokuhirimia ndani ya ndege ikiwa wanaanza manaasik zao kwa 'Umrah.

[111] Rejea Mlango wa 'Yanayohusu Wanawake.'

### 15- Utekelezaji wa 'Umrah

Endelea kutamka *Talbiyah* ukiwa safarini hadi ufike Masjid Al-Haraam kwa ajili ya kutekeleza taratibu zilobakia za 'Umrah. Ikiwa una mizigo unayohitaji kuiweka hotelini, fanya hivyo. Unaweza kwenda msalani kufanya haja ndogo au kubwa, ukafanya wudhuu, unaweza kula ikiwa umebanwa na njaa. Lakini inapendekezwa kukimbilia kumaliza taratibu za 'Umrah.

**Aina za *Twawaaf***

**Tanbihi:** Sehemu za kutufu zimeongezwa kwa kuwekwa daraja juu kwa sababu ya upanuzi wa Haram, na ni bora zaidi kutufu huko kwa sababu utaweza kutufu kwa sahali kabisa bila ya msongamano na watu na utasaidia kupunguza zahma katika *Twawaaf* ya ardhini, wala haibadili lolote katika kutekeleza kwake wala haiathiri lolote katika kupata thawabu zake. Kwa miaka ijayo hali itakuwa hivyo hadi upanuzi wa Masjid Al-Haraam umalizike ambao sehemu za kutekeleza *Twawaaf* itazidishwa kiasi kikubwa kuweko mizunguko kadhaa ili iwatosheleze watu.

- ***Twawaaf Al-'Umrah***: Ni nguzo mojawapo ya 'Umrah. Ni *Twawaaf* inayotekelezwa na kila aliyeingia Ihraam kwa ajili ya kutekeleza 'Umrah.

- ***Twawaaf Al-Quduwm:*** Ni *Twawaaf* inayotekelezwa na aliyeingia Ihraam kwa ajili ya kutekeleza Hajj ya *Qiraan* au *Ifraad* nayo ni Sunnah kama walivyokubaliana Wanachuoni. Kwa hiyo kuachwa kwake haibatilishi Hajj, lakini inapendekeza kutekelezwa. Ama madhehebu ya Imaam Maalik ni waajib kwa kuwa kachukua dalili ya kauli ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alipoelekea *Al-Ka'bah* akasema: **(*(Chukueni kutoka kwangu manaasik zenu*))**.[112]

- ***Twawaaf Al-Ifaadhwah***: Ni *Twawaaf* inayowapasa Mahujaji wa aina zote za Hajj kuitekeleza pindi watakapomaliza kusimama *'Arafah* na kukesha *Muzdalifah*. Nayo ni nguzo mojawapo ya Hajj, kuiacha kuitekeleza, Hajj haitimii.

- ***Twawaaf Al-Wadaa'i:*** Ni *Twawaaf* ya kuaga inayotekelezwa mwisho kabisa baada ya kumaliza Umrah au Hajj, nayo iwe ni

---

[112] Muslim.

'amali yako ya mwisho kabla ya kuondoka Makkah. Wanachuoni wamekubaliana kwamba hukmu yake ni waajib kwa hiyo atakayeacha kutekeleza atawajibika kufanya *kaffaarah* ya kuchinja. Ama wanawake wenye hedhi au nifaas wao wameruhusika nayo.

- ***Twawaaf At-Tatwawwu'***: *Twawaaf* inayotekelezwa akipenda mtu anapoingia Masjid Al-Haraam kisha aswali rakaa mbili Maqaam Ibraahiym au popote pale.

**Ya kutekeleza unapofika Masjid Al-Haraam**

- Mahujaji anapoingia Msikitini atangulize mguu wake wa kulia na kusoma du'aa ya kuingia Masjid:

أَعُوذُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ, وَبِوَجْهِهِ الْكَرِيمِ, وَسُلْطَانِهِ الْقَدِيمِ, مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ،, (بِسْمِ الله، وَالصَّلاةُ) (وَالسَّلامُ عَلى رَسولِ الله)، اللّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوابَ رَحْمَتِك

***A'uwdhu biLlaahil-'Adhwiym, wabi Wajhihil-Kariym wa-Sultwaanihil-qadiym, minash-shaytwaanir-rajiym (BismiLLaah was-swalaatu) (was-salaamu 'alaa Rasuwli-Llaah) Allaahummaftah-liy abwaaba Rahmatika***

"Najikinga na Allaah Mtukufu, na kwa Wajihi Wake Mkarimu, na kwa utawala Wake wa kale, dhidi ya shaytwaan aliyeepushwa na Rahmah za Allaah (Kwa jina la Allaah na Rahmah na amani zimfikie Rasuli wa Allaah) Ee Allaah nifungulie milango ya Rahmah Yako."

- Niyyah iwekwe moyoni ya aina *Twawaaf* unayotekeleza.

- Anza *Twawaaf* katika *Al-Hajar Al-As-wad*. Libusu ukiweza kupata nafasi na dalili ni Hadiyth ya 'Umar bin Khatwaab (رضي الله عنه) kwamba alilifikia *Al-Hajar Al-As-wad* akalibusu kisha akasema:

"إني أَعْلَمُ أَنَّكَ حَجَرٌ لا تَضُرُّ ولا تَنْفَعُ، وَلَوْلا أَنِّيْ رأيت النبي صلى الله عليه وسلم يُقَبِّلُكَ ما قَبَّلْتُكَ" – البخاري و مسلم

"Hakika mimi najua kwamba wewe ni jiwe usiloweza kudhuru wala kunufaisha, na ingelikuwa sikumuona Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) anakubusu basi nami nisingelikubsu."

- Ikiwa kuna zahma, haipasi kabisa kusukumana na watu kwa ajili ya kubusu *Al-Hajar Al-As-wad*, inatosheleza kulielekea hata ukiwa mbali kisha nyanyua mkono wako wa kulia kuliashiria (*istilaam*) useme:

بِسْمِ اللَّهِ اللَّهُ أَكْبَرُ

***BismiLLaah, Allaahu Akbar***

Kwa Jina la Allaah, Allaah ni Mkubwa.

**Tanbihi**: Usibusu mkono wako kwani si katika Sunnah!

- Utaanza kutufu *Al-Ka'bah* kuanzia pembe ya *Al-Hajar Al-As-wad*.

- Lazima utembee huku *Al-Ka'bah* liko kushotoni mwako. Unapofika *Rukn Al-Yamaaniy* uiguse lakini usibusu. Na utakapokuwa baina yake na *Al-Hajar Al-As-wad* useme:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

***Rabbanaa Aatinaa fid-dun-yaa hasanataw-wafil- Aakiharati hasanataw-waqinaa 'adhaaban-Naar*.**

"Rabb wetu Tupe katika dunia mema na katika Aakhirah [pia Tupe] mema na Tukinge na adhabu ya Moto."[113]

- Kila mara ukilipita *Al-Hajar Al-As-wad* kuanza mzunguko wa pili na kuendelea, unatakiwa useme "*Allaahu Akbar*" huku ukiwa umenyanyua mkono wako wa kulia na kuliashiria, na bila ya kutanguliza kusema '*BismiLLaah*'.

- Katika kufanya *Twawaaf* zilizobakia unaweza kusema unachopenda katika dhikru-Allaah; kusoma Qur-aan, kuleta Istighfaar, du'aa, *tasbiyh*, *tahliyl*, *tahmiyd*, *takbiyr*,

[113] Al-Baqarah (2: 201).

*kumswalia* Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). Hii kwa sababu *Twawaaf, As-Sa'-y* na *Jamaraat* imehusishwa kwa ajili ya kumdhukuru Allaah.

- Katika *Twawaaf* hii wanaume wanahitajia wafanye vitu viwili:

  i. Uweke *Al-Idhwtwibaa'* kutoka mwanzo wa *Twawaaf* mpaka mwisho. *Al-Idhwtwibaa'* ina maana kwamba ni kuweka sehemu ya katikati ya vazi (ridaa) chini ya kwapa lako la kulia na kipande cha ridaa akipitishe juu ya bega la mkono wa kushoto. Unapomaliza kufanya *Twawaaf* unaweza kurudisha ridaa yako katika hali yake ya mwanzo kwa sababu wakati wa *Idhwtwibaa'* ni wakati wa *Twawaaf* tu.

  ii. Kufanya *Ar-Raml* katika *Twawaaf* tatu za mwanzo. *Ar-Raml* ina maana kwamba kuzunguka kwa mwendo wa haraka kwa hatua ndogo ndogo. Kisha unatakiwa utembee mwendo wa kawaida katika *Twawaaf* zako nne za mwisho, na dalili yake ni Hadiyth ya Jaabir (رضي الله عنه)

"أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم لَمَّا قَدِمَ مَكَّةَ أتى الْحَجَرَ فَاسْتَلَمَهُ ثُمَّ مَشَى على يَمِينِهِ فَرَمَلَ ثَلَاثًا وَمَشَى أَرْبَعًا" – مسلم

"Rasuli wa Allaah alipofika Makkah alilifikia *Al-Hajar Al-As-wad* akaliashiria kisha akatembea kuliani mwake akafanya *Ar-Raml* mizunguko mitatu na akatembea (kikawaida) mizunguko minne."[114]

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Kuanza *Twawaaf* katika chanzo kingine kisichokuwa sehemu ya *Al-Hajar Al-As-wad* na hali ni fardhi kuanzia *Twawaaf* hapo.

---

[114] Muslim.

- Kutufu ndani ya eneo la Hijr kutokana na msongamano mkubwa wa watu. Kimsingi hili ni kosa kubwa kwa sababu kishariy'ah, eneo la Hijr liko ndani ya *Al-Ka'bah* na *Twawaaf* inatakiwa iwe nje ya *Al-Ka'bah* na sio ndani ya *Al-Ka'bah*. Kwa hiyo kwa kupita ndani ya Hijr unapotufu unakuwa umetufu katika sehemu ya *Al-Ka'bah* na si *Al-Ka'bah* yote ambayo ndiyo inayotakiwa.

- Kufanya *Ar-Raml* katika *Twawaaf* zote saba na hali *Ar-Raml* inatakikana kufanywa katika mizunguko mitatu tu ya mwanzo.

- Kusukumana na watu na kusababisha zahma, kuwaumiza watu kutaka kulifikia *Al-Hajar Al-As-wad* ili kulibusu. Vitendo kama hivi vinaleta madhara kwa Waislamu na haturuhusiwi kufanya hivyo. Itambulike kuwa *Twawaaf* inabakia kuwa sahihi bila ya kulibusu *Al-Hajar Al-As-wad*.

- Kubusu mkono baada ya kuashiria *Al-Hajar Al-As-wad* unapokuwa mbali nalo, kwani ni kinyume na Sunnah.

- Mahujaji kufuta au kusugua mkono wake katika *Al-Hajar Al-As-wad* akitegemea kupata baraka. Hili ni jambo lisilokuwa na dalili katika shariy'ah ya Kiislam, hivyo ni bid'ah na shirki. Sunnah ni kuligusa tu au kulibusu inapokuweko uwezekano wa kufanya hivyo bila ya tabu yoyote.

- Kugusa pembe nne za *Al-Ka'bah* au kuta zake, kusugua na kujipangusa nayo kwa kutegemea kupata baraka. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) hakugusa sehemu yoyote ya *Al-Ka'bah* isipokuwa *Al-Hajar Al-As-wad* na *Ar-Ruknul-Yamaaniy*.

- Kusoma du'aa zilizotajwa kuwa ni maalumu kwa kila *Twawaaf* moja. Utakuta kuna vijitabu vidogo vidogo vinauzwa vyenye du'aa maalum kwa kila *Twawaaf*. Vitabu hivyo havina mashiko. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) hakueleza bayana du'aa yoyote isipokuwa ni kusema 'Allaahu Akbar' anapofikia *Al-Hajar Al-As-wad* na kila anapomaliza *Twawaaf* moja baina ya *Ar-Ruknul-Yamaaniy* na *Al-Hajar Al-As-wad* akisoma du'aa iliyotajwa juu. Amesema Shaykhul Islaam Ibn Taymiyah (رحمه الله): "Hakuna katika kutufu dhikri au

du'aa maalumu kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم); si kwa amri yake wala kauli yake wala mafunzo yake, bali anachotakiwa mtu ni kuomba du'aa mbalimbali na kile kitajwacho na watu wengi kuwa kuna du'aa maalumu za kuzungukia *Al-Ka'bah* hilo halikuthibiti kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

- Kupandisha sauti ya anayeongoza watu kutufu na wale wanaoongozwa katika hizo du'aa ambazo watu wamejipangia. Kufanya hivyo kunasababisha kubabaisha Mahujaji wengine wanaomdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa pole pole na wanawakosesha *khushuu'*. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى): **((Muombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa khofu, hakika Yeye Hapendi wavukao mipaka)).**[115]

- Kusimama kuomba du'aa baada ya kumaliza *Twawaaf.*

### *Maqaam Ibraahiym*

- Utakapomaliza mizunguko saba ya *Twawaaf*, utakaribia Maqaam Ibraahiym na utasoma:

﴿ وَٱتَّخِذُواْ مِن مَّقَامِ إِبۡرَٰهِـۧمَ مُصَلًّىۖ ﴾

**((Na chukueni kutoka mahali pa kusimama Ibraahiym kuwa ni pahala pa kuswalia**)).[116]

- Utaswali rakaa mbili fupi, ukiwa karibu kiasi iwezekanavyo na nyuma ya Maqaam Ibraahiym. Katika rakaa ya mwanzo utasoma Suratul-Kaafiruwn (Qul yaa ayyuhal-kaafiruwn) na rakaa ya pili utasoma Suratul-Ikhlaasw (Qul-Huwa-Allaahu Ahad) baada ya kuisoma Suratul Faatihah katika kila rakaa.

- Utakapomaliza rakaa mbili, ni Sunnah kuelekea kwenye mifereji ya Zamzam kunywa maji yake. Unapokunywa

---

[115] Al-A'raaf (7: 55).
[116] Al-Baqarah (2: 125).

omba du'aa unayotaka kwani kwa kuyanywa du'aa hutakabaliwa kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

((مَاءُ زَمْزَمَ لِمَا شُرِبَ لَهُ))

***((Maji ya Zamzam kwa (jambo liloombewa) wakati wa kunywa))***.[117]

- Utarudi kuligusa *Al-Hajar Al-As-wad* kama itawezekana. Ikiwa kuna zahma basi hakuna lazima kufanya, bali ni makosa kuingia kusababisha msukumano na watu.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Kujilazimisha kuswali karibu na Maqaam Ibraahiym kunapokuwa kuna zahma za watu. Hivi husababisha maudhi na misongamano ambayo huishia kuumizana na Mahujaji wengine. Inatosheleza kuswali rakaa mbili baada ya kumaliza *Twawaaf* mahali popote nyuma ya Maqaam hata kwa mbali na ikiwa ni zahma hapo basi popote pale katika Masjid Al-Haraam. Hivi itakuepusha kuudhi watu na kuudhiwa na watu na utaweza kuswali kwa unyenyekevu zaidi na utulivu.

- Kuswali zaidi ya rakaa mbili na kusababisha zahma na hali watu wanahitaji nao kutimiza hizo rakaa mbili na mahali panakuwa pa dhiki mno.

[117] Ibn Maajah, Ahmad na Al-Albaanyi ameipa daraja ya Swahiyh katika Swahiyh Ibn Maajah.

**Taratibu Za Kutekeleza Twawaaf Kwa Mukhtasari**




***Asw-Swafaa* Na *Al-Mar-wah***

- Utakwenda *Al-Mas-'aa*, utakapofika karibu na *Asw-Swafaa* utasoma:

﴿ إِنَّ ٱلصَّفَا وَٱلْمَرْوَةَ مِن شَعَآئِرِ ٱللَّهِ ۖ ﴾

**((Hakika *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah* ni katika alama za [Dini ya] Allaah)).**[118]

- Utapanda (kilima cha) *Asw-Swafaa* mpaka uweze kuona *Al-Ka'bah* (ikiwezekana). Elekea *Al-Ka'bah* na nyanyua mikono yako, umtukuze Allaah na useme ifuatavyo kisha uombe du'aa upendayo:

لا إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ وَلَهُ الحَمْدُ وهُوَ عَلى كُلِّ شَيءٍ قَديرٌ، لا إِلَهَ إِلا اللهُ وَحْدَهُ أَنْجَزَ وَعْدَهُ، وَنَصرَ عَبْدَهُ وَهَزَمَ الأَحْزابَ وَحْدَهُ

***Laa Ilaaha Illa-Allaah Wahdahu laa shariyka Lahu, Lahul-Mulku Walahul-Hamdu wa Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr. Laa Ilaaha Illa-Allaahu Wahdahu, Anjaza wa'dahu wa-Naswara 'Abdahu wa-hazamal-ahzaaba Wahdahu***

"Hapana ilaah (muabudiwa wa haki) ila Allaah, Hana mshirika, ni Wake Ufalme na ni Zake sifa njema Naye juu ya kila kitu ni Muweza. Hapana ilaah ila Allaah, hali ya kuwa Peke Yake, Ametekeleza ahadi Yake, na Amemnusuru mja Wake, na Amevishinda vikosi peke Yake."

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alisoma hivi mara tatu na baina yake akiomba du'aa, kisha akafanya alipokuwa *Al-Mar-wah* kama alivyofanya alipokuwa *Asw-Swafaa*[119].

- Kisha teremka *Asw-Swafaa* na elekea *Al-Mar-wah* kwa mwendo wa kawaida mpaka unapofika katika alama ya taa za kijani utafanya *Ar-Rakdhw*. Alama ya kijani inadhihirika juu ya sakafu kwa taa rangi ya kijani. Hapo utakwenda mwendo wa kukimbia mpaka alama hiyo ya taa za kijani zinapomalizikia. Wanawake hawatakiwi kufanya *Ar-Rakdhw*. Endelea kuelekea *Al-Mar-wah* kwa mwendo wa kawaida. Utakapofikia kilima na kuelekea Qiblah, nyanyua mikono na kurudia kusema kama ulivyosema ulipokuwa *Asw-Swafaa*. Kisha teremka *Al-Mar-wah* kuelekea *Asw-Swafaa*, ukihakikisha unatembea

[118] Al-Baqarah (2:158).
[119] Muslim (2/8880).

sehemu zinazohusika na kukimbia katika sehemu zinazohusika.

- Eendelea kufanya hivyo mpaka umalize mizunguko saba. Kutoka *Asw-Swafaa* kwenda *Al-Mar-wah* ni mzunguko mmoja na kurudi ni mzunguko mwengine. Unatakiwa kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) wakati wote wa *As-Sa'-y* kwa kusoma au kusema unachopenda; Qur'aan, du'aa, *Istighfaar, tasbiyh, tahliyl, tahmiyd, takbiyr,* kumswalia Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) n.k.

- Utakapomaliza *As-Sa'-y* utanyoa nywele. Mwanamke utakata nywele kiasi cha urefu wa ncha ya kidole. Kwa wanaume, inapendekezeka kunyoa nywele zote, na kunyoa ni bora kuliko kukata kwani Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliwaombea du'aa Maswahaba walionyoa mara tatu na waliokata mara moja kwa dalili Hadiyth ya 'Abdullaah bin 'Umar (رضي الله عنه) kwamba Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم)alisema:

**((رَحِمَ اللهُ المحلِّقينَ))** قالوا: والمقصِّرينَ يا رسولَ الله؟ قال: **((رحِم اللهُ المحلِّقين))** قالوا: والمقصِّرينَ يا رسولَ الله؟ قال: **((رحِم اللهُ المحلِّقين))** قالوا: والمقصِّرينَ يا رسولَ الله؟ **قال: ((والمقصِّرينَ))** مسلم وغيرهم

***((Allaah Awarehemu walionyoa))*** Wakauliza: "Na waliopunguza ee Rasuli wa Allaah?" Akasema: ***((Allaah Awarehemu walionyoa))*** Wakauliza: "Na waliopunguza ee Rasuli wa Allaah?" Akasema: ***((Allaah Awarehemu walionyoa))*** Wakauliza: "Na waliopunguza ee Rasuli wa Allaah?" Akasema: ***((Na waliopunguza)).***[120]

Isipokuwa ikiwa tarehe 8 ya Hajj iko karibu na hakuna wakati wa kutosha kwa nywele kurudi kukua, basi ni bora kukata ili nywele zibakie kwa ajili ya kunyoa baada ya kulala Muzdalifah, kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliwaamrisha Maswahaba kukata nywele katika 'Umrah kwani walifanya asubuhi ya tarehe nne ya Dhul-Hijjah.

[120] Muslim na wengineo kwa maelezo tofauti kidogo.

- Baada ya hapo 'Umrah itakuwa imemalizika na utakuwa huru kuvaa nguo nyingine, kutia manukato (mwanamume) na kurudia hali ya ndoa (kujimai) na kadhalika.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Kwenye kupanda kilima cha *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah*, baadhi ya Mahujaji wanaelekea *Al-Ka'bah* na kuiashiria kwa mikono wakisema *'Allaahu Akbar'* kama vile wanavyosema *takbiyrah* ya Swalaah. Kuashiria hivyo ni makosa kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alinyanyua mikono yake kumdhukuru Alllaah na komba du'aa pekee.

- Kufanya *Ar-Rakdhw* katika masafa yote baina ya vilima viwili. Sunnah ni kuchapuza mwendo baina ya alama zilowekwa za taa ya kijani sakafuni na kutembea mwendo wa kawaida kwengine kote.

- Wanawake kufanya *Ar-Rakdhw* kwani *Ar-Rakdhw* ni kwa ajili ya wanaume pekee.

- Kusoma adhkaar kwa pamoja akiwa mtu mmoja anaongoza wenziwe. Ni makosa makubwa kufanya hivi kwani inasababisha zahma za magurupu ya watu kutembea pamoja na sauti moja na kuwababaisha Mahujaji wengineo katika adhkaar zao.

- Kuleta mazungumzo wakati wa *As-Sa'-y* na hali hapo ni mahali pa kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى).

## Taratibu Za Kutekeleza  As-Sa'yi Kwa Mukhtasari



## 16- Utekelezaji Wa Hajj

### Tarehe 8 Dhul-Hijjah Siku ya *At-Tarwiyah*

- Tarehe 8 Dhul-Hijjah inajulikana kuwa ni siku ya *At-Tarwiyah* ambayo Mahujaji wataelekea *Minaa*. Ikiwa ni mwenye kutekeleza *Hajj Tamattu'*, unatakiwa siku hiyo kujitwaharisha tena kuingia katika Ihraam kama ulivyofanya wakati wa 'Umrah mahali hapo ulipo hotelini. Utavaa Ihraam yako na kusema:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ حَجًّا

***Labbayka-Allaahumma Hajjaa***

لَبَّيْكَ حَجّاً لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لا شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إنَّ الْحَمْدَ، وَالنِّعْمَةَ، لَكَ وَالْمُلْكُ، لا شَرِيكَ لَكَ

***Labbayka Hajja labbayka-Allaahumma labbayk, labbayka, laa shariyka Laka labbayk, Innal-Hamda, wan-ni'matah Laka wal-Mulk, laa shariyka Lak***

- Ikiwa utakhofu kuwa jambo litakuzuia kukamilisha Hajj yako basi useme:

وَإِنْ حَبَسَنِي حَابِسٍ فَمَحَلِّي حَيْثُ حَبَسْتَنِي

***((Ikiwa nitazuiliwa na kizuizi chochote sehemu yangu ni popote nilipozuiliwa)).***

- Ikiwa huna khofu kama hiyo basi hakuna haja ya kujishurutisha hivyo.

- Kisha utakwenda *Minaa* na huko utaswali Swalaah ya Adhuhuri, Alasiri, Magharibi, 'Ishaa na Alfajiri. Utaswali *qaswran* Swalaah za rakaa nne kuwa mbili mbili kila moja bila ya *jam'an*, yaani kuswali kila *Swalaah* kwa wakati wake ila uzifupishe tu kama alivyofanya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Kutokuleta *Talbiyah* - wengi hawafanyi hivo wakighafilika nayo jambo ambalo ni kinyume na Sunnah kwani *Talbiyah* inamalizika baada ya *Jamrat Al-'Aqabah*.

- Kujumuisha Swalaah badala ya kufupisha pekee. Ni kinyume na Sunnah kuunga Swalaah za Adhuhuri na Alasiri, na pia Magharibi na 'Ishaa. Inavyopasa ni kuziswali kila moja kwa wakati wake huku ukizifupisha.

- Mahujaji kupoteza muda wao katika mahema kwa kupiga soga badala ya kufanya *dhikru-Allaah* au badala ya kuelimishana hapo mambo ya Dini na hasa yanayohusu utekelezaji sahihi wa 'ibaadah hii ya fardhi. Mahujaji wengi kabisa wanafika huko kutekeleza fardhi hii wakiwa hawana elimu ya kutosha ya jinsi ya kuitekeleza 'ibaadah hii, na hapo ni fursa ya kuwaelimisha badala ya kupoteza muda kwa mambo yasiyofaa.

- Kukusanyika kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa pamoja, kuomba du'aa kwa pamoja, kusoma Mawlid, na kusoma adhkaar zisizokuwa zenye dalili na 'ibaadah nyinginezo zisizothibiti katika Sunnah ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

**Tarehe 9 Dhul-Hijjah – Siku Ya '*Arafah***

Hatua za kufanya:

- Jua litakapochomoza siku ya pili ambayo ni tarehe 9 Dhul-Hijjah, utakwenda '*Arafah* na huko utaswali Adhuhuri na Alasiri *jam-'an* wa *qaswran* wakati wa Adhuhuri. Kisha utabakia katika Msikiti wa Namirah au maeneo yoyote ya '*Arafah* pale mtakapowekwa mpaka jua litakapokuchwa. Hapo kaa kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kila aina ya kumdhukuru; kusoma Qur-aan, *istighfaar, tasbiyh, tahmiyd, tahliyl, takbiyr,* kuomba du'aa kwa wingi uwezavyo huku ukielekea Qiblah na sio kuelekea jabali la '*Arafah*.

Usipojaaliwa kuweko katika Msikiti wa Namirah karibu na jabali la *'Arafah* basi popote utakapokuwa kwani Rasuli ( صلى الله عليه وآله وسلم) alisimama katika jabali la *'Arafah* na akasema:

((وَوَقَفْتُ هَاهُنَا وَعَرَفَةُ كُلُّهَا مَوْقِفٌ))

***((Nimesimama hapa na 'Arafah yote ni kisimamo [cha 'Arafah])).*** [121]

Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akiomba:

**لا إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ ولَهُ الحَمْدُ وهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَديرٌ**

***Laa Ilaaha Illa-Allaah Wahdahu laa shariyka Lah, Lahul-Mulku walahul-Hamud wa-Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr***

"Hapana ilaah (muabudiwa wa haki) ila Allaah, Hana mshirika, ni Wake Ufalme na ni Zake Sifa njema zote, Naye juu ya kila kitu ni Muweza". [122]

- Utakapochoka unaruhusiwa kuzungumza na wenzako kidogo mas-alah ya Dini, au kusoma vitabu vyenye faida khasa kuhusu ukarimu, Rahmah ya Allaah (سبحانه وتعالى), neema Zake kwetu ili uzidi kupata matumaini kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى) ya kufutiwa dhambi na kutakabaliwa unayoyahitaji. Kisha endelea kuomba du'aa na kuhakikisha kuwa unatumia wakati wako wa mwisho wa siku hiyo katika du'aa nyingi kwa sababu du'aa zilizo bora kabisa ni *du'aa* za siku ya *'Arafah*.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa *'Arafah***

- Baadhi ya Mahujaji wanapiga kambi nje ya maeneo ya *'Arafah* na kubakia hapo hadi jua kuzama, kisha wanaelekea *Muzdalifah* bila ya kusimama *'Arafah* kama inavyopasa. Hili ni kosa kubwa ambalo linabatilisha Hijja yao kwani kusimama *'Arafah* ni kilele cha Hajj na pia ni

[121] Muslim.

[122] At-Tirmidhiy na ameisahihisha Al-Abaaniy katika *Swahiyh At-Tirmidhiy* 3585.

fardhi kubakia ndani ya eneo la '*Arafah* na si nje ya eneo lake. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

((الْحَجُّ عَرَفَة، مَنْ جَاءَ قَبْلَ طُلُوعِ الْفَجْرِ مِنْ لَيْلَةِ جَمْعٍ فَقَدْ أَدْرَكَ الْحَجّ))

***((Al-Hajj ni 'Arafah, atakayekuja kabla kutoka Alfajiri usiku wa kujumuika atakuwa ameipata Hajj)).***[123]

- Kuondoka '*Arafah* kabla ya jua kuzama hairuhusiwi kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alibakia '*Arafah* hadi jua kuzama kabisa.

- Kujilazimisha katika zahma ya watu kupanda jabali la '*Arafah* hairuhusiwi, kwa sababu inakusababisha madhara na madhara kwa Mahujaji wengine. Eneo lote la '*Arafah* linahesabiwa kuwa ni kisimamo cha '*Arafah*, na si kupanda jabali la '*Arafah* wala kuswali katika hilo jabali au karibu yake hata idhaniwe kuwa mtu amepata kisimamo cha '*Arafah*.

- Kuomba du'aa akiwa anaelelekea jabali la '*Arafah* ni makosa kwa sababu inapasa kuelekea Qiblah wakati wa kuomba du'aa.

- Kurundika chungu ya mchanga au vijiwe siku ya '*Arafah* katika sehemu fulani, jambo ambalo haliko katika shariy'ah ya Allaah.

- Kulipa jina Jabali la '*Arafah* kuwa ni *Jabal Ar-Rahmah*.

[123] *Swahiyh Al-Jaami'*.

***Muzdalifah***

- Jua litakapozama utaondoka *'Arafah* kwenda *Muzdalifah* na huko utaswali Magharibi na 'Ishaa. Ikiwa utachoka au umepungukiwa na maji, unaruhusiwa kuunganisha Magharibi na 'Ishaa. Ikiwa utakhofu kuwa hutofika *Muzdalifah* mpaka baada ya usiku wa manane, basi swali kabla ya kufika huko kwani hairuhusiwi kuchelewesha Swalaah mpaka usiku wa manane.

- Utabakia huko *Muzdalifah* usiku kukesha, na hapo omba sana du'aa na mdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) mpaka Alfajiri. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ فَإِذَآ أَفَضۡتُم مِّنۡ عَرَفَٰتٖ فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ عِندَ ٱلۡمَشۡعَرِ ٱلۡحَرَامِۖ وَٱذۡكُرُوهُ كَمَا هَدَىٰكُمۡ وَإِن كُنتُم مِّن قَبۡلِهِۦ لَمِنَ ٱلضَّآلِّينَ ١٩٨ ثُمَّ أَفِيضُواْ مِنۡ حَيۡثُ أَفَاضَ ٱلنَّاسُ وَٱسۡتَغۡفِرُواْ ٱللَّهَۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٞ ١٩٩ ﴾

**((Basi mtakapomiminika kutoka *'Arafaat* mdhukuruni Allaah kwenye *Mash'aril- Haraam* (Muzdalifah) na mdhukuruni Yeye kama Alivyokuongozeni kwani hakika mlikuwa kabla ya hapo miongoni mwa waliopotea. Kisha miminikeni kutoka pale wamiminikapo watu; na ombeni maghfirah kwa Allaah. Hakika Allaah ni *Ghafuwrur-Rahiym* (Mwenye kughufuria - Mwenye kurehemu))).**[124]

- Utaswali Alfajiri mapema kwa adhaan na Iqaamah, kisha utaelekea *Mash'aril-Haraam* na utafanya *tahliyl*, yaani utasema ***"Laa Ilaaha Illa Allaah***" pia **"*Allaahu Akbar*"** na utaomba du'aa mpaka kupambazuke vizuri. Ikiwa hukujaaliwa kwenda *Mash'aril-Haraam*, utaomba hapo hapo ulipo kutokana na kauli ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

((وَوَقَفْتُ هَاهُنَا وَجَمْعٌ كُلُّهَا مَوْقِفٌ))

[124] Suratul Baqarah (2: 198).

***((Nimesimama hapa na kote hapa ni kisimamo [cha Muzdalifah]))***.[125]

Unapoomba du'aa uelekee Qiblah na huku ukinyanyua mikono.

- Utaondoka *Muzdalifah* kuelekea *Minaa* huko utaokota vijiwe kwa ajili ya kurusha katika *Jamrat Al-'Aqabah*.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa *Muzdalifah***

- Kutokumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) usiku huo na badala yake kulala tu na hali hapo ni mahali patukufu mno na panapotakiwa kumdhukuru mno Allaah (سبحانه وتعالى) kama ilivyotajwa katika Aayah hapo juu.

- Baadhi ya Mahujaji wanapofika tu *Muzdalifah* na kabla ya kuswali Swalaah za Magharibi na 'Ishaa huanza kukusanya vijiwe vya kurusha katika *Jamaraat*.

- Kudhania kwamba vijiwe lazima viokotwe *Muzdalifah* na hali vinaweza kuokotwa popote katika maeneo ya Al-Haram ikiwa ni *Muzdalifah* au *Minaa*. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) hakuamrisha vijiwe vya *Jamrat Al-'Aqabah* viokotwe *Muzdalifah* bali Maswahaba walimuokotea yeye vijiwe asubuhi baada ya kuondoka *Muzdalifah* na kuingia *Minaa*. Aliokotewa vijiwe vyote viilobakia kutoka *Minaa* pia.

***Minaa – Ar-Ram-y* Katika *Jamaraat***

Ukiwa ni dhaifu na huwezi kustahamili zahma za watu wakati wa *Ar-Ram-yu*, (kama mwanamke na mtu mzima), basi unaruhusiwa kwenda *Minaa* mwisho wa usiku huo kurusha vijiwe katika *Jamrat Al-'Aqabah* pekee kabla ya zahma ya watu kuwa kubwa.

Kurusha vijiwe kuna maana zifuatazo:

---

[125] Muslim.

**i-** Imekusudiwa kuwa ni njia ya kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa hiyo ni kitendo cha 'ibaadah.

**ii-** Kufuata mafunzo ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliposema: *((Chukueni kwangu taratibu zenu [za Hajj]))*.

**iii-** Kukumbuka kisa cha Nabiy Ibraahiym na mwanawe Nabiy Ismaa'iyl (عليهما السلام).

**iv-** Kumhizi shaytwaan atakapoona ummah wa watu wanarusha vijiwe mahali alipomtia shaka na kutaka kumpotosha Nabiy Ibraahiym (عليه السلام).

**Tarehe 10 Dhul-Hijjah**

Siku hii ni siku iliyo bora kabisa kwa Allaah (سبحانه وتعالى) kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

**((إِنَّ أَعْظَمَ الْأَيَّامِ عِنْدَ الله تبارك وتعالى يَوْمُ النَّحْرِ ثُمَّ يَوْمُ الْقَرِّ))** رواه أبو داود والنسائي وصححه الألباني

***((Siku iliyo tukufu kabisa kwa Allaah ni siku ya kuchinja, kisha siku ya kutulia)).***[126] (yaani siku ya kukaa *Minaa*)

Karibu na jua kuchomoza utaondoka *Muzdalifah* kuelekea *Minaa*. Unapokwenda unatakiwa uendelee kuleta *Talbiyah* mpaka umalize kurusha vijiwe katika *Jamrah* hiyo ya *Al-'Aqabah* ndipo *Talbiyah* inamalizika. Utakapofika utafanya yafuatayo:

- Utarusha vijiwe saba kimoja baada ya kimoja katika Al-Jamrat Al-'Aqabah (*Jamratul-Kubraa*) pekee ambalo liko karibu na mnara wa Makkah na kusema ifuatavyo kwa kila kijiwe utakachokirusha:

[126] Abu Daawuwd na An-Nasaaiy na ameisahihisha Al-Abaaniy.

اللهُ أَكْبَرَ

***Allaahu Akbar***

- Utachinja mnyama, na kula baadhi ya nyama na utatoa nyingine kuwapa masikini. Kuchinja ni fardhi kwa wale wanaofanya Hajj ya *Tamattu'*u na *Qiraan*. (Kwa hali ilivyo sasa huwa haiwezekani kufanya hivi, hivyo unaweza kutekeleza kama unavyoamrishwa yaani kulipa na kuacha jukumu hili kwa serikali ifanye kazi ya kuchinja).

- Utanyoa au kukata nywele. Inapendekezwa kunyoa kuliko kukata kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).[127] Mwanamke atakata nywele zake urefu wa ncha ya kidole.

- Utakwenda Makkah kufanya *Twawaaful-Ifaadhwah* na *As-Sa'-y*. Ni Sunnah kujitia manukato kabla ya kwenda Makkah (kwa wanaume) kutokana na kauli ya Mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها) kwamba:

كُنْتُ أُطَيِّبُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لِإِحْرَامِهِ حِينَ يُحْرِمُ وَلِحِلِّهِ قَبْلَ أَنْ يَطُوفَ بِالْبَيْتِ

"Nilikuwa nikimpaka manukato Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) kabla ya kuingia katika Ihraam na baada ya kutoka katika Ihraam kabla ya kutufu *Al-Ka'bah.*"[128]

Mambo manne hayo yafanywe kama ilivyo taratibu yake ikiwezekana, lakini hakuna ubaya au sharti ikiwa mtu atatanguliza kitendo chochote kabla ya chengine.

- Imeruhusika kuchelewesha *Twawaaful-Ifaadhwah* na *As-Sa'-y* kwa aliye na dharura kurudi Makkah, na inaweza ikacheleweshwa mpaka tarehe 12. Utakapomaliza hayo mambo matatu utaruhusika kujitoa katika Ihraam ndogo. Na unaweza kuvaa nguo zako za kawaida na kufanya kila jambo la halali isipokuwa kuingia katika kitendo cha ndoa, huku ukisubiri kumaliza *Twawaaful-Ifaadhwah* na *As-Sa'-y,* na hapo utakapomaliza ndipo utaruhusika kujivua kabisa

---

[127] Tazama 'Utekelezaji wa 'Umrah' baada ya As-Sa'-y.

[128] Al-Bukhaariy na Muslim.

Ihraam yako na kuwa huru na yote yaliyoharamishwa wakati wa Ihraam.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa Katika *Jamaraat***

- Baadhi ya Mahujaji wanadhania kwamba kurusha vijiwe katika nguzo za *Jamaraat* ni kumpiga shaytwaan, hivyo wanapinduka mipaka katika kitendo hiki cha 'ibaadah.

- Wengine wanarusha vijiwe vikubwa, viatu, mbao n.k. na hurusha kwa ghadhabu. Wengine hufikia hadi kutukana! Hivyo ni kusababisha madhara kwa Mahujaji wengine kwani mtu anaweza kurusha jiwe kubwa kwa mbali likampiga Haaj aliye mbele yake badala ya kupiga nguzo. Vijiwe vidogo vyenye ukubwa wa harage au kunde au punje za mahindi ndio bora zaidi kuvitumia.



- Kuacha kwao kuomba du'aa baada ya kutupa vijiwe mnara wa kwanza na wa pili katika yale masiku yanayoitwa *Ayyaam At-Tashriyq*. Ilivyothibiti ni kuwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa pindi akimaliza kurusha vijiwe minara miwili likuwa akisimama na akielekea Qiblah na kunyanyua mikono yake na kuomba du'aa ndefu. Na miongoni mwa sababu za watu kuacha kufanya hivi aidha kwa kutokujua au kupupia kwao kutaka kumaliza haraka kurusha vijiwe waondoke.

- Kusababisha zahma, kusukumana na kugombana na wengine katika maeneo hayo. Inavyopasa ni kuwa na upole na kurusha vijiwe bila ya madhara kwa wengine.

- Kurusha vijiwe vyote kwa mara moja. 'Wanachuoni wamesema kwamba hii itahesabika kuwa ni kama kurusha kijiwe kimoja kwa sababu shariy'ah imetaja kurusha kijiwe kimoja baada ya kimoja na huku Haaj anasema 'Allaahu Akbar' kila kijiwe kimoja kinaporushwa.

- Kumuwakilisha mtu kurusha vijiwe, kwa kukhofia zahma au tabu na mashaka, na hali Haaj mwenyewe anao uwezo wa kutekeleza 'ibaadah hii. Wagonjwa tu na wale walio dhaifu ndio wanaruhusiwa kuwakilishwa na mtu kufanya 'amali hii. Ama kila mwenye uwezo na afya njema akarushe vijiwe mwenyewe pasina kuwakilishwa na Mtu. Watu wafahamu kuwa Hija ni moja kati ya aina za jihaad ambayo ni lazima mwenye kuhiji akabiliane na tabu mbalimbali na lazima aikamilishe 'ibaadah hii kama alivyoamrisha Allaah na Rasuli Wake.

- Kuzidisha kwao du'aa wakati wa kurusha vijiwe, yaani du'aa ambazo hazikuthibiti katika Sunnah kama kusema kwao; "Ee Allaah! Jaalia vijiwe hivi kuwa ni radhi Kwako na ni ghadhabu kwa shaytwaan". Mara nyingine wao huacha Takbiyrah iliyothibiti kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

- Baadhi ya Mahujaji huosha vijiwe jambo ambalo halimo katika mafunzo ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

**Tarehe 11, 12 na 13 Dhul-Hijjah**

Kubakia *Minaa* masiku haya kumaliza kurusha vijiwe katika Jamrah zote tatu kuanzia *Jamrat Asw-Swughraa, Jamrat Al-Wuswtwaa* na *Jamrat Al-'Kubraa*. Na hizi ni siku tulizoamrishwa kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa wingi:

﴿ ۞ وَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ فِىٓ أَيَّامٍ مَّعْدُودَٰتٍ ۚ فَمَن تَعَجَّلَ فِى يَوْمَيْنِ فَلَآ إِثْمَ عَلَيْهِ وَمَن تَأَخَّرَ
فَلَآ إِثْمَ عَلَيْهِ ۚ لِمَنِ ٱتَّقَىٰ ۗ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ وَٱعْلَمُوٓا۟ أَنَّكُمْ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٢٠٣﴾ ﴾

**((Na mdhukuruni Allaah katika siku za kuhesabika. Atakayeharakisha (kuondokwa kwake) katika siku mbili, basi hakuna dhambi juu yake; na atakayechelewesha (mpaka siku ya tatu) basi hakuna dhambi juu yake; kwa mwenye kuwa na taqwa. Na mcheni Allaah na jueni kwamba Kwake mtakusanywa.))**[129]

Baada ya kufanya *Twawaaf* na *As-Sa'-y* utarudi *Minaa* kulala huko usiku wa tarehe 11 na 12 Dhul-Hijjah.

- Utarusha vijiwe Jamrah zote tatu jioni siku ya tarehe 11 na 12 Dhul-Hijjah. Utaanza kwanza *Jamrat Asw-Swughraa* ambayo iko mbali na Makkah, kisha utaelekea Qiblah na kuomba du'aa ndefu kwa kunyanyua mikono. Kisha utarusha *Jamrat Al-Wuswtwaa*, kisha utaelekea Qiblah na kuomba du'aa ndefu na kunyanyua mikono. Kisha *Jamrat Al-Kubraa* (*Jamrat Al-'Aqabah*) lakini ukimaliza hapo huombi du'aa bali utaondoka. Katika kila Jamrah utarusha vijiwe saba, moja baada ya moja na huku ukisema '***Allaahu Akbar'*** kwa kila kijiwe unachorusha.

- Haipasi kuacha kuomba du'aa tena iwe ndefu ikiwezekana baada ya kurusha vijiwe katika *Jamrat Asw-Swughraa* na *Jamrat Al-Wuswtwaa* kwani ni Sunnah na watu wengi sana hawatekelezi hivi aidha kwa kutokujua au kupuuza. Na kila inapokuwa Sunnah haitekelezwi ndipo inapokuwa haitambuliki kwa watu na huenda ikaachwa kabisa na kupotea.

[129] Al-Baqarah (2: 203).

| Tarehe | *Jamrat Asw-Swughraa* | Du'aa | *Jamrat Al-Wustwaa* | Du'aa | *Jamrat Al-Kubraa (Jamrat Al-'Aqabah)* | Du'aa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 10 | X | X | X | X | √ | x |
| 11, 12, 13 | √ | √ | √ | √ | √ | X |

- Hairuhusiwi kurusha vijiwe kabla ya Adhuhuri katika siku mbili hizi.

- Ni bora kabisa kutembea kwenda kurusha vijiwe, ingawa kipando kinaruhusiwa.

- Ikiwa una haraka ya kurudi, baada ya kurusha vijiwe siku ya 12 Dhul-Hijjah, unaweza kuondoka *Minaa* lakini iwe kabla ya jua kuzama. Lakini ukipenda kuzidisha makazi yake, ambayo ni bora zaidi, basi ulale *Minaa* usiku wa 13 na kuendelea kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) na kurusha vijiwe *Jamaraat* jioni kama ulivyofanya siku ya kumi na mbili. Dalili na kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) iliyotajwa juu.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa *Ayyaam At-Tashriyq***

- Baadhi ya Mahujaji hawalali siku ya tarehe 11 na 12 bali wanakuwa nje ya *Minaa* bila ya udhuru.

- Wengineo huondoka mchana na kwenda Makkah kukimbia kubakia katika mahema huko *Minaa*.

- Wengine huchanganya katika kurusha vijiwe na kuanza ndivyo sivyo katika *Jamaraat*. Tazama chati juu.

***Twawaaf Al-Wadaa'i***

- Utakapokuwa tayari kusafiri, kabla ya kuondoka fanya *Twawaaf Al-Wadaa'i* ambayo ni mizunguko saba katika *Al-Ka'bah* kutokana na kauli ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

((لَا يَنْفِرَنَّ أَحَدٌ حَتَّى يَكُونَ آخِرُ عَهْدِهِ بِالْبَيْتِ))

***((Asikimbie mtu [asiondoke zake] mpaka iwe shughuli yake [kitendo chake cha mwisho] katika Nyumba [Al-Ka'bah*]))**.[130]

- Wanawake wenye hedhi na nifaas hawana lazima kufanya *Twawaaf Al-Wadaa'i* kutokana na dalili ifuatayo:

أُمِرَ النَّاسُ أَنْ يَكُونَ آخِرُ عَهْدِهِمْ بِالْبَيْتِ إِلَّا أَنَّهُ خُفِّفَ عَنْ الْحَائِضِ

"Aliamrisha watu iwe shughuli zao za mwisho ni *Al-Ka'bah* isipokuwa waliruhusiwa (wanawake) wenye hedhi."[131]

- Ikiwa baada ya *Twawaaf Al-Wadaa'i* umebakia kidogo wakati huo unasubiri wenzako au kipando chako au kununua kitu njiani hakuna ubaya, wala hakuna haja ya kurudia *Twawaaf Al-Wadaa'i* isipokuwa ikiwa umetia niyyah ya kuchelewesha safari yako; mfano ukitaka kuondoka mwanzo wa siku, ukatufu *Al-Ka'bah*, kisha ukachelewesha safari hadi mwisho wa siku, basi itakulazimu urudie kutufu *Al-Ka'bah* ili iwe ni kitendo chako cha mwisho.

130 Muslim.
131 Al-Bukhaariy na Muslim.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa Kuhusu *Twawaaf Al-Wadaa'i***

- Kuondoka *Minaa* wakaenda Makkah na wakafanya *Twawaaf Al-Wadaa'i* kisha wakarudi tena *Minaa* kumalizia kurusha vijiwe ndipo baadaye waondoke Makkah. Kufanya hivyo, ina maana kwamba, kurusha vijiwe ni kitendo cha mwisho kufanya kabla ya kuondoka Makkah na hii ni kinyume na alivyoagiza Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

- Kukaa kwao kitambo Makkah baada ya kutufu *Twawaaf Al-Wadaa'i* na hivyo ifahamike kuwa jambo lao la mwisho walilofanya si kutufu. Na hili pia ni kinyume na amri ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kwani Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) Alifanya *Twawaaf Al-Wadaa'i* kisha akaondoka na hivi ndivyo walivyokuwa wakifanya Maswahaba zake. Isipokuwa Wanachuoni wameruhusu mtu kubakia kidogo baada ya kuiaga *Al-Ka'bah* kama kuna dharura kubwa kama ya kuingia wakati wa Swalaah au kuswalia jeneza au jambo lenye kuambatana na safari yake kama kununua kitu au kusubiri kidogo wenzake. Ama yule ambae atakaa Makkah baada ya *Twawaaf Al-Wadaa'i* pasina dharura atalazimika airudie *Twawaaf* baadaye.

- Kutoka katika milango ya *Al-Ka'bah* hali ya kuwa wanapiga piga vichogo vyao wakidhani kuwa kwa kufanya hivyo wanaitukuza *Al-Ka'bah* kumbe wanazua katika Dini na hivyo kumaliza 'ibaadah hii tukufu kwa kufanya bid'ah.

- Kuilekea kwao *Al-Ka'bah* wakiwa mlangoni wamemaliza kutufu *Twawaaf Al-Wadaa'i* na wakawa wanaomba du'aa zao kama wenye kuiaga *Al-Ka'bah*. Na jambo hili halikuthibiti kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

## 17- Kuzuru Madiynah

Mwenye kuhiji atakwenda Madiynah kabla au baada ya Hajj kwa niyyah ya kutembelea Msikiti wa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) na kuswali humo na si kwa niyyah ya kutembelea kaburi kwa sababu haikuthibiti hivyo kutokana na Hadiyth ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ifuatayo:

((لَا تُشَدُّ الرِّحَالُ إلا إلى ثَلَاثَةِ مَسَاجِدَ: مَسْجِدِي هذا وَمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَمَسْجِدِ الْأَقْصَى)) رواه البخاري ومسلم

***((Msifanye ziara ila kwa Misikiti mitatu; Msikiti wangu huu [Madiynah], Masjidil-Haraam [wa Makkah], na Masjidil-Aqswaa [wa Palestina*])).**[132]

Swalaah moja humo ni bora kuliko Swalaah elfu mahali pengine isipokuwa Masjid Al-Haraam wa Makkah.

Utakapofika Msikitini tanguliza mguu wa kulia na uombe du'aa ya kuingia Msikitini:

أَعُوذُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ, وَبِوَجْهِهِ الْكَرِيمِ, وَسُلْطَانِهِ الْقَدِيمِ, مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ، (بِسْمِ الله، وَالصَّلاةُ) (وَالسَّلامُ عَلى رَسولِ الله)، اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوابَ رَحْمَتِك

***A'uwdhu biLlaahil-'Adhwiym, wa bi-Wajhihil-Kariym wa-Sultwaanihil-qadiym, minash-shaytwaanir-rajiym (BismiLLaah was-swalaatu) (was-salaamu 'alaa Rasuwuli-Llaah) Allaahumma-ftah-liy abwaaba Rahmatika***

"Najikinga na Allaah Aliye Mtukufu, na kwa Wajihi Wake Mkarimu, na kwa utawala Wake wa kale, dhidi ya shaytwaan aliyeepushwa na Rahmah za Allaah[133] (Kwa jina la Allaah) (Na amani[134] zimfikie Rasuli wa Allaah).[135] Ee Allaah nifungulie milango ya Rahmah Yako."[136]

---

[132] Al-Bukhaariy, Muslim.
[133] Abu Daawuwd. Tazama *Swahiyh Al-Jaami'* (4591).
[134] Ibn As-Sunniy namba 88 na ameipa daraja ya Hasan Al-Albaaniy.
[135] Abu Daawuwd (1/126) na tazama *Swahiyh Al-Jaami'* (1/528).
[136] Muslim (1/494), na katika Sunan ibn Maajah kutoka Hadiyth ya Faatwimah (رضي الله عنها) ((***Allaahumma-ghfir-liy dhunuwbiy waf-tah-liy abwaaba Rahmahtika***)) na ameipa Al-Albaaniy daraja ya Swahiyh. Tazama *Swahiyh Ibn Maajah* (1/128-129).

Kisha unatakiwa uswali rakaa mbili za Sunnah kama ni *Tahiyyat Al-Masjid*. Kisha ubakie hapo kuswali Swalaah za fardhi unapoingia wakati wake.

Kisha utakwenda katika kaburi la Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) katika nyakati zilizopangwa huko, utasimama mbele yake, utamsalimia kwa kusema:

السَّلاَمُ عَلَيْكَ أَيُّها النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُه

***Assalaamu 'Alayka ayyuhan-Nabiyyu wa-Rahmatu-Allaahi wa Barakaatuh.***

"Amani zishuke juu yako Ee Nabiy na Rahmah za Allaah na Baraka Zake."

اللّهُمَّ صَلِّ عَلى مُحَمَّدٍ وَعَلى آلِ مُحَمَّد كَما صَلَّيْتَ عَلى آلِ إبْراهيم وَعَلى آلِ إبْراهيم إِنَّكَ حَميدٌ مَجيد, اللّهُمَّ بارِكْ عَلى مُحَمَّدٍ وَعَلى آلِ مُحَمَّد كَما بارَكْتَ عَلى إبْراهيم وَعَلى آلِ إبْراهيم إِنَّكَ حَميدٌ مَجيد

***Allaahumma Swalli 'alaa Muhammad wa 'alaa aali Muhammad kamaa Swallayta 'alaa Ibraahiyma wa 'alaa aali Ibraahiyma Innaka Hamiydum-Majiyd. Allaahumma Baarik 'alaa Muhammad wa 'alaa aali Muhammad kamaa Baarakta 'alaa Ibraahiyma wa 'alaa aali Ibraahiyma Innaka Hamiydum-Majiyd.***

Ee Allaah! Mswalie Muhammad, na familia ya Muhammad, kama Ulivyomswalia Ibraahiym na familia ya Ibraahiym, Hakika Wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu. Ee Allaah! Mbariki Muhammad na familia ya Muhammad kama Ulivyombariki Ibraahiym na familia ya Ibraahiym, hakika Wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu.

أشْهَد أنَّكَ رَسُولُ الله حَقاً، وَأنَّكَ قَدْ بَلَّغْتَ الرِّسَالَةَ، وَأدَّيْتَ الأَمَانَةَ، وَنَصَحْتَ الأُمَّةَ، وَجَاهَدْتَ فِي اللهِ حَقَّ جِهَادِه، فَجَزاكَ اللهُ عَنْ أُمَّتك أَفْضَل ما جَزَى نَبيًّا عَنْ أُمَّتِه.

***Ash-hadu Annaka Rasuwlu-LLaah haqqan, wa annaka qad ballaghtar-Risaalah, wa addaytal-amaanah, wa naswahtal-Ummah, wa jaahadta fiLlaahi haqqa jihaadih, fa-Jazaaka-Allaahu 'an Ummatika afdhwal maa jazaa Nabiyyan 'an Ummatih***

"Nashuhudia kwamba wewe hakika ni Mjumbe wa Allaah, na kwamba umebalighisha ujumbe, na umetimiza amana. Na umenasihi Ummah, na umefanya jihaad katika njia ya Allaah ipasavyo hakika, basi Allaah Akulipe kwa Ummah wako bora kuliko Alivyomlipa Nabiy (yeyote) kwa Ummah wake".

Kisha sogea hatua moja au mbili upande wa kulia ambako kuna kaburi la Abu Bakr Asw-Swiddiyq (رضي الله عنه) na kumsalimia kwa kusema:

السَّلاَمُ عَلَيْكَ

***Assalaamu 'Alayka***

"Amani zishuke juu yako."

Ukipenda muombee du'aa munaasib kama kusema:

رَضِيَ اللَّهُ عَنْكَ وَجَزَاكَ اللَّهُ عَنْ أُمَّةِ مُحَمَّد أَفْضَل جَزَاء

***Radhiya-Allaahu 'anka wa Jazaaka-Allaahu 'an Ummati Muhammad afdhwal jazaa***

"Allaah Aridhike na wewe na Akulipe malipo bora kwa niaba ya Ummah wa Muhammad."

Kisha sogea hatua moja au mbili upande wa kulia kidogo kuelekea kaburi la 'Umar bin Al-Khattwaab (رضي الله عنه) na kumsalimia kwa kusema:

السَّلاَمُ عَلَيْكَ

***Assalaamu 'Alayka***

رَضِيَ اللَّهُ عَنْكَ وَجَزَاكَ اللَّهُ عَنْ أُمَّةِ مُحَمَّد أَفْضَل جَزَاء

***Radhiya-Allaahu 'anka wa Jazaaka-Allaahu 'an Ummati Muhammad afdhwal jazaa***

Haifai mtu kujikurubisha kwa Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kugusa ukuta wa chumba cha Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) au kufanya *Twawaaf* (kulizunguka). Pia haifai kuelekea huko kwa kuomba du'aa bali unapaswa uelekee Qiblah. Kwa sababu kujikurubisha kwa Allaah

(سبحانه وتعالى) haiwi ila kama Alivyotuwekea shariy'ah Yeye pamoja na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) na 'ibaadah zinatakiwa zifuatwe sio zizushwe.

Ingawa kuna baadhi ya Wanachuoni wamejuzisha wanawake kuzuru makaburi, lakini kutokana na hali ilivyo sasa sehemu hiyo, fitnah za wanawake zimezidi na madhara yamedhihirika kwa wingi, kwani wanafika kupandisha sauti zao, kupiga kelele, kugombana na kupigana, na wengine wanafika kupandisha mashaytwaan na kupiga vigelegele! Kutokana na haya, haipendekezwi wanawake kuzuru kaburi la Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم), wala kuzuru kaburi la yeyote mwingine ili kuepukana na fitnah hizo. Lakini ikiwa mwanamke atapendelea kuzuru basi achunge sana kutimiza adabu za kuzuru makaburi. Na akishindwa, basi anapofika Masjid An-Nabawiy, anatakiwa kumtolea salamu na kumswalia Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) mahali hapo hapo alipo kwani zinamfikia salamu kama alivyosema:

((صَلُّوا عليَّ، فإنَّ صَلاتَكُمْ تَبْلُغُنِي حَيْثُ كُنْتُمْ))

***((Niswalieni kwani Swalah zenu zinanifikia popote mlipo).***

Na akasema:

((إِنَّ لِلَّهِ مَلائِكَةً سَيَّاحِينَ فِي الأَرْضِ يُبَلِّغُونِي مِنْ أُمَّتِي السَّلامَ))

***((Hakika Allaah Anao Malaika wanaozunguka katika ardhi na kunitumia salamu kutoka kwa ummah wangu)).***[137]

**Rawdhah**: Kipande cha Jannah kama alivyobashiria Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ambacho kipo sehemu iliyokuwa baina ya chumba chake na mimbar yake.

Ukipenda utakwenda hapo na kuswali rakaa mbili. Lakini la muhimu kabisa kuzingatia ni kwamba sehemu hiyo ni kipande kidogo mno, kimetiwa alama ya zulia la kijani. Kwa vile zahma ya watu ni kubwa, haiwezekani kabisa kuwatosheleza watu kukipata kuswali hapo! Hivyo unaweza kuswali sehemu yoyote iliyowekwa

[137] An-Nasaaiy, Ahmad.

kwa ajili yake na niyyah inatosheleza kabisa hata kama hukujaaliwa kufika hapo.

Kisha unaweza kwenda kufanya ziara za sehemu zifuatazo za historia:

**Masjidul-Qubaa**: Msikiti wa kwanza kujengwa na Waislamu wa wakati wa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) walipohama kutoka Makkah kuelekea Madiynah. Utaswali rakaa mbili *Tahiyyat Al-Masjid*. Fadhila za kuswali hapo ni kama thawabu za 'Umrah:

((مَنْ تَطَهَّرَ فِي بَيْتِهِ ثُمَّ أَتَى مَسْجِدَ قُبَاءَ، فَصَلَّى فِيهِ صَلاَةً، كَانَ لَهُ كَأَجْرِ عُمْرَةٍ))

***((Atakayejitwahirisha nyumbani kwake kisha akafika Masjid Qubaa akaswali humo atapata ujira kama wa 'Umrah))***[138]

Kuzuru sehemu zifuatazo si lazima kwani baadhi ya Wanachuoni wameona kuwa hakuna dalili za kuzuru. Lakini ukipenda kuzuru hakuna ubaya.

**Al-Baqi'i**: Makaburi walipozikwa Maswahaba wengi.

Utatembelea kaburi la 'Uthmaan bin 'Afaan (رضي الله عنه). Utasimama mbele yake na kumsalimia kwa kusema:

السَّلاَمُ عَلَيْكَ

***Assalaamu 'Alayka***

رَضِيَ اللَّهُ عَنْكَ وَجَزَاكَ اللَّهُ عَنْ أُمَّةِ مُحَمَّدٍ أَفْضَلَ جَزَاء

***Radhiya-Allaahu 'anka wa Jazaaka-Allaahu 'an Ummati Muhammad afdhwal jazaa.***

Kisha utawasalimia Waislamu wengine waliofariki waliopo hapo makaburini Al-Baqi'i kwa kusema:

السَّلامُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الدِّيارِ مِنَ المؤْمِنينَ وَالْمُسْلِمِينَ، وَإِنَّا إِنْ شاءَ اللهُ بِكُمْ لاحقون، وَ يَرْحَمُ اللَّهُ الْمُسْتَقْدِمِينَ مِنَّا وَالْمُسْتَأْخِرِينَ, نَسْأَلُ اللهَ لَنا وَلَكُمُ العافِيَةَ.

---

138 At-Tirmidhiy na amesema Hadiyth Hasan Swahiyh, An-Nasaaiy, Ibn Maajah, Ahmad, na tazama *Silsilat Asw-Swahiyhah* ya Al-Abaaniy (3446).

***Assalaamu 'Alaykum Ahlad-Diyaari Minal-Muuminiyna Wal-Muslimiyn, Wa innaa In-shaa-Allaah Bikum Laahiquwn, Wayarhamu-Llahul-Mustaqdimiyna Minnaa Wal musta-akhiriyn) Nas-alu-Allaaha Lanaa Wa Lakumul-'Aafiyah***

"Amani ishuke juu yenu watu wa nyumba miongoni mwa Waumini na Waislamu, nasi Apendapo Allaah tutakutana nanyi, Na Allaah Awarehemu waliotangulia na watakaokuja mwisho. Tunamuomba Allaah Atupe sisi nanyi afya njema."

**Uhud:** Jabali ambalo vita vya pili vikuu vilitokea kati ya Waislamu na Makafiri na wakashindwa Waislamu kwa kutokumtii Rasuli ( صلى الله عليه وآله وسلم) baadhi ya amri zake.

Utakwenda kutembelea kaburi la Hamzah (رضي الله عنه) pamoja na mashahidi waliozikwa hapo. Utawatolea salamu na kuwaombea hivyo hivyo Du'aa ya kuzuru makaburi.

**Masjid Qiblatayn:** Msikiti ambao Waislamu kwanza walikuwa wakiswali kuelekea Masjidul-Aqswaa Palestina kisha Allaah ( سبحانه وتعالى) Akaamrisha kuelekea Masjid Al-Haraam kuwa ni Qiblah.

Ukipenda utakwenda na kuswali rakaa mbili *Tahiyyat Al-Masjid*.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa Madiynah**

- Kuitakidi kwamba kuswali Masjid An-Nabawiy siku arubaini, japo mashirika mengi ya Hajj ya Afrika Mashariki yanatanguliza kuwapeleka Mahujaji kuzuru Madiynah kwanza kwa siku nane ili Mahujaji wapate fadhila za kuswali Swalah arobaini katika Masjid An-Nabawiy, lakini kitendo hicho si sahihi na huwa wanategemea Hadiyth isiyo sahihi kuhusu Hadiyth iliyotaja fadhila za kuswali Swalah arobaini bila kukosa hata moja ili kepushwa na Moto, adhabu na unafiki, ambayo haikuthibiti! Ni bora kuepuka jambo hilo na ikiwa Mahujaji watahitaji kuzuru Msikiti wa Rasuli ( صلى الله عليه وآله وسلم), anaweza kufanya hilo baada ya kumaliza 'ibaadah yake ya Hajj.

- Kugusa na kusugua mikono katika kuta na nondo za chuma, kufunga nyuzi katika mihimili yake na vitendo vingine vya namna hiyo wakati wa kuzuru kaburi la Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa kutegemea kupata baraka. Hivyo ni bid'ah. Baraka zinapatikana kwa kufuata amri za Allaah (سبحانه وتعالى) na Rasuli Wake (صلى الله عليه وآله وسلم) na si kufuata mambo ya kuzushwa yasiyo na manufaa.

- Kulazimisha kuswali katika Rawdhwah ambayo ni sehemu ndogo mno, na kufanya hivyo ni kusababisha zahma, misukumano na Waislamu hadi kujeruhiana na kusababisha kukanyagana. Baadhi ya watu huingia kwa kukimbia mbio na kusababisha fujo mno.

- Katika ziara, kupanda na kuingia mapango ya jabali la Uhud au mapango ya jabali la *Al-Hiraa* au *Ath-Thawr* karibu na Makkah na kutundika vitambara au kuomba du'aa huko. Haya hayamo katika mafunzo ya Dini na yote hayo ni kujitakia mashaka na tabu kwani ni mambo ya bid'ah katika Dini na wala hayana msingi katika shariy'ah.

- Kuzuru sehemu nyingine kwa kudhania kuwa sehemu hizo ni athari za mabaki ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم). Mfano sehemu ambayo ngamia wake alikaa, au kisima cha 'Uthmaan (رضي الله عنه) na kukusanya udongo sehemu hizo kwa kutegemea kupata baraka, yote ni mambo ya bid'ah.

- Kuwaita waliokufa wakati wa kuzuru makaburi ya Al-Baqi'i au makaburi ya Mashuhadaa wa Uhud na kurusha sarafu ili kutegemea kupata baraka za sehemu waliozikiwa watu. Hayo ni makosa makubwa kabisa bali ni shirki na Qur-aan na Sunnah imekemea mno vitendo hivo. 'Ibaadah zote zinapasa ziwe kwa ajili ya Allaah (سبحانه وتعالى) Pekee Ambaye Anasema:

﴿ وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ ﴾

**((Na hawakuamrishwa (chochote kile) isipokuwa wamwabudu Allaah wakiwa wenye kumtakasia Dini, *Hunafaa* (wakielemea haki na kujiengua na upotofu))**[139]

﴿ وَأَنَّ ٱلۡمَسَٰجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدۡعُواْ مَعَ ٱللَّهِ أَحَدٗا ١٨ ﴾

**((Na kwamba Misikiti ni (kwa ajili) ya Allaah, basi msiombe yeyote pamoja na Allaah)).**[140]

﴿ قُلۡ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحۡيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ١٦٢ ﴾

**((Sema: "Hakika Swalaah yangu, na *nusukiy* (kuchinja kafaara na 'ibaadah zangu) na uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allaah (Pekee) Rabb wa walimwengu"))**[141]

---

139 Al-Bayyinah (98: 5).
140 Al-Jinn (72: 18).
141 Al-An'aam (6: 162).

## 18- Swalaah Ya Janaazah

Du'aa za Maiti Katika Swalaah Ya Janaazah:

Jumla ni takibrah nne;

1. Ya kufungulia Swalaah na kusoma Suratul-Faatihah.
2. *Swalaatul-Ibraahimiyyah* (kumswalia Nabiy صلى الله عليه وسلم kama kwenye Swalaah).
3. Kumwombea maiti du'aa zinazotajwa chini hapa.
4. Kutoa salamu upande wa kulia.

**Maiti mwanamume utamuombea du'aa ifuatayo**:

اللَّهُمِّ اغْفِرْ لَهُ وَارْحَمْه، وَعافِهِ وَاعْفُ عَنْه، وَأَكْرِمْ نُزُلَه، وَوَسِّعْ مُدْخَلَه، وَاغْسِلْهُ بِالْماءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدْ، وَنَقِّهِ مِنَ الْخَطايا كَما نَقّيْتَ الثَّوْبُ الأَبْيَضُ مِنَ الدَّنَسْ، وَأَبْدِلْهُ داراً خَيْراً مِنْ دارِه، وَأَهْلاً خَيْراً مِنْ أَهْلِه، وَزَوْجاً خَيْراً مِنْ زَوْجِه، وَأَدْخِلْهُ الْجَنَّة، وَأَعِذْهُ مِنْ عَذابِ القَبْر وَعَذابِ النّار

***Allaahumma-Ghfir-lahu warhamhu, wa 'aafihi wa'afu 'anhu, wa akrim nuzulahu, wawassi' mudkhalahu, waghsilhu bilmaai wath-thalji walbaradi, wanaqqihi minal-khatwaayaa kamaa yunaqqath-thawbul abyadhwu minad-danas, wa abdilhu daaran khayran min daarihi, wa ahlan khayran min ahlihi, wazawjan khayran min zawjihi, wa adkhilhul-Jannah, wa a'idh-hu min 'adhaabil-qabri, wa 'adhaabin-naar***

Eee Allaah, Mghufurie na Mrehemu, na Muafu na Msamehe na Mtukuze kushuka kwake (kaburini) na Mpanulie kuingia kwake, na Muoshe na maji na kwa theluji na barafu na Mtakase na makosa kama inavyotakaswa nguo nyeupe kutokana na uchafu, na Mbadilishie nyumba bora kuliko nyumba yake na jamaa bora kuliko jamaa zake, na mke bora kuliko mke wake, na Muingize Jannah na Mkinge na adhabu ya kaburi (na adhabu ya moto).[142]

[142] Muslim (2/663), An-Nasaaiy, Musnad Ahmad.

**Maiti mmoja mwanamke utamuombea du'aa ifuatayo:**

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لَهَا وَارْحَمْهَا, وَعَافِهَا وَاعْفُ عَنْهَا, وَأَكْرِمْ نُزُلَهَا, وَوَسِّعْ مُدْخَلَهَا, وَاغْسِلْهَا بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدِ, وَنَقِّهَا مِنْ الْخَطَايَا كَمَا نَقَّيْتَ الثَّوْبَ الأَبْيَضَ مِنْ الدَّنَسِ, وَأَبْدِلْهَا دَارًا خَيْرًا مِنْ دَارِهَا, وَأَهْلاً خَيْرًا مِنْ أَهْلِهَا, وَزَوْجًا خَيْرًا مِنْ زَوْجِهَا, وَأَدْخِلْهَا الْجَنَّةَ, وَأَعِذْهَا مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ وَعَذَابِ النَّارِ

***Allaahumma-Ghfir lahaa warhamhaa, wa 'aafihaa wa'fu 'anhaa, wa akrim nuzulahaa, wawassi' mudkhalahaa, waghsilhaa bilmaai wath-thalji walbarad, wanaqqiha minal-khatwaayaa kamaa yunaqqath-thawbul abyadhwu minad-danas, wa abdilhaa daaran khayran min daarihaa, wa ahlan khayran min ahlihaa, wazawjan khayran min zawjihaa, wa adkhilhal-jannah, waa'idh-haa min 'adhaabil-qabri, wa 'adhaabin-naar***

**Maiti zaidi ya mmoja utawaombea du'aa ifuatayo**

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لَهُمْ وَارْحَمْهُمْ, وَعَافِهِمْ وَاعْفُ عَنْهُمْ, وَأَكْرِمْ نُزُلَهُمْ, وَوَسِّعْ مُدْخَلَهُمْ, وَاغْسِلْهُمْ بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدِ, وَنَقِّهِمْ مِنْ الْخَطَايَا كَمَا نَقَّيْتَ الثَّوْبَ الأَبْيَضَ مِنْ الدَّنَسِ, وَأَبْدِلْهُمْ دَارًا خَيْرًا مِنْ دَارِهِمْ, وَأَهْلاً خَيْرًا مِنْ أَهْلِهِمْ, وَزَوْجًا خَيْرًا مِنْ زَوْجِهِمْ, وَأَدْخِلْهُمْ الْجَنَّةَ, وَأَعِذْهُمْ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ وَعَذَابِ النَّارِ

***Allaahumma-Ghfir lahum warhamhum, wa 'aafihim wa'fu 'anhum, wa akrim nuzulahum, wawassi' mudkhalahum, waghsilhum bilmaai wath-thalji walbarad, wanaqqihim minal-khatwaayaa kamaa yunaqqath-thawbul abyadhwu minad-danas, wa abdilhum daaran khayran min daarihim, wa ahlan khayran min ahlihim, wa azwaajan khayran min azwaajihim, waadkhilhumul-Jannah, wa a'idh-hum min 'adhaabil-qabri, wa 'adhaabin-naar***

**Du'aa nyinginezo**

**اللهُمّ اغْفِرْ لِحَيِّنا وَمَيِّتِنا وَشاهِدِنا، وَغائِبِنا، وَصَغيرِنا وَكَبيرِنا، وَذَكَرِنا وَأُنْثانا. اللهُمّ مَنْ أَحْيَيْتَهُ مِنّا فَأَحْيِهِ عَلى الإِسْلام ،وَمَنْ تَوَفَّيْتَهُ مِنّا فَتَوَفَّهُ عَلى الإِيمان، اللهُمّ لا تَحْرِمْنا أَجْرَه، وَلا تُضِلَّنا بَعْدَهُ**

***Allaahumma-Ghfir li-hayyinaa wamayyitinaa, washaahidinaa, waghaaibinaa, waswaghiyrinaa, wakabiyrinaa, wadhakarinaa, waunthaanaa. Allaahumma man ahyaytahu minnaa fa-Ahyihi 'alal-Islaami, waman tawaffaytahu minnaa fatawaffahu 'alal-iymaan. Allaahumma laa tahrimnaa ajrahu, walaa tudhwillanaa ba'dahu***

Ee Allaah, Mghufurie aliyehai katika sisi na aliyekufa, aliyepo na asiyekuwepo, mdogo kati yetu na mkubwa, mwanamume kati yetu na mwanamke. Ee Allaah, Unaemweka hai kati yetu basi Muweke katika Uislamu, na Unayemfisha basi mfishe juu ya iymaan. Ee Allaah, Usitunyime thawabu zake wala usitupoteze baada yake.[143]

---

[143] Ibn Maajah (1/480) Ahmad (2/368), Abu Daawuwd, At-Tirmidhiy, tazama *Swahiyh Abi Daawuwd* (3201) *Swahiyh Ibn Maajah* (1/251).

### 19- Du'aa Zilizopokelewa Kutoka Kwa Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم)

Muislamu anatakiwa ahakikishe du'aa anazoziomba ni ambazo zimethibiti katika Sunnah ya Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). Makosa yanatendeka watu kuacha du'aa hizo na kusoma du'aa zilotungwa ambazo nyinginezo zimekuwa maarufu mno katika vijitabu vinavyouzwa au kugaiwa.

Zifuatazo ni du'aa zilothibiti kutoka kwa Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) na zinamtosheleza kabisa mtu kuziomba kwa kuwa zimejaa hikmah, fadhila na manufaa ya duniani na Aakhirah:

❖ **Du'aa Alizokuwa Akiomba Sana Rasuli** (صلى الله عليه وآله وسلم):

Kuomba kheri za dunia na Aakhirah:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الأَخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

***Rabbaana aatinaa fid-ddun-yaa hasanatan wafil Aakhirati hasanatan wa qinaa adhaaban-naari***[144]

Rabb wetu, tupe katika dunia mema na katika Aakhirah mema na Tukinge adhabu ya Moto.[145]

Kuthibitika Katika Dini Na Utiifu:

يَا مُقَلِّبَ الْقُلُوبِ ثَبِّتْ قَلْبِي عَلَى دِينِك

***Yaa muqallibal quluwbi, thabbit qalbiy 'alaa Diynika***

Ee Mwenye kupindua nyoyo, Thibitisha moyo wangu katika Dini Yako.[146]

اللَّهُمَّ مُصَرِّفَ الْقُلُوبِ صَرِّفْ قُلُوبَنَا عَلَى طَاعَتِكَ

---

[144] Hii pia ni Du'aa zenye mjumuisho wa maana nyingi katika maneno machache.
[145] Al-Bukhaariy, Muslim.
[146] At-Tirmidhiy, Ibn Maajah, Ahmad, Al-Haakim na tazama *Swahiyh Al-Jaami'* 7987.

***Allaahumma Muswarrifal quluwbi, swarrif quluwbanaa 'alaa twaa'atika***

Ee Allaah, Mwenye kugeuza nyoyo, zigeuze nyoyo zetu katika utiifu Wako.[147]

### ❖ Du'aa Za Maombi Ya Ujumla:

اللَّهُمَّ إِنِي أَسْأَلُكَ مِنَ الْخَيْرِ كُلِّهِ عَاجِلِهِ وَآجِلِهِ مَا عَلِمْتُ مِنْهُ وَمَا لَمْ أَعْلَمْ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الشَّرِّ كُلِّهِ عَاجِلِهِ وَآجِلِهِ مَا عَلِمْتُ مِنْهُ وَمَا لَمْ أَعْلَمْ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِ مَا سَأَلَكَ عَبْدُكَ وَنَبِيُّكَ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا استعَاذَ بِكَ مَنْهُ عَبْدُكَ وَنَبِيُّكَ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْجَنَّةَ وَمَا قَرَّبَ إِلَيْهَا مِنْ قَوْلٍ أَوْ عَمَلٍ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ النَّارِ وَمَا قَرَّبَ إِلَيْهَا مِنْ قَوْلٍ أَوْ عَمَلٍ، وَأَسْأَلُكَ أَنْ تَجْعَلَ كُلَّ قَضَاءٍ قَضَيْتَهُ لِي خَيْرًا

***Allaahumma inniy as-aluka minal-khayri kullihi 'aajilihi wa aajilihi, maa 'alimtu minhu wamaa lam a'lam. Wa a'uwdhu Bika minash-sharri kullihi 'aajilihi wa aajilihi maa 'alimtu minhu wamaa lam a'lam. Allaahumma inniy as-aluka min khayri maa saalaka 'Abduka wa Nabiyyuka, wa a'uwdhu Bika min sharri masta'aadha Bika minhu 'Abduka wa Nabiyyuka. Allaahumma inniy as-alukal-Jannata wamaa qarraba ilayhaa min qawlin aw 'amal, wa a'uwdhu Bika minan-nnaari wamaa qarraba ilayhaa min qawlin aw 'amal, wa as-aluka antaj-'ala kulla qadhwaai qadhwaytahu liy khayraa***

Ee Allaah, hakika mimi nakuomba kheri zote zilizokaribu na mbali nizijuazo na nisizozijua. Najikinga Kwako shari zote za karibu na za mbali nizijuazo na nisizozijua. Ee Allaah, hakika nakuomba kheri alizokuomba mja Wako na Nabiy Wako, na najikinga Kwako shari alizojikinga nazo mja Wako na Nabiy wako. Ee Allaah, hakiki mimi nakuomba Jannah na yanayokaribisha kwayo katika kauli au 'amali, na najikinga Kwako Moto na yanayokaribisha kwayo katika kauli au 'amali, na nakuomba Ujaalie kila majaaliwa yangu [uliyonikidhia] yawe kheri.[148]

---

[147] Muslim.
[148] Ibn Maajah – Ametaja katika mlango aliosimulia Hadiyth kwa anuani ya 'Du'aa za '*Jawaami Al-Kalimi*'.

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى

***Allaahumma inniy as-alukal-hudaa wat -ttuqaa wal 'afaafa wal ghinaa***

Ee Allaah hakika mimi nakuomba uongofu na uchaji Allaah na kujichunga[149] na kutosheka.[150]

❖ **Du'aa Kuomba Hidaaya:**

اللَّهُمَّ اهْدِنِي وَسَدِّدْنِي, اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالسَّدَادَ

***Allaahumma-hdiniy wasaddid-niy, Allaahumma inniy as-alukal-hudaa was-ssadaad***

Ee Allaah, niongoe na nionyoshe sawasawa. Ee Allaah hakika mimi nakuomba hidaaya na unyofu[151]

❖ **Du'aa Kuomba Hesabu Nyepesi Aakhirah Na Kuwa Pamoja na Nabiy** (صلى الله عليه وآله وسلم):

اللَّهُمَّ حَاسِبْنِي حِسَابًا يَسِيرًا

***Allaahumma haasibniy hisaaban -yasiyraa***

Ee Allaah nihesabie hisabu iliyo sahali.[152]

---

149 Staha na sitara, kujichunga na machafu.
150 Muslim.
151 Muslim.
152 Ahmad - 'Aaishah (رضي الله عنها) alimuuliza Rasuli (صلى الله عليه وسلم) alipomaliza kuisoma du'aa katika Swalaah: "Ipi hesabu iliyo sahali?" Akasema: **((Kwamba [Allaah] Atazame kitabu chake (kilorekodiwa 'amali] kisha Amsamehe, hakika mwenye kuhojiwa hesabu siku hiyo ee 'Aaishah ameangamia, na kila kinachomsibu Muumini Allaah** عز وجل **Humfutia ([dhambi] japo ikiwa ni mwiba umchomao)).**

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ إِيمَانًا لاَ يَرْتَدُّ, وَنَعِيمًا لاَ يَنْفَدُ, وَمُرَافَقَةَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي أَعْلَى غُرَفِ الْجَنَّةِ جَنَّاتِ الْخُلْدِ

***Allaahumma inniy as-aluka iymaanan laa yartaddu, wa na'iyman laa yanfaddu, wa muraafqatan-Nabiyyi Swalla-Allaahu 'alayhi wa sallam fiy a'-laa ghurafil-Jannah, Jannaatil-khuldi***

Ee Allaah, hakika nakuomba iymaan isiyoritadi [isiyobadilika], na neema zisizoisha na kuambatana na Nabiy Swalla-Allaahu 'alayhi wa sallam katika vyumba vya ghorofa za juu kabisa Jannah, Jannah za kudumu milele.[153]

❖ **Du'aa Kuomba Wingi Wa Iymaan, Taqwa Na Hifadhi:**

اللَّهُمَّ أَعِنِّي عَلَى ذِكْرِكَ وَشُكْرِكَ وَحُسْنِ عِبَادَتِكَ

***Allaahumma a'inniy 'alaa dhikrika, wa shukrika wa husni 'ibaadatika***

Ee Allaah nisaidie juu ya utajo Wako [kukudhukuru], na kukushukuru na uzuri wa 'ibaadah Zako.[154]

اللَّهُمَّ اقْسِمْ لَنَا مِنْ خَشْيَتِكَ مَا يَحُولُ بَيْنَنَا وَبَيْنَ مَعَاصِيكَ، وَمِنْ طَاعَتِكَ مَا تُبَلِّغُنَا بِهِ جَنَّتَكَ، وَمِنَ الْيَقِينِ مَا تُهَوِّنُ بِهِ عَلَيْنَا مُصِيبَاتِ الدُّنْيَا، وَمَتِّعْنَا بِأَسْمَاعِنَا وَأَبْصَارِنَا وَقُوَّتِنَا مَا أَحْيَيْتَنَا, وَاجْعَلْهُ الْوَارِثَ مِنَّا، وَاجْعَلْ ثَأْرَنَا عَلَى مَنْ ظَلَمَنَا وَانْصُرْنَا عَلَى مَنْ عَادَانَا، وَلا تَجْعَلْ مُصِيبَتَنَا فِي دِينِنَا، وَلا تَجْعَلْ الدُّنْيَا أَكْبَرَ هَمِّنَا وَلا مَبْلَغَ عِلْمِنَا، وَلا تُسَلِّطْ عَلَيْنَا مَنْ لا يَرْحَمُنَا

***Allaahumma-qsim-lanaa min khash-yatika maa yahuwlu baynanaa wa bayna ma'swiyk, wamin twaa'atika maa tuballighunaa bihi Jannatak, wa minal-yaqiyni maa tuhawwinu***

---

[153] Ahmad, na Ibn Hibbaan kwa njia nyingine. Tazama pia *As-Silsilah Asw-Swahiyhah* (5/379).

[154] Abu Daawuwd, Ahmad na kwa usimilizi tofauti kidogo kutoka kwa An-Nasaaiy. Wasia wa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alompa 'Mu'aadh bin Jabal (رضي الله عنه) aombe du'aa hii kila baada ya Swalaah.

***bihi 'alaynaa muswiybaatid-dun-yaa, wa matti'-naa biasmaa'inaa wa abswaarinaa wa quwwaatinaa maa ahyaytanaa waj-'alhul-waaritha minnaa waj-'al thaaranaa 'alaa man dhwalamanaa wanswurnaa 'alaa man 'aadaana, walaa taj-'al muswiybatanaa fiy diyninaa, walaa taj-'alidduniya akbara hamminaa walaa mablagha 'ilminaa, walaa tusallitw 'alaynaa man-llaa yarhamunaa***

Ee Allaah tugawanyie sisi khofu Yako itakayotenganisha baina yetu na baina maasi Yako, na utiifu utakaotufikisha katika Jannah Yako, na yaqini itakayotusahilishia misiba ya dunia, na tustareheshe kwa masikio yetu, na macho yetu, na nguvu zetu madamu Utatuweka hai, na yajaalie yawe ni urithi wetu na Jaalia iwe lipizo kwa anayetudhulumu, na tunusuru dhidi ya anayetufanyia uadui, na wala Usitufanyie msiba wetu ni Dini yetu, wala Usifanye dunia kuwa ndio hima yetu kubwa kabisa, na wala upeo wa elimu yetu, wala Usitusaliti kwa asiyetuhurumia.[155]

### ❖ Du'aa Akitamani Mtu Kufa Kutokana Na Mateso Ya Dunia:

اللَّهُمَّ بِعِلْمِكَ الْغَيْبَ وَقُدْرَتِكَ عَلَى الْخَلْقِ أَحْيِنِي مَا عَلِمْتَ الْحَيَاةَ خَيْرًا لِي، وَتَوَفَّنِي إِذَا عَلِمْتَ الْوَفَاةَ خَيْرًا لِي، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَشْيَتَكَ فِي الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ، وَأَسْأَلُكَ كَلِمَةَ الْحَقِّ فِي الرِّضَا وَالْغَضَبِ، وَأَسْأَلُكَ الْقَصْدَ فِي الْغِنَى وَالْفَقْرِ، وَأَسْأَلُكَ نَعِيمًا لا يَنْفَدُ، وَأَسْأَلُكَ قُرَّةَ عَيْنٍ لا تَنْقَطِعُ وَأَسْأَلُكَ الرِّضَاءَ بَعْدَ الْقَضَاءِ، وَأَسْأَلُكَ بَرْدَ الْعَيْشِ بَعْدَ الْمَوْتِ وَأَسْأَلُكَ لَذَّةَ النَّظَرِ إِلَى وَجْهِكَ وَالشَّوْقَ إِلَى لِقَائِكَ فِي غَيْرِ ضَرَّاءَ مُضِرَّةٍ وَلا فِتْنَةٍ مُضِلَّةٍ، اللَّهُمَّ زَيِّنَّا بِزِينَةِ الإِيمَانِ وَاجْعَلْنَا هُدَاةً مُهْتَدِينَ

***Allaahumma bi'ilmikal-ghayba wa qudratika 'alal-khalqi, ahyiniy maa 'alimtal-hayaata khayral-liy, wa tawaffaniy idhaa 'alimtal-wafaata khayral-liy. Allaahumma inniy as-aluka khash-yataka fil-ghaybi wash-shahaadah, wa as-aluka kalimatal-haqqi fir-ridhwaa wal-ghadhwabi, wa as-alukal-qaswda fil-ghinaa wal-faqri, wa as-aluka na'iyman-llaa yanfadu, wa as-aluka qurrata 'aynin-llaa tanqatwi'u, wa as-alukar-ridhwaa ba'-dal-qadhwaai, wa as-aluka bardal-'ayshi ba'-dal-mawti, wa as-aluka laddhatan-nadhwari ilaa Wajhika, wash-shawqa ilaa liqaaika fiy***

155 *Swahiyh At-Tirmidhiy* 3502, *Swahiyh Al-Jaami'* 1268.

***ghayri dhwarraai mudhwirratin walaa fitnatin mudhwillatin. Allaahumma zayyinaa biziynatil-iymaani waj-'alnaa hudaatan muhtadiyna***

Ee Allaah naomba kwa ujuzi Wako wa ghayb na uwezo Wako juu viumbe, nihuishe ikiwa Unajua uhai ni kheri kwangu, na nifishe ikiwa Unajua kufa ni kheri kwangu. Ee Allaah, nakuomba khofu Yako katika siri na dhahiri, na nakuomba Unifanye mkweli katika kauli wakati wa furaha na ghadhabu, na nakuomba unifanye wastani wakati wa utajiri na umasikini, na nakuomba neema isiyokoma, na kitulizo cha macho kisichokatika, na nakuomba niridhike Uliyonikidhia na nakuomba maisha mepesi baada ya mauti, na nakuomba ladha ya kuutazama Wajihi Wako na shauku ya kukutana Nawe, pasi na madhara yanayodhuru au fitnah itakayosababisha upotofu. Ee Allaah, tupambie kwa pambo la iymaan na tujaalie wenye kuongoza na kuongoka.[156]

❖ **Du'aa Kutengenezewa Dini Na Maisha Bora Duniani Na Aakhirah:**

اللَّهُمَّ أَصْلِحْ لِي دِينِي الَّذِي هُوَ عِصْمَةُ أَمْرِي, وَأَصْلِحْ لِي دُنْيَايَ الَّتِي فِيهَا مَعَاشِي, وَأَصْلِحْ لِي آخِرَتِي الَّتِي فِيهَا مَعَادِي, وَاجْعَلْ الْحَيَاةَ زِيَادَةً لِي فِي كُلِّ خَيْرٍ, وَاجْعَلْ الْمَوْتَ رَاحَةً لِي مِنْ كُلِّ شَرٍّ

***Allaahumma aswlih-liy diyni-lladhiy huwa 'iswmatu amriy, wa aswlih-liy dun-yaaya-llatiy fiyhaa ma'aashiy, wa aswlih-liy Aakhirati-llaty fiyhaa ma'aadiy, waj-'alil-hayaata ziyaadatan-lliy fiy kulli khayr, waj-'alil-mawta raahatan-lliy min kulli sharr.***

Ee Allaah, nitengenezee Dini yangu ambayo ndio asasi ya mambo yangu, na nitengenezee dunia yangu ambayo humo ni maisha yangu, na nitengenezee Aakhirah yangu ambayo humo ni marejeo yangu, na Jaalia uhai wangu uwe wenye ziada ya kila kheri, na Jaalia mauti kwangu yawe ya raha kutokana na kila shari.[157]

---

[156] *Swahiyh Sunan An-Nasaaiy* (1/280/281), Ahmad (4/364) kwa isnaad nzuri.
[157] Muslim.

### ❖ Du'aa Kuomba Baraka Za Mali, Watoto, Umri Wa Utiifu:

اللَّهُمَّ أَكْثِرْ مَالِي وَوَلَدِي وَبَارِكْ لِي فِيمَا أَعْطَيْتَنِي وَأَطِلْ حَيَاتِي عَلى طَاعَتِكَ وَأَحْسِنْ عَمَلِي وَاغْفِرْلِي

***Allaahumma akhthir maaliy wa waladiy wa Baarikliy fiymaa a'twaytaniy. Wa atwil hayaatiy 'alaa twaa'atika wa ahsin 'amaliy, waghfir-liy***

Ee Allaah, ikithirishe mali yangu na watoto wangu, na nibarikie katika Uliyonipa,[158] na nipe uhai mrefu niwe katika utiifu Wako, na boresha 'amali zangu na nighufurie.[159]

### ❖ Du'aa Kuomba Afya Duniani Na Aakhirah:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَافِيَةَ فِي الدُّنْيَا وَالأَخِرَةِ

***Allaahumma inniy as-alukal-'aafiyata fid-dun-yaa wal-Aakhirah***

Ee Allaah hakika mimi nakuomba afya duniani na Aakhirah.[160]

أللَّهُمَّ أَحْسِنْ عَاقِبَتَنَا فِي الأَمُورِ كُلِّهَا وَأَجِرْنَا مِنْ خِزْيِ الدُّنْيَا وَعَذَابِ الأَخِرَةِ

***Allaahumma ahsin 'aaqibatanaa fil-umuwri kullihaa wa ajirnaa min khizyid-dun-yaa wa adhaabil-Aakhirah***

Ee Allaah fanya mwema mwisho wetu katika mambo yote, na tuokoe hizaya ya dunia na adhabu ya Aakhirah.[161]

---

[158] Al-Bukhaariy, Muslim, At-Tirmidhiy, Ahmad – Du'aa ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa Anas (رضي الله عنه).

[159] Al-Bukhaariy katika *Aadaab Al-Mufrad* (653) na ameipa daraja Swahiyh Al-Albaaniy katika *Silsilatul-Ahaadiyth Asw-Swahiyhah* (2241).

[160] *Swahiyh At-Tirmidhiy* (3/180, 185, 170).

[161] Ahmad.

رَبِّ أَعِنِّي وَلاَ تُعِنْ عَلَيَّ, وَانْصُرْنِي وَلاَ تَنْصُرْ عَلَيَّ , وَامْكُرْ لِي وَلاَ تَمْكُرْ عَلَيَّ, وَاهْدِنِي وَيَسِّرِ الْهُدَى إِلَيَّ, وَانْصُرْنِي عَلَى مَنْ بَغَى عَلَيَّ. رَبِّ اجْعَلْنِي لَكَ شَكَّارًا, لَكَ ذَكَّارًا, لَكَ رَهَّابًا, لَكَ مُطِيعًا, إِلَيْكَ مُخْبِتًا أَوَّاهًا مُنِيبًا. رَبِّ تَقَبَّلْ تَوْبَتِي, وَاغْسِلْ حَوْبَتِي, وَأَجِبْ دَعْوَتِي, وَثَبِّتْ حُجَّتِي, وَاهْدِ قَلْبِي, وَسَدِّدْ لِسَانِي, , وَاسْلُلْ سَخِيمَةَ قَلْبِي

***Rabbi a'inniy walaa tu'in 'alayya, wanswurniy walaa tanswur 'alayya, wamkur-liy walaa tamkur 'alayya, wahdiniy wa yassiril-hudaa ilayya, wanswurniy 'alaa man baghaa 'alayya. Rabbij-'alniy Laka shakkaaraa, Laka dhakkaaraa, Laka Rahhaaba, Laka mutwi'y-aa, ilayka mukhbitan awwaaham-muniybaa. Rabbi taqabbal tawbatiy, waghsil hawbatiy, wa ajib da'-watiy wahdi qalbiy, wa saddid lisaaniy, wa thabbit hujjatiy, waslul sakhiymata qalbiy***

Ee Mola wangu nisaidie na Usisaidie dhidi yangu, na ninusuru wala Usinusuru dhidi yangu, na nipangie na Usipange dhidi yangu, na niongoze na usahilishe uongofu kunijia na ninusuru dhidi ya atakayenifanyia uovu. Mola wangu nijaalie niwe mwenye kukushukuru, mwenye kukudhukuru, mwenye kukuogopa, mwenye kukutii, mwenye kukukhofu, mwenye kunyenyekea na kurudia kuomba tawbah. Mola wangu pokea tawbah yangu, na osha madhambi yangu, na Itikia du'aa zangu, na thibitisha hoja zangu, na Ongoa moyo wangu, na Nyosha ulimi wangu [useme kweli], na futa [ondosha] uovu wa moyo wangu.[162]

❖ **Du'aa Kuomba Hifadhi, Kheri Zote, na Kujikinga Shari Zote:**

اَللَّهُمَّ احْفَظْنِي بِالإِسْلاَمِ قَائِمًا، وَاحْفَظْنِي بِالإِسْلاَمِ قَاعِداً، وَاحْفَظْنِي بِالإِسْلاَمِ رَاقِداً، وَلاَ تُشْمِتْ بِي عَدُوًا وَلاَ حَاسِداً. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ كُلِّ خَيْرٍ خَزَائِنُهُ بِيَدِكَ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ كُلِّ شَرٍّ خَزَائِنُهُ بِيَدِك

***Allaahummah-fadhwniy bil Islaami qaaimaa, wahfadhwniy bil Islaami qaaidaa, wahfadhwniy bil Islaami raaqidaa, walaa tushmit biy 'aduwwan walaa haasidaa. Allaahumma inniy as-***

[162] Abu Daawuwd, At-Tirmidhiy, Ibn Maajah – tazama *Swahiyh At-Tirmidhiy* (3/178) na Ahmad (1/127).

***aluka min kulli khayrin khazaainuhu Biyadika, wa a'uwdhu Bika min kulli sharrin khazaainuhu Biyadika***

Ee Allaah, nihifadhi katika Uislamu nikiwa nimesimama, na nihifadhi katika Uislamu nikiwa nimekaa, na nihifadhi katika Uislamu nikiwa nimelala, wala Usinijaalie kuwa bezo la adui wala hasidi. Ee Allaah, hakika mimi nakuomba kila kheri ambazo hazina zake zimo Mikononi Mwako, na najikinga Kwako shari zote ambazo hazina zake zimo Mikononi Mwako.[163]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مُوجِبَاتِ رَحْمَتِكَ, وَعَزَائِمَ مَغْفِرَتِكَ, وَالسَّلامَةَ مِنْ كُلِّ إِثْمٍ, وَالْغَنِيمَةَ مِنْ كُلِّ بِرٍّ, وَالْفَوْزَ بِالْجَنَّةِ, وَالنَّجَاةَ مِنَ النَّارِ

***Allaahumma inniy as-aluka muwjibaati Rahmatik wa 'azaaima maghfiratik was salaamata minkulli ithm, wal ghaniymata minkulli birr, wal fawza bil Jannati, wan najaata minan-naari***

Ee Allaah hakika mimi nakuomba azima za Rahmah Yako, azimio la maghfirah Yako, na amani katika kila dhambi, na ghanima katika kila jema, na kufuzu Jannah na kuokoka na Moto.[164]

اللَّهُمَّ اجْعَلْ أَوْسَعَ رِزْقِكَ عَلَيَّ عِنْدَ كِبَرِ سِنِّي وَانْقِطَاعِ عُمُرِي

***Allaahummaj-'al awsa'a rizqika 'alayya 'inda kibari sinniy wanqitwaa'i 'umriy***

Ee Allaah, Jaalia ukunjufu wa rizki Yako kwangu wakati wa uzee wangu, na kukatika umri wangu.[165]

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ذَنْبِي، وَوَسِّعْ لِي فِي دَارِي، وَبَارِكْ لِي فِيمَا رَزَقْتَنِي

***Allaahummagh-fir-liy dhambiy, wa wass'i fiy daariy, wa Baarik fiymaa razaqtaniy***

---

[163] Al-Haakim, tazama *Swahiyh Al-Jaami'* (2/398) na *Ahaadiyth Asw-Swahiyhah* (4/54 – 1540).
[164] Al-Haakim (1/525) na ameipa daraja ya Swahiyh na ameiwafiki Adh-Dhahabiy.
[165] Al-Haakim, *Swahiyh Al-Jaami'* (1/396), *Ahaadiyth Asw-Swahiyhah* (1539)

Ee Allaah nighufurie dhambi zangu, na nipanulie katika nyumba yangu, na nibarikie katika Uliyoniruzuku.[166]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ وَرَحْمَتِكَ, فَإِنَّهُ لاَ يَمْلِكُهَا إِلاَّ أَنْتَ

***Allaahumma inniy as-aluka min-fadhwlika wa Rahmatika fainnahu laa yamlikuhaa illa Anta***

Ee Allaah, hakika mimi nakuomba kutokana na fadhila Zako na Rahmah Zako, kwani hakuna anayezimiliki ila Wewe.[167]

اللَّهُمَّ أَلِّفْ بَيْنَ قُلُوبِنَا, وَأَصْلِحْ ذَاتَ بَيْنِنَا, وَاهْدِنَا سُبُلَ السَّلاَمِ, وَنَجِّنَا مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ, وَجَنِّبْنَا الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ, وَبَارِكْ لَنَا فِي أَسْمَاعِنَا, وَأَبْصَارِنَا, وَقُلُوبِنَا, وَأَزْوَاجِنَا, وَذُرِّيَّاتِنَا, وَتُبْ عَلَيْنَا إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ, وَاجْعَلْنَا شَاكِرِينَ لِنِعْمَتِكَ مُثْنِينَ بِهَا قَابِلِيهَا وَأَتِمَّهَا عَلَيْنَا

***Allaahumma allif bayna quluwbinaa, wa aswlih dhaata bayninaa, wahdinaa subulas-ssalaami, wanajjinaa minadhw-dhwulumaati ilan-nnuwri, wa jannibnal-fawaahisha maa dhwahara minhaa wamaa batwan, wa Baarik-lanaa fiy asmaa'inaa, wa abswaarinaa, wa quluwbinaa, wa azwaajinaa, wa dhurriyaatinaa, watub 'alaynaa innaka Antat-Tawaabur-Rahiym, waj-'alnaa shaakiriyna lini'matika muthniyna bihaa qaabiliyhaa wa atimmahaa 'alaynaa***

Ee Allaah, unganisha baina ya nyoyo zetu, na Suluhisha yaliyo baina yetu na tuongoze njia ya amani, na tuokoe kutokana na kiza hadi kwenye Nuru, na tuepushe machafu ya dhahiri na ya siri, na tubarikie katika kusikia kwetu, kuona kwetu, nyoyo zetu, na wake zetu, na vizazi vyetu, na pokea tawbah zetu, hakika Wewe ni Mwingi wa kupokea tawbah, Mwenye Kurehemu, na tujaalie kuwa wenye kushukuru neema Zako, mwenye kukusifu kwazo wakati wa kuzipokea na zitimize kwetu.[168]

---

[166] At-Tirmidhiy, Ahmad, tazama *Swahiyh Al-Jaami'* (1265). Tazama pia *Zaad-Al-Ma'aad* (2/354).
[167] At-Twabaraaniy, *Swahiyh Al-Jaami'* (1/404), As-Sisilatul-*Ahaadiyth Asw-Swahiyhah* (4/57).
[168] Abu Daawuwd, Al-Haakim akasema ni Swahiyh kwa sharti ya Muslim, na ameikubali Adh- Dhahabiy (1/265).

❖ **Du'aa Kuomba Ya Kheri Kabisa Na Mengineyo Na Daraja Ya Juu katika Jannah:**

أللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَ الْمَسْأَلَةِ, وَخَيرَ الدُّعَاءِ, وَخَيْرَ النَّجَاحِ, وَخَيرَ الْعَمَلِ, وَخَيْرَ الثَّوَابِ, وَخَيْرَ الْحَيَاةِ, وَخَيرَ الْمَمَاتِ, وَثَبِّتْنِي, وَثَقِّلْ مَوَازِينِي, وَحَقِّقْ إِيمَانِي, وَارْفَعْ دَرَجَاتِي, وَتَقَبَّلْ صَلاَتِي, وَاغْفِرْ خَطِيئَتِي, وَأَسْأَلُكَ الدَّرَجَاتِ الْعُلَى مِنَ الْجَنَّةِ آمِينْ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ فَوَاتِحَ الْخَيْرِ, وَخَوَاتِمَهُ, وَجَوَامِعَهُ, وَأَوَّلَهُ, وَآخِرَهُ, وَظَاهِرَهُ, وَ بَاطِنَهُ, وَالدَّرَجَاتِ الْعُلَى مِنَ الْجَنَّةِ آمِينْ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَ مَا آتِي، وَخَيْرَ مَا أَفْعَلُ، وَخَيْرَ مَا أَعْمَلُ، وَخَيْرَ مَا بَطَنَ، وَخَيْرَ مَا ظَهَرَ، وَالدَّرَجَاتِ الْعُلَى مِنَ الْجَنَّةِ آمِينْ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ أَنْ تَرْفَعَ ذِكْرِي, وَتَضَعَ وِزْرِي, وَتُصْلِحَ أَمْرِي, وَتُطَهِّرَ قَلْبِي, وَتُحَصِّنَ فَرْجِي, وَتُنَوِّرَ قَلْبِي, وَتَغْفِرَ لِي ذَنْبِي, وَاَسْأَلُكَ الدَّرَجَاتِ الْعُلَى مِنَ الْجَنَّةِ آمِينْ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ أَنْ تُبَارِكَ فِي نَفْسِي, وَفِي سَمْعِي, وَفِي بَصَرِي, وَفِي رُوحِي, وَفِي خَلْقِي, وَفِي خُلُقِي, وَفِي أَهْلِي, وَفِي مَحْيَايَ, وفِي مَمَاتِي, وَفِي عَمَلِي, فَتَقَبَّلْ حَسَنَاتِي, وَاَسْأَلُكَ الدَّرَجَاتِ الْعُلَى مِنَ الْجَنَّةِ آمِينْ

***Allaahumma inniy as-aluka khayral-mas-alah, wa khayrad-du'aai, wa khayran-najaah, wa khayral-'amali, wa khayrath-thawaabi, wa khayral-hayaati, wa khayral-mamaati, wa thabbitniy, wa thaqqil mawaaziyniy, wa haqqiq iymaaniy, warfa' darajaatiy, wa taqabbal Swalaatiy, waghfir khatwiy-atiy, wa as-alukad-darajaatil 'ulaa minal-Jannah. Aamiyn. Allaahumma inniy as-aluka fawaatihal-khayri wa khawaatimahu, wa jawaami'ahu, wa awwalahu, wa- aakhirahu, wa dhwaahirahu, wa baatwinahu, wad-darajaatil 'ulaa minal-Jannati. Aamiyn. Allaahumma inniy as-aluka khayra maa aatiy, wa khayra maa af-'alu, wa khayra maa a-'malu, wa khayra maa batwana, wa khayra maa dhwahara, wad-darajaatil 'ulaa minal-Jannati. Aamiyn. Allaahumma inniy as-aluka an Tarfa'a dhikriy, wa tadhwa'a wizriy, wa tuswliha amriy, wa tutwahhira qalbiy, wa tuhaswina farjiy, wa tunawwira qalbiy, wa taghfiraliy dhambiy, wa as-alukad-darajaatil 'ulaa minal-Jannati. Aamiyn. Allaahumma inniy as-aluka an Tubaarika fiy nafsiy, wafiy sam-'iy, wafiy baswariy, wafiy ruwhiy, wafiy khalqiy, wafiy khuluqiy, wafiy ahliy, wafiy mahyaaya, wafiy mamaatiy, wafiy 'amaliy, fataqabbal hasanaatiy, wa as-alukaddarajaatil 'ulaa minal-Jannati. Aamiyn***

Ee Allaah hakika mimi nakuomba kheri ya maombi, na kheri ya du'aa, na kheri ya kufuzu, na kheri ya 'amali bora, na kheri ya thawabu na kheri ya uhai, na kheri ya mauti, na nithibitishe, na fanya nzito mizani yangu, na thibitisha iymaan yangu, na nyanyua daraja zangu, na kubali Swalaah zangu, na ghufuria madhambi yangu, na nakuomba daraja ya juu katika Jannah, Aamiyn. Ee Allaah hakika mimi nakuomba funguo za kheri, na hitimisho zake, na ujumla wake, na mwanzo wake, na mwisho wake, na dhahiri yake na undani wake, na daraja za juu katika Jannah, Aamiyn. Ee Allaah hakika mimi nakuomba kheri yanayokuja, kheri ya niyafanyayo, na mazuri niyatendayo, na mazuri yanayofichika, na mazuri yanayodhihiri, na daraja za juu katika Jannah, Aamiyn. Ee Allaah hakika mimi nakuomba upandishe utajo wangu na uondoe dhambi zangu, na utengeneze mambo yangu, na utwaharishe moyo wangu, na uhifadhi tupu zangu, na nawirisha moyo wangu, na unighufurie madhambi yangu, na nakuomba daraja za juu katika Jannah, Aamiyn. Ee Allaah hakika mimi nakuomba unibariki katika nafsi yangu, na kusikia kwangu, na kuona kwangu, na roho yangu, na umbile langu, na tabia yangu, na katika familia yangu, na katika uhai wangu, na katika mauti yangu, na katika 'amali zangu, basi nitakabalie mazuri yangu, na nakuomba daraja za juu katika Jannah, Aamiyn.[169]

**اللَّهُمَ قَنِّعْنِي بِمَا رَزَقْتَنِي, وَبَارِكْ لِي فِيهِ, وَاخْلُفْ عَلَيَّ كُلَّ غَائِبَةٍ لِي بِخَيرٍ**

***Allaahumma qanni-'niy bimaa razaqtaniy, wa Baarikliy fiyhi, wakhluf 'alayyah kulla ghaaibatin-liy bikhayr***

Ee Allaah, nikinaishe kwa Ulivyoniruzuku, na nibarikie ndani yake, na nifuatilishie [nibadilishie] kila kilicho mbali nami kwa kheri.[170]

**اللَّهُمَ إِنِّي أَسْأَلُكَ عِيشَةً تَقِيَّةً وَمِيتَةً سَوِيَّةً وَمَرَدًّا غَيْرَ مُخْزٍ**

***Allaahumma inni as-aluka 'iyshatan taqiyyatan wa miytatan sawiyyatan wa maraddan ghayra mukhzin***

---

[169] Ameitoa Al-Haakim kutoka kwa Ummu Salamah marfu'aa na ameipa daraja ya Swahiyh na ameikubali Adh-Dhahabiy (1/520).

[170] Al-Haakim na ameipa daraja ya Swahiyh na ameikubali Adh-Dhahabiy (1/510). Ibn Hajar Al-'Asqalaaniy ameipa daraja ya Hasan katika *Al-Futuhaat Ar-Rabbaaniyah* (4/384).

Ee Allaah hakika mimi nakuomba maisha ya uchaji Allaah na mauti ya sawasawa na marejeo [Kwako] bila ya hizaya.[171]

❖ **Du'aa Kuomba Wingi Wa Iymaan, Kujikinga Dhini Ya Kufru, Ufasiki Na Kuomba Husnul-Khaatimah (Mwisho Mwema), Na Mengineyo:**

اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ كُلُّهُ. اللَّهُمَّ لاَ قَابِضَ لِمَا بَسَطْتَ, وَلاَ بَاسِطَ لِمَا قَبَضْتَ, وَلاَ هَادِيَ لِمَا أَضْلَلْتَ, وَلاَ مُضِلَّ لِمَنْ هَدَيْتَ, وَلاَ مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ, وَلاَ مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ, وَلاَ مُقَرِّبَ لِمَا بَاعَدْتَ, وَلاَ مُبَاعِدَ لِمَا قَرَّبْتَ. اللَّهُمَّ ابْسُطْ عَلَيْنَا مِنْ بَرَكَاتِكَ, وَرَحْمَتِكَ, وَفَضْلِكَ ,وَرِزْقِكَ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ النَّعِيمَ الْمُقِيمَ الَّذِي لاَ يَحُولُ وَلاَيَزُولُ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ النَّعِيمَ يَوْمَ الْعَيْلَةِ وَالأَمْنَ يَوْمَ الْخَوْفِ. اللَّهُمَّ إِنِّي عَائِذٌ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا أَعْطَيْتَنَا, وَشَرِّ مَا مَنَعْتَ. اللَّهُمَّ حَبِّبْ إِلَيْنَا الإِيمَانَ وَزَيِّنْهُ فِي قُلُوبِنَا وَكَرِّهْ إِلَيْنَا الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ وَاجْعَلْنَا مِنَ الرَّاشِدِينَ. اللَّهُمَّ تَوَفَّنَا مُسْلِمِينَ وَأَحْيِنَا مُسْلِمِينَ وَأَلْحِقْنَا بِالصَّالِحِينَ غَيْرَ خَزَايَا وَلاَ مَفْتُونِينَ. اللَّهُمَّ قَاتِلْ الْكَفَرَةَ الَّذِينَ يُكَذِّبُونَ رُسُلَكَ وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِكَ, وَاجْعَلْ عَلَيْهِمْ رِجْزَكَ وَعَذَابَكَ. اللَّهُمَّ قَاتِلْ الْكَفَرَةَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ إِلَهَ الْحَقِّ

***Allaahumma lakal-Hamdu kulluhu. Allaahumma laa qaabidhwa limaa basattwa, walaa baaswitwa limaa qabadhwta, walaa haadiya limaa adhw-lalta, walaa mudhwilla liman hadayta, walaa mu'-twiya limaa mana'-ta, walaa maani'a limaa a'-twayta, walaa muqarriba limaa baa'adta, walaa mubaa'idaa limaa qarrabta. Allaahumma absitw 'alaynaa min Barakaatika, wa Rahmatika, wa fadhwlika, wa rizqika. Allaahumma inniy as-alukan-nna'iymal-muqiyma alladhiy laa yahuwlu walaa yazuwlu. Allaahumma inniy as-alukan-na'iyma yawmal-'aylati wal amna yawmal-khawfi. Allaahumma inniy 'aaidhum bika min sharri maa a'-twaytanaa, wa sharri maa mana'-ta. Allaahumma habbib ilaynaal-iymaana wa zayyanahu fiy quluwbina wa karrih ilaynal-kufra wal fusuwqa wal 'iswyaana waj-'alnaa minar-raashidiyna. Allaahumma tawaffanaa Muslimiyna wa ahyinaa Muslimiyna wa***

[171] Musnad Ahmad, Atw-Twabaraaniy kwa isnaad nzuri, na tazama *Majma' Az-Zawaaid* (10/179).

***alhiqnaa bisw-Swaalihiyna ghayra khazaaya walaa maftuwniyna. Allaahumma qaatilil-kafarata alladhiyna yukadh-dhibuwna Rusulaka wa yaswudduwna 'an Sabiylika, waj-'al 'alayhim rijzika wa 'adhaabika. Allaahumma qaatilil-kafarata alladhiyna uwtul-Kitaaba Ilaahal-haqq***

Ee Allaah, kuhimidiwa ni Kwako. Ee Allaah, hakuna mwenye kukunja [kuzuia] Ulivyovikunjua, wala mwenye kukunjua Ulivyokunja [Ulivyozuia], wala mwenye kuongoa Ulichokipotoa, wala mpotoshaji kwa Uliyemuongoa, wala mwenye kutoa Ulichonyima, wala mwenye kunyima Ulichoruzuku, wala mwenye kukurubisha Ulichoweka mbali, wala mwenye kuweka mbali Ulichokiweka karibu. Ee Allaah tukunjulie katika baraka Zako, na Rahmah Zako, na fadhila Zako, na rizki Yako. Ee Allaah hakika mimi nakuomba neema ya kudumu isiyobadilika wala kutoweka. Ee Allaah, hakika mimi nakuomba neema siku ya ufukara, na amani Siku ya khofu. Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako shari Ulizotupa, na Ulizozizua. Ee Allaah, Pendezesha kwetu iymaan na ipambe katika nyoyo zetu, na chukiza kwetu kufru, ufasiki, uasi na tujaalie miongoni mwa waongofu. Ee Allaah, tufishe tukiwa Waislamu na tuhuishe tukiwa Waislamu na tukutanishe na waja wema bila hizaya wala kufitinishwa. Ee Allaah Wapige vita makafiri wanaokanusha Mitume Wako na wanaozuia njia Yako, na wajaalie juu yao maangamizi Yako na adhabu Zako. Ee Allaah, Wapige vita makafiri waliopewa Kitabu, ee Allaah wa haki. [Aamiyn].[172]

اللَّهُمَّ زِدْنَا وَلاَ تَنْقُصْنَا, وَأَكْرِمْنَا وَلاَ تُهِنَّا, وَأَعْطِنَا وَلاَ تَحْرِمْنَا, وَآثِرْنَا وَلاَ تُؤْثِرْ عَلَيْنَا, وَارْضِنَا وَارْضَ عَنَّا

***Allaahumma zidnaa walaa tanquswnaa, wa akrimnaa walaa tuhinnaa, wa a'-twinaa walaa tahrimnaa, wa aathirnaa walaa tu-uthir 'alaynaa, wardhwinaa wardhwa 'annaa.***

[172] Ahmad, na ameitoa Al-Bukhaariy katika *Adaabul-Mufrad* (699) na ameipa daraja ya Swahiyh Al-Albaaniy katika *Takhriyj Fiqhis-Siyrah* (348), Swahiyh *Adaabil-Mufrad lil-Bukhaariy* (538/259). Tazama pia *Majma'Az-Zawaaid* (6/124).

Ee Allaah Tuzidishie wala usitupunguze, na tukirimu wala usitudunishe, na tupe wala usitunyime, na tupendelee wala Usipendelee dhidi yetu, na Turidhishe, na Turidhie.[173]

### ❖ Du'aa Za Kutakasa Nafs Na Taqwa:

Hifadhi yawe hazina yako maneno yafuatayo yenye kheri kuliko hazina ya dhahabu na fedha.

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الثَّباتَ فِي الأَمْرِ، والْعَزِيمَةَ عَلى الرُّشْدِ، وَأَسْأَلُكَ مُوجِبَاتِ رَحْمَتِكَ، وَعَزَائِمَ مَغْفِرَتِكَ، وأَسْأَلُكَ شُكْرِ نِعْمَتِكَ، وحُسْنَ عِبَادَتِكَ، وأَسْأَلُكَ قَلْبًا سَلِيمًا، ولِسَانًا صَادِقًا، وأَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِ ما تَعْلَمُ، وأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا تَعْلَمُ، وأَسْتَغْفِرُكَ لِمَا تَعْلَمُ، إِنَّكَ أَنْتَ عَلاَّمُ الغُيُوب

***Allaahumma inniy as-alukath-thabaat fil-amri, wal-'aziymata 'alar-rushdi, wa as-aluka muwjibaati Rahmatika, wa 'azaaima maghfiratika, wa as-aluka shukri ni'matika, wa husna 'ibaadatika, wa as-aluka qalban saliyman, wa lisaanan swaadiqan, wa as-aluka min-khayri maa Ta'alamu wa a'uwdhu bika min sharri maa Ta'alamu, wa astaghfiruka limaa Ta'lamu innaka Anta 'Allaamul-ghuyuwbi***

Ee Allaah, hakika mimi nakuomba kuthibitika katika mambo, na azimio juu ya uongofu, na nakuomba haki yenye kupasisha [kuwajibisha] Rahmah Zako, na azimio la Maghfirah Yako, na nakuomba kushukuru neema Zako, na uzuri wa 'ibaadah Zako, na nakuomba moyo uliosalimika,[174] na ulimi usemao kweli [usiosema uongo], na nakuomba kheri Unazozijua na najikinga Kwako shari Unazozijua, na nakuomba maghfirah kwa Unayoyajua, hakika Wewe ni Mjuzi mno wa ya ghayb [yasiyoonekana].[175]

---

[173] At-Tirmidhiy, Ahmad Isnaad Swahiyh, Al-Haakim amepia daraja ya Swahiyh (2/98).
[174] Moyo uliosalimika na kufru, shirki, unafiki, maovu, husda, chuki n.k.
[175] At-Twabaraaniy Tazama *As-Silsilat Asw-Swahiyhah* (3228) – kutoka kwa Shaddaad bin Aws kwamba Rasuli (صلى الله عليه وسلم) amesema: **((Ee Shaddaad bin Aws, ukiona watu wanaweka hazina dhahabu na fedha, basi zidisha maneno haya**)).

اللَّهُمَّ آتِ نَفْسِي تَقْوَاهَا, أَنْتَ وَلِيّهَا وَمَوْلاَهَا, وَخَيْر مَنْ زَكَّاهَا

***Allaahumma aati nafsiy taqwaahaa, Anta Waliyyuhaa wa Mawlaahaa, wakhayru man zakkaahaa***

Ee Allaah, Ipe nafsi yangu taqwa yake, Wewe ni Waliyy wake na Mlinzi wake na Mbora wa mwenye kuitakasa.[176]

اللَّهُمَّ أَحْسَنْتَ خَلْقِي فَأَحْسِنْ خُلُقِي

***Allaahumma ahsanta khalqiy, fa ahsin khuluqiy***

Ee Allaah, Umeboresha umbo langu, basi boresha tabia yangu.[177]

اللَّهُمَّ آتِنِي الْحِكْمَةَ الَّتِي مَنْ أُوتِيَهَا فَقَدْ أُوتِيَ خَيْرًا كَثِيرًا

***Allaahumma aatinil-hikmah allaty man uwtiyahaa faqad uwtiya khayran kathiyraa***

Ee Allaah, Nipe Hikmah ambayo atakayepewa basi kwa yakini amepewa kheri nyingi.[178]

اللَّهُمَّ أَلْهِمْنِي رُشْدِي وَأَعِذْنِي مِنْ شَرِّ نَفْسِي

***Allaahumma alhimniy rushdiy wa a'idhniy min sharri nafsiy***

Ee Allaah, nifunulie uongofu wangu, na nikinge dhidi ya shari ya nafsi yangu.[179]

❖ **Du'aa Kupata Mapenzi Ya Allaah** (سبحانه وتعالى):

---

[176] At-Twabaraniy (11:106) Kutoka kwa Ibn 'Abbaas ( رضي الله عنهما) kwamba Rasuli (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akisita kila anapofikia Aayah **((Na (kwa) nafsi na Aliyeisawazisha. Kisha Akaitia ilhamu (ya kuelewa) uovu wake na taqwa yake.))** [Ash-Shams 91: 7 -8] kisha huomba du'aa hiyo. Tazama pia *Majma' Az-Zawaaid* (7/141) kwa isnaad Hasan.

[177] Ahmad na ameipa daraja ya Swahiyh Al-Abaaniy katika *Al-Irwaa Al-Ghaliyl* (1/115).

[178] Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) katika Suwratul-Baqarah (2:269).

[179] At-Tirmidhiy. Tazama *Takhriyj Mishkaat Al-Miswbaah* Ibn Hajar Al-'Asqalaaniy (3/24).

Inajumuisha pia kuomba kuwapenda masikini, kuacha maovu, kuomba maghfirah na Rahmah, kuomba mauti inapotokea fitnah. Du'aa hii amesema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ***((Hakika hii ni haki basi jifunzeni kisha muifunze)).***

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ فِعْلَ الْخَيْرَاتِ وَتَرْكَ الْمُنْكَرَاتِ وَحُبَّ الْمَسَاكِينِ وَأَنْ تَغْفِرَ لِي وَتَرْحَمَنِي وَإِذَا أَرَدْتَ فِتْنَةَ قَوْمٍ فَتَوَفَّنِي غَيْرَ مَفْتُونٍ أَسْأَلُكَ حُبَّكَ وَحُبَّ مَنْ يُحِبُّكَ وَحُبَّ عَمَلٍ يُقَرِّبُنِي إِلَى حُبِّكَ

***Allaahumma inniy as-aluka fi'-lal khayraati wa tarkal-munkaraati, wa hubbal masaakiyni, wa antaghfiraliy wa tarhamaniy waidhaa aradta fitnata qawmin fatawaffaniy ghayra maftuwni. As-aluka hubbaka, wa hubba man yuhibbuka, wahubba 'amaliyy yuqarribuniy ilaa hubbika***

Ee Allaah, hakika mimi nakuomba kutenda mema, na kuacha machukizo, na kuwapenda masikini, na Unighufurie na Unirehemu, na Unapowatakia watu fitnah, basi nifishe bila ya kufitinishwa. Nakuomba mapenzi Yako, na mapenzi ya anayekupenda, na mapenzi yatakayonikaribisha katika mapenzi Yako.[180]

اللَّهُمَّ ارْزُقْنِي حُبَّكَ وَحُبَّ مَنْ يَنْفَعُنِي حُبُّهُ عِنْدَكَ اللَّهُمَّ مَا رَزَقْتَنِي مِمَّا أُحِبُّ فَاجْعَلْهُ قُوَّةً لِي فِيمَا تُحِبُّ اللَّهُمَّ مَا زَوَيْتَ عَنِّي مِمَّا أُحِبُّ فَاجْعَلْهُ فَرَاغًا لِي فِيمَا تُحِبُّ

***Allaahummar-zuqniy hubbaka wa hubba man yanfa'uniy hubbuhu 'indaka. Allaahumma maa razaqtaniy mimmaa uhibbu faj-'alhu quwwatal-lliy fiymaa tuhibbu. Allaahumma maa zawayta 'anniy mimmaa uhibbu faj-'alhu faraaghal-lliy fiymaa Tuhibbu***

Ee Allaah, niruzuku mapenzi Yako, na mapenzi ya atakayeninufaisha mapenzi yake Kwako. Ee Allaah Uliyoniruzuku kati ya niyapendayo, basi yajaalie yawe ni nguvu kwangu kwa Uyapendayo. Ee Allaah, Uliyoniondoshea kati ya niyapendayo, basi yajaalie kuwa ni wasa'aa kwangu katika Uyapendayo.[181]

---

[180] At-Tirmidhiy, Ahmad Hadiyth Hasan.
[181] At-Tirmidhiy (5/523 ) na ameipa daraja ya Hasan.

❖ **Du'aa Za Maghfirah, Rahmah, Hidaaya, Rizki, Kupandishwa Cheo:**

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي، وَارْحَمْنِي، وَاهْدِنِي، وَاجْبُرْنِي, وَعَافِنِي, وَارْزُقْنِي, وَارْفَعْنِي

***Allaahummagh-fir-liy warhamniy, wahdiniy, wajburniy, wa 'aafiniy, warzuqniy, warfa'-niy***

Ee Allaah, nighufurie, na nirehemu, na niongoe, na niunge, na nipe afya, na niruzuku, na nipandishe [daraja].[182]

❖ **Du'aa Za Kujikinga Shari Na Maovu:**

اللَّهُمَّ إِنِّيَ أَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ النَّارِ وَعَذَابِ النَّارِ وَفِتْنَةِ الْقَبْرِ وَعَذَابِ الْقَبْرِ وَشَرِّ فِتْنَةِ الْغِنَى وَشَرِّ فِتْنَةِ الْفَقْرِ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ فِتْنَةِ الْمَسِيحِ الدَّجَّالِ. اللَّهُمَّ اغْسِلْ قَلْبِي بِمَاءِ الثَّلْجِ وَالْبَرَدِ وَنَقِّ قَلْبِي مِنَ الْخَطَايَا كَمَا نَقَّيْتَ الثَّوْبَ الأَبْيَضَ مِنَ الدَّنَسِ, وَبَاعِدْ بَيْنِي وَبَيْنَ خَطَايَايَ كَمَا بَاعَدْتَ بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْكَسَلِ وَالْمَأْثَمِ وَالْمَغْرَمِ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika min fitnatin-naari wa 'adhaabin-naari wa fitnatil-qabri, wa adhaabil-qabri, wa sharri fitnatil-ghinaa, wa sharri fitnatil-faqri. Allaahumma inniy a'uwdhu bika min sharri fitnatil-Masiyhid-dajjaal. Allaahummagh-sil qalbiy bimaaith-thalji walbaradi, wanaqqi qalbiy minal-khatwaayaa kamaa naqqaytath-thawbal-abyadhw minad-ddanasi, wa baa'id bayniy wa bayna khatwaayaaya kamaa baa'adta baynal-Mashriqi wal-Maghribi. Allaahumma inniy a'uwdhu bika minal-kasali wal-ma-thami wal-maghrami.***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako fitnah za Moto na adhabu za Moto, na fitnah za kaburi, na adhabu za kaburi, na

[182] *Aswhaabus-Sunan* isipokuwa An-Nasaaiy. Nyiradi katika kikao baina ya Sajdah mbili.

shari za fitnah za utajiri, na shari za fitnah za ufakiri. Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako shari za fitnah za Masiyhid-Dajjaal. Ee Allaah, Osha moyo wangu kwa theluji na barafu na Takasa moyo wangu madhambi kama Ulivyotakasa nguo nyeupe kutokana na uchafu, na niweke mbali baina yangu na baina ya madhambi kama Ulivyoweka mbali baina ya Mashariki na Magharibi. Ee Allaah, hakika najikinga Kwako uvivu na madhambi na deni.[183]

- **Du'aa Za Kinga Ya Kila Shari, Kukidhiwa Deni Na Kujikinga Ufakiri[184]**

اللَّهُمَّ رَبَّ السَّمَاوَاتِ السَّبْعِ وَرَبَّ الأَرْضِ وَرَبَّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ, رَبَّنَا وَرَبَّ كُلِّ شَيْءٍ, فَالِقَ الْحَبِّ وَالنَّوَى, وَمُنْزِلَ التَّوْرَاةِ وَالإِنْجِيلِ وَالْفُرْقَانِ, أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ كُلِّ شَيْءٍ أَنْتَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهِ, اللَّهُمَّ أَنْتَ الأَوَّلُ فَلَيْسَ قَبْلَكَ شَيْءٌ, وَأَنْتَ الآخِرُ فَلَيْسَ بَعْدَكَ شَيْءٌ, وَأَنْتَ الظَّاهِرُ فَلَيْسَ فَوْقَكَ شَيْءٌ, وَأَنْتَ الْبَاطِنُ فَلَيْسَ دُونَكَ شَيْءٌ, اقْضِ عَنَّا الدَّيْنَ وَأَغْنِنَا مِنَ الْفَقْرِ

***Allaahumma Rabbas-samaawatis-sab-'i wa Rabbal-ardhwi, wa Rabbal-'Arshil-'Adhwiym, Rabbanaa wa Rabba kulli shay-in, faaliqal-habbi wan-nnawaa, wa munzilat-Tawraati wal-Injiyli wal-Furqaan. A'uwdhu bika min sharri kulli shay-in Anta aakhidhun binaaswiyatihi. Allaahumma Antal-Awwalu falaysa qablaka shay-un, wa Antal-Aakhiru falaysa ba'-daka shay-un wa Antadhw-Dhwaahiru falaysa fawqaka shay-un, wa Antal-Baatwinu falaysa duwnaka shay-un. Iqdhwi 'anna-d-dayna wagh-ninaa minal-faqri***

Ee Allaah, Mola wa mbingu saba na Mola wa ardhi, na Mola wa 'Arshi tukufu, Mola wetu na Mola wa kila kitu, Mpasuaji wa mbegu na kokwa na Aliyeiteremsha Tawraati na Injiyl na Qur-aan. Najikinga Kwako shari ya kila kitu, Wewe Ndiye mwenye kukamata utosi wake. Ee Allaah, Wewe Ndiye wa Mwanzo hakuna kabla Yako kitu, Nawe Ndiye wa Mwisho hakuna baada Yako kitu, Nawe Ndiye Uliyedhahiri hakuna kitu juu Yako, Nawe

[183] Al-Bukhaariy na Muslim.
[184] Nyiradi ya wakati wa kulala pia.

Ndiye Uliyefichika hakuna kilicho karibuni Nawe, Nilipie madeni yangu na Niepushe na ufakiri.[185]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ الْعَجْزِ وَالْكَسَلِ وَالْجُبْنِ وَالْبُخْلِ وَالْهَرَمِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاتِ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika minal-'ajzi wal-kasali, wal-jubni, wal-bukhli, wal-harami, wa a'uwdhu bika min 'adhaabil-qabri, wamin fitnatil-mahyaa wal-mamaati***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako kushindwa nguvu [kutojiweza], na uvivu, na uoga, na ubakhili, na kudhoofika [kutokana na uzee], na najikinga Kwako adhabu ya kaburi na najikinga Kwako fitnah za uhai na mauti.[186]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ الْعَجْزِ وَالْكَسَلِ, وَالْجُبْنِ وَالْبُخْلِ, وَالْهَرَمِ وَعَذَابِ الْقَبْرِ. اللَّهُمَّ آتِ نَفْسِي تَقْوَاهَا, وَزَكِّهَا أَنْتَ خَيْرُ مَنْ زَكَّاهَا, أَنْتَ وَلِيُّهَا وَمَوْلاَهَا. اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عِلْمٍ لاَ يَنْفَعُ, وَمِنْ قَلْبٍ لاَ يَخْشَعُ ,وَمِنْ نَفْسٍ لاَ تَشْبَعُ, وَمِنْ دَعْوَةٍ لاَ يُسْتَجَابُ لَهَا

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika minal-'ajzi wal-kasali, wal-jubni, wal-bukhli, wal-harami, wa 'adhaabil-qabri, Allaahumma aati nafsiy taqwaahaa, wa zakkihaa Anta khayru man zakkaahaa, Anta Waliyyuhaa wa Mawlaaha. Allaahumma inniy a'uwdhu bika min 'ilmin-laa yanfa'u, wamin qalbin-laa yakhsha'u, wamin-nafsil-laa tashba'u, wamin da'-watin-laa yustajaabu lahaa***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako kushindwa nguvu [kutojiweza], na uvivu, na uoga, na ubakhili, na kudhoofika [kutokana na uzee] na adhabu za kaburi. Ee Allaah, Ipe nafsi yangu taqwa yake, na Itakase kwani Wewe ni Mbora wa kuitakasa, Wewe ni Waliyy wake na Mlinzi wake. Ee Allaah, hakika najikinga Kwako elimu isiyonufaisha, na moyo usionyenyekea na nafsi isiyoshiba, na du'aa isiyojibiwa.[187]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا عَمِلْتُ وَمِنْ شَرِّ مَا لَمْ أَعْمَلْ

[185] Muslim.
[186] Al-Bukhaariy na Muslim.
[187] Muslim, An-Nasaaiy, Ahmad.

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika min sharri maa 'amiltu wamin sharri maa lam a'-amal***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako shari niliyotenda na shari nisiyoitenda.[188]

أللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ سَمْعِي وَمِنْ شَرِّ بَصَرِي وَمِنْ شَرِّ لِسَانِي وَمِنْ شَرِّ قَلْبِي وَمِنْ شَرِّ مَنِيِّي

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika min sharri sam-'iy wamin sharri baswariy, wamin sharri lisaaniy wamin sharri qalbiy, wamin sharri maniyyi***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako shari ya kusikia kwangu [masikio yangu], na shari ya kuona kwangu [macho yangu], na shari ya ulimi wangu, na shari ya moyo wangu, na shari ya manii yangu.[189]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ مُنْكَرَاتِ الاَخْلاَقِ وَالاَعْمَالِ وَالاَهْوَاءِ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika min munkaraatil-akhlaaqi wal a'-maali wal ahwaai***

Ee Allaah, hakika najikinga Kwako machukizo ya tabia na matendo na matamanio.[190]

اللَّهُمَّ جَنِّبْنِي مُنْكَرَاتِ الاَخْلاَقِ, وَالاَهْوَاءِ, وَالاَعْمَالِ, والأَدْوَاءِ

***Allaahumma jannibniy munkaraatil-akhlaaqi, wal ahwaahi, wal 'amaali, wal adwaai***

Ee Allaah niepushe machukizo ya tabia na matamanio, na matendo, na maradhi.[191]

---

[188] Muslim, Abu Daawuwd, An-Nasaaiy, Ibn Maajah, Ahmad.

[189] Abu Daawuwd, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy – Tazama *Swahiyh At-Tirmidhiy* (3/166) na Swahiyh An-Nasaaiy (3/1108).

[190] At-Tirmidhiy, Ibn Maajah, Al-Haakim, At-Twabaraniy na Tazama *Swahiyh At-Tirmidhiy* (3/184).

[191] Al-Haakim na kasema Swahiyh kwa sharti ya Muslim na ameikubali Adh-Dhahabiy. *Kitabus-Sunnah* (13) na Al-Albaaniy ameipa daraja ya Swahiyh.

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْجُوعِ فَإِنَّهُ بِئْسَ الضَّجِيعُ وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الْخِيَانَةِ فَإِنَّهَا بِئْسَتِ الْبِطَانَةُ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika minal-juw'iy fainnahu bi-isa-dhw-dhwajiy'u wa a'uwdhu bika minal-khiyaanati fainnahaa bi-isatil-bitwaanatu***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako njaa kwani hiyo ni mwenzi muovu na najikinga Kwako khiyana kwani hiyo ni msiri muovu.[192]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْجُبْنِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الْبُخْلِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ أَنْ أُرَدَّ إِلَى أَرْذَلِ الْعُمُرِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الدُّنْيَا وَعَذَابِ الْقَبْرِ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika minal-jubni, wa a'uwdhu bika minal-bukhli, wa a'uwdhu bika min an uradda ilaa ardhalil 'umuri, wa a'uwdhu bika min fitnatid-dun-yaa wa 'adhaabil-qabri***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako uoga, na najikinga Kwako ubakhili, na najikinga Kwako kurudishwa katika umri wa kudhalilika [uzee], na najikinga Kwako fitnah za dunia na adhabu za kaburi.[193]

أَللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْعَجْزِ, وَالْكَسْلِ, والْجُبْنِ, وَالْبُخْلِ, وَالْهَرَمِ, وَالْقَسْوَةِ, وَالْغَفْلَةِ, وَالْعَيْلَةِ, وَالذِّلَّةِ وَالْمَسْكَنَةِ, وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الْفَقْرِ, وَالْكُفْرِ, وَالْفُسُوقِ, وَالشِّقَاقِ, وَالنِّفَاقِ, وَالسُّمْعَةِ, وَالرِّيَاءِ, وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الصَّمَمِ, وَالْبُكَمِ, والْجُنُونِ, وَالْجُذَامِ, والْبَرَصِ, وَسَيِّءِ الأَسْقَامِ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika minal-'ajzi, wal-kasli, wal-jubni, wal-bukhli, wal-harami, wal-qas-wati, wal-ghaflati, wal-'aylati, wadh-dhillati, wal-maskanati, wa a'uwdhu bika minal-faqri, wal-kufri, wal-fusuwqi, wash-shiqaaqi, wan-nifaaqi, wassum-'ati, war-riyaai, wa a'uwdhu bika minasw-swamami, wal-bukami, wal-junuwni, wal-judhaami, walbaraswi, wasayyiil-asqaami***

---

[192]Abu Daawuwd, An-Nasaaiy, Ibn Maajah, Tazama *Swahiyh An-Nasaaiy* (3/1112).

[193] Al-Bukhaariy.

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako kushindwa nguvu [kutokujiweza], na uvivu, na uoga, na ubakhili, na kudhoofika [kutokana na uzee], na moyo mgumu, na kughafilika, na kufedheheka, na kudhalilika, na umasikini, na najikinga Kwako ufakiri na kufru na ufasiki na magomvi na unafiki na kupenda kusikika [umaarufu] na riyaa na najikinga Kwako dhidi ya uziwi na ububu na ukichaa na ukoma na mbalanga na maradhi mabaya.[194]

أَللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ التَّرَدِّي, وَالْهَدْمِ, وَالْغَرَقِ, وَالْحَرَقِ, وَأَعُوذُ بِكَ أَنْ يَتَخَبَّطَنِي الشَّيْطَانُ عِنْدَ الْمَوْتِ, وَأَعُوذُ بِكَ أَنْ أَمُوتَ فِي سَبِيلِكَ مُدْبِرًا, وَأَعُوذُ بِكَ أَنْ أَمُوتَ لَدِيغًا

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika minat-taraddiy, wal-hadmi, wal-gharaqi, wal-gharaqi, wa a'uwdhu bika an yatakhabbatwniyash-shaytwaanu 'indal-mawti, wa a'uwdhu bika an amuwta fiy sabiylika mudbiraa, wa a'uwdhu bika an amuwta ladiyghaa***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako kuangamia na kubomoka na kufa kwa kuzama na kuungua na Moto, na najikinga Kwako kughilibiwa na shaytwaan wakati wa mauti, na najikinga Kwako kufa nikiwa mwenye kugeuka nyuma katika njia Yako [kukimbia vita] na najikinga Kwako kufa kwa kung'atwa [na mdudu wa sumu].[195]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ الْفَقْرِ وَالْقِلَّةِ وَالذِّلَّةِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ أَنْ أَظْلِمَ أَوْ أُظْلَمَ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika minal-faqri wal-qillati, wadh-dhillati, wa a'uwdhu bika min an adhwlima aw udhwlama***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako ufakiri na uchache na udhalilifu na najikinga Kwako kudhulumu au kudhulumiwa.[196]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ الْجُبْنِ, وَالْبُخْلِ, وَسُوءِ الْعُمُرِ, وَفِتْنَةِ الصَّدْرِ, وَعَذَابِ الْقَبْرِ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika minal-jubni, wal-bukhli, wa suuil-'umri wa fitnatisw-swadri, wa 'adhaabil-qabri***

---

[194] Al-Haakim, Al-Bayhaqiy, na tazama *Swahiyh Al-Jaami'* (1/406).
[195] Abu Daawuwd, An-Nasaaiy, tazama *Swahiyh An-Nasaaiy* (3/1123).
[196] Abu Daawuwd, Ahmad – Tazama *Swahiyh Abi Daawuwd* (1544).

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako uoga na ubakhili na uovu wa umri na fitnah za moyo na adhabu ya kaburi.[197]

### ❖ Du'aa Kujikinga Balaa, Majaaliwa Mabaya, Maadui:

أَللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ جَهْدِ الْبَلاَءِ وَدَرَكِ الشَّقَاءِ وَسُوءِ الْقَضَاءِ وَشَمَاتَةِ الأَعْدَاءِ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika min jahdil-balaai wa darakish-shiqaai wa suw-il-qadhwaai, wa shamaatatil-a'daai***

Ee Allaah hakika mimi najikinga Kwako shida ya balaa [mitihani n.k.] na kukumbwa na uovu na majaaliwa mabaya na bezo la maadui.[198]

### ❖ Du'aa Kujikinga Na Jirani Muovu:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ جَارِ السَّوْءِ فِي دَارِ الْمُقَامِ فَإِنَّ جَارَ الْبَادِيَةِ يَتَحَوَّلُ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika min jaaris-suw-i fiy daaril-muqaami fainna jaaral-baadiyati yatahawwal***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako na jirani muovu katika nyumba ya makazi kwani jirani wa shambani hubadilika [huondoka].[199]

أَللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ يَوْمِ السُّوءِ وَمِنْ لَيْلَةِ السُّوءِ وَمِنْ سَاعَةِ السُّوءِ وَمِنْ صَاحِبِ السُّوءِ وَمِنْ جَارِ السُّوءِ فِي دَارِ الْمُقَامَةِ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika min yawmis-suw-i wamin laylatis-suw-i, wamin saa'atis-suw-i, wamin swaahibis-suw-i, wamin-jaaris suw-i fiy daaril-muqaamati***

---

[197] An-Nasaaiy, *Sunan Abi Daawuwd* kwa usimulizi kuwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akijikinga nayo mambo hayo.
[198] Al-Bukhaariy na Muslim.
[199] An-Nasaaiy kwa usimulizi **((Jikingeni na jirani muovu...))**, *As-Silsilat Asw-Swahiyhah* (3943), *Swahiyh Al-Jaami'* (2967).

Ee Allaah hakika mimi najikinga Kwako mchana muovu, na usiku muovu, na saa ovu, na rafiki muovu, na jirani muovu katika nyumba ya makazi.[200]

### ❖ Du'aa Kujitosheleza Kwa Halali na Kujiepusha Na Haraam:

اللَّهُمَّ اكْفِنِي بِحَلالِكَ عن حَرَامِكَ وَأغْنِنِي بِفَضْلِكَ عَمَّنْ سِوَاكَ

***Allaahumma akfiniy bi-halaalika 'an-haraamika waghniniy bi-fadhwlika 'amman siwaak***

Ee Allaah nitosheleze kwa halali Yako dhidi ya haramu Yako, Kwako na nitosheleze kwa fadhila Zako dhidi ya asiyekuwa Wewe.[201]

### ❖ Du'aa kujikinga Mambo Manne; Moyo Usionyenyekea, Du'aa Isiyosikilizwa, Nafsi Isiyoshiba Na Elimu Isiyonufaisha:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ قَلْبٍ لاَ يَخْشَعُ وَمِنْ دُعَاءٍ لاَ يُسْمَعُ وَمِنْ نَفْسٍ لاَ تَشْبَعُ وَمِنْ عِلْمٍ لاَ يَنْفَعُ أَعُوذُ بِكَ مِنْ هَؤُلآءِ الأَرْبَعِ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika min-qalbin-laa yakh-sha'u, wamin du'aain-laa yusma'u, wamin nafsin-laa tashba'u, wamin ilmin-laa yanfa'u, a'uwdhu bika min haaulail-arba'i***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga moyo usionyenyekea na du'aa isiyosikizwa na nafsi isiyoshiba na elimu isiyonufaisha, najikinga Kwako dhidi ya haya manne.[202]

### ❖ Du'aa Kujikinga Upotofu:

---

200 At-Twabaraanyi katika *Majma' Az-Zawaaid* (10/144), *Swahiyh Al-Jaami'* (1/411).

201 At-Tirmidhiy, tazama *Swahiyh Sunan At-Tirmidhiy* (2822).

202 Abu Daawuwd, At-Tirmidhiy, *Swahiyh An-Nasaaiy*, *Swahiyh Al-Jaami'* (1297).

اللَّهُمَّ لَكَ أَسْلَمْتُ وَبِكَ آمَنْتُ وَعَلَيْكَ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْكَ أَنَبْتُ وَبِكَ خَاصَمْتُ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِعِزَّتِكَ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ أَنْ تُضِلَّنِي أَنْتَ الْحَيُّ الَّذِي لاَ يَمُوتُ وَالْجِنُّ وَالإِنْسُ يَمُوتُونَ

***Allaahumma laka aslamtu, wa bika aamantu, wa 'alayka tawakkaltu, wa ilayka anabtu, wa bika khaaswamtu. Allaahumma inniy a'uwdhu bi'izzatika laa ilaaha illa Anta an-tudhwillaniy Antal-Hayyu Alladhiy laa yamuwtu wal-jinnu wal-insu yamuwtuwna.***

Ee Allaah, Kwako najisalimisha, na Kwako naamini, na Kwako natawakali, na Kwako narejea [kutubu], na Kwako nagombana [dhidi ya adui]. Ee Allaah, hakika mimi najikinga kwa 'Izzah [Nguvu] Yako, hapana muabudiwa wa haki ila Wewe Usije kunipotoa Wewe Uliye Hai [daima] Ambaye Hafi ilhali majini na watu wanakufa.[203]

## ❖ Du'aa Kujikinga Shirki:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ أَنْ أُشْرِكَ بِكَ وَأَنَا أَعْلَمُ, وَأَسْتَغْفِرُكَ لِمَا لاَ أَعْلَمُ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika an-ushrika bika wa anaa a-'lamu, wa astaghfiruka limaa laa a'lamu***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako kukushirikisha na hali najua, na nakuomba maghfirah kwa nisiyoyajua.[204]

## ❖ Du'aa Kujikinga Moto:

اللَّهُمَّ رَبَّ جِبْرَائِيلَ وَمِيكَائِيلَ وَرَبَّ إِسْرَافِيلَ, أَعُوذُ بِكَ مِنْ حَرِّ النَّارِ وَمِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ

***Allaahumma Rabba Jibraaiyla wa Mikaaiyla wa Rabba Israafiyla, a'uwdhu bika min harrin-naari, wamin 'adhaabil-qabri***

---

[203] Muslim na Ahmad.

[204] Ahmad, tazama *Swahiyh At-Targhiyb wat-Tarhiyb* ya Al-Albaaniy (1/19).

Ee Mola wa Jibriyl na Mikaaiyl na Mola wa Israafiyl, najikinga Kwako Moto na adhabu ya kaburi.[205]

### ❖ Du'aa Kujikinga Kuondokewa Neema Na Kujikinga Ghadhabu Za Allaah (سبحانه وتعالى):

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ زَوَالِ نِعْمَتِكَ وَتَحَوُّلِ عَافِيَتِكَ وَفُجَاءَةِ نِقْمَتِكَ وَجَمِيعِ سَخَطِكَ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika min zawaali ni'matika, watahawwuli 'aafiyatika, wafujaa-ati niqmatika, wajamiy'i Sakhatwika.***

Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako kuondoka na Neema Zako, na kubadilika afya Yako [uzima wangu] na adhabu Yako ya ghafla na hasira Zako zote.[206]

### ❖ Du'aa Kuomba Elimu Na Manufaa Yake:

اللَّهُمَّ انْفَعْنِي بِمَا عَلَّمْتَنِي، وَعَلِّمْنِي مَا يَنْفَعُنِي، وَزِدْنِي عِلْمًا

***Allaahuuma anfa'-niy bimaa 'allamtaniy wa-'allimniy maa yanfa'uniy wazidniy 'ilmaa***

Ee Allaah, ninufaishe kwa Uliyonifundisha, na nifundishe yanayoyonifaa na Nizidishie elimu.[207]

رَبِّ زِدْنِي عِلْماً

***Rabbi zidniy 'ilmaa***
Mola wangu, Nizidishie elimu.[208]

اللَّهُمَّ فَقِّهْنِي فِي الدِّينِ

***Allaahumma faqqihniy fid-Diyn***

---

[205] An-Nasaaiy, tazama *Swahiyh An-Nasaaiy* (3/1121).
[206] Muslim na Abu Daawuwd.
[207] Ibn Maajah 1/92, *Swahiyh Ibn Maajah* (3091).
[208] Twaahaa (20:114).

Ee Allaah, Nipe ufaqihi [ufahamu wa ndani]) wa Dini.[209]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ عِلْماً نَافِعًا وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ عِلْمٍ لاَ يَنْفَعُ

***Allaahumma inniy as-aluka 'ilman naafi'aa wa a'uwdhu bika min 'ilmin-laa yanfa'u***

Ee Allaah, hakika mimi nakuomba elimu yenye manufaa, na najikinga Kwako elimu isiyonufaisha.[210]

❖ **Du'aa Kuomba Jannah Na Kujikinga Moto:**

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِأَنَّ لَكَ الْحَمْدَ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ وَحْدَكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ الْمَنَّانُ يَا بَدِيعَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ يَا ذَا الْجَلاَلِ وَالإِكْرَامِ, يَا حَيُّ يَا قَيُّومُ, إِنِّي أَسْأَلُكَ الْجَنَّةَ وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ النَّارِ

***Allaahumma inniy as-aluka bianna lakal-hamdu laa ilaaha illa Anta Wahdaka laa shariyka Laka, Al-Mannaanu yaa Badiy-'as-samaawati wal-ardhwi, yaa dhal-Jalaali wal-ikraami, yaa Hayyu yaa Qayyuwmu, inniy as-alukal-Jannata wa a'uwdhu bika minan-naari***

Ee Allaah, nakuomba, hakika kuhimidiwa ni Kwako hapana muabudiwa wa haki ila Wewe, Peke Yako Huna mshirika, Mwenye Fadhila. Ee Mwanzishi wa mbingu na ardhi ee Mwenye Utukufu na Ukarimu, ee Aliye Hai [daima], ee Msimamizi wa yote, hakika mimi nakuomba Jannah na najikinga kwako Moto.[211]

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْجَنَّةَ وَأَسْتَجِيرُ بِكَ مِنَ النَّارِ (ثلاث مرات)

***Allaahumma inniy as-alukal-Jannata wa astajiyru bika minan-naari*** *[mara 3]*

[209] Al-Bukhaariy, Ahmad – Du'aa ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما).
[210] *Swahiyh Ibn Maajah* na Tazama *Majma' Az-Zawaaid* (10/185).
[211] Abu Daawuwd, AT-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Ibn Maajah.

Ee Allaah, hakika mimi nakuomba Jannah na najilinda Kwako dhidi ya Moto.[212]

### ❖ Du'aa Ya Kuomba Maghfirah:

اللَّهُمَّ قِنِي شَرَّ نَفْسِي, وَاعْزِمْ لِي عَلَى أَرْشَدِ أَمْرِي, اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي مَا أَسْرَرْتُ, وَمَا أَعْلَنْتُ, وَمَا أَخْطَأْتُ, وَمَا عَمَدْتُ, وَمَا عَلِمْتُ, وَمَا جَهِلْتُ

***Allaahumma qiniy sharri nafsiy, wa a'-zim-liy 'alaa arshadi amriy, Allaahummagh-fir-liy maa asrartu, wamaa a'-lantu, wamaa akh-twa-atu, wamaa 'amadtu, wamaa 'alimtu, wamaa jahiltu***

Ee Allaah Nikinge shari ya nafsi yangu, na Nithibitishe katika uongofu bora kabisa wa mambo yangu, Ee Allaah, nighufurie niliyoyafanya siri, na niliyoyatangaza, na niliyoyakosea, na niliyoyakusudia, na niliyoyajua na niliyofanya kwa kutokujua.[213]

### ❖ Du'aa Kujikinga Shari Na Adui:

Kujikinga Na Adui.[214]

اللَّهُمَّ إِنِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ غَلَبَةِ الدَّيْنِ, وَغَلَبَةِ الْعَدُوِّ, وَشَمَاتَةِ الأَعْدَاءِ

***Allaahumma inniy a'uwdhu bika min ghalabatid-dayni, wa ghalabatil-'aduwwi wa shamaatatil-a'-daai***

Ee Allaah hakika mimi najikinga Kwako kushindwa deni, na kushindwa na adui, na bezo la maadui.[215]

---

[212]At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Ibn Maajah – *Swahiyh At-Tirmidhiy* (2/319) na lafdhi yake **((Atakayemwomba Allaah Jannah mara tatu [asubuhi na jioni], Jannah itasema: Ee Allaah muingize katika Jannah na atakayejilinda kwa Allaah na Moto mara tatu, Moto utasema: Ee Allaah mlinde na Moto)).** Inasomwa hii katika Swalaah baada ya Tashahhud kabla ya kutoa salaam.

[213] Ahmad. Al-Haakim Adh-Dhahabiy amekubali na kuipa daraja ya Swahiyh. Tazama pia *Majma' Zawaaid* (10/184).

[214] Inahusu pia kukidhiwa deni.

[215] An-Nasaaiy, Ahmad. Tazama *Swahiyh An-Nasaaiy* (3/1113).

اللَّهُمَّ إِنَّا نَجْعَلُكَ فِي نُحُورِهِمْ, وَنَعُوذُ بِكَ مِنْ شُرُورِهِم

***Allaahumma innaa naj-'aluka fiy nuhuwrihim, wa na'uwdhu bika min shuruwrihim***

Ee Allaah, hakika sisi tunakuweka katika shingo zao na tunajikinga Kwako dhidi ya shari zao.[216]

حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ

***Hasbuna-Allaahu wa Ni'-mal-Wakiyl***

Allaah Anatutosheleza, Naye ni Mbora wa kutegemewa.[217]

### ❖ Du'aa Mwenye Kuogopa Dhulma Ya Mwenye Kutawala:

أللَّهُمَّ رَبَّ السَّمواتِ السَّبْعِ وَرَبَّ الْعَرْشِ الْعَظِيْمِ, كُنْ لِي جاراً مِنْ (فُلانِ بْنِ فُلاَنٍ), وَأَحْزَابِهِ مِنْ خَلاَئِقِكَ أَنْ يَفْرُطَ عَلَيَّ أحَدٌ مِنْهُمْ أَوْ يَطْغَى, عَزَّ جارُكَ وَجَلَّ ثَناؤُكَ, وَ لاَ إِلَهَ إلاَّ أَنْتَ

***Allaahumma Rabbas-ssamaawatis-sab-'i wa Rabbal-'Arshil-'Adhwim, kun-liy jaaran-min*** [fulaan bin fulaan] ***wa ahzaabihi min khalaaiqika an-yafrutwa 'alayya ahadun-minhum aw yatwghaa, 'azza jaaruka, wa jalla thanaauka, wa laa ilaaha illa Anta***

Ee Allaah, Mola wa mbingu saba, na Mola wa 'Arshi tukufu, kuwa mlinzi wangu dhidi ya [fulani bin Fulani - taja mtu unayemkhofu] na vikosi vyake miongoni mwa viumbe Vyako, kwa kunisaliti yeyote miongoni mwao, au kunifanyia uadui, umetukuka ulinzi Wako, na zimetukuka sifa Zako na hapana muabudiwa wa haki ila Wewe.[218]

---

[216] Abu Daawuwd, Ahmad. Tazama *Swahiyh Abi Daawuwd* (1537).

[217] Al-Bukhaariy kutoka kwa Ibn 'Abbaas: "Ameisema Ibraahiym (عليه السلام) alipotupwa Motoni na ameisema Muhammad (صلى الله عليه وسلم) waliposema (Surat Al'-Imraan 3: 173) **(("Hakika watu wamejumuika dhidi yenu, basi waogopeni" [Haya] Yakawazidishia iymaan; na wakasema: "Allaah Anatutosheleza Naye ni Mbora wa kumtegemea")).**

[218] Al-Bukhaariy katika *Adaabul-Mufrad* (707) na Al-Albaaniy ameipa daraja ya Swahiyh katika *Swahiyh Al-Adaab Al Mufrad* (545).

اللهُ أكْبَرُ، اللهُ أعَزُّ مِنْ خَلْقِهِ جَمِيْعاً، اللهُ أعَزُّ مِمَّا أخَافُ وَأحْذَرُ, أعُوذُ بِاللهِ الَّذِي لاَ إِلَهَ إلاَّ هُوَ ، الْمُمْسِكِ السَّمَوَاتِ السَّبْعِ أَنْ يَقَعْنَ عَلَى الأَرْضِ إلاَّ بِإِذْنِهِ، مِنْ شَرِّ عَبْدِكَ (فلان) وَجُنُوْدِهِ وَأَتْبَاعِهِ وَأَشْيَاعِهِ، مِنَ الْجِنِّ والإِنْسِ، اَللّٰهُمَّ كُنْ لِيْ جَاراً مِنْ شَرِّهِمْ، جَلَّ ثَنَاؤُكَ وَعَزَّ جَارُكَ، وَتَبَارَكَ اسْمُكَ، وَلاَ إِلَهَ غَيْرُكَ

***Allaahu Akbar, Allaahu A'azzu min Khalqihi jamiy'-aa. Allaahu A'azzu mimmaa akhaafu wa ahdharu. A'uwdhu biLLaahil-LLadhiy laa ilaaha illaa Huwa Al-Mumsikis-samawaatis-sab-'i an-yyaqa'-na 'alal-ardhwi illaa bi-idhnihi min-sharri 'abdika*** *[fulaan]* ***wa junuwdihi, wa atbaa'ihi, wa ashyaa'ihii minal-jinni wal-insi. Allaahumma kun-liy jaaram-min sharrihim, Jalla Thanaauka, wa 'Azza Jaaruka, wa Tabaarakas-Smuka walaa ilaaha Ghayruka*** *[mara 3]*

Allaah ni Mkubwa, Allaah, ni Mwenye nguvu [cheo[ kuliko viumbe Vyake vyote, Allaah ni Mwenye nguvu, kuliko kila nikiogopacho nakujihadhari, najikinga kwa Allaah Ambaye hapana muabudiwa wa haki ila Yeye, Ambaye ameshikilia mbingu saba zisiangukie ardhi ila kwa idhini Yake, dhidi ya shari ya mja wako [Fulani - mtaje mtu unayemkhofu] na majeshi yake, na wanaomfuata, na wafuasi wake miongoni mwa majini na watu. Ee Allaah, kuwa mlinzi wangu dhidi ya shari yao. Zimetukuka sifa Zako na Umehishimika ulinzi Wako na limetakasika Jina Lako, na hapana muabudiwa wa haki asiyekuwa Wewe.[219]

### ❖ Kuomba Nusra Dhidi Ya Anayedhulumu:

اللَّهُمَّ مَتِّعْنِي بِسَمْعِي, وَبَصَرِي, وَاجْعَلْهُمَا الْوَارِثَ مِنِّي, وَانْصُرْنِي عَلَى مَنْ يَظْلِمُنِي, وَخُذْ مِنْهُ بِثَأْرِي

***Allaahumma matti'-niy bisam-'iy, wa baswariy, waj-'al-humaal-waaritha minniy, wanswurniy 'alaa man yadhwlimuniy, wa khudh minhu bitha-ariy***

[219] Al-Bukhaariy katika *Adaabul-Mufrad* (708) na Al-Albaaniy ameipa daraja ya Swahiyh katika *Swahiyh Al-Adaab Al-Mufrad* (546).

Ee Allaah, ninufaishe kwa masikio yangu, na macho yangu, na vijaalie [viwili hivyo] viwe hivyo kwa warithi wangu na ninusuru dhidi ya anayenidhulumu, na nilipizie dhidi yake.[220]

[220] At-Tirmidhiy, tazama *Swahiyh At-Tirmidhiy* (3/188).

## 20- Mazingatio Na Mafunzo Ya Hajj

Ukitafakari na kuzingatia yote yanayojiri katika safari ya Hajj, ukalinganisha na mafunzo yaliyomo katika Qur-aan na Sunnah yanayohusiana na Aakhirah, utapata mafunzo mengi. Allaah (سبحانه وتعالى) Ameanza Suwratul-Hajj kwa Aayah tukufu inayogusia hali itakavyokuwa Siku ya Qiyaamah:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱتَّقُواْ رَبَّكُمۡۚ إِنَّ زَلۡزَلَةَ ٱلسَّاعَةِ شَيۡءٌ عَظِيمٞ ١ يَوۡمَ تَرَوۡنَهَا تَذۡهَلُ كُلُّ مُرۡضِعَةٍ عَمَّآ أَرۡضَعَتۡ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمۡلٍ حَمۡلَهَا وَتَرَى ٱلنَّاسَ سُكَٰرَىٰ وَمَا هُم بِسُكَٰرَىٰ وَلَٰكِنَّ عَذَابَ ٱللَّهِ شَدِيدٞ ٢ ﴾

**((Enyi watu! Mcheni Rabb wenu. Hakika zilizala la Saa (Qiyaamah) ni jambo adhimu. Siku mtakapoiona (hiyo Saa) kila mnyonyeshaji atamsahau anayemnyonyesha, na kila mwenye mimba ataizaa mimba yake, na utawaona watu (kama) wamelewa, kumbe hawakulewa lakini ni adhabu ya Allaah kali))**[221]

Mafunzo mengineyo:

- Inamkumbusha Muislamu kuhusu safari ya Aakhirah na huwa na khofu kwamba, huenda ikawa ni safari yako ya mwisho, kwani utaagana na kufarikiana na ahli zako, jamaa, jirani, marafiki, mali yako na makazi yako, na safari ya Aakhirah hali kadhalika huwa hivyo.

- Kama unavyojiandaa safari ya kawaida kuandaa zawadi na vitu na mahitaji ya kukufikisha safarini na hasa safari hii ya Hajj ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) Anasema:

وَتَزَوَّدُواْ فَإِنَّ خَيۡرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقۡوَىٰۖ وَٱتَّقُونِ يَٰٓأُوْلِي ٱلۡأَلۡبَٰبِ ١٩٧

**((Na chukueni masurufu. Na hakika bora ya masurufu ni taqwa. Na nicheni Mimi enyi wenye akili!))**[222]

[221] Al-Hajj (1-2).
[222] Al-Baqarah (2: 197).

Hivyo basi, zingatia kwamba safari ya Aakhirah pia inahitaji kujiandaa kwa 'amali njema ili iwe ni akiba yako ya Aakhirah.

- Kama utakavyopata tabu katika kusafiri mji kwa mji au nchi kwa nchi, hali kadhalika kumbuka kwamba kuna tabu na mashaka ya safari ya Aakhirah ambayo ni nzito zaidi kwani safari hiyyo inahusiana na *Sakaraat Al-Mawt,* adhabu za kaburini, kufufuliwa, kuhesabiwa, kupimwa 'amali katika mizani, kuvuka *Asw-Swiraatw*, na mtu akiwa ni muovu hatimaye ni adhabu za motoni (Tunajikinga kwa Allaah سبحانه وتعالى).

- Unapovaa nguo za Ihraam, kumbuka kafani (sanda) yako kwani hizo ni nguo mbili tu nyeupe zinazokutosheleza kufunikwa mwilini. Pia, kama zilivyokuwa nguo hizo ni nyeupe, unapaswa moyo wako uwe hali hiyo hiyo mweupe bila ya madoa meusi ya madhambi. Pia unapokuwa kwenye Ihraam unazuilika kutenda vitendo fulani usiharibu Ihraam yako, basi na iwe ukumbusho wa kujiepusha na maasi usiharibu Aakhirah yako.

- Unaposema "*Labbayka-Allaahumma Labbayka*" unakusudia kumuitikia Mola wako Mtukufu, hivyo kumbuka kwamba hivyo ndivyo inavyopasa kubakia hali yako daima kuitikia amri zote za Allaah (سبحانه وتعالى) na Rasuli Wake (صلى الله عليه وآله وسلم).

- Kuingia kwako katika *Baytul-Haraam* Makkah ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) Ameijaalia kuwa ni amani kama Anavyosema:

وَإِذْ جَعَلْنَا ٱلْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا

**((Na (taja) Tulipoifanya Nyumba kuwa ni mahali pa kurejewa na watu na (pa) amani))**[223]

Ukumbuke umuhimu wa kupata amani Siku ya Qiyaamah, nayo haipatikani ila kwa juhudi zako duniani kufuata

---

[223] Al-Baqarah (2: 125).

maamrisho ya Allaah (سبحانه وتعالى) na Rasuli Wake (صلى الله عليه وآله وسلم). Kumbuka ndugu Muislamu kwamba kujiepusha na kumshirikisha Allaah (سبحانه وتعالى) na kubakia katika Tawhiyd ndio jambo kuu litakalokupatia amani Siku hiyo kama Anavyosema Allaah (سبحانه وتعالى):

ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَلَمۡ يَلۡبِسُوٓاْ إِيمَـٰنَهُم بِظُلۡمٍ أُوْلَـٰٓئِكَ لَهُمُ ٱلۡأَمۡنُ وَهُم مُّهۡتَدُونَ ﴿٨٢﴾

**((Wale ambao wameamini na hawakuchanganya iymaan zao na dhulma (ya kumshirikisha Allaah). Hao ndio watakaopata amani nao ndio walioongoka.))**[224]

- Tafakari kwamba mamilioni ya watu wanajumuika huko, wanaume wakiwa wamevaa aina moja ya nguo, wakimuabudu Mola Mmoja kwa wakati mmoja, wakielekea Qiblah kimoja, hakuna tofauti kati yao; tajiri na masikini, mfalme na mtumwa, mweusi na mweupe. Basi zingatia kwamba huu ni uadilifu wa Allaah (سبحانه وتعالى) wa Dini hii tukufu na kwamba aliye mbora kati yetu ni mwenye taqwa zaidi. Pia zingatia kwamba Siku ya kufufuliwa itakuwa hali ni hiyo hiyo katika *Ardhw Al-Mahshar*[225].

- *Al-Ka'bah* ni nyumba ya kwanza duniani, Ameijaalia Allaah (سبحانه وتعالى) kuwa ni yenye baraka na Amejaalia kuweko katikati ya dunia nzima ili wana-Aadam wote waelekee huko wanapomuabudu kufuata Dini ya Uislamu ya baba yetu Nabiy Ibraahiym (عليه السلام), kwa hiyo Mitume na watu wote kabla yake walitakiwa waelekee hapo kuitekeleza 'ibaadah ya Hajj. Basi zingatia kwamba Uislamu ni Dini ya watu wote anayeitaka, na si kwa ummah wa Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) pekee.

- Tanabahi na kumbuka taadhima ya mwanamke aliyokirimiwa na Allaah (سبحانه وتعالى) kinyume na wanavyodhania makafiri kwamba mwanamke hana hadhi katika Uislamu. 'Ibaadah ya *As-Sa'-y* imeanzishwa na Haajar (عليها السلام) mama yake Ismaa'iyl (عليه السلام) na tokea zama hizo mpaka Siku ya Qiyaamah mamilioni ya Waislamu

224 Al-An'aam (6: 82).
225 Ardhi ya kukusanywa viumbe wote Siku ya Qiyaamah.

wanaitekeleza ‘ibaadah hii tukufu. Pia, zingatia kwamba huo ulikuwa ni mtihani wa Haajar (عليها السلام) alipoachwa katika bonde lisilokuwa na wakazi wala chochote, lakini alitawakali kwa Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kuwa Ndiye Aliyemuamrisha Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) amwache yeye na mwanawe sehemu hiyo peke yao.

- Kuadhimisha Sunnah na kutambua kwamba amri yoyote ya Allaah (سبحانه وتعالى) na Rasuli Wake (صلى الله عليه وآله وسلم) ina hikmah ndani yake, hata kama hatukutajiwa manufaa yake. Mfano tunapotakiwa kulibusu *Al-Hajar Al-As-wad* tunafanya hivyo kufuata amri bila ya kuitikadi kwamba jiwe hilo lina manufaa au dhara na ndipo ‘Umar bin Khatwaab (رضي الله عنه) alisema alipolibusu:

  إِنِّي أَعْلَمُ أَنَّكَ حَجَرٌ لَا تَضُرُّ وَلَا تَنْفَعُ وَلَوْلَا أَنِّي رَأَيْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُقَبِّلُكَ مَا قَبَّلْتُكَ

  “Hakika mimi najua kwamba wewe ni jiwe hudhuru wala hunufaishi, na lau kama nisingelimuoma Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) anakubusu nisingelikubusu.”[226]

- Unapokunywa maji ya Zamzam, kumbuka neema za Allaah (سبحانه وتعالى) kwani hayo ni maji yenye baraka na ni poza ya kila maradhi ukitilia niyyah, na pia sababu ya kutakabaliwa mtu du’aa zake. Zingatia maajabu yake kwamba maji hayo yalitumiwa na watu tokea yalipoanza na watu wanayanywa wala hayamaliziki!

- Unaposimama ‘*Arafah* pamoja na Mahujaji wote siku moja, wakati mmoja, kila mmoja akiwa na hamasa ya kuomba du’aa na kuomba tawbah na maghfirah. Mkusanyiko huo mkubwa mno ni kiasi cha milioni tano na hapo kuna tabu na mashaka, basi zingatia kwamba itakuwaje Siku ya mkusanyo wa kufufuliwa viumbe vyote? Hali yao itakuwa kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

[226] Al-Bukhaariy, Muslim na wengineo.

عَنْ عَائِشَةَ قَالَتْ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: ((**يُحْشَرُ النَّاسُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ حُفَاةً عُرَاةً غُرْلًا**)) قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ النِّسَاءُ وَالرِّجَالُ جَمِيعًا يَنْظُرُ بَعْضُهُمْ إِلَى بَعْضٍ؟ قَالَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ((**يَا عَائِشَةُ الْأَمْرُ أَشَدُّ مِنْ أَنْ يَنْظُرَ بَعْضُهُمْ إِلَى بَعْضٍ**))

Imepokelewa toka kwa 'Aaishah (رضي الله عنها) amesema: "Nilimsikia Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: ***((Watu watafufuliwa Siku ya Qiyaamah wakiwa hawana viatu, wakiwa uchi, hawakutahiriwa))***. Nikasema: Ee Rasuli wa Allaah! Wanawake na wanaume watakuwa pamoja wakitazamana? Akasema (صلى الله عليه وآله وسلم): ***((Ee 'Aaishah! Hali siku hiyo itakuwa ngumu mno hadi kwamba hakuna atakayejali kutazamana!))***[227]

- *Katika Jamaraat*, kumbuka kwamba unatekeleza amri ya Allaah (سبحانه وتعالى) upate Radhi zake japokuwa huoni faida au hikmah ndani yake.

- Unapochinja, kumbuka utiifu wa Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) na kutawakali kwake pamoja na mwanawe Ismaa'iyl (عليه السلام) waliposalimu wote kwa Allaah (سبحانه وتعالى) kutekeleza amri ya ndoto.

- Utakapojivua katika Ihraam baada ya kujizuia makatazo yake, utakuwa umepata faida ya subira yako, na baada ya tabu umefarijika, basi furaha iliyoje kuitekeleza Hajj ipasavyo ukategemea malipo yake ya kufutiwa madhambi yote na kulipwa Jannah! Hali kadhalika utakapovuta subira duniani katika kutii amri za Mola wako, utafaulu Aakhirah.

- Mwishowe utakaporudi kwa ahili zako, furaha iliyoje kukutana nao, basi kumbuka hapo kwamba kuna furaha kubwa zaidi ya kukutana nao katika Jannah. Na kumbuka kinyume chake kwamba ni khasara kubwa Siku ya Qiyaamah ambayo ni khasara ya nafsi na ahli kama Anavyosema Allaah (سبحانه وتعالى):

[227] Al-Bukhaariy, Muslim na wengineo.

قُلْ إِنَّ ٱلْخَٰسِرِينَ ٱلَّذِينَ خَسِرُوٓا۟ أَنفُسَهُمْ وَأَهْلِيهِمْ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ ۗ أَلَا ذَٰلِكَ هُوَ ٱلْخُسْرَانُ ٱلْمُبِينُ ﴿١٥﴾

**((Sema: "Hakika waliokhasirika ni wale waliokhasiri nafsi zao na ahli zao Siku ya Qiyaamah. Tanabahi! Huko ndiko kukhasirika bayana))[228]**

[228] Az-Zumar (39: 15).

**21- Aayaat Katika Surwatul-Hajj Kuhusu Hajj**

أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

*A'uwdhu BiLLaahi Mina-shaytwaanir-Rajiym*

﴿ إِنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ ٱلَّذِى جَعَلْنَٰهُ لِلنَّاسِ سَوَآءً ٱلْعَٰكِفُ فِيهِ وَٱلْبَادِ ۚ وَمَن يُرِدْ فِيهِ بِإِلْحَادٍۭ بِظُلْمٍ نُّذِقْهُ مِنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٢٥﴾ ﴾

**25. Hakika wale waliokufuru na wanazuia (watu) njia ya Allaah na (pia wanazuia watu wasifike) *Al-Masjid Al-Haraam* ambao Tumeujaalia kwa watu kuwa ni sawasawa; kwa wakaao humo na wageni. Na yeyote anayekusudia humo kufanya upotofu kwa dhulma Tutamuonjesha adhabu iumizayo.**

﴿ وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَٰهِيمَ مَكَانَ ٱلْبَيْتِ أَن لَّا تُشْرِكْ بِى شَيْـًٔا وَطَهِّرْ بَيْتِىَ لِلطَّآئِفِينَ وَٱلْقَآئِمِينَ وَٱلرُّكَّعِ ٱلسُّجُودِ ﴿٢٦﴾ ﴾

**26. Na (taja) Tulipomwonyesha Ibraahiym mahali pa Nyumba (*Al-Ka'bah*, Tukamwambia): kwamba: "Usinishirikishe na chochote; na twaharisha Nyumba Yangu kwa wafanyao *Twawaaf*, na wanaosimama (kuswali) na wanaorukuu (na) kusujudu.**

﴿ وَأَذِّن فِى ٱلنَّاسِ بِٱلْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِن كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ ﴿٢٧﴾

**27. Na tangaza kwa watu Hajj; watakufikia kwa miguu na juu ya kila ngamia aliyekonda, watakuja kutoka katika kila njia pana za milima zilioko mbali kabisa.**

﴿ لِّيَشْهَدُواْ مَنَٰفِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُواْ ٱسْمَ ٱللَّهِ فِىٓ أَيَّامٍ مَّعْلُومَٰتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنۢ بَهِيمَةِ ٱلْأَنْعَٰمِ ۖ فَكُلُواْ مِنْهَا وَأَطْعِمُواْ ٱلْبَآئِسَ ٱلْفَقِيرَ ﴿٢٨﴾ ﴾

**28. Ili washuhudie manufaa yao; na walitaje Jina la Allaah katika siku maalumu kwa yale Aliyowaruzuku kati ya wanyama wenye miguu minne wa mifugo. Basi kuleni humo, na lisheni mwenye shida fakiri.**

﴿ ثُمَّ لْيَقْضُوا۟ تَفَثَهُمْ وَلْيُوفُوا۟ نُذُورَهُمْ وَلْيَطَّوَّفُوا۟ بِٱلْبَيْتِ ٱلْعَتِيقِ ﴿٢٩﴾ ﴾

**29. Kisha wamalize taka zao (mwilini), na watimize nadhiri zao, na watufu kwenye *Baytil-'Atiyq*.**

﴿ ذَٰلِكَ وَمَن يُعَظِّمْ حُرُمَٰتِ ٱللَّهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَّهُۥ عِندَ رَبِّهِۦ ۗ وَأُحِلَّتْ لَكُمُ ٱلْأَنْعَٰمُ إِلَّا مَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ ۖ فَٱجْتَنِبُوا۟ ٱلرِّجْسَ مِنَ ٱلْأَوْثَٰنِ وَٱجْتَنِبُوا۟ قَوْلَ ٱلزُّورِ ﴿٣٠﴾ ﴾

**30. Hayo, (yameamrishwa) na yeyote anayeadhimisha vitukufu vya Allaah basi hivyo ni kheri kwake mbele ya Rabb wake. Na mmehalalishiwa (kula) wanyama wa mifugo isipokuwa wale mnaosomewa. Basi jiepusheni na *rijsi* (uchafu wa kuabudu) masanamu, na jiepusheni na kauli za uongo.**

﴿ حُنَفَآءَ لِلَّهِ غَيْرَ مُشْرِكِينَ بِهِۦ ۚ وَمَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَكَأَنَّمَا خَرَّ مِنَ ٱلسَّمَآءِ فَتَخْطَفُهُ ٱلطَّيْرُ أَوْ تَهْوِى بِهِ ٱلرِّيحُ فِى مَكَانٍ سَحِيقٍ ﴿٣١﴾ ﴾

**31. Muelemee haki kwa (kumwabudu Pekee) Allaah bila ya kumshirikisha. Na yeyote anayemshirikisha Allaah basi kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, wakamnyakua ndege au upepo ukamtupa mahali mbali mno.**

﴿ ذَٰلِكَ وَمَن يُعَظِّمْ شَعَٰٓئِرَ ٱللَّهِ فَإِنَّهَا مِن تَقْوَى ٱلْقُلُوبِ ﴿٣٢﴾ ﴾

**32. Hivyo (ndivyo) na yeyote anayeadhimisha alama (za Dini) ya Allaah, basi hayo ni katika taqwa ya nyoyo.**

﴿ لَكُمْ فِيهَا مَنَٰفِعُ إِلَىٰٓ أَجَلٍ مُّسَمًّى ثُمَّ مَحِلُّهَآ إِلَى ٱلْبَيْتِ ٱلْعَتِيقِ ﴿٣٣﴾ ﴾

**33. Katika hao (wanyama) mnapata humo manufaa mpaka muda maalumu. Kisha mahali pake (pa kuchinjwa) ni (karibu na) *Baytil-'Atiyq*.**

﴿ وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنسَكًا لِّيَذْكُرُوا۟ ٱسْمَ ٱللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنۢ بَهِيمَةِ ٱلْأَنْعَٰمِ ۗ فَإِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَٰحِدٌ فَلَهُۥٓ أَسْلِمُوا۟ ۗ وَبَشِّرِ ٱلْمُخْبِتِينَ ﴿٣٤﴾ ﴾

**34. Na kwa kila Ummah Tumeweka taratibu za 'ibaadah ili wataje Jina la Allaah kwa yale Aliyowaruzuku ya wanyama wa miguu minne wa mifugo. Kwa hiyo *Ilaah* (Muabudiwa wa haki) wenu ni *Ilaah* Mmoja (Pekee); basi kwake Pekee jisalimisheni. Na wabashirie wanyenyekevu.**

﴿ ٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ ٱللَّهُ وَجِلَتۡ قُلُوبُهُمۡ وَٱلصَّٰبِرِينَ عَلَىٰ مَآ أَصَابَهُمۡ وَٱلۡمُقِيمِي ٱلصَّلَوٰةِ وَمِمَّا
رَزَقۡنَٰهُمۡ يُنفِقُونَ ٣٥ ﴾

**35. Ambao Anapotajwa Allaah nyoyo zao hushtuka (kwa khofu), na wanaosubiri juu ya yale yaliyowasibu, na wanaosimamisha Swalaah na katika vile Tulivyowaruzuku wanatoa.**

﴿ وَٱلۡبُدۡنَ جَعَلۡنَٰهَا لَكُم مِّن شَعَٰٓئِرِ ٱللَّهِ لَكُمۡ فِيهَا خَيۡرٞۖ فَٱذۡكُرُواْ ٱسۡمَ ٱللَّهِ عَلَيۡهَا صَوَآفَّۖ فَإِذَا
وَجَبَتۡ جُنُوبُهَا فَكُلُواْ مِنۡهَا وَأَطۡعِمُواْ ٱلۡقَانِعَ وَٱلۡمُعۡتَرَّۚ كَذَٰلِكَ سَخَّرۡنَٰهَا لَكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَشۡكُرُونَ
٣٦ ﴾

**36. Na ngamia na ng'ombe Tumekufanyieni kuwa ni miongoni mwa alama (za Dini) ya Allaah; kwa hao mnapata kheri (nyingi). Basi tajeni Jina la Allaah juu yao wanapopangwa safu (kuchinjwa). Na waangukapo ubavu, basi kuleni kutoka humo, na lisheni waliokinai (hawaombi) na wanaolazimika kuomba. Hivyo ndivyo Tulivyowatiisha (wanyama hao) kwa ajili yenu ili mpate kushukuru.**

﴿ لَن يَنَالَ ٱللَّهَ لُحُومُهَا وَلَا دِمَآؤُهَا وَلَٰكِن يَنَالُهُ ٱلتَّقۡوَىٰ مِنكُمۡۚ كَذَٰلِكَ سَخَّرَهَا لَكُمۡ
لِتُكَبِّرُواْ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمۡۗ وَبَشِّرِ ٱلۡمُحۡسِنِينَ ٣٧ ﴾

**37. Haimfikii Allaah nyama zake wala damu yake, lakini inamfikia taqwa kutoka kwenu. Hivyo ndivyo Tulivyowatiisha (hao wanyama) kwenu ili mpate kumtukuza Allaah (kusema: *Allaahu Akbar*) kwa yale Aliyokuongozeni; na wabashirie wafanyao ihsaan.**

## 22- Wasiojaaliwa Kwenda Kutekeleza Hajj

Waislamu wasiojaaliwa kwenda kutekeleza Hajj watambue kwamba nao wana fursa ya kujichumia thawabu tele kwa kutekeleza 'ibaadah zenye fadhila tukufu kuanzia tarehe 1 Dhul-Hijjah mpaka tarehe 13 Dhul-Hijjah kama Alivyotuamrisha Allaah (سبحانه وتعالى) na Rasuli Wake (صلى الله عليه وآله وسلم).

### 1 - Allaah Ameziapia Siku Kumi Hizi

Kwa jinsi zilivyokuwa na umuhimu mkubwa siku hizo kumi, hadi kwamba Allaah (سبحانه وتعالى) Ameziapia katika Qur-aan Anaposema:

﴿ وَٱلْفَجْرِ ۝١ وَلَيَالٍ عَشْرٍ ۝٢ ﴾

**((Naapa kwa Alfajiri. Na (kwa) masiku kumi))**[229]

Wanachuoni wafasiri wa Qur-aan wamekubaliana kwamba zilizokusudiwa hapo ni Siku kumi za Dhul-Hijjah.

### 2 - 'Amali Zake Ni Bora Kuliko Kwenda Katika Jihaad Fiy SabiyliLLaah

Kutokana na ilivyotajwa katika usimulizi wa Hadiyth ifuatayo, kwamba 'amali yoyote utendayo katika masiku kumi hayo, ni bora kuliko kwenda kupigana jihaad vitani. Ukizingatia kwenda kupigana jihaad ni jambo zito mtu kuliitikia, kwani huko kuna mashaka mbali mbali, ikiwemo khofu ya kujeruhiwa na kupoteza viungo vya mwili, kufariki, kupoteza mali n.k. Ila hilo si zito kwa mwenye iymaan ya hali ya juu kabisa kutaka kuyakabili mashaka hayo na kutamani kufa shahidi. Kwa hiyo usidharau 'amali yoyote hata iwe ndogo vipi itekeleze kwani Allaah (سبحانه وتعالى) ni *Al-Jawwaad* (Mwingi wa ukarimu), *Al-Kariym* (Mkarimu), *Al-Wahhaab* (Mwingi wa kutunuku, Mpaji wa yote), *Al-Majiyd* (Mwingi mno wa vipawa na ukarimu).

---

229 Al-Fajr (89: 1-2).

Hadiyth ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

((مَا مِنْ أَيَّامٍ الْعَمَلُ الصَّالِحُ فِيهَا أَحَبُّ إِلَى اللَّهِ مِنْ هَذِهِ الأَيَّامِ)) يَعْنِي أَيَّامَ الْعَشْرِ. قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ: وَلاَ الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ؟ قَالَ: ((وَلاَ الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ إِلاَّ رَجُلٌ خَرَجَ بِنَفْسِهِ وَمَالِهِ فَلَمْ يَرْجِعْ مِنْ ذَلِكَ بِشَيْءٍ))

***((Hakuna siku ambazo vitendo vyake vyema Anavipenda Allaah kama siku kumi hizi)) yaani siku kumi za mwanzo wa mwezi wa Dhul-Hijjah)).*** Akaulizwa, je, hata jihaad katika njia ya Allaah? Akasema: ***((Hata jihaad katika njia ya Allaah isipokuwa mtu aliyekwenda na nafsi yake na mali yake ikawa hakurudi na kimojawapo))***[230]

### 3 - Siku Za Manufaa Na Kumkumbuka Allaah

Inapasa kumdhukuru mno Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kukumbuka Neema Zake zisizohesabika:

﴿ لِّيَشْهَدُواْ مَنَـٰفِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُواْ ٱسْمَ ٱللَّهِ فِىٓ أَيَّامٍ مَّعْلُومَـٰتٍ﴾

**((Ili washuhudie manufaa yao; na walitaje Jina la Allaah katika siku maalumu))**[231]

Ibn 'Abbaas kasema: "Hizo ni siku kumi za Dhul-Hijjah." Na Amesema: "Manufaa ya dunia hii na ya Aakhirah." Manufaa ya Aakhirah yanajumuisha kupata Radhi za Allaah. Manufaa ya vitu vya dunia inajumuisha wanyama wa kuchinjwa na biashara.[232]

### 4 - 'Ibaadah Zote Zimejumuika Katika Siku Hizi

'Ibaadah zote zimejumuika katika siku kumi hizi nazo ni Swalaah, Swawm, Swadaqah na Hajj; wala hazijumuiki hizi katika wakati mwengine.

---

[230] Al-Bukhaariy, Abu Daawuwd, Ahmad, Ibn Maajah.
[231] Al-Hajj (22: 28).
[232] Tafsiyr Ibn Kathiyr.

## 5 - 'Amali Njema Za Kufanya Katika Siku Kumi Hizi

### i- Kuomba Tawbah ya kweli na kujiepusha na maasi:

Muislamu anapaswa kila siku kuomba tawbah kwa Allaah (سبحانه وتعالى). Juu ya kuwa Allaah (سبحانه وتعالى) Anamghufuria madhambi mja Wake, tawbah pia ina faida kadhaa tukufu kama zilivyotajwa katika Qur-aan na Sunnah. Kwa hiyo, masiku haya usikose kujizidishia fadhila zake. Allaah (سبحانه وتعالى) Ameamrisha mpaka Waumini kuomba tawbah:

﴿ وَتُوبُوٓاْ إِلَى ٱللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهَ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ ﴿٣١﴾ ﴾

**((Na tubuni kwa Allaah nyote, enyi Waumini mpate kufaulu))**[233]

### ii- Kumdhukuru sana Allaah (سبحانه وتعالى):

Inapasa kumdhukuru mno Allaah (سبحانه وتعالى) kwa *Tasbiyh, Tahmiyd, Tahliyl, Takbiyr* (kusema: Subhaana Allaah, AlhamduliLlaah, Laa Ilaaha Illa Allaah, Allaahu Akbar).

عن ابْنِ عُمَرَ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: **((مَا مِنْ أَيَّامٍ أَعْظَمُ عِنْدَ اللَّهِ وَلَا أَحَبُّ إِلَيْهِ مِنَ الْعَمَلِ فِيهِنَّ مِنْ هَذِهِ الْأَيَّامِ الْعَشْرِ فَأَكْثِرُوا فِيهِنَّ مِنَ التَّهْلِيلِ وَالتَّكْبِيرِ وَ التَّحْمِيدِ))** أخرجه أحمد

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Hakuna siku zilizokuwa tukufu kwa Allaah na zilizokuwa vitendo vyake vipenzi kabisa Kwake kama siku hizi, basi zidisheni Tahliyl na Takbiyr na Tahmiyd))***[234]

Inavyopasa kufanya takbiyr:

**الله أكبر. الله أكبر. لا إله إلا الله. والله أكبر. الله أكبر ولله الحمد**

---

[233] An-Nuwr (24: 31).

[234] Ahmad.

***"Allaahu Akbar, Allaahu Akbar, Laa Ilaaha Illa Allaah Wa-Allaahu Akbar, Allaahu Akbar WaliLLaahil-Hamd"***

"Allaah ni Mkubwa, Allaah ni Mkubwa, hapana ilaah (muabudiwa wa haki) isipokuwa Allaah, na Allaah ni Mkubwa, Allaah ni Mkubwa, na kuhimidiwa ni kwa Allaah (Pekee)

Takbiyr hii ni aina mbili:

***Takbiyr Al-Mutwlaq***: Za Nyakati Zote: Takbiyr wakati wote usiku au mchana tokea unapoingia mwezi wa Dhul-Hijjah na inaendelea mpaka siku ya mwisho ya *Tashriyq* (tarehe 13 Dhul-Hijjah) baada ya magharibi. Inaletwa mahali popote; sokoni, njiani, majumbani n.k.

***Takbiyr Al-Muqayyad***: Za Nyakati Maalumu: Takbiyr baada ya kila Swalaah na huanza baada ya Swalaah ya Alfajiri siku ya *'Arafah* mpaka baada ya Swalaah ya Alasiri ya tarehe 13 Dhul-Hijjah.

**iii- Kufufua Sunnah ya Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم):**

Wanaume wanatakiwa waseme kwa sauti ili kuwakumbusha wengine na kufufua Sunnah ya Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) na wanawake waseme kimya kimya isipokuwa wakiwa na mahaarim wao. Kufufua Sunnah ya Nabiy ni muhimu kwani bila ya kufanya hivyo tutakuwa kwanza tunakosa fadhila zake, pili zitapotea Sunnah za kiongozi wetu Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم):

**كَانَ ابْنُ عُمَرَ وَأَبُو هُرَيْرَةَ يَخْرُجَانِ إِلَى السُّوقِ فِي أَيَّامِ الْعَشْرِ يُكَبِّرَانِ وَيُكَبِّرُ النَّاسُ بِتَكْبِيرِهِمَا**

"Ibn 'Umar na Abu Hurayrah walikuwa wakienda sokoni katika siku kumi na kufanya Takbiyr kwa sauti na watu wakiwaigiza."[235]

**iv- Kuzidisha 'amali njema mbali mbali:**

[235] Al-Bukhaariy.

Kutekeleza fardhi ya Swalaah kwa kuswali kwa wakati wake, kuswali Sunnah zaidi, kusoma Qur-aan, swadaqah, du'aa, kutii wazazi na kuwafanyia wema, kuwasiliana na jamaa (kuunga undugu), kuwafanyia wema jirani, kuamrishana mema na kukatazana maovu, kufanyiana wema na ihsani na kila aina ya jema hata dogo vipi, kwani huenda likawa ni lenye kumridhisha Allaah (سبحانه وتعالى) mno.

**v- Kufunga siku hizi khaswa siku ya *'Arafah*[236]:**

عَنْ أَبِي قَتَادَةَ رضي الله عنه أن النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: **((صِيَامُ يَوْمِ عَرَفَةَ أَحْتَسِبُ عَلَى اللَّهِ أَنْ يُكَفِّرَ السَّنَةَ الَّتِي قَبْلَهُ وَالسَّنَةَ الَّتِي بَعْدَهُ))** أخرجه مسلم

Imepokelewa toka kwa Abu Qataadah (رضي الله عنه) ambaye amesema: Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) kasema kuhusu Swawm ya *'Arafah* kuwa ***((inafuta madhambi ya mwaka uliopita na wa baada yake))***[237]

**vi- Kuchinja baada ya Swalaah ya 'Iyd:**

'Ibaadah tukufu na ni Sunnah iliyosisitizwa na Wanachuoni wameona kuwa ni waajib kwa kila aliyekuwa na uwezo kwake kuchinja. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنۡحَرۡ ۝٢ ﴾

**((Basi Swali kwa ajili ya Rabb wako na uchinje))[238]**

فعَنْ أَنَسٍ رضي الله عنه قَالَ: **((ضَحَّى النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِكَبْشَيْنِ أَمْلَحَيْنِ أَقْرَنَيْنِ ذَبَحَهُمَا بِيَدِهِ وَسَمَّى وَكَبَّرَ وَوَضَعَ رِجْلَهُ عَلَى صِفَاحِهِمَا))** متفق عليه

Imepokelewa toka kwa Anas (رضي الله عنه) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) alichinja kondoo wawili weupe[239] wenye pembe,

[236] Rejea Mlango wa "Historia Fupi Ya Makkah Na Kuhusu Hajj Na 'Umrah."
[237] Muslim.
[238] Al-Kawthar (108- 2).

amewachinja kwa mikono yake, akasema *BismiLLaah* na *Allaahu Akbar* na akaweka mguu wake upande wa nyuma yao."[240]

Kuchinja kuna hikmah kubwa ndani yake na fadhila zake ni adhimu. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ لَن يَنَالَ ٱللَّهَ لُحُومُهَا وَلَا دِمَآؤُهَا وَلَٰكِن يَنَالُهُ ٱلتَّقْوَىٰ مِنكُمْ ۚ كَذَٰلِكَ سَخَّرَهَا لَكُمْ لِتُكَبِّرُوا۟ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمْ ۗ وَبَشِّرِ ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿٣٧﴾ ﴾

**((Haimfikii Allaah nyama zake wala damu yake, lakini inamfikia taqwa kutoka kwenu. Hivyo ndivyo Tulivyowatiisha (hao wanyama) kwenu ili mpate kumtukuza Allaah (kusema: *Allaahu Akbar*) kwa yale Aliyokuongozeni; na wabashirie wafanyao ihsaan.))**[241]

عَنْ عَائِشَةَ (رضي الله عنها) أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((**مَا عَمِلَ آدَمِيٌّ مِنْ عَمَلٍ يَوْمَ النَّحْرِ أَحَبَّ إِلَى اللهِ مِنْ إِهْرَاقِ الدَّمِ, إِنَّهَا لَتَأْتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِقُرُونِهَا, وَأَشْعَارِهَا, وَأَظْلَافِهَا وَأَنَّ الدَّمَ لَيَقَعُ مِنَ اللهِ بِمَكَانٍ قَبْلَ أَنْ يَقَعَ مِنَ الْأَرْضِ فَطِيبُوا بِهَا نَفْسًا**))

Imepokelewa toka kwa 'Aaishah (رضي الله عنها) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Hakuna kitendo cha bin Aadam kilichokuwa ni kipenzi kabisa kwa Allaah siku ya kuchinja kama kumwaga damu. Atakuja (huyo mnyama) siku ya Qiyaamah na pembe zake, kucha zake na nywele zake. Damu yake itamwagika mahali fulani Allaah Anapajua kabla ya kumwagika katika ardhi. Hivyo zipendezesheni nafsi kwayo))***[242]

Na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) alipoulizwa:

مَا هَذِهِ الْأَضَاحِيُّ؟ قَالَ: ((**سُنَّةُ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ**)) قَالُوا: فَمَا لَنَا فِيهَا يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ قَالَ: ((**بِكُلِّ شَعَرَةٍ حَسَنَةٌ**)) قَالُوا: فَالصُّوفُ يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ قَالَ: ((**بِكُلِّ شَعَرَةٍ مِنْ الصُّوفِ حَسَنَةٌ**))

---

[239] Baadhi ya wanachuoni wamesema kuwa ni weupe ulio na alama nyeusi, wengine wamesema uliochanganyika na wekundu.
[240] Al-Bukhaariy na Muslim.
[241] Al-Hajj (22: 37).
[242] At-Tirmidhiy, Sunan Ibn Maajah.

"Nini hivi vichinjo?" Akajibu: ***((Ni Sunnah ya baba yenu Ibraahiym)).*** Wakasema, "Nini umuhimu wake kwetu?" Akasema: ***((Katika kila unywele kuna jema moja))*** Wakasema: "Na sufi?" Akasema: ***((Katika kila unywele wa sufi kuna jema moja))***[243]

**Yanayompasa Kufanya Mwenye Kutaka Kuchinja**

Baada ya kutia niyyah ya kuchinja, asikate mtu nywele wala kucha mpaka 'amalize kuchinja kama tulivyoamrishwa katika Hadiyth ifuatayo:

عَنْ أُمِّ سَلَمَةَ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((**إِذَا رَأَيْتُمْ هِلَالَ ذِي الْحِجَّةِ وَأَرَادَ أَحَدُكُمْ أَنْ يُضَحِّيَ فَلْيُمْسِكْ عَنْ شَعْرِهِ وَأَظْفَارِهِ**)) وفي راوية: ((**فَلَا يَأْخُذْ مِنْ شَعْرِهِ وَلَا مِنْ أَظْفَارِهِ حَتَّى يُضَحِّيَ**)) مسلم

Imepokelewa toka kwa Ummu Salamah (رضي الله عنها) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Ukiandama mwezi wa Dhul-Hijjah na ikiwa yuko anayetaka kuchinja basi azuie (asikate) nywele zake na kucha zake))***[244]**.** Na katika riwaya nyingine: ***((Asikate nywele wala kucha mpaka akimaliza kuchinja))***[245]

Hii ni fadhila na neema kwa Waislamu wasiojaaliwa Hajj kwamba nao watakuwa katika aina ya 'Ihraam'. Ukisahau, mfano ukakata kucha basi endelea tu na niyyah yako mpaka umalize kuchinja.

**vii- Kuhudhuria Swalah ya 'Iyd:**

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amewahimiza mpaka wanawake walio katika hedhi na wazee waende kusikiliza khutbah ya Swalaah. Wakati wa Swalaah ukifika, wanawake wenye hedhi wajitenge kando hadi itakapomalizika Swalaah na kisha wajiunge na wenzao kusikiliza khutbah.

---

243 Ahmad, Ibn Maajah.
244 Muslim.
245 Ibn Maajah.

**viii- Siku Za Tashriyq[246]:**

Ni siku ya kumi na moja na kumi na mbili na kumi na tatu ya Dhul-Hijjah yaani baada ya siku ya 'Iyd. Na siku hizi tatu zimeitwa siku za *Tashriyq* kwa sababu watu walikuwa wakikatakata nyama na kuzianika juani. Siku za kuanika (nyama) juani. Na pia siku hizi hujulikana kwa 'siku za *Minaa*'. Ni masiku ya kumdhukuru mno Allaah (سبحانه وتعالى). Haifai kufunga Swawm masiku haya hata kama ni kawaida yake mtu kufunga Swawm za Sunnah kwa sababu amekataza Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kupitia Hadiyth ya Abu Hurayrah (رضي الله عنه) isemayo:

أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَعَثَ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ حُذَافَةَ يَطُوفُ فِي مِنًى أَنْ: **((لَا تَصُومُوا هَذِهِ الْأَيَّامَ فَإِنَّهَا أَيَّامُ أَكْلٍ وَشُرْبٍ وَذِكْرِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ))**

Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alimtuma 'Abdullaah bin Hudhaafah azunguke *Minaa* na atangaze: ((***Msifunge siku hizi, kwani hizi ni siku za kula na kunywa na kumdhukuru Allaah*** عزَّ وجلّ))[247]

---

[246] Rejea Mlango wa 'Utekelezaji Wa Hajj' Kupata fadhila zake.
[247] Ahmad.

## 23- Makosa Yanayofanywa Baada Ya Kumaliza Hajj Na Kurudi Nyumbani

Muislamu anapomaliza Hajj anapaswa kuthibitika katika 'Ibaadah zake. Kubakia katika istiqaamah (kuthibitika) ni dalili ya kutakabaliwa Hajj yako. Aayah na Hadiyth kadhaa zimetaja kuhusu jambo hili; baadhi ni hizi zifuatazo:

Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

وَٱعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ ٱلْيَقِينُ ﴿٩٩﴾

**((Na mwabudu Rabb wako mpaka ikufikie yakini (mauti))**[248]

Ndugu Muislamu usije kuwa mfano wa yule mwanamke wa Makkah aliyekuwa akisonga uzi wake tokea asubuhi hadi jioni kisha alikuwa anaufumua wote na kazi yake yote ikawa ni ya bure. Amemtaja Allaah (سبحانه وتعالى) katika kauli Yake:

وَلَا تَكُونُوا۟ كَٱلَّتِى نَقَضَتْ غَزْلَهَا مِنۢ بَعْدِ قُوَّةٍ أَنكَـٰثًا

**((Na wala msiwe kama yule mwanamke aliyezongoa uzi wake vipande vipande baada ya (kuusokota na) kuwa mgumu))**[249]

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ametupa nasaha kuhusu kuthibitisha iymaan na 'amali zetu:

عَنْ أَبِي عَمْرَةَ سُفْيَانَ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ (رضي الله عنه) قَالَ: قُلْتُ يَا رَسُولَ اللَّهِ قُلْ لِي فِي الإِسْلاَمِ قَوْلاً لاَ أَسْأَلُ عَنْهُ أَحَدًا غَيْرَكَ)) قَالَ: ((**قُلْ آمَنْتُ بِاللَّهِ ثُمَّ اسْتَقِمْ**)) رواه مسلم

Imepokelewa kutoka kwa Abu 'Amrah Sufyaan bin 'Abdillaah (رضي الله عنه) amesema: Nilisema: "Ee Rasuli wa Allaah! Niambie neno katika Uislamu ambalo sitomuuliza yeyote isipokuwa wewe." Akasema: *((**Sema: Nimemwamini Allaah kisha uwe na istiqaamah** [msimamo]))*[250]

Jitahidi kuthibitika katika 'amali za 'ibaadah japo kwa kiasi kidogo ambacho cha uwezo wako ili uweze kuendeleza

---

248 Al-Hijr (15: 99).
249 An-Nahl (16: 92).
250 Muslim.

'ibaadah zako bila ya kuchoka ubakie katika istiqaamah. Hivyo ndivyo Anavyopenda Allaah (سبحانه وتعالى) kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

(( أَحَبُّ الأَعْمَالِ إِلَى اللهِ أَدْوَمُهَا وَإِنْ قَلَّ)) متفق عليه

***((Vitendo Anavyovipenda Allaah zaidi (kuliko vyote) ni vile vinavyodumishwa japokuwa ni kidogo)***[251]

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa Baada Ya Kumaliza Hajj Na Kurudi Nyumbani**

- Baadhi ya Mahujaji wanaporudi makwao, hufanyiwa sherehe, mialiko ya watu na karamu kwa ajili ya kupongezwa. Wengine husomewa Mawlid. Hakuna uthibitisho wowote kwamba Mahujaji wafanyiwe jambo lolote lile. Kufanya hivyo ni uzushi katika Dini. Hakuna lolote lipasalo kufanywa ila tu inaruhusiwa jamaa wa karibu na marafiki kumtembelea aliyehiji nyumbani kwake kumpongeza na kumuombea.

- Kuwaita waliohiji 'Haaj fulani' au 'Haajah fulani'. Haipasi kwani hivyo si katika Sunnah na haipasi kujitakasa mtu kwa sifa ya 'amali aliyoitenda.

- Kudhania kwamba mtu anaporejea Hajj anakuwa na makarama kwa muda wa masiku arubaini, na hivyo watu hukimbilia kumtembelea kupata baraka zake.

- Kuchinja kwa ajili Mahujaji kabla ya kuingia nyumbani kwake.

- Wengine hurudia katika maasi na hivyo ni kuharibu juhudi zao za Hajj.

*Subhaanaka-Allaahumma wa bihamdika, nash-hadu an laa ilaaha illa Anta, nastagh-firuka wa natuwbu Ilayka wal-*

[251] Al-Bukhaariy na Muslim.

*hamduliLlaahi Rabbil-'aalamiyn, wa-Swalla-Allaahu 'alaa Nabiyyinaa Muhammad wa 'alaa aalihi wa swahbihi wa sallam.*

**24- Faharasa**

| Neno | Maana Yake |
|---|---|
| *'Arafah* | Sehemu muhimu kabisa ya kusimama katika Hajj ambayo ndio kilele cha Hajj, na bila yake Hajj haikamiliki. Iko baada ya *Muzdalifah* kutoka Makkah, na jabali lake huitwa Jabal *'Arafah*. |
| *Al-Baqiy'* | Sehemu Madiynah ambako kuna makaburi ya Maswahaba. |
| Al-Haaj | Mwanaume mwenye kutekeleza fardhi ya Hajj huko Makkah. Lakini haifai kuitwa baada ya kurudi nyumbani. |
| Al-Haajah | Mwanamke mwenye kutekeleza fardhi ya Hajj huko Makkah Lakini haifai kuitwa baada ya kurudi nyumbani |
| *Al-Hajar Al-As-wad* | Jiwe jeusi lilioko pembeni mwa *Al-Ka'bah*. |
| *Al-Haram* | Sehemu tukufu kama *Masjid Al-Haraam*, *Masjid An-Nabawiy*, *Mash'ar Al-Haraam* (*Muzdalifah*). |
| *Al-Idhwtiba'a* | Kuweka sehemu ya katikati ya shuka (Ridaa) chini ya kwapa ya mkono wa kulia na ncha zake juu ya bega la mkono wa kushoto katika *Twawaaf*. |
| *Al-Ifraad* | Aina ya Hajj inayotekelezwa bila ya 'Umrah. Mahujaji hahitajiki kuchinja. |
| *Al-Jamrat Al-'Aqabah* | Nguzo kubwa ya Jamrah (kurusha vijiwe) iliyoko karibu na Makkah. |
| *Al-Jamrat Al-Wustwaa* | Nguzo ya katikakati ya Jamrah (kurusha vijiwe) iliyoko *Minaa* |
| *Al-Jamrat Asw-Swughraa* | Nguzo ndogo ya Jamrah (kurusha vijiwe) iliyoko *Minaa* |
| *Al-Ka'bah* | Nyumba tukufu iliyoko katika Msikiti mtukufu wa Makkah. |
| *Al-Mar-wah* | Jina la jabali ambako Muislamu anamalizia *As-Sa'-y* yake. |

| | |
|---|---|
| *Al-Mas-'aa* | Eneo la kufanya *As-Sa'-y* katika *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah* |
| *Al-Qiraan* | Hajj anayotekeleza mtu kwa kuunganisha 'Umrah na Hajj bila ya kujitoa katika Ihraam. Mahujaji huwa amefika Makkah akiwa na mnyama wa kuchinja. |
| *Ar-Rakdhw* | Kukimbia katika *As-Sa'-y* baina ya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah* kwenye alama za kijani. |
| *Ar-Raml* | Kwenda mwendo wa mbio mbio kwa hatua ndogo ndogo katika mizunguko mitatu ya mwanzo kwenye *Twawaaf*. |
| *Ar-Ram-y* | Kurusha vijiwe. |
| *As-Sa'-y* | Kutembea baina ya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah*. |
| *As-Sa'-y* | Kutembea baina ya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah*. |
| *Asw-Swafaa* | Jina la jabali ambako Muislamu anaanza *As-Sa'-y*. |
| *Asw-Swiraatw* | Njia watakayopita watu Siku ya Qiyaamah kuingia katika Jannah au kuangukia Motoni. |
| *Atw-Twawaaf* | Kuzunguka *Al-Ka'bah* mara saba. |
| *Ayyaam Al-Biydhw* | Masiku meupe ya mwezi unapokuwa umejaa katikati ya mwezi yaani tarehe 13, 14 na 15 za kalenda ya Kiislamu. |
| *Bid'ah* | Uzushi – kitendo au 'amali inayotekelezwa bila ya kuthibiti dalili yake kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم), Maswahaba na *Salafus-Swaalih*. |
| *Burqah* | Aina ya niqaab ya kufunika uso kwa wanawake. |
| *Dhul-Hijjah* | Mwezi wa kumi na mbili katika kalenda ya Kiislamu. |
| *Dhul-Qa'dah* | Mwezi wa kumi na moja katika kalenda ya Kiislamu |
| *Du'aa* | Kumuelekea Allaah (سبحانه وتعالى) katika kuomba haja. |
| *Ghashwah* | Mtandio au shungi jepesi la kufunika uso bila ya kubanika uso. |
| *Ghayr* | Isiyosisitizwa. Mfano Swalaah za kabla ya |

| | |
|---|---|
| *Muakkadah* | Swalaah ya Alasiri au rakaa mbili kabla ya Magharibi na 'Ishaa. |
| *Ghuslu* | Josho. Kuoga kwa ajili ya kujitwaharisha janaba, hedhi, nifaas au kuoga kwa ajili ya Ijumaa, kumwosha maiti. |
| *Hajj Mabruwr* | Hajj iliyofanikiwa ambayo jazaa yake ni Jannah. |
| Hamzah | 'Ami yake Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliyekufa Shahiyd katika vita vya Uhud. |
| *Haniyfaa* | Kuelemea upande mmoja tu wa haki na kujiengua na ubatilifu. Sifa ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) Amempa Nabiy Ibraahiym (عليه السلام). |
| Hedhi | Damu anayopata mwanamke kila mwezi |
| *Hijr* | Sehemu iliyoko pembezoni mwa *Al-Ka'bah*. Wengi wanaiita kimakosa kuwa ni '*Hijr* Ismaaiyl' na hali inapaswa itajwe kuwa ni *Hijr* pekee kwani ni sehemu ya *Al-Ka'bah*. |
| *Ihraam* | Kuingia katika niyyah ya 'ibaadah ya Hajj au 'Umrah. Shuka mbili wanazovaa wanaume katika hali hiyo pia huitwa hivyo. |
| *Ikhlaasw* | Kusafisha niyyah na 'amali kwa ajili ya Allaah (سبحانه وتعالى) Pekee. |
| Istilaam | Kuligusa kwa mkono *Al-Hajar Al-As-wad* katika kutufu *Al-Ka'bah* na mtu akishindwa kulifikia ni kuashiria kwa mkono na hivyo ni kama kuliamkia. |
| *Istiqaamah* | Kuthibitika katika 'Ibaadah na 'amali njema. |
| *'Iyd Al-Adhw-haa* | Sikukuu ya kuchinja yaani 'Iyd katika mwezi wa Dhul-Hijjah. |
| *Jaahiliyyah* | Wakati wa ujinga yaani kabla ya Uislamu. |
| *Jabal Al-Hiraa* | Jabali alilokuwa akikaa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kutafakari na akateremshiwa Wahyi wa mwanzo kabisa. |
| *Jabal Ath-Thawr* | Jabali alojificha Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) na Abu Bakr (رضي الله عنه) wakati walipokuwa wakifanya hijrah kuelekea Madiynah, wakalifikia Makafiri wa ki-Quraysh mlangoni mwake ila Allaah (سبحانه وتعالى) Aliwalinda kwa Qudra Yake. |
| *Jamaraat* | Ujumla wa Jamrah – Minara wanayorushia |

| | |
|---|---|
| | vijiwe Mahujaji. |
| *Kaffaarah* | Fidia ya kuchinja au kufunga Swawm au kutoa sadaka, au kulisha masikini au kuacha huru mtumwa n.k. |
| *Khushuu'* | Unyenyekevu unaokusudiwa khasa katika Swalaah kwa kusilimisha akili, moyo na viungo kumnyenyekea Allaah (سبحانه وتعالى). |
| *Lawh Al-Mahfudhw* | Ubao Uliohifadhiwa ambao umeandikwa na Allaah (سبحانه وتعالى) *Qadhwaa* na *Qadar*. |
| *Manaasik* | Matendo ya Hajj au ya 'Umrah. |
| *Maqaam Ibraahiym* | Jiwe alilokanyaga Nabiy Ibraahiym na kusimama kuomba Du'aa baada ya kujenga *Al-Ka'bah*. |
| *Mas-'aa* | Eneo lilonyooka baina ya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah*. |
| *Mas-h Al-Khuffayn* | Fiqhi ya wudhuu kuhusu kupangusa juu ya soksi za ngozi zilizovuka makongo mawili ya miguu kwenda juu, au hata soksi za kawaida au viatu kwa ajili ya kutekeleza wudhuu. |
| *Mash'ar Al-Haraam* | Bonde tukufu lililoko *Muzdalifah*. |
| *Masjid Al-Haraam* | Msikiti Mtukufu wa Makkah. |
| *Masjid An-Nabawiy* | Msikiti wa Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) – Madiynah. |
| *Minaa* | Bonde karibu na Makkah na mahali patukufu wanapokwenda kulala wanaofanya Hajj kutekeleza baadhi ya vitendo vya fardhi za Hajj. |
| *Muakkadah* | Iliyosisitizwa. Mfano Sunnah iliyosisitizwa au Swalaah zilosisitizwa za kabla ya Swalaah na baada ya Swalaah za fardhi. |
| *Mustahabb* | Inapendekezeka kutendwa. |
| *Muzdalifah.* | Sehemu tukufu wanapokesha Waislamu katika 'ibaadah ya Hajj ipo baina ya *'Arafah* na *Minaa*. |
| *Naafilah* | Vitendo vya 'ibaadah ambavyo havikufaridhishwa na Allaah (سبحانه وتعالى) bali ni ambavyo Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم)amevitenda katika Sunnah zake, mfano Swalaah ya |

| | |
|---|---|
| | *Dhwuhaa, Witr, Tahajjud*, kufunga Jumatatu na Alkhamiys, *Ayyaam Al-Biydhw*, kutekeleza Hajj mara ya pili na 'Umrah n.k. |
| *Namirah* | Msikiti uliopo '*Arafah*. |
| *Nifaas* | Damu ya uzazi. |
| Nikaah | Kufunga ndoa. |
| *Niqaab* | Kifuniko cha uso wanachovaa wanawake Waislamu. |
| *Niyyah* | Kutia *niyyah* ya 'amali fulani ambayo mahali pake ni moyoni na si kutamkwa. |
| *Qadhwaa* Na *Qadar* | Majaaliwa na Makadario yaliyoandikwa katika Lawhim-Mahfudwh |
| *Qubaa* | Msikiti wa mwanzo waliojenga Waislamu walipoingia Madiynah kutoka Makkah pamoja na Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم). |
| *Rukn Al-Yamaaniy* | Pembe katika *Al-Ka'bah* baina ya kona hiyo na ya *Al-Hajar Al-As-wad.* |
| *Sakaraat Al-Mawt* | Mateso ya mtu wakati anapofariki. |
| *Salafus-Swaalih* | Wema waliotangulia katika karne tatu za mwanzo alizozisifu Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). Karne ya kwanza ikiwa ni karne ya Maswahaba na mbili zinazofuatia ndio jumla ni tatu. |
| *Shariy'ah* | Shariy'ah au hukmu za Dini. |
| *Shawwaal* | Mwezi wa kumi katika kalenda ya Kiislamu |
| *Sunnah* | Mwenendo wa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) katika kauli na matendo, au jambo waliotenda Maswahaba akalinyamazia kwa kuwa amelikubali. |
| *Sunnat Al-Wudhuu* | Sunnah ya wudhuu, inayoswaliwa rakaa mbili baada ya kuchukua wudhuu. |
| *Suwratul-Ikhlaasw* | Suwrah Namba 112 katika Qur-aan. |
| *Suwratul-Kaafiruwn* | Suwrah Namba 109 katika Qur-aan. |
| *Swahaabah* | Wanaume walioishi na kumuona Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). |
| *Swahaabiyaat* | Wanawake walioishi na kumuona Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). |

| | |
|---|---|
| *Swahiyh* | Sahihi. |
| *Tahajjud* | Swalaah inayoswaliwa usiku baada ya mtu kuamka usingizini kama ni 'amali ya naafilah. |
| *Tahiyyat Al-Masjid* | Swalaah ya rakaa mbili anayoswali mtu anapoingia tu Msikitini kwa ajili ya kuamkia Msikiti. |
| *Tahliyl* | Kumpwekesha Allaah: *Laa ilaaha illa-Allaah*. |
| *Tahmiyd* | Aina zote za kumhimidi Allaah mfano kusema AlhamduliLLaah. |
| *Takbiyr* | Kumtukuza Allaah: *Allaahu Akbar*. |
| *Takbiyr* | Kusema *Allaahu Akbar* (Allaah Mkubwa). |
| *Takbiyrah* | *Takbiyr*. Kusema *Allaahu Akbar* (Allaah Mkubwa). |
| *Talbiyah* | Du'aa ya Muislamu anayosema anapoingia katika Ihraam baada ya kutia niyyah. |
| *Tamattu'* | Aina ya Hajj ya kustarehe (mapumziko) kwa kuwa anatekeleza 'Umrah kwanza kisha anajitoa katika Ihraam kisha anatekeleza Hajj. Mwenye kuhiji hutakiwa kuchinja na awe hakufika Makkah na mnyama huyo. |
| *Tarwiyah* | Tarehe 8 ya Dhul-Hijjah. |
| *Tasbiyh* | Aina zote za kumtakasa Allaah mfano Subhaana-Allaah, *Subhaana Allaahi wa Bihamdihi, Subhaana-Allaahi Al-'Adhwiym* n.k. |
| *Tawfiyq* | Kuwezeshwa na Allaah (سبحانه وتعالى) kutekeleza jambo. |
| *Twaaf Al-Ifaadhwah* | *Twawaaf* ya Hajj ambayo ni moja nguzo katika taratibu za Hajj. |
| *Twawaaf* | Mzunguko katika *Al-Ka'bah*. |
| *Twawaaf Al-Quduwm* | *Twawaaf* ya kuingia (mwanzo unapowasili) Makkah ambayo inatekelezwa na mwenye kuhiji Hajj ya *Al-Qiraan* na *Al-Ifraad* kama ni kitendo cha Sunnah. |
| *Twawaaf Al-Wadaa'i* | *Twawaaf* ya kuaga |
| *Twawaaf At-Tatwawwu'* | *Twawaaf* ya kupenda mtu kufanya kama ni 'amali njema. Hutekelezwa pale mtu kila anapoingia Masjid Al-Haraam kabla ya kuketi Msikitini. |

| | |
|---|---|
| *Uhud* | Jabali lilioko Madiynah umeitwa hivyo kutokana na vita vilivyotokea hapo. |
| *'Umrah* | Hajj ndogo inayofanywa kwa *Twawaaf* na kuswali *Maqaam Ibraahiym* na *As-Sa'-y* pekee. Au mtu kuitekeleza kwa ajili yake pekee bila ya kuwa katika misimu ya Hajj. |
| *Waswiyyah* | Wasiya anaopaswa Muislamu kuandika kabla ya kufariki dunia. |
| *Yawm An-Nahr* | Siku ya kuchinja yaani tarehe 10 ya Dhul-Hijjah ambayo ni sikukuu ya *'Iyd Al-Adhw-haa.* |